Kitabu cha 3 katika mfululizo
Hatua za Uamsho Binafsi

Siku 40
Mgawanyo wa Mafunzo

# Washirika wa Yesu

## Waliojazwa Roho

Yesu Kristo
*"Akaaye ndani Yangu, Nami ndani yake, huyo huzaaSana"*

HELMUT HAUBEIL

**Usawiri na Uzalishaji:**
Konrad Print & Medien, www.konrad-medien.de

**Tahania za picha:**
Simon Eitzenberger, www.desim.de

**Ufasiri** kutoka sanifi ya 1 ya Kijerumani: Holly Tarita

**Mawasiliano na uagizaji katika lugha za ughaibuni:**
© Helmut Haubeil
Rosenheimer Str.49, D-83043 Bad Aibling, Germany Simu: +49 (0) 8061 4900 712
Baruapepe: helmut@haubeil.net Lugha: Kijerumani na Kiingereza

**Fasiri Mbalimbali:**

Kijerumani (Asilihali), Kiingereza. Katika fasiri: Kireno/Ureno, Kireno/Brazili, Kihispania. Ufasiri kwenda lugha zingine kadiri zinavyohitajika. Tafadhali wasiliana na Helmut Haubeil, ili aweze kusaidia.

**Mtandao:**

**www.steps-to-personal-revival.info Kijerumani: www.schritte-zur-persönlichen-erweckung.info**

Vipi vitabu vitolewavyo bure katika mfululizo mdogo uitwao Hatua za Uamsho Binafsi:

**Hatua za Uamsho Binafsi** – Kujazwa Roho Mtakatifu – Unadhahamuje hili? Katika lugha zaidi ya 40, yenye vipengele vya mgawanyo wa Kujifunza, mihadhara ya Video, kitabulahani na kitabu-e

**Kaeni Ndani ya Yesu** – Unafanyaje hili? Katika lugha 20, yenye vipengele vya mgawanyo wa Kujifunza, mihadhara ya Video

**Washirika wa Yesu Waliojazwa Roho** katika Kijerumani na Kiingereza.

**Barua 17 kwa Andrew**

**Siku Kumi za Maombi: Kutafuta Uamsho**

Lugha zote zilizofasiriwa hazitozwi gharama bali husomwa, huchapishwa, na kutumwa kwa rafiki. Kuna dondoo za maudhui:

Shuhuda (150), (Wasomaji wanasimulia *uzoefu* wao kuhusu kuishi katika Roho Mtakatifu) Maendeleo (Njia ambayo kwayo Bwana aliandaa vitabu husika)

Jinsi gani ya kuamsha shauku? (Katika maisha pamoja na Kristo, yaliyojawa Roho Mtakatifu) Nukuu kuhusu Roho Mtakatifu (Nukuu muhimu zilizoteuliwa kuhusu Roho Mtakatifu) Kiongozi (Vidokezo na Uzoefu kwa ajili ya viongozi)

Mshirikishe mwingine (Mbinu ni zipi?)

Mawasiliano

**Biblia:**

The Holy Bible, New King James Version, Hakinakili 1982 cha Thomas Nelson, Inc. Hazi zote zimehifadhiwa, New International Version, Hakinakili 1973, 1978, 1984 International Bible Society. Hazi zote zimehifadhiwa ulimwenguni kote.

Haki miliki ©2023
Kibidula(Family Development International)
P.O. Box 17 Mafinga
Wachapaji ni Springs of Life, Poland

**ISBN 978-9987-726-23-3**

**www.mwangaza.info**

Kitabu cha 3

# Washirika wa Yesu Waliojazwa Roho

## Taarifa Muhimu za Awali

Tunadiriki kupasua ardhi mpya tukiwa na WASHIRIKA WA YESU WALIOJAZWA ROHO. SETI-ANZILISHI yenye nyenzo zilizojaribiwa na kupimwa—zinazoitwa Barua kwa Andrew—zimejumuishwa. Hizi zina manufaa 12 (uk. 125), jambo ambalo hufanya iwe rahisi sana kwa ajili ya wasaidizi na washiriki pale wanapotaka kumsaidia mtu fulani awe na uhusiano binafsi pamoja na Yesu. Kitabu hiki kinaelezea kwa kina jinsi ya kutumia barua hizi. (Pia vinaitwa vijitabu, broshua, vijizuu). Unapovijaribu, utajawa furaha. Hatua mbili muhimu wakati wa kukutana ni: Kuambatana na mtu fulani ili ampokee Yesu (Barua kwa Andrew 13 – fupi: LA 13) na Jinsi ya kuishi katika nguvu ya Roho Mtakatifu (LA 14). Baada ya hapo hamasa na nguvu mpya ya kumfuata Yesu hujengeka.

Tunataka kutumaini katika andiko la Biblia: Lakini ashukuriwe Mungu atupaye ushindi kupitia Bwana wetu Yesu Kristo (1 Wakorintho 15:57).

**Marekani**
*Remnant Publications* 649 E. Chicago Rd Coldwater MI, 49036
Simu: 800-423-1319
au 517-279-13043
Anuani tovuti ya uagizaji:

**Kanada**
*Lucas Jurek*
118 G First Avenue North Williams Lake, BC
V2G 1Y8
Baruapepe:lucasjurek@gmail.com Simu: 250 983 - 2650

**Australia**
*Colin Hone*
Vijitabu katika Kiingereza
Baruapepe: emailcolinfhone@gmail.com

**Himaya ya Uingereza**
*ADVENT PRESS LIMITED*
141 Cressex Road High Wycombe
Buckinghamshire, HP12 4PZ
Simu: +44 7545 23 00 83
Baruapepe: info@adventpress.eu

**Ufilipino**
*Allan D. Faina*
Baruapepe: berevived7.14@gmail.com SDA Church
Fidela Herrera Subd
Bgy. Santol, Tanza,
Cavite-4108
Simu: +63 997 6003397

**Urusi**
*Source of Life Publishing House*
Vostochanya St. 9, Zaoksky 301000 Tula Region,
Russia
Simu +78 73 42 01 01
www.lifesource.ru

**Machapisho ya Lugha za Ulaya - Urusi**
*Christa Medien GmbH*
Pulverweg 6 D-21337 Lüneburg (Ujerumani) Simu: +49 (0)4131 9835-580
www.christa-medien.eu und www.christa-shop.eu
E-Mail: info@christa-medien.eu

**Ujerumani na ughaibuni**
*Wertvoll leben*
Ziegeleistr. 23, D-73635 Rudersberg www.wertvollleben.com
Baruapepe: info@wertvollleben.com Simu: +49 (0)7183 3071332

**Austria**
*TOP LIFE Wegweiser-Verlag*
Prager Str. 287, A-1210 Wien/Vienna www.toplife-center.com
Baruapepe: info@wegweiser-verlag.at Simu: +43 (0)1 229 4000

**Austria na Ujerumani**
*Adventist Book Center* Bogenhofen, A-4963 St.Peter/Hart www.adventistbookcenter.at
Baruapepe: info@adventistbookcenter.at Simu: +43 (0)2294000

**Uswisi**
*Advent-Verlag*
Leissigenstr. 17, CH-3704 Krattigen www.av-buchshop.ch
Baruapepe: info@adventverlag.ch Simu: +41 33 654 1065

**Uhispania**
*Safeliz Publishing House*
Pradillo 6, Poligono Industrial 'La Mina'
28770 Colmenar Viejo - Madrid
Simu: +34 (91)845-9877
Baruapepe: adm@safeliz.com www.publicacionesadventistas.com

MHUTUBU WA SEMINA MBALIMBALI

**Marekani na nchi nyingi:** www.spiritbaptism.org – anza ukurasa wa mwanzo kisha biringiza kushuka chini

**Ujerumani, Austria, Uswisi, Nchi za Ulaya:**
www.steps-to-personal-revival.info – bofya toleo la Kijerumani – ukurasa wa mawasiliano – biringiza kushuka chini

**Wafilipino:** Allan D. Faina, Baruapepe: berevived7.14@gmail.com, SDA Church: Fidela Herrera Subd, Bgy. Santol, Tanza, Cavite-4108, Simu: (63) 926 054 1175

Siku 40
Mgawanyo
wa Mafunzo

# Washirika wa Yesu

## Waliojazwa Roho

Jinsi gani ya kuwa mmojawapo?

HELMUT HAUBEIL

*Kitabu hiki kina ukurasa wa kujifunza mwishoni mwa kila sura: Dondoo binafsi na msaada wa mjadala + Muda Wetu wa Maombi. Pia hujumuisha mpango wa Siku 40 kwa vikundi vinavyotaka kukitumia kwa ajili ya masomo ya Siku 40. Seti-Anzilishi pia imeambatanishwa pamoja na nyenzo zilizojaribiwa na kupimwa – zinazoitwa Barua kwa Andrea – ili kuwaongoza watu waje kwa Yesu Kristo.*


DIBAJI

**ISHI KWA HAMASA NA USHINDI KUPITIA YESU!**

*Nawezaje kuwa mwenye mafanikio kama Mkristo?*

*Ni ahadi gani atupazo Mungu kwa ajili ya maisha yenye mafanikio?. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 12*

UTANGULIZI

**WASHIRIKA WA YESU WALIOJAWA ROHO**

*Jinsi gani unakuwa mmojawapo? . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 20*

SURA YA 1

**MUNGU ANAKUPENDA!**

*Nawezaje kudhahimu utimilifu wa upendo wa Mungu?*
*Je tumaini langu kwa Mungu hufanya kazi gani? . . . . . . 30*

SURA YA 2

**NJIA MAHIRI YA MUNGU**

*Kutumika, kusaidia, kutoa, kubariki! Kwa nini na kwa kusudi gani?*
*Utayari – mtazamo upatanao na moyo wa Mungu . . . . . . . .53*

SURA YA 3

**NANI ATENDAYE KAZI:
MUNGU KUPITIA KWANGU AU MIMI KWA AJILI YA MUNGU?**

*Inahusisha maswali kadhaa muhimu sana:
Je namfanyia Mungu kazi kwa uwezo wangu wa kibinadamu?
Au Mungu anaweza kutenda kazi kupitia kwangu kwa uwezo Wake wa kiungu? . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 77*

SURA YA 4

**MIAKA MAKINI YA MAFUNZO**

*Ni umuhimu gani ambao mbinu bora inayo katika kuwaongoza watu kuja kwa Yesu Kristo? . . . . . . . . . . . . . 99*

SURA YA 5

**"NITAWAFANYA KUWA WAVUVI WA WATU"**

*Nini kinachomfanya Yesu amvutie kila mmoja kifaharidi?
Kwa nini anataka tuwaongoze watu wengine waje Kwake?
Kwa nini na jinsi gani Yesu hutufanya kuwa wavuvi wa watu?
Nawezaje kuwa shuhuda fanisi kwa ajili ya Yesu? . . . . .114*

SURA YA 6

**KWA NINI TUNAPASWA KUWAONGOZA WATU WAJE KWA YESU KWANZA?**

*Sababu nzuri za utaratibu sahihi:
Sababu 10 kwa nini tuwaongoze watu waje kwa Yesu kwanza, kabla hatujawafundisha kuhusu itakidi za Biblia.
Mtiririko: Kwanza Yesu, kisha uanafunzi na Roho Mtakatifu, itakidi za Biblia, ubatizo, mafunzo. . . . . . . . 136*

SURA YA 7 - Barua kwa Andrea Na. 13.

**TUNAWEZAJE KUWAONGOZA WATU WAJE KWA YESU?**

*Kupitia kusoma pamoja somo la Biblia kwa kutumia mwongozo uitwao Barua kwa Andrea Na. 13. Jitwalie uzima kupitia uhusiano binafsi pamoja na Mungu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 152*

SURA YA 8 - Barua kwa Andrea Na. 14

**TUNAWEZAJE KUWAONGOZA WATU WAISHI KATIKA NGUVU YA MUNGU?**

*Kupitia kujifunza somo la Biblia pamoja kwa kutumia Barua kwa Andrea Na. 14 –*
*Maisha katika nguvu ya Mungu – kwa namna gani?. . . . 171*

SURA YA 9

**MSAADA WA KIVITENDO KUSAIDIA KUWAONGOZA WAPENDWA WAMWENDEE YESU**

*Barua kwa Andrea (BA) ili kuwaongoza watu waje kwa Yesu Mfululizo wa Video ili kufundishia imani*
*Nawezaje kujitafutia binafsi kanisa la kweli?. . . . . . . . . .184*

SURA YA 10

**MWANZO MPYA KIROHO– KIMISHENARI KATIKA HATUA TATU**

*Jinsi gani watu binafsim na makundi, makanisa na konferensi mbalimbali huweza kudhahimu hili?*
*“Roho Wangu atalitimiza hilo!”. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .200*

**KUJAZWA ROHO UPYA KILA SIKU!. . . . . . . . . . . . . . . .218**

**BARAKA. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 222**

**MAPENDEKEZO**

*Tafadhali simulia uzoefu wako mpya. . . . . . . . . . . . . . . . . . .  223*

**KIAMBATISHO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .225**

*Kiambatisho A: Ahadi kwa ajili ya Maombi ya upatanisho . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .  225*

*Kiambatisho B: Mapendekezo ya Namna ya Kuwafikia Watu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 225*

*Kiambatisho D: Muhtasari wa Barua kwa Andrea. . .227*

*Kiambatisho F: Mfululizo wa Video za Kufundishia Imani. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 233*

# Maisha Yazaayo Matunda

Yesu:

"… **akaaye** ndani Yangu, Nami ndani yake, huyo **HUZAA SANA**…" (Yohana 15:5)

**Nawezaje kukaa ndani ya Yesu?**

Yesu anatualika: Njoni Kwangu! (Mathayo 11:28) Yeyote ambaye amekuja kwa Yesu anaalika pia adumu Kwake. (Yohana 15:4) Na hili linafanyikaje?

> ***"Kaeni ndani Yangu, Nami ndani yenu."***
> **"Kukaa ndani ya Kristo" humaanisha:**
> **kumpokea Roho Wake daima,**
> **maisha ya kujisalimisha kikamilifu**
> **kwenye huduma Yake."** (The Desire of Ages, 676.2)

Maelezo haya hakika yalifumbua macho yangu na kunipatia ubainifu kwa ajili ya mwenendo wangu pamoja na Mungu. Kwangu mimi, hii ni siri ya maisha ya Kikristo yenye furaha. (Yohana 15:11) Ni ombi langu na shauku yangu maalumu kwamba hii pia itawaonesha wengi njia ya kupata maisha ya furaha na timilifu. Maneno haya ni msingi wa vijitabu vitatu katika mfululizo *Hatua za Uamsho Binafsi.*

**Je kuna uhusiano gani kati ya vijitabu vitatu katika mfululizo wa Hatua za Uamsho Binafsi?**

**Na. 1** Hatua za Ushindi Binafsi
Kujazwa Roho Mtakatifu
Jinsi gani unaweza kupata uzoefu huu?
Inahusu kuomba daima na **kumpokea Roho Wake.**

**Na. 2** Kaeni Ndani ya Yesu
Hii hufanyikaje?
Inahusu **maisha ya kujisalimisha kikamilifu kwa Yesu Kristo.**

**Na. 3** Washirika wa Yesu Waliojazwa Roho
Jinsi gani unaweza kuwa mshirika uliyejazwa Roho?

Inahusu **kujisalimisha kikamilifu kwenye huduma Yake pamoja na matokeo yote adhimu.**

**Neno la Faraja**

Uzoefu umeonesha kwamba usomaji wa kweli hizi za thamani huwa na baraka mahususi, pale watu wawili wanapofuata mpango wa usomaji na kuutumia kwa ajili ya muda wao wa ibada kila siku pamoja. Kuna baraka maradufu kwa wanandoa! (Kwa wengine, hii inaweza kufanyika pia kwa simu, Skaipu, nk.). Pia, muda wa mjadala kila siku ama juma pamoja na maombi katika kikundi huchangamsha sana.

DIBAJI

# Ishi kwa Hamasa na Ushindi Kupitia Yesu!

Nawezaje kuwa mwenye mafanikio kama Mkristo?
Ni ahadi gani atupazo Mungu kwa ajili ya maisha yenye mafanikio?

## Mafanikio ni nini maishani?

Kila mtu anafasili mafanikio kwa namna tofauti. Watu wengi hufikiria fedha, ushawishi, mamlaka na umaarufu. Kiasili, hii inaweza kuhesabiwa kama aina ya mafanikio, lakini hivi mafanikio maishani siyo maisha timilifu katika maana ya kina zaidi?

Katika mwaka 1923 watu tisa matajiri zaidi ulimwenguni wakati huo walikutana Chikago kwenye mkutano. Hakuna ajuaye hasa walichojadili. Lakini miaka 25 baadaye, mtu fulani alichunguza kuona nini kilichokuwa kimewatokea. Takriban wote hao walikuwa ama wamefilisika, wakiepuka kukamatwa, wakiwa gerezani kwa sababu ya udanganyifu au walikuwa wamekufa kwa shambulio la moyo au kujiua. Walikuwa na ukwasi uliokubuhu na walikuwa wamejipatia ushawishi na mamlaka makubwa. Lakini hawakuwa na mafanikio ya kweli maishani – wala hata siyo mafanikio ya kiuchumi yadumuyo. Yesu alisema: "…uzima wa mtu haumo katika wingi wa vitu vyake alivyo navyo." (Luka 12:15) (Imechukulia katika: "Helmut Haubeil & Gerhard Padderatz, Gott, Geld & Glaube – Christliches Handeln in Wirtschaftsfragen" (God, Money & Faith – Christian Conduct in Economic Matters), Eckental 2009, uk. 15, 16).

**Walikuwa wamepuuza kitu fulani muhimu sana maishani mwao: uhusiano binafsi na urafiki(sahibu) pamoja na Mungu;** Biblia huiita hii "kuwa ndani ya Kristo" (mara 170)

au *“kuzaliwa mara ya pili”* (Yohana 3:1-17) au “kuzaliwa na Mungu” (1 Yohana 5:18). Kristo anaishi ndani yetu, tunapokuwa tumejazwa Roho Mtakatifu. Mungu anatuahidi mafanikio “ndani ya Kristo” – **mathalani mafanikio** maishani. Anaambatana nasi kwenye safari yetu maishani. Anabeba wajibu, tunapobaki tukiwa tumeungana Naye kwa karibu zaidi wakati wote. Pamoja na hilo, anatupatia baraka adhimu za kiroho pamoja na uzima wa milele. E.G. White alisema: “Ufahamu wa siri hii [Kristo ndani yetu] hutupatia ufunguo wa kila baraka nyingineyo. Huufungulia nafsi hazina za ulimwengu, stamani za maendeleo halida.” (Education, uk. 172.1)

Kwa mujibu wa ulimwengu, mafanikio hutokana na uthubutu-nafsi: Maamuzi yangu huamua karibu kila kitu. Tunapopitia njia hii, basi tunawajibika binafsi kwa matokeo. Tunalazimika kushughulikia matatizo na mapungufu yote ya kibinadamu. Naam, mtu anawezakupata uzoefu wa mafanikio kwa muda kitambo. Lakini njia hii hatimaye huishia katika uangamivu (Ufunuo 14:17-20).

**Ahadi za Mungu kwa ajili ya mafanikio:** Tunaye Mungu stadi na wa pekee ajabu. Ahadi ni ushindi ulioandaliwa kwa ajili yetu. Yesu alisema kwamba alikuja ili kutukirimia uzima maridhawa. Biblia inatuahidi mafanikio ya kweli, japo neno hili halikutumika kama lilivyo. Tafadhali chunguza ibara zifuatazo:

- Zaburi 1 huonesha: yeyote ayaendeaye mapito ya Mungu, atakuwa *“kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji.”*
- Yoshua 1:7-9: *“...Bwana, Mungu wako, yu pamoja nawe kila uendako.”* (tutachunguza zaidi kuhusu hili baadaye)
- Mithali 3:5-6: *“Katika njia zako zote mkiri Yeye, Naye atayanyosha mapito yako.”*
- “Yohana 15:1-17: Agano Jipya huzungumzia “matunda”. Katika fungu la 5:

“Akaaye ndani Yangu Nami ndani yake, huyo huzaa sana.”

Mungu na wanadamu daima hutenda kazi kwa ukaribu katika mchakato huu.

## Mfano wa kivitendo wa mafanikio

Nilipokuwa na umri wa miaka 19, nilivutiwa sana na mienendo ya Danieli. Sura ya kwanza ya kitabu cha Danieli kiligusa maisha yangu yote kama baraka kuu. Hii pia ilihusika na safari yangu ya kazi, katika uchumi pamoja na kazi ya kichungaji/umishenari. Danieli, aliyekuwa mfungwa wa vita, akawa mtawala mashuhuri na wazi mkuu katika falme mbili za ulimwengu, naye alikuwa nabii wa Mungu. Leo, bado angali akihusudiwa sana na Wakristo, Waislamu na Wayahudi.

## Mwanzo wa kazi (amali) ya Danieli

Je Danieli na mateka wenzake walikuwa watu wa aina gani? Sura ya 1 hudhihirisha hilo:

Fungu la 4: Walikuwa vijana, wenye siha nzuri na sura nzuri, werevu na wenye hekima nao walitokea kwenye nyumba zinazomcha Mungu. Pamoja na hilo, walikuwa watoto katika familia za kifalme. Walitokea Yuda. Walikuwa wateka na wafungwa wa vita.

Fungu la 5: Mfalme Nebukadneza mkuu alitaka kuwasahibu vijana hawa. Alitaka kuwalea kwa namna mahususi. Aliagiza kwamba wapewe chakula na divai yake. Kufuatia hilo, Danieli na marafiki zake walitatizika: chakula aghali na cha anasa kwenye meza ya mfalme huyu kilikinzana na maagizo kwenye Biblia. Je Danieli na marafiki zake wangepaswa kufanya nini? Ilhali wakiwa mateka wa vita, walikuwa wakitegemea kabisa fadhila ya mfalme. Hakika, walishauriana wao kwa wao kwa dhati na pia wakamuuliza Mungu. Walilazimika kufanya uamuzi: Ama wale na kunywa kwa utulivu kile kilichowekwa mezani pao – kinyume na dhamiri zao – au kutafuta mbadala tofauti. Tunaambiwa tu kuhusiana na uamuzi wa Danieli, lakini bila shaka wote walikubaliana.

Fungu la 8: *"Lakini Danieli aliazimu moyoni mwake kuwa asingejitia unajisi kwa mgawo wa chakula cha kifahari cha mfalme, wala kwa mvinyo aliokunywa."* (NKJV) Danieli alikusudia kuwa mwaminifu kwa Mungu na hivyo kujiepusha kula vyakula vyovyote najisi. Katika safari ya maisha yake,

tunaona huu ulikuwa uamuzi msingi(hamali) kwa ajili ya maisha yake yote.

Danieli pia hakutaka kukubali aina yoyote ya “fadhila za kidunia” huko mbeleni, ambazo zingemfanya ashindwe kuwa mwaminifu kwa Mungu. Alitaka kufuata maagizo ya Biblia. Bila shaka Danieli alikuwa akifahamu kitabu cha Yoshua na utume husika ambao Mungu alimpatia Yoshua! (Dondoo ndogo: chunguza Yoshua 1:7-9 na kuikariri moyoni!) toleo fupi:

Fungu la 7: Daima lifuate Neno la Mungu. Usikengeuke kulia wala kushoto, NDIPO utapata mafanikio!

Fungu la 8: Daima jishughulishe na Neno la Mungu na kutenda kulingana na kile kilichoandikwa, HAPO NDIPO utapata mafanikio!

Fungu la 9: Kuwa jasiri na hodari! Usiogope chochote! KWA KUWA Mungu yu pamoja nawe kila uendako. Yeye anachukua wajibu. Anatupatia nguvu, furaha na mafanikio.

Uamuzi wa kwanza tayari ulionesha wazi kwamba Danieli aliishi katika hali ya kujisalimisha kikamilifu kwa Mungu. **Hiki ndicho kipengele cha msingi kwa ajili ya mafanikio yanayoshabihiana na mapenzi ya Mungu: Daima fanya maamuzi kama ambavyo Mungu, katika upendo Wake, anataka na wala siyo nitakavyo au kama mamlaka fulani yapendekezavyo au yanavyoamuru.**

**Je maamuzi ni muhimu kiasi gani maishani?** Uwezo wa kufanya maamuzi mazuri huongoza maisha yetu yote. Meli ya kifahari ya abiri iitwayo “Queen Elizabeth” ilikuwa na uzito mara 1,300 ya usukani wake, iliyokuwa ikiendesha meli hiyo kubwa sana. Usukani kama huo hushabihiana na uwezo wetu wa kufanya maamuzi. Maamuzi yanaweza kuwa mguso mkubwa. Tunapoamua kufanya mapenzi ya Mungu na kuchukua hatua stahiki, basi Yeye atatupatia msaada unaohitajika. Halafu anaambatana nasi. Ndipo tunapata uzoefu wa kimbingu na wa kibinadamu pamoja kama timu, ambapo Mungu anabeba wajibu husika. (Kwa maelezo zaidi angalia katika kitabu cha Kaeni Ndani ya Yesu, sura ya “Utii Kupitia Yesu”.)

Danieli na marafiki zake walifanya uamuzi yanayoshabihi mapenzi ya Mungu. Je hatua gani walizochukua baada ya hapo?

walifanya walichoweza, Naye Mungu akaleta ufumbuzi wa tatizo lao.

## Tunawezaje kushughulikia vema maamuzi magumu?

Danieli 1 Fungu la 8 b: "…basi [Danieli] akamwomba yule mkuu wa matowashi ampe ruhusa asijitie unajisi." Walitumia mbinu gani? Mbinu ya kuomba. Mambo huwa tofauti kabisa tunapowasilisha matatizo yetu kama maombi badala ya kusema: "Sitafanya hilo!" au "Sitaki hilo!" au "Hilo halina mjadala!" Ombi huonesha imani. Tunapowasilisha ombi fulani, uwezekano ni mkubwa kwamba mtu anayelengwa atajaribu kutusaidia. Lakini tukidai au kuonesha kukataa katika kauli zisizo za kiungwana, basi mtu husika ataitikia kwa namna hasi. Atakuwa na mwelekeo wa kuonesha nani mwenye kauli ya mwisho. Nilijifunza mtazamo huu muhimu kwenye kambi la vijana na kamwe sikuusahau. Nimetanda kwa kuzingatia hilo maisha yangu yote, kwa sababu hii ni njia bora na sahihi. Imehimili kipimo cha wakati.

Vilevile Danieli aliongeza kitu fulani: Alisisitiza kwamba tatizo hili lilikuwa suala la dhamiri kwake. Tunapofikiri kwa jinsi hii, mara nyingi tutazingatiwa kwa namna ya uelewa zaidi. Lakini kamwe hatupaswi katika mazingira yoyote kutenda kinyume na dhamiri yetu. Kwa namna hii tu ndipo tunaweza kuwa na amani ya ndani pamoja na Mungu.

Fungu la 9: "*Basi **Mungu alimjalia*** Danieli kupata kibali na huruma machoni pa huyo mkuu wa matowashi." (NKJV) Nini kilitokea hapa? Danieli alifanya uamuzi wa kumtii Mungu. Kwa namna hii, alikuwa amefanya kila kitu alichoweza – alifikiria kwa makini na kutenda kwa uungwana mkubwa. Ndipo Mungu aliingilia kati ya kuugusa moyo wa mkuu huyu. Mungu **ndiye alifanikisha hilo.** (Mara nyingi, Mungu wetu wa pekee ajabu huwa anaingilia kati ili kutufadhili. Lakini pia anaweza kuamua vingine. Pengine hatujakidhi masharti yote au pengine ana mtazamo bora zaidi kwa nini asifanye hivyo.)

Kwa mujibu wa fungu la 10 afisa mkuu alikuwa na hofu sana. Kama angetimiza ombi la Danieli, basi angekuwa akitenda kinyume cha agizo bayana la mfalme.

Tunaona hatua ya Danieli inayofuata katika Fungu la 12. Anamgeukia mfawidhi, ambaye binafsi alikuwa akimsimamia Danieli na marafiki zake. Danieli anaendelea na mbinu yake ya kuomba. Pamoja na hilo, anabainisha pendekezo mahususi – alipata muda wa kulifikiria hili. Alimwambia mfawidhi kwa upole na kwa urafiki mkubwa: Jaribu hili juu yetu kwa siku kumi. Kwa ombi hili, kwa mara nyingine tena anaonesha imani yake kwa mkuu wake. Jambo moja ni bayana: Danieli alikuwa hapangi kula chakula najisi baada ya siku kumi! Kinyume chake, alitegemea kabisa Mungu aingilie kati kama alivyokuwa ameomba: *"Tafadhali utujaribu sisi watumishi wako muda wa siku kumi; na watupe mtama* [kihalisia, vyakula vya mbegu] tule, na maji tunywe." [1]

Kwa nini Danieli aliomba "vyakula vya mbegu"? Ni wapi istilahi hii inakopatikana? Inasema katika Mwanzo 1:29: "Mungu akasema, Tazama, nimewapa kila mche utoao mbegu, ulio juu ya uso wa nchi yote pia, na kila mti, ambao matunda yake yana mbegu; vitakuwa ndivyo chakula chenu." Hiyo ni sawa, Danieli alikuwa akilifahamu vema neno la Mungu. Aliomba chakula bora ambacho Mungu alikuwa amekikusudia kwa wanadamu wakati wa uumbaji: vyakula vya mimea. Pia kina manufaa ya kutokuwa aghali. Mungu **alikumbushia hili** kiasi kwamba mfawidhi huyu alisikia na kuridhia ombi lake. Kisha tena Mungu akafanya jambo fulani la pekee ajabu:

Fungu la 15 "Hata mwisho wa zile siku kumi nyuso zao zilikuwa nzuri zaidi, na miili yao ilikuwa imenenepa zaidi, kuliko wale vijana wote waliokula chakula cha mfalme." Matokeo yake, tatizo husika lilisuluhishwa. Je Mungu aliwapatia nini? **Mwonekano mzuri, nguvu na uwezo mkubwa wa akilini. Mungu alifanikisha hilo!**

Lakini Mungu aliendelea kuwakirimia: Fungu la 17 – *"Basi, kwa habari za hao vijana wanne, Mungu* ***aliwapa*** *maarifa na ujuzi katika elimu na hekima; Danieli naye alikuwa na ufahamu katika maono yote, na ndoto."* Nini kingine alichowapatia Mungu? **Maarifa na ujuzi,** na kwa nyongeza Danieli alipata **karama ya kinabii. Mungu alitoa!**

1 William H. Shea, Das Buch Daniel, Teil 1 (Advent-Verlag Lüneburg, 1998), S. 52

Lakini haikuishia hapo. Ilikuwepo tunu nyingine mwishoni mwa mafunzo yao. Tunasoma katika fungu la 20: *"Na katika kila jambo la hekima na ufahamu alilowauliza mfalme, akawaona kuwa walifaa mara kumi zaidi ya waganga na wachawi waliokuwa katika ufalme wake."* Je unaweza kuzidisha uwezo wa akili yako mara tano au kumi? Ni pekee aliyewakirimia hili. Mungu **anatoa.**

Njia hii huonesha jinsi gani unavyoweza kuishi maisha yenye mafanikio hasa: Kama kitu fulani kinakinzana na mapenzi ya Mungu, basi fanya uamuzi **kwa ajili ya** mapenzi ya Mungu! Kisha tafakari na kutumia njia ya kuomba. Kuwa muungwana na rafiki. Kama inawezekana au kama ni lazima, pendekeza ufumbuzi wa busara unaoshabihi mapenzi ya Mungu. Ndipo Mungu anakuwa pamoja nasi. Yesu alisema katika Mathayo 6:33, NIV: *"Bali utafuteni kwanza ufalme Wake na haki Yake, ndipo vilevile* ***mtapewa*** *haya mengine yote."*

Pengine bado hujajisalimisha kikamilifu kwa Kristo. Au kwa wakati huu umetanga mbali na kuupoteza "upendo wa kwanza" (Ufunuo 2:4). Tunapokuwa katika hali hii, basi huwa tuna mtazamo tofauti kabisa na tunaona mambo mengi kwa namna tofauti. Ni huoneka kuwa "kawaida" kwetu. Warumi 8:5, GNT: *"Wale waishio kama ambavyo asili yao ya kibinadamu inawaambia kufanya, nia zao zinatazaliwa na kila ambacho asili ya kibinadamu inataka.* ***Wale waishio kama ambavyo Roho anawaambia kufanya,*** *nia zao zinatazaliwa na kila ambacho Roho anataka."* Andiko hili hutuonesha mitazamo miwili tofauti ya msingi kutegemeana na endapo tumejazwa Roho Mtakatifu au la. Nilipokuwa sijajisalimisha kikamilifu kwa Kristo, mara kadhaa niligundua kuwa ni jambo gumu na zito sana kuishi kama Mkristo. Lakini sasa maisha yangu yamejawa furaha, uhakikisho, nguvu na ushindi. E.G. White alisema: "Siri ya mafanikio ni muunganiko wa nguvu ya kiungu na juhudi ya kibinadamu." *(Patriarchs and Prophets, uk. 509.1)* Hii ndiyo sababu tunataka kutafakari maswali ya msingi katika kitabu hiki, ambayo, kupitia uhusiano wa karibu pamoja na Kristo, yatatuongoza kwenye mafanikio au

katika lugha ya Biblia, maisha yenye matunda – maisha kama mshirika wa Mungu aliyejazwa Roho na aongozwaye na Roho.

UTANGULIZI

# Washirika wa Yesu Waliojawa Roho

*Jinsi gani unakuwa mmojawapo?*

" Hutafanikisha kile ukusudiacho kufanya, si kwa uwezo wa kibinadamu
wala nguvu za jeshi:
Hapana, Roho Wangu atalifanya hilo!
Naahidi, Bwana Mungu Mwenyezi."

Zekaria 4:6 imefasiriwa kutoka kwenye sanifi ya Kijerumani, Hoffnung für alle

Kazi ya Mungu hapa duniani haitamalizika kupitia kwetu kwa nguvu zetu wenyewe na kwa uwezo wetu wenyewe, hata viwe na thamani jinsi gani. **Mungu Mwenyewe ndiye anayepaswa na ndiye atakayeikamilisha kazi ya injili.** Atalifanya hilo kupitia **washirika waliojazwa roho wa Yesu;** kupitia wanaume, wanawake, wazee, vijana na watoto, walijazwa Roho Mtakatifu. Kupitia watu waishio katika hali ya kujisalimisha kikamilifu kwa Kristo na huduma Yake.

Tunapaswa kujiuliza maswali ambayo huamua kila kitu: Je namfanyia Mungu kazi kwa uwezo wangu wa kibinadamu? Au Mungu anaweza

## Uzoefu Madhubuti (zaidi katika sura ya 3)

Wanafunzi wa Teolojia kutoka katika huduma yetu ya kichungaji huko Bogenhofen, Austria walialikwa kuendesha mfululizo wa mkutano wa injili barani Afrika. Miongoni mwa wengine, Zsolt Halmi alijitolea kwa ajili ya mkutano huu. Mnamo mwaka 2006 alikuwa katika mwaka wake wa pili wa masomo. Hapo kabla alikuwa ameendelea mfululizo wa mkutano wa injili huko Romania. Yeye pamoja na wanafunzi

wengine walipangia kwenda Kisumu, Kenya katika Afrika Mashariki.

Zsolt alitegemea Mungu atende mambo ya pekee ajabu huko, kwa vile alikuwa amesikia mambo makuu kuhusu shauku ya watu barani Afrika. Alitegemea maelfu ya wahudhuriaji. Alipaswa kuhubiri kwenye eneo la soko. Jukwaa lilikuwa limejengewa hapo. Kwanza walionesha filamu ya Yesu, kisha hubiri likafuatia. Lakini wageni 30 tu wakaja. Ilikuwa kama kuoga maji baridi kwa Zsolt. Watu 20 wakaja siku ya pili jioni na 10 tu wakati siku ya tatu jioni. Hali iliendelea hivi juma zima. Alivunjika moyo, na hali haikuimarika. Alimimina fadhaa yake mbele ya Mungu. Alimuuliza: "Kwa nini umenileta hapa?" Alijisalimisha kwa Mungu kwa nafsi yake yote. Alihisi alikuwa ameimarisha uhusiano wake pamoja na Mungu kupitia maombi haya. Vilevile, Mungu alikuwa amempatia ahadi kutokana na ombi lake: "Utamtukuza Bwana." Alitambua kwamba Mungu alikuwa amemsikia. Hata hivyo, bado alikuwa amekabiliwa na hofu na mashaka. Lakini jioni hiyo watu 600 wakaja. Sasa alijua: Mungu hakuwa amemwacha. Kisha watu 700 wakahudhuria, kisha idadi ikapanda hadi 1,000 na mwishowe kwa neema ya Mungu wakabatizwa watu 39.

Je unaweza kuona tofauti mahususi kati ya kumfanyia Mungu kazi kwa uwezo wetu na Mungu kufanya kazi kupitia sisi kwa upendo na uwezo Wake wa kiungu? Huu ni mfano pekee zaidi. Lakini natumaini kwamba tunaweza kuona bayana hatua ya mageuzi. Nini kilibadilika? Mtu yuleyule alihutubu, kwa elimu ileile, na kwa ujumbe uleule, kwa mawazo yaleyale, kwa mbingu ileile na mahali palepale. Nini kilibadilika? Hakuna chochote kabisa isipokuwa kiwango cha uhusiano wake pamoja na Mungu. Alikuwa amejisalimisha kikamilifu kwa Mungu. Kujisalimisha kwetu kikamilifu ndicho kigezo cha Mungu. Na ndilo hili tu, hakuna lingine. Bwana wetu wa pekee ajabu anataka kuunganika nasi pamoja na upendo Wake wote na stamani Zake zote za kiungu. – Tutazingatia suala hili kwa kina zaidi katika sura ya 3.

## Mito ya Maji Hai – Matendo Makuu

Yesu alisema: *"Aniaminiye Mimi, kama vile Maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake.* ***Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho…****"* (Yohana 7:38-39)

*"Amin, amin, nawaambieni,* ***Yeye aniaminiye Mimi,*** *kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya,* ***kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba.****"* (Yohana 14:12)

Kwa nini mito ya maji ya uhai yatabubujika kutoka kwa wanafunzi Wake? Kwa nini wanafunzi nao wataifanya kazi aifanyayo Yeye na hata matendo makuu zaidi? Yesu anabainisha sababu: "…kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba." Nini kilichotokea alipoenda kwa Baba Yake?

1. Yesu alisimikwa upya katika mamlaka na utukufu. *"Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani."* (Mathayo 28:18)

2. Kama ishara ya kusimikwa kwenye mamlaka, Yesu aliwapatia wanafunzi Wake tunu Yake kuu zaidi: Alimtuma Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu ni karama bora kabisa kutoka kwa Yesu. Hilo humaanisha: Yesu Mwenyewe ndiye anapaswa kufanya na ndiye atakayefanya kazi kubwa zaidi na kububujikia mito ya maji ya uhai – kupitia wanafunzi waliojazwa Roho Mtakatifu.

Kumfanyia Mungu kazi kwa nguvu zetu wenyewe huleta matokeo ya kibinadamu tu. Na mashaka endapo hayo huweza kuja kutosheleza. Lakini katika wakati na zama zetu ambapo watu wengi wamekuwa wagumu kumsikiliza Mungu, ni hakika hayatoshelezi kabisa.

**Kazi ya Mungu itatimizwa na Mungu Mwenyewe, Yeye Mwenyewe akitenda kazi kupitia wale ambao wamejisali-misha kikamilifu KWAKE.** Hii huleta matokeo ya kiungu. Kwa mfano, Yesu, Paulo, Danieli, Nehemia, Esta na wengineo.

## Maneno ya Msingi ya Yesu kwa wanafunzi Wake

***"Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe."*** (Marko 16:15) Hili linaweza kufanyikaje?

***"Nifuateni, Nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu."*** (Mathayo 4:19) Tunapomfuata Yesu katika mambo yote, ndipo anatufanya tuwe wavuvi wa watu. Hakuna bingwa mwenye mafanikio zaidi kuliko yeye. Tutaangalia kwa ukaribu jinsi anavyotufanya tuwe wavuvi wa watu katika sura ya 5.

Nini ambacho Yesu aliwaambia baadaye? Je walipaswa kuanza mara moja baada ya kupaa Kwake?

*"...**aliwaagiza** wasitoke Yerusalemu, bali **waingoje Ahadi ya Baba,…. mtabatizwa katika Roho Mtakatifu.** ..."* (Matendo 1:4-5)

Je yapi maneno ya mwisho ya Yesu wakati akiwa duniani?

*"Lakini mtapokea nguvu **[uwezeshwaji, uimarishwaji], akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu;** nanyi mtakuwa mashahidi Wangu… hata mwisho wa nchi."* (Matendo 1:8)

Je yapi Yake maneno ya mwisho kutoka mbinguni kwenda kwa kanisa Lake la mwisho?

*"Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa." (*Ufunuo 3:22)

Taanani ya Yesu hapa inatambulika bayana: Katika mazingira yote, tunamhitaji Roho Mtakatifu.

**… ndipo ule mwisho utakapokuja**

Mataifa yote yatakapokuwa yamefikiwa, ndipo Yesu atakuja tena: *"Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja."* (Mathayo 24:14)

Injili imeenezwa kwa  hali kubwa ya kujiweka wakfu – na hii imefanikiwa. Lakini lengo kamilifu **haliwezi** kufikiwa kwa uwezo wa kibinadamu!

Vyombo vya kisasa vimetusaidia katika nyakati za hivi karibuni. Je kazi itakamilishwa kwa njia hii? Kinachosta-ajabisha hasa, teknolojia ya mawasiliano ilianza na Samuel Morse mnamo mwaka 1844. Hivi tunaweza kuona ushahiri wa mwaka husika kwamba teknolojia itachangia? Hakika! Lakini, hatupaswi kusahau kwamba Bwana pekee ndiye huifanya Biblia iwe hai kwa wasikilizaji wakati ule maneno yanapozungumzwa na wanafunzi

waliowekwa kwafu kwa Mungu na waliojazwa Roho Mtakatifu.

Nini kinachopaswa kutokea ili lengo lifikiwe na ulimwengu wote usikie na kuielewa injili? Hebu tusome maneno ya Mungu makini na bayana katika Zekaria 4:6:

*“Hutafanikisha kile ukusudiacho kufanya, si kwa uwezo wa kibinadamu wala nguvu za jeshi:* ***Hapana, Roho Wangu atalifanya hilo!*** *Naahidi, Bwana Mungu Mwenyezi.”* (imefasiriwa kutoka kwenye sanifi ya Kijerumani ya *Tumaini kwa Wote)*

Jambo hili limekuwa kweli wakati wote. Na hata bado lingali muhimu zaidi leo. Mwishoni mwa ulimwengu, hali kama ile ya wakati wa Nuhu itaenea (Mathayo 24:37-39). Je tatizo kuu la wanadamu wakati huo lilikuwa lipi? Uovu! (Mwanzo 6:5-6) Kwa vile maovu ya mwanadamu – ambayo yamefichika na kufungashwa vizuri – yameongezeka sana, tunahitaji uwezeshwaji kutoka kwa Mungu katika nyakati hizi kwa haraka zaidi kuliko kipindi chochote kilichopita.

## Je nguvu na uwezo vinatoka wapi?

Yesu alisema: “*Lakini mtapokea* ***nguvu*** *[uwezeshwaji, uimarishwaji],* ***akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu;*** *nanyi mtakuwa* ***mashahidi Wangu****…”* (Matendo 1:8) Yesu anarejelea nguvu turufushani – nguvu ya Mungu.

Hebu tuilinganishe na nguvu ya umeme. Tukiwa na nguvu hii, tunaweza kuangaza, kupasha yote, kupooza, na kuendesha mota na vifaa vingine, mathalani kompyuta, mtandao, redio, TV, simu, treni, magari ya umeme na mengine mengi. Hata pale mbegu ardhini zinapoota, umeme unahusika. Nishati ni msingi wa kila kitu. Kila kitu hufanyika kupitia nguvu ya umeme.

Hivyo, msingi wa maisha na huduma yetu ni Kristo ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu na matokeo husika ya Mungu. Ni kwa njia hii pekee ndipo tunaweza kuwa mashahidi wa Mungu – kupitia maneno na matendo yetu. Roho Mtakatifu pamoja na Kristo ndani yetu ni vigezo vya msingi ili Yesu awafikie watu kupitia kwetu. Katika wakati wetu wa mafunzo pamoja na Yesu, tutakuwa wajumbe wake wa furaha kupitia uongozi na maelekezo Yake na kujazwa nguvu ya kiungu ya Mungu.

## Nini alichobainisha Yesu waziwazi katika hotuba mausia Yake ya maagano?

**Roho Mtakatifu humwakilisha Yesu**

*"Lakini Mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa ninyi Mimi niondoke, kwa maana Mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali Mimi nikienda Zangu, nitampeleka kwenu."* (Yohana 16:7)

Hii huumaanisha: **Yesu aliondoka. Roho Mtakatifu katika nafasi Yake. Amekuwepo hapa tangu wakati huo.**

Roho Mtakatifu humwakilisha Yesu hapa duniani. Yesu alielezea kwamba ufumbuzi huu ni bora kwetu, kuliko kama engebaki Yeye binafsi.

**Yesu anaishi ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu**

*"Nami nitamwomba Baba, Naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele; ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, Naye atakuwa ndani yenu. Sitawaacha ninyi yatima; naja kwenu."* (Yohana 14:16-18)

Kwa maneno mengine: **Roho Mtakatifu huleta uwepo wa Yesu maishani mwetu** (Waefeso 3:16-17). Yesu anaweza kuishi ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu – licha ya mahali tulipo.

**Roho Mtakatifu ni mwalimu wetu**

*"Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina Langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia."* (Yohana 14:26)

Maana yake: **Roho Mtakatifu hutufundisha ukweli wa Yesu.** Tunamhitaji Roho Mtakatifu ili tuweze kuujua ukweli na kuupambanua dhidi ya upotofu na vishawishi.

**Kupitia Roho Mtakatifu Yesu anashuhudia juu ya nafsi Yake ndani yangu na kupitia kwangu**

*"Lakini ajapo huyo Msaidizi, nitakayewapelekea kutoka kwa Baba, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba, Yeye atanishuhudia."* (Yohana 15:26)

Kwa maneno mengine:

**Yesu anaishuhudia nafsi Yake maishani mwetu kupitia Roho Mtakatifu. Na: Roho Mtakatifu huwapatia wengine ushuhuda wa Yesu kupitia kwetu.**

Roho Mtakatifu huimarisha uhusiano wangu pamoja Naye na kuufanya uwe urafiki wa kina.

## Roho Mtakatifu humtukuza Yesu

*"Yeye* [Roho Mtakatifu] *atanitukuza Mimi, kwa kuwa atatwaa katika yaliyo Yangu na kuwapasha habari."* (Yohana 16:14)

Yaani, Roho Mtakatifu hudhihirisha ukuu na utukufu wa Kristo aliyefufuka na kufunua siri za mpango wa wokovu. Hivyo, kupitia Roho Mtakatifu aongozaye atua kwa hatua, Yesu huwa mkuu zaidi maishani mwangu; atakuwa karibu zaidi, mpendwa zaidi, wa thamani zaidi, wa maana zaidi: Yesu atakuwa kila kitu kwangu.

## Matokeo yangu, matokeo yake ya thamani ni yapi?

*"Mimi nalikuja ili wawe na **uzima**, kisha wawe nao **tele**."* (Yohana 10:10)

"*...**Mtu akiona kiu, na aje Kwangu anywe.** Aniaminiye Mimi, kama vile Maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake. Na **neno hilo alilisema katika habari ya Roho,** ambaye wale wamwaminio watampokea. ...*'" (Yohana 7:37-39)

Je unataka fanaka nyingi zaidi maishani – maisha tilimifu? Kila mmoja ana shauku ya kupata hili, kwa sababu Mungu wetu wa rehema *"ameiweka hiyo milele ndani ya mioyo yao"* (Mhubiri 3:11). Unapokuwa na shauku ya jambo hili, ndipo Yesu atakuonesha njia. Anataka tuwe na maisha timilifu hapa na sasa. Baada ya ujio Wake wa pili, tunaweza kuendeleza maisha haya katika nyanja tofauti kabisa katika ufalme wa Mungu wa milele. Yesu anapoishi ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu, ndipo tutapata uzoefu maridhawa maisha (Yohana 10:10; Waefeso 3:19; Wakolosai 2:9-10).

Kwa maneno mengine: **Yesu maisha tele kupitia Roho Mtakatifu.** Je Bwana wetu wa fadhili anaweza kutupatia hata mengi zaidi? Siyo tu kwamba Roho Mtakatifu ni tunu kuu kabisa kwa ajili ya wanafunzi Wake, ambayo huleta tunu zingine zote, bali pia Roho Mtakatifu Mwenyewe ni mpaji wa tunu mbalimbali. Sitaki tena kuishi bila uhusiano huu wa kina! Je unautaka vilevile?

## Yesu alitendaje kazi?

"Asubuhi baada ya asubuhi aliwasiliana na Baba Yake aliye mbinguni, **akipokea kutoka Kwake ubatizo mpya (ujazo) wa Roho Mtakatifu kila siku**." (E.G. White, *Signs of the Times,* November 21, 1895, par. 3)

Kwanza kabisa, Yesu alitafuta uwepo wa Baba kisha akaenda Zake akiwa amejazwa Roho Mtakatifu na akiwa chini ya uongozi Wake kwa watu.

***"Njia ya Kristo pekee ndiyo italeta ufanisi wa kweli katika kuwafikia watu. Mwokozi alichangamana na watu kama yule mwenye shauku ya ustawi wao. Aliwaonesha huruma Yake, akahudumia mahitaji yao, na akakubalika katika(kuisahabu) imani yao. Kisha akawaalika, "Nifuateni." kwa juhudi binafsi kuna haja ya kuwa karibu na watu (E.G. White, The Ministry of Healing, uk.143***

Yesu alikuwa amejawa nguvu ya Mungu kupitia Roho Mtakatifu, Naye alifanya kadiri alivyoweza chini ya uongozi wa Roho ili kuwasaidia watu katika fadhaa zao binafsi. Kwa namna hii, aliteka imani yao na mwaliko Wake wa kumfuata ulitua kwenye ardhi iliyoandaliwa vizuri.

Hebu Mungu wetu wa pekee ajabu atusaidie tuwe washirika wa Yesu wenye kupenda, wafanisi, na tuliojazwa Roho na tuendelee kukua katika haya.

Jinsi gani kuomba kwa ajili ya utimizwaji wa Roho Mtakatifu, ili kuwa na hakika kwamba umepokea, hufafanuliwa kwa kina na katika *Hatua za Uamsho Binafsi*– tazama uk. 205

## Mawazo binafsi na mwongozo wa mjadala

1. *Nini matokeo ya mikakati ya injili inayofanywa kwa nguvu zako binafsi?*

   ______________________________________________

2. *Kwa nini wanafunzi walitakiwa kungoja wakiwa Yerusalemu baada ya Yesu kupaa mbinguni? Walifanya nini kwa muda huu?*

   ______________________________________________

   ______________________________________________

3. *Nini ambacho Roho Mtakatifu hufanikisha ndani yetu kwa ajili ya wanadamu wenzetu?*

   ______________________________________________

   ______________________________________________

4. *Nini matokeo pale wanadamu wanapojazwa Roho Mtakatifu?*

   ______________________________________________

## Muda Wetu wa Maombi

- Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.
- Sali pamoja na mwanamaombi mwenzio…

  1. … kwamba Mungu aweze kutuonesha eneo ambapo tungali tunajaribu kumfanyia kazi kwa nguvu zetu wenyewe.
  2. … kwa ajili ya subira na uvumilivu katika kumruhusu Mungu akuandae kuwa wakala Wake.
  3. … kwamba tuweze kujifunza kuendelea zaidi kumjua na kumpenda Yesu.
  4. … kwa ajili ya moyo ulio tayari kuomba na kumpokea Roho Mtakatifu.

Siku ya 3

SURA YA 1

# Mungu Anakupenda!

Nawezaje kudhahimu utimilifu wa upendo wa Mungu?
Je tumaini langu kwa Mungu hufanya kazi gani?

## Ufunuo Usio Kifani: UPENDO WA MUNGU

Tunajuaje kwamba hakika Mungu ni upendo, kwamba tabia Yake ni upendo? Mungu alitudhihirishia hili kwa namna ya pekee – kupitia maisha na mauti ya Mwanawe Yesu Kristo, aliyesema: *"... **Aliyeniona Mimi amemwona Baba. …** Husadiki ya kwamba Mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani Yangu? Hayo maneno niwaambiayo Mimi siyasemi kwa shauri Langu; lakini Baba akaaye ndani Yangu huzifanya kazi Zake."* (Yohana 14:9-10)

Hivyo, Mungu ni kama Yesu.

Biblia hutuambia yafuatayo kuhusu Yesu, alipoishi hapa duniani: alikuwa akitumainika, kwa sababu kwa furaha akina mama walimletea watoto wao; japo alikuwa maskini, aligawana kila kitu pamoja na wengine; aliwaponya wagonjwa; hakuweka tofauti yoyote baina ya watu; aliwatia moyo waliokata tamaa; daima alitumia fursa husika, pale mtu fulani alipohitaji msaada Wake – hata wakati wa usiku watu walimjia, Naye alimsaidia yeyote aliyekuwa na shauku ya kuupata uzima wa milele. Kwa ajili ya kusudi hili, alilazimika kukabili mauti kama mbadala wa kila mdhambi atubuye.

Biblia inasema:

*"**Hakuna** aliye na **upendo mwingi** kuliko huu, wa mtu **kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake.**"* (Yohana 15:13)

Kwa kweli, Yesu alifanya kitu fulani hata kikubwa zaidi! **Alikufa** kwa ajili yetu **tulipokuwa** tungali **maadui Zake:** "... *alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi."* (Warumi 5:8)

Alistahimili dharau na mateso makali ya kimwili kwa ajili yangu na wewe. Kwa nini alikufa mapema zaidi kuliko wale waliosulubiwa pamoja Naye? Alikufa mapema zaidi kwa sababu ya mzigo wa dhambi, kwa sababu ya dhambi zangu na zako. Ni jambo la kustaajabisha tu kiasi gani kuhusu upendo wa kafara, usio na ubinafsi na wa pekee aliouonesha na angali akiuonesha kwetu!

## Upendo wa Mungu Usio Kifani

Kitu cha pekee kuhusu Mungu ni kwamba **siyo tu kwamba ana upendo, bali Yeye Mwenyewe ni upendo.** Nini tofauti kati ya kuwa na kitu fulani na kuwa kitu hicho? Kitu fulani nilicho nacho, kinaweza kupotea au kisiwepo. Kitu fulani kilicho nafsi yangu, wakati wote kipo kwangu. Kwa vile **Mungu** ni upendo, **anaweza tu kutekeleza matendo ya upendo, hata pale yanapokuwa hayaonekani kuwa hivyo kwa wakati huo.** Ipo tofauti kubwa sana – ikilinganishwa na fikra na matendo yetu – kati yetu wadhambi, tunaokosea, na Mungu wetu mwenye uwezo wote, ajuaye yote na Mwenevu!

**Upendo wa Mungu** (Kiyunani: agape) **ni aina ya upendo makini na wa kina zaidi.** Upendo huu una msingi wake katika tabia ya Mungu. Haukujengwa kwenye dhana kwamba mpokeaji wa upendo huu anastahili (mfano: upendo wa baba kwa mwana-mpotevu).

Tunagundua jinsi upendo huu unavyojidhihirisha wenyewe kwa kina katika 1 Wakorintho 13:4-7 NIV. *"Upendo ni mvumilivu, upendo ni mfadhili. Hauhusudu, hautakabari, wala haujivuni. Hauwafedheheshi wengine, haujitafutii ubinafsi, haukasirishwi kirahisi, hauhifadhi kumbukumbu ya mabaya. Upendo hautaanisi katika uovu bali hufurahi pamoja na kweli. Hulinda daima, hudhamani daima, hutumaini daima, hustahimili daima."*

Na kwa vile Mungu ni wa milele, **upendo huu faridi nao ni wa milele!**

## Uwezo wa Mwanadamu Kupenda Ulidhoofishwa na Dhambi

Dhambi imeharibu sura ya Mungu ndani ya wanadamu na hivyo pia kuathiri vibaya uwezo wao wa kupenda. Kadiri mtu

anavyoishi mbali zaidi na Mungu ndivyo alivyo na uwezekano mdogo zaidi kupenda na ndivyo asili yake ubinafsi inavyojidhihirisha zaidi.

Mtu fulani aliwahi kuuelezea upendo wa mwanadamu hivi: Nakupenda ili nawe unipende vivyo hivyo. Hii huonekana kuwa kweli kwa wahusika mbali mbali leo. Mtoto mdogo haraka sana hutambua kadiri anavyokuwa mwema mara nyingi kwa Bibi, ndivyo mara nyingi anavyopata pipi!

Wanadamu wenye dhambi wana uwezo tu kwa ajili ya upendo usio kamilifu. Inastaajabisha kiasi gani kwamba Mungu anataka kuweka upendo Wake mkamilifu mioyoni mwetu!

## Wema wa Mungu ni Upendo Wake katika Matendo

Ni bayana, kamwe Yohana hakuwa na tatizo la kutilia mashaka upendo mkamilifu wa Mungu– ila kinyume chake. Alipata uzoefu wa maisha na mauti ya Yesu. Ndiyo maana aliandika: ***"Nasi tumelifahamu pendo alilo nalo Mungu kwetu sisi, na kuliamini. …"*** (1 Yohana 4:16)

Tabia ya Mungu ni upendo. Asili Yake ni upendo. Upendo Wake huamua matendo Yake yote. Ndiyo maana sheria Zake zote zimetokana na nguvu ya upendo. Mungu amehakikisha utimilifu wa upendo Wake – baraka hii isiyoelezeka – inakuwepo kwa viumbe Wake wote. Anataka kuonesha wema Wake kwa kila mmoja; **wema Wake, ambao ni upendo katika matendo.** Wema wa Mungu ni matendo Yake yenye fanaka, ambayo huamuliwa kwa upendo. Neno wema hudokezea: kuwa mwema, utayari wa kusaidia, urafiki na huruma. Kwa kuiweka kwa namna nyingine: wema wa Mungu ni kutoa, kukasimisha na kutekeleza matendo ya upendo.

## Maisha katikati ya Upendo wa Mungu

Baba mmoja alifanya safari baharini akiwa pamoja na mwanawe na alitaka kumwelezea upendo wa Mungu. Alimwambia mwanawe: "Angalia umbali kadiri uwezao juu ya guberi ya meli hii halafu juu ya shetri—hivyo ndivyo ulivyo urefu wa upendo wa Mungu. Na sasa angalia umbali kadiri

uwezao kushoto na kisha kulia. Hivyo ndivyo ulivyo upana wa upendo wa Mungu. Sasa angalia juu ya anga lisilo na ukomo—hivyo ndivyo kilivyo kimo cha upendo wa Mungu. Tazama chini kwenye vina vya bahari—hivyo ndivyo kilivyo kina cha upendo wa Mungu." Baada ya muda kitambo, mvulana huyo akasema kwa furaha: "Baba, hivi unajua sehemu bora kabisa ya jambo hili ni nini? Tuko katikati." – Hebu tutafakari hilo kwenye maisha yetu ya kiroho na kujiuliza: Lini tunakuwa katikati ya upendo wa Mungu? Kwa maneno mengine:

## Jinsi gani tunaweza kupata uzoefu mtimilifu wa upendo wa Mungu au wema Wake?

Mtume Paulo alilijua jibu husika. Tafadhali zingatia hatua tatu alizotuonesha:

1. Uwezo kupitia Roho Wake
2. Kristo anakaa ndani yetu kupitia imani
3. Kuimarishwa katika upendo Wake

Matokeo:

Unaweza kutambua kiwango cha upendo Wake.

*"Naomba kwamba kutokana na utajiri Wake mtukufu, aweze kuwaimarisha kwa kuwajalia nguvu katika utu wenu wa ndani* ***kupitia Roho Wake****, ili* ***Kristo aweze kukaa mioyoni mwenu kwa imani****. Nami naomba kwamba ninyi, ilhali mmekita mizizi na kuthibitishwa katika upendo, mweze kupata nguvu, pamoja na watu wote watakatifu wa Bwana,* ***ili kutambua jinsi gani upendo wa Kristo ulivyo mpana na mrefu na wenye kimo na kina****."* (Waefeso 3:16–18 NIV)

Sisi binafsi tunaweza kupata uzoefu mtimilifu wa upendo wa Mungu na wema Wake, pale Kristo anapoishi mioyoni mwetu kwa imani kupitia Roho Mtakatifu, pale tunapokuwa na uhusiano binafsi pamoja Naye. Na kadiri uhusiano huu kwa Yesu ulivyo wa karibu zaidi, ndivyo mtu husika anavyokuwa zaidi katika kujisalimisha kwake kwa Yesu, ndivyo watakavyopata uzoefu zaidi na utimilifu wa upendo wa Mungu!

Kuhusiana na upendo wa Mungu, mara nyingi nimeomba: "Baba, tafadhali hebu nitambue kwa namna bora zaidi upendo

Wako, tabia Yako na asili Yako ya neema." Kwa (taanisi) kufurahishwa kwangu, nimegundua kwamba Mungu amenipa tena na tena mawazo mapya kuhusu upendo Wake, na pia katika jambo hili amenipatia uzoefu mpya. Na uhusiano wangu pamoja Naye umekuwa wa kirafiki (kisahibu) zaidi. Mara nyingi huwa hatutambua upendo na wema wa kustaajabisha, ambao kwao Baba yetu wa mbinguni hutufuata na kutuzunguka.

Anasema kwangu na kwako: *"Naam nimekupenda kwa upendo wa milele,* ***ndiyo maana nimekuvuta kwa fadhili Zangu.****"* (Yeremia 31:3)

Pengine umebaini vipengele tofauti kabisa vya upendo wa Mungu kuliko nilivyofanya mimi; lakini jambo moja ni hakika: Tunashughulika na mada hapa tutakayojihusisha nayo milele!

## Hivi ni muhimu kuelewa tabia ya Mungu?

Je ni lazima kweli kwamba niwe na utambuzi sahihi wa tabia ya Mungu? Jibu ni: Ndiyo, hakika ni muhimu sana! Maelezo haya hapa: Mungu ananiomba nisalimishe Kwake uongozi wa maisha yangu. Mungu ananiomba nimtumaini Yeye kabisa, naam, nifungamanishe Kwake na uwepo wangu kamili. Mungu ananiomba nifanye kila kitu yasemacho maneno Yake. Hata hivyo, ningefanya hili tu endapo ningegundua kuwa Mungu anatumainika, mwenye upendo na mwelewa. Ni pale tu ninapokuwa na ufahamu sahihi wa tabia pekee ya Mungu, ndipo nitakuwa radhi kuisalimisha na kuiadhimu nafsi yangu. Ndivyo hivyo kwa kiasi kikubwa katika ulimwengu wa magharibi. Watu wengi sana wanatumaini tu upendo wa Mungu.

Siku ya 4

## Kwa nini baadhi ya watu wana mtazamo potofu kabisa juu ya Mungu?

Mshairi wa Austria, Peter Rosegger, alijenga mtazamo akiwa mtoto kwamba babaye alikuwa mkali sana. Siku moja alifanya kitu fulani cha utukutu. Kwa sababu aliogopa kwamba babaye angemwadhibu, alijificha kwenye kisanduku kikubwa cha saa sebuleni. Aliweza kutazama kupitia ufa na kuona jinsi baba yake alivyoingia kwenye chumba hicho na kuwaambia watumishi wamt-

afute. Walipokuwa wameondoka, baba yake akaanza kulia. Peter hakuweza kuvumilia kwa muda mrefu zaidi, akaibuka kutoka kwenye kisanduku cha saa. Baba yake hata hakufikiri kumwadhibu. Baadaye Peter Rosegger aliandika: "Tangu wakati huo na kuendelea nilijua kwamba baba yangu hakuwa mkali kupindukia." Tangu muda huo, alijua jinsi moyo wa babaye ulivyokuwa!

Hivi si kwamba watu wengi sana hufikiri kama ilivyokuwa kwa Peter Rosegger kuhusu baba yake – kwamba alikuwa mkali sana kupitiliza?! Baadhi yetu huwa tu tunahusisha picha tuliyo nayo ya baba yetu wa kidunia kwa Baba yetu wa mbinguni. Mara nyingi hili ni kosa kiasili.

Swali: Ni wapi ulikotoka utambuzi potofu kuhusu Mungu na tabia Yake? Jibu: mbinguni. Lusifa alikuwa wa kwanza kutathmini vibaya tabia ya Mungu na kuiwasilisha kwa wengine visivyo. Hadi leo yule mwovu hudiriki kuwashawishi watu kwa kila namna iwezekanayo waifikirie tabia ya Mungu vibaya.

## Tahadhari dhidi ya Udanganyifu Mkuu!

Shetani amewapotosha baadhi waamini kwamba Mungu ana sifa za uovu, ambazo kihalisia ndiye aliye nazo. Kwa kueneza fundisho la uongo la mateso ya milele jehanamu, amefaulu kuwafanya baadhi ya Wakristo wamwone Mungu kama mkatili (jahili) alipizaye kisasi. Matokeo yake ni kwamba amefanikiwa kuwashawishi watu wengi kanisani wasitake kusikiliza tena na hustahibu kujishughulisha na falsafa, kama vile (atheism), ambayo huelezea kutokuwepo kwa Mungu. Kwa watu wasiojali, wanaotaka kuamini bila kuchunguza Biblia yao katika upendo wa Mungu, Shetani hutumia mbinu nyingine: Mungu ni mwenye upendo sana kiasi kwamba tunaweza kufanya lolote tunalotaka – mwishoni atamwokoa kila mtu. (Sulemani alijua hakika kwamba mwishowe Mungu angemwajibisha kila mtu! Mhubiri 11:9) Shetani anajaribu kuwashawishi waoga kwamba maisha ya Ukristo ni magumu, yenye matatizo na yasiyokuwa na furaha. (Yohana alisema kinyume kabisa na jambo hili! 1 Yohana 5:3) Ni bayana ana hoja yenye mantiki kwa ajili ya matajiri – wangepaswa kuachana na vingi zaidi kuliko vile watakavyokuja kuvipata kama wakimfuata Yesu. (Lakini tunajua kwamba Paulo alikuwa na uzoefu tofauti kabisa! Wafilipi

3:4) Shetani huwahimiza wale wenye fikra hafifu wadhani kwamba Mungu ni mtafuta makosa na mkali (Ndiyo, Mungu anapaswa kuwa mkarimu sana kwao, lakini kwa wale ambao wamewadhuru, anapaswa kuwalipa vilivyo!) Na Shetani bado amewaongoza wengine wadhani kwamba nadharia ya uibukaji ni yenye mantiki. Amewashawishi wengine waamini kwamba Mungu ni mzee dhaifu tu ambaye hapaswi kutiliwa maanani.

**Shetani hurudia tena na tena kubuni kitu fulani kipya ili kuamsha dhana potofu juu ya Mungu akilini mwa watu** au kumwondoa Mungu mawazoni mwao. Analijua hilo hasa: yeyote asiyejua au asiyethamini tabia halisi ya Mungu, ni nadra kwamba atapenda lolote linalohusiana na Mungu. Na hapo ndipo hasa anapotaka awafikishe.

Roger Morneau aliandika: "'Pepo wachafu hupenda kucheza na akili za wanadamu,' mpunga-pepo aliniambia katika siku ambazo nilikuwa mwabudu-pepo. 'Wanaangaza mawazo na taswira akilini mwa wanadamu kwa ustadi wa kina kiasi kwamba wapokeaji huyaamini kuwa ni fikra zao.'" *(When you need incredible answers to prayer,* Review and Herald Publishing Association, 1995, uk. 70)

Shetani na pepo wake hujaribu kulaghai mawazo ya wale wanaodai kuwa Wakristo, kiasi kwamba kwa mawazo na matendo yao mabaya wanapotosha tabia ya Mungu au kuidhihirisha isivyostahili.

## Nyenzo ya Majaribu yenye Ufanisi Sana

Shetani anataka kuwashawishi watu wengi kadiri iwezekanavyo! Siyvo pasipo na sababu ambapo **Yesu alionya wazi wazi kuhusu ukengeufu,** ambao wafuasi Wake mwenye wangepitia **katika nyakati za mwisho.**

**Mtandao** ni nyenzo fanisi hasa kwa ajili ya kuwashawishi watu. Hakuna anayeweza kudhibiti mtandao! Kwa namna hii mwovu anaweza kushawishi mawazo na matendo, hususan kwa vijana. Kwa mfano, kijana (shahabi) **anaweza wakati wowote kuangalia chochote kinachomvutia** kwenye mtandao. Kimsingi wazazi hawana udhibiti husika. Nini kinachowavutia zaidi vijana(mashababi), wanapokuwa miongoni mwao

wenyewe? Tasnia ya filamu imelifahamu hilo kwa muda mrefu: mapenzi na ukatili. Kinachosikitisha, siyo tu kwamba vijana ndio wanaoathirika na mada hizi, lakini watu wazima wengi vilevile. Tunahitaji kujiuliza daima: Ni wapi nilipo katika hatari ya kushawishiwa na Shetani?

## Upendo wa Mungu na Uhuru Wetu

Baba yetu wa mbinguni amefungamanisha kabisa upendo Wake pamoja na uhuru. Upendo wa kweli unaweza tu kudhihirishwa kikamilifu katika uhuru. Uhuru ni rasilimali ya thamani kwa Mungu kiasi kwamba **aliwapatia viumbe Wake wote** – malaika, wakazi wa sayari zingine na sisi wanadamu – **uhuru**. Tunaamua **kwa ajili ya Mungu au dhidi Yake.** Hata hivyo, inajumuisha kuyakubali matokeo ya maamuzi yetu. Hivyo, mtu anayeamua dhidi ya Mungu, analazimika kukabili athari yeye mwenyewe; na kinachosikitisha, watu wengine nao wanaathiriwa na matokeo hayo hasi.

## Upendo wa Mungu na Haki Yake

Kwa sababu Mungu ni upendo, daima atatenda kwa haki. Katika upendo Wake, Mungu hawezi kukubali kwamba mtu fulani amedanganywa, amepigwa, amebakwa au amejeruhiwa vyovyote vile. Hivyo, kila mmoja, ambaye hajatubu makosa yake, mwishowe **atalazimika kubeba hatia ya dhambi yake mwenyewe.** Upendo wa Mungu huweka tu makosa ambayo mtu amefanya juu yake mwenyewe. Kila mtu huamua kipimo chake mwenyewe. Kwa vile Mungu huwapenda wadhambi pia, angependa badala yake aone mdhambi akitubu na kuruhusu nafsi yake iokolewe. Lakini **mdhambi** anapokataa fadhila ya wokovu, basi kwa mujibu wa Biblia atapokea "mshahara" wa dhambi yake: *"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti* [ya mwisho]*."* (Warumi 6:23)

Pia hushabihiana na **haki ya Mungu** kwamba mwishoni mwa wakati **waaminifu** wanatuzwa kwa **uzima wa milele** (Ufunuo 22:12). Wameikubali fadhila ya wokovu: **Yesu kwa niaba yao** amejitwalia **adhabu** kwa ajili ya dhambi zao **juu ya nafsi Yake Mwenyewe** (Isaya 53:5).

Kwa vile kawaida Mungu hamwadhibu mtu mara hiyo anapotenda dhambi, baadhi ya watu huwa washupavu na kadiri muda uendavyo hutenda dhambi hata zaidi. Hata hivyo, mdhambi asiyetubu analazimika kubeba matokeo hasi ya matendo yake wakati wa maisha yake. Wakati mwingine, matokeo haya hasi kwa nadra huonekana au hutambulika kwa mtu huyu, lakini daima yanatokea.

## Upendo wa Mungu na Mateso ya Ulimwengu Huu

Wakati wa kuzungumzia mada hii, watu huwa na maswali mengi sana. Mateso ni matokeo ya dhambi. lakini jinsi gani dhambi iliweza kuibuka ndani ya Lusifa ni fumbo halisi kwetu. Lusifa – sasa anaitwa Ibilisi au Shetani – vyovyote vile ndiye chanzo cha mateso yote. Na Mungu anamruhusu kiwango fulani cha uhuru kwa muda fulani, ili kila mmoja aweze kuona madhara ya dhambi. Hata hivyo, kipimo kinapojaa – na kwa mtazamo wangu kimekaribia kufikia kiwango hicho – ndipo Yesu atakuja ili kukomesha mateso yote duniani. Kwa kuzingatia maarifa yao kuhusu kile ambacho dhambi imefanya, waliokombolewa hawataweza tena kuwa na shauku ya kutenda dhambi. Ndipo utakuwepo tena umoja, upatanifu na upendo ulimwenguni kote. (Kwa maelezo zaidi juu ya mada hii: E.G. White, *Pambano Kuu,* sura ya 29 “Chanzo cha Uovu”)

## Kukabili Dhuluma – Kutenda Makosa

Kuna dhuluma nyingi sana katika dunia hii kwa sababu ya dhambi. Kwa kawaida huwa tuna mengi sana ya kusema kuhusu mada ya kukabili dhuluma, kwa vile mara nyingi huwa tunahisi kuathiriwa. Tungetamani hilo, kama daima Mungu angeingilia kati mara moja kabla dhuluma yoyote haijatupata. Lakini ndipo mtu aliyetaka kutenda dhuluma angemshutumu kwa kuondoa uhuru wake. Ndiyo maana ni nadra sana, sana Mungu huingilia kati mjo kwa moja. Yeye pekee ndiye anajua wakati **analazimika** kutenda ili kuzuia kitu fulani kibaya kisitokee. (Mfano: Adhabu ya uasi wa Kora katika Hesabu 16). Ni mwisho wa wakati tu ndipo waaminifu watashuhudia hilo: ***“BWANA ndiye afanyaye mambo ya haki Na hukumu kwa wote.”*** (Zaburi 103:6)

Kijumla, tunajishughulisha kidogo na mada kutenda mabaya. Na kwa kawaida, Mkristo ana uwezekano mkubwa zaidi katika kukabiliwa na dhuluma kuliko kutenda mabaya. Lakini hebu tufikie kifupi kuhusu nini kinachotutokea tunapotenda mabaya. Kwanza, dhamiri yetu hulemewa. Dhamiri yetu hutupatia "ishara" kwamba tuko katika njia mbaya. "Ishara" hii inapaswa kutukumbusha kutubu. Lakini tusipotubu na kuiacha dhambi, itakuwa na matokeo hasi kwenye tabia yetu. Halikadhalika, amani ya Mungu huondoka mioyoni mwetu. Na mara nyingi "dhambi za wazazi" hurithishwa kwenda kwa watoto wao.

Siku ya 5

## Kuitikia Upendo Uokoao na Kudumu Ndani Yake

Njia adhimu imefunguliwa kwetu, ambayo ni kuitikia hivi sasa upendo wa Mungu uokoao. *"**Leo**, kama mtaisikia sauti Yake, **Msifanye migumu mioyo yenu**..."* (Waebrania 3:15) **Tunapomkubali Yesu kama Mwokozi wetu na kudumu pamoja Naye,** ndipo tunaweza kuwa na hakika kwamba ametuweka huru dhidi ya hatia: ***"Yeye Mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili Wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki… ."*** (1 Petro 2:24)

Mtume Yohana aliandika: *"Mungu ni upendo, **Naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake."*** (1 Yohana 4:16) Kadiri uhusiano wetu ulio wa urafiki zaidi kwa Yesu, ndipo tutakuwa wenye furaha zaidi, tulioridhika zaidi na wenye shukrani zaidi! Na tunapomshukuru Mungu, daima huwa na matokeo chanya juu yetu na kwenye tabia yetu. Hata huwa tunashawishika kwa maneno yetu wenyewe *(The Desire of Ages,* uk. 322-323). Lakini siyo hilo tu – vilevile tunashawishika kwa kile tunachoona na kusikia. "Kwa kutazama tunabadilishwa." (E.G. White, *Patriarchs and Prophets,* uk. 459.1) Hii ndiyo sababu ni vema kujiweka chini ya nguvu ya Roho Mtakatifu kila siku na kusoma kisa cha uumbaji katika Biblia na kukitafakari.

Tunapokaa katika Kristo, hatutaendelea tena kuwa wepesi wa kutenda dhambi. Lakini kama ikitokea nasibu au bila kujua tukatenda dhambi, basi 1 Yohana 2:1 inahusika: "*Watoto wangu*

*wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki."*

Tunapokuwa na Yesu, basti tunaweza kusema pamoja na Paulo: *"Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao* ***walio katika Kristo Yesu****. Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima* [nguvu ya Roho Mtakatifu iletayo uzima] *ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti."* (Warumi 8:1-2)

Hali hii ya kuwa ndani ya Kristo humaanisha kukaa ndani Yake. Maneno haya hupatikana kwenye Agano Jipya mara 170 – 97 miongoni mwa hayo yako kwenye nyaraka za Paulo. Ni maneno mengine yanayomaanisha kuzaliwa mara ya pili. Yesu alisema katika Yohana 3:5: *"...Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi* [= kwa jinsi alivyo kwa asili] *kuuingia ufalme wa Mungu."*

Hebu tufupishe: Yeyote ambaye siku kwa siku huitikia upendo wa Mungu uokoao, atahisi mabadiliko maishani mwake na katika ubora wa maisha yake, ambao hakuujua hapo kabla, na hatimaye atapokea uzima wa milele. Naiona hii kama barabara ya kifalme ya upendo wa Mungu. Upendo Wake unataka kutubariki kila siku na kutuokoa hatimaye!

## Upendo wa Mungu Hufuzu Kila Mtihani!

Wengi wetu tunafahamu mfano wa mwana-mpotevu katika Luka 15:11-32. Siku moja, kijana mdogo anamwendea babaye (ambaye humwakilisha Mungu) na kumwambia kwamba anataka kuondoka nyumbani na kuishi maisha yake mwenyewe. Ni dhahiri, kanuni na taratibu za baba yake (amri za Mungu) hazikumfaa. Kabla mwana huyu hajaondoka, alidai urithi, ambao hata kuwaustahili wakati huo. Hata hivyo, babaye alimpatia mgawo wake. Babaye alimpatia uhuru kamili, kwa sababu alimpenda. (Hivi ndivyo Mungu anavyotutendea.)

Mwana huyu alienda nchi ya mbali. Alifanya chochote alichopenda. Alitumia pesa yake katika karamu za anasa na wanawake wapotovu. Pesa yake ilipokaribia kuisha, "duara lake la marafiki" haraka likawa dogo zaidi. Hatimaye, hakuwa

na chochote kilichosalia. Halafu, ili kuyafanya mambo kuwa mabaya zaidi, njaa ikapiga kwenye eneo hilo alikokuwa. Ili kustahimili, alilazimika kutafuta kazi. Nafasi pekee aliyoipata ni kuwa kama mchunga-nguruwe. Kwa kusita, alikubali kazi hiyo. Mara nyingi njaa ilimtesa, lakini hata hakuruhusiwa kula chakula cha nguruwe. Wakati wa madhila haya alikumbuka maisha yake pamoja na babaye, ndipo akafikia hitimisho lifuatalo: Watumishi wa baba yangu wanasaza chakula nami hapa nakufa njaa. Nitaenda kwake na kusema: "*Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena; nifanye kama mmoja wa watumishi wako."* (fungu la 18-19) (Tunapokuwa tumehuzunika kwamba tumetenda dhambi dhidi ya Baba yetu wa mbinguni na kumwambia hiyvo, kwenye Biblia hii inaitwa "toba" na "maungamo.") Alianza safari yake kurudi kwa babaye akiwa na hisia mchanganyiko. Tayari babaye alimtambua mwanawe akingali mbali. Ni bayana, baba huyu alikuwa akimtazamia kwa upendo. (Baba yetu wa mbinguni hungojea kwa shauku akitumaini kwamba hatutaendelea tena katika njia zetu, bali tutarudi Kwake!) Akiwa amejaa huruma baba huyu alimkimbilia mwanawe, akamwangukia shingoni pake na kumbusu sana, japo mwanawe alikuwa mchafu sana na mwenye kutoa harufu mbaya. Hata mwanawe hakuweza kukamilisha maungamo yake kabla ya babaye kuwaita watumishi wake. Aliwaambia watumishi walete mavazi bora na kuandaa karamu. Ni wazi, baba huyu alimpenda mwanawe vilevile kama hapo awali. (Mungu hupenda bila masharti! Upendo huu hufuzu kila mtihani!) Lakini hilo halitusaidii kama tusipoishi pamoja Naye. Baba hakuweza kumfanyia chochote wakati ambapo hakuwa pamoja naye; hata kama alikuwa mgonjwa au alikuwa na matatizo makubwa.

## Wakati gani ambapo Upendo wa Mungu ni Muhimu Kwangu?

Nini kilichomfanya mwana huyu ghafla kiasi hicho athamini upendo wa babaye? Ni pale tu alipotambua jinsi gani alivyokuwa ameufurahia akiwa nyumbani, ndipo alitaka kwenda kwa babaye. Zahama ilimrudisha kwenye fahamu zake. Kupitia "maisha

yake magumu” mwenendo wake wa ujeuri ulitoweka ukaruhusu mwenendo halisia. Aliona kwamba wale aliodhani ni marafiki zake walikuwa “wamependa” fedha zake badala ya kumpenda yeye. Lakini daima baba yake alikuwa amemwonesha upendo, hata wakati ambapo alikuwa akimdharau.

Na nina hakika kwamba baada ya baba yake kumpokea kwa upendo wa namna hiyo, kwamba kamwe hakufikiri kuondoka tena.

**Sasa,** babaye angeweza kumwonesha upendo wake kamili. Ni wakati wa **sasa** tu ndipo mwana huyu alikuwa radhi kwa upendo huu. Hapo awali, baba yake alilazimika kuzuia ishara za upendo kwa sababu wakati wote mwanawe alipokuwa akimpuuza. Lakini sasa hapakuwepo chochote cha kuzuia uhusiano wakina kati ya baba na mwana!

Ninapofungua nafsi yangu wazi kabisa kwa Mungu, ninapoungama hatia yangu na kuyakabidhi maisha yangu Kwake, basi hapo naweza kupata uzoefu mkamilifu wa upendo Wake!

Ni mtu yule tu anayeinyenyekesha nafsi yake mbele ya Mungu na kutambua kwamba hastahili kupendwa na Mungu (kama alivyofanya yule mwana mdogo aliporejea nyumbani), ndipo anaweza kuwa mwana au binti halisi wa Mungu. Ni wale tu wanaokabidhi maisha yao kwa Baba ndio mwishowe watapokea urithi wao – uzima wa milele.

## Kuomba kwa ajili ya Upendo

Nini nipaswacho kufanya kama nikigundua kiasi kidogo sana cha upendo kwa ajili ya Mungu na jirani yangu? Naam, tunaweza kuombea jambo lolote, ikiwa ni pamoja na kuomba tuweze kupokea upendo zaidi kwa ajili ya Mungu na majirani zetu. Ombi letu linaweza kuwa na jumbe kama: “Baba mpendwa, tafadhali nisaidie nikupende kwa moyo wangu wote, kwa nafsi yangu yote, kwa hisia zangu zote na kwa nguvu zangu zote. Tafadhali tenda ndani yangu ili nipate nia na kutenda kadiri ya mapenzi yako mema katika suala hili. Pia nataka kuwa na uwezo wa kuwapenda zaidi wanadamu wenzangu. Na pia nisaidie niweze kujipenda mwenyewe. Asante kwamba naweza kupata uzoefu wa upendo wako kamili. Nifanye kuwa mfereji wa upendo Wako kwa ajili ya

mazingira yangu. Amina." (Tunaweza kuomba kwamba Mungu atuwezeshe kutimiza Mathayo 22:37, 39!)

## Elimu, Ghadhabu na Hukumu

Kila nafsi inayojisalimisha kwa Mungu itaelimishwa Naye. **Elimu** yetu ni suala muhimu kwa Mungu. Ni **sifa ya upendo Wake** kwamba anatudahili katika "shule" Yake. Anataka kuwaandaa kutoka miongoni mwetu watu wanaopendeka, wenye uwezo na walio huru, japo aina ya mbinu za elimu atumiazo hutegemea sana na namna gani bora tujifunzavyo. Tunapomfikiria kijana Samweli, bila shaka alikuwa mwanafunzi mzuri sana machoni pa Mungu tangu mwanzo. Kwa sababu alimtumaini Mungu, alikuwa na shauku ya kujifunza na alikuwa mtii kwa Eli, "mwalimu" wake, kabla ya kutokea mbinu zingine za elimu zisisofaa. Hii ilikuwa na matokeo chanya sana kwake na kwa mazingira yake. Biblia inasema: *"Lakini Samweli alikuwa akitumika mbele ya Bwana…. Na yule mtoto, Samweli, akazidi kukua akapata kibali kwa Bwana, na kwa watu pia."* (1 Samweli 2:18, 26) Kinyume chake, wana wa Eli hawakuwa wanafunzi watiifu: *"Lakini hawakuisikia sauti ya baba yao. ..."* (1 Samweli 2:25) Na hivyo ilitokea kwamba walifika kwenye mwisho mbaya. Walikabiliana na ghadhabu ya Mungu kwa sababu ya huduma yao ya kufuru ya kikuhani.

**Sifa nyingine ya upendo wa Mungu** ni **ghadhabu Yake.** Mwanzoni hilo linaweza kusikika kama jambo geni, lakini tunahitaji kukumbuka kwamba ghadhabu ya Mungu siyo sawa na ghadhabu ya mwanadamu. Ubinafsi wetu kwa kawaida hufanya kazi muhimu katika ghadhabu ya mwanadamu. Kwa upande mwingine, ghadhabu ya Mungu kijumla huelekezwa kwenye dhambi au mwenendo wa dhambi (Warumi 1:18), kwa sababu kile ambacho dhambi inaleta kinatisha.

**Sifa nyingine ya upendo wa Mungu** ni kwamba **anamhukumu kila mtu kwa haki.** Yeye pekee ndiye mwenyewe uwezo wa kufanya hili, kwa vile anajua kila kuhusu kila mmoja. Tayari Daudi alilijua hilo: *"Mungu ni mwamuzi mwenye haki."* (Zaburi 7:11) Na: ***"Haki na hukumu ndio msingi wa kiti Chake."*** (Zaburi 97:2)

Kila mmoja wetu ana uwezekano wa kufanya lolote apendalo. Lakini Biblia inatuonya: *"Mche Mungu, nawe uzishike amri Zake, Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu.* ***Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi,*** *pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya."* (Mhubiri 12:13-14) Kwa vile watu wengi katika siku na zama hizi hawazingatii onyo hili, kuna mateso mengi ulimwenguni hapa. Yesu alijua mambo yangekuwa hivi na hivyo alitabiri kuhusu wakati wetu: ***"Na kwa sababu ya kuongezeka maasi, upendo wa wengi utapoa."*** (Mathayo 24:12) Kwenye nyakati ngumu, utambuzi kwamba haki ya Mungu itashinda hatimaye, hutuimarisha.

Siku ya 6

## Msaada wakati wa Dhoruba: Sheria ya Mungu – Sheria ya Upendo

Watu wengi huishi bila Mungu; hujihesabu kuwa kipimo cha mambo yote. Ndiyo sababu maadili mengi zaidi na zaidi yamepotea leo. Viwango vya kanuni, ambavyo awali vilikuwa halali, vimesahaulika. Matokeo yake, watu wengi zaidi wanapoteza dira yao ya maisha na hivyo wanaugua kisaikolojia au kujiua, kwa sababu kila kitu kinaonekana hakina maana. Tunahitaji kitu fulani thabiti na kinachotumainika kwa ajili ya maisha yetu; tunahitaji viwango na taratibu zinazotumainika. Mshairi, Matthias Claudius, aliisema kwa namna hii: "Watu wanahitaji kitu fulani thabiti, mahali wanakoweza kutweka nanga. Kitu fulani kisichowategemea wao wenyewe, bali kitu fulani wanachoweza kukitegemea." (Matthias Claudius, Edition Steinkopf, 1982, uk. 10)

Nani basi, kama si Muumbaji wetu, anayejua ni taratibu zipi zilizo njema kwetu! Siyo tu kwamba Biblia inasema kuwa Mungu ndiye pekee awezaye kuamua kile kilicho sahihi na chema kwetu (Zaburi 99:4), lakini pia anasema kwamba sheria Zake hazina kifani na zitadumu milele: *"Maagizo Yake yote ni* ***amini, Yamethibitika milele na milele,*** *Yamefanywa katika* ***kweli*** *na* ***adili."*** (Zaburi 111:7-8)

Kila muumini wa kila kizazi amekuwa na uhusiano chanya kwenye sheria ya Mungu. Hebu tumwangalie Daudi, kwa mfano; alitamka mengi ya kuvutia kuhusu sheria ya Mungu: ***"Sheria ya***

***Bwana ni kamilifu, Huiburudisha nafsi.”*** (Zaburi 19:7) ***“Sheria ya kinywa Chako ni njema kwangu, Kuliko maelfu ya dhahabu na fedha.”*** (Zaburi 119:72) ***“Kama sheria Yako isingalikuwa furaha yangu, Hapo ningalipotea katika taabu zangu.”*** (Zaburi 119:92) Kwa upande mmoja, sheria ya Mungu ni udhihirisho wa upendo Wake, na kwa upande mwingine, kwa mujibu wa Paulo: ***“…pendo ndilo utimilifu wa sheria.”*** (Warumi 13:10)

## Amri Mpya: Penda kama Yesu

Yesu aliwapatia wanafunzi Wake – na kupitia kwao, kwetu pia tuaminio – amri mpya. Alisema: *“Amri mpya nawapa, Mpendane.* ***Kama vile nilivyowapenda ninyi****, nanyi mpendane vivyo hivyo. Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi Wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi.*” (Yohana 13:34-35)

Yesu anatuita, kwa kweli anatuamuru, tupendane ***“kama vile nilivyowapenda ninyi.”*** Hilo humaanisha tunapaswa kuwa na upendo uleule kama wa Yesu. Ni aina gani ya upendo unaomaanishwa hapa? Ni aina ya upendo ambapo Bwana anamwonesha Mwanawe, Yesu Kristo. Ni aina ya upendo ambapo Mwana aliuonesha pale msalabani alipotufia. Mungu aliufanya upendo huu wa kiungu, wa milele, usio badilika, usio na masharti wala ubinafsi upatikane kwetu kupitia Roho Mtakatifu katika Kristo. Biblia inasema wazi: *“...pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu…”* (Warumi 5:5; angalia pia Waefeso 3:16-17) Kwa maneno mengine: Tunapokuwa tumejazwa Roho Mtakatifu, wakati huohuo tunakuwa tumejazwa upendo wa Mungu.

Hivyo, kupenda kama Yesu humaanisha: kupenda kwa upendo wa kiungu (agape). Ellen White alisema kwa kiasi fulani kuhusu hili – hizi hapa nukuu tatu fupi: “Upendo turufu kwa ajili ya Mungu na upendo usio na ubinafsi wa mtu na mtu – hii ni tunu bora ambayo Baba yetu wa mbinguni anaweza kutukirimia. Upendo huu siyo mhemko, bali kanuni ya kiungu, nguvu yakudumu. Moyo usiosafi [kila mmoja, asiyejazwa Roho Mtakatifu, anao] hauwezi kuuzua wala kuuzalisha. Ni katika moyo tu ambamo Yesu anatawala ndimo hupatikana.” *(Acts of the Apostles,* uk. 551.2) “Unahitaji ubatizo wa kila siku wa upendo ambao katika siku za mitume

uliwafanya wote wawe na nia moja." *(Counsels for the Church,* uk. 175.3). Kuomba kila na kumpokea Roho Mtakatifu huleta matokeo ambatani ya ubatizo wa upendo – kujazwa upendo wa Mungu. "Kwa kuvaa pambo la roho ya upole na utulivu, matatizo tisini na tisa kati ya mia ambayo kwa namna ya kutisha sana hutia uchungu maishani yangeweza kudhibitiwa." *(Testimonies for the Church, vol. 4,* uk. 348.3)

## Bila Upendo Kila Kitu ni Bure(Dufufi)!

Kwa mtazamo wa haraka, kauli hii huonekana kwa namna fulani imekolezwa. Lakini tunapoangalia 1 Wakorintho 13:1-3, ndipo tunatambua haraka kwamba kauli hii ni kweli: *"Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao. Tena nijapokuwa na unabii, na kujua siri zote na maarifa yote, nijapokuwa na imani timilifu kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo, si kitu mimi. Tena nikitoa mali zangu zote kuwalisha maskini, tena nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama sina upendo, hainifaidii kitu."* Nini tuwezacho kujifunza kutokana na hili? Ni pale tu matendo yetu yanapoongozwa kwa upendo, ndipo yanapokuwa ya thamani machoni pa Mungu. Shairi lifuatalo hulenga kwenye mwelekeo huo:

## Bila Upendo Kitu Fulani Muhimu Hukosekana!

| | | |
|---|---|---|
| Majukumu | bila upendo | ni wasiswasi (wahaka) |
| Wajibu | bila upendo | ni kutojali |
| Haki | bila upendo | ni ukatili, |
| Ukweli | bila upendo | ni ukosoaji, |
| Elimu | bila upendo | ni ukaidi, |
| Akili | bila upendo | ni ulaghai |
| Urafiki | bila upendo | ni unafiki, |
| Utaratibu | bila upendo | ni uchwara, |
| Umahiri | bila upendo | ni ushupavu, |
| Heshima | bila upendo | ni kiburi, |

| | | |
|---|---|---|
| Mali | bila upendo | ni madhila |
| Imani | bila upendo | ni (usharidi) ubinafsi. |

(Mwandishi hajulikani)

Tunaweza kuona kwamba bila upendo – upendo wa kiungu unamaanishwa – matendo yetu na uwepo wetu kimsingi huweza kuleta tu matokeo yasiyoridhisha.

Ni muhimu sana kwamba **kila tufanyalo, kifanyike kutokana na moyo wa upendo wa Mungu na kwa jirani yetu.** Tutaweza kufanya hili endapo Kristo akikaa mioyoni mwetu kupitia Roho Mtakatifu.

Ni muhimu **kwamba tuweze** kukua katika upendo kupitia tabia ya Mungu ya upendo.

## Upendo katika Silika ya Kina Zaidi

Hitaji kuu zaidi la mwanadamu ni kupenda na kupendwa. Uhusiano kati ya Mungu na muumini hulinganishwa na ndoa nzuri kwenye Biblia (Isaya 54:5; Waefeso 5:32). Nini kinachoashiria ndoa nzuri hapa duniani? Wanandoa hujaribu kufurahishana, wanatumia muda mwingi pamoja kadiri wawezavyo, wanazungumzia kila kitu kigusacho mioyo yao, wanarudiarudia kuambiana jinsi gani wanavyo-pendana na kuna mbadilishano ya mahaba.

Kuna uhusiano ambao kila mmoja anaweza kuwa nao – ama yuko kwenye ndoa au la – ambao huzama kina kirefu zaidi kuliko uhusiano wa ndoa kati ya mwanaume na mwanamke. Ni uhusiano alio nao Mkombozi na Mungu wangu: Yesu Kristo! Kupitia Yesu, naweza kupata uzoefu wa hali ya juu kabisa iwezekanavyo ya usalama, msaada wadhati, na upendo wa kina zaidi. Anatumainika kabisa na wala hana ubinafsi. Kamwe Yesu hanifadhaishi! Upendo Wake haubadiliki! Ana muda kwa ajili yangu mchana au usiku. Sihitaji misaada yoyote ya kiufundi ili kuwasiliana Naye. Hakuna tatizo lililo kubwa zaidi Kwake – daima ana ufumbuzi ulioandaliwa kwa ajili yangu. Ananionesha kwenye neno Lake jinsi gani ananipenda! Anawatumia walinzi bora kabisa kwa ajili ya usalama wangu binafsi; natazamia siku ambayo naweza kukutana na malaika hawa! Na kwa sababu Yesu

ananipenda, anataka hivi karibuni niwe pamoja Naye milele! Alilipa gharama ya juu zaidi kwa ajili ya "kubadilisha maskani yangu" na tayari ameniandalia makao mazuri mno. Ananililia, pale ninapoidhuru nafsi yangu! Naye anatazamia ili hatimaye anibebe mikononi Mwake, siku moja nitakapokuwa pamoja Naye katika Yerusalemu Mpya!

Je unaweza kufikiria upendo mkuu zaidi kuliko huu?! Mimi siwezi!

## Upendo na Uaminifu Hukaa Pamoja

Je unajua kwamba Mungu ana wivu wakati mwingine? Ndiyo, umeisoma hiyo kwa usahihi! Katika kitabu cha Nahumu 1:2 kinasema: ***"Mungu ni mwenye wivu…"*** (NKJV)

Swali ni kwamba nini kinamfanya awe na wivu? Jibu linapatikana katika Ezekieli 16. Inafaa kusoma sura nzima katika muktadha wake. Nimepambanua fungu la 8 na 15: *"... Naam, nalikuapia, nikafanya agano nawe, asema Bwana MUNGU, ukawa Wangu* [Yerusalemu = watu wa Mungu]…. *Lakini uliutumainia uzuri wako, ukafanya mambo ya kikahaba kwa sababu ya sifa zako, ukamwaga mambo yako ya kikahaba juu ya kila mtu aliyepita; ulikuwa wake."*

Tunaona hapa kile kinachomfanya Mungu awe na wivu: mathalani, pale watoto Wake wanapojihusisha katika **ukahaba wa kiroho.** Lakini tunapaswa kutambua kwamba **wivu wa Mungu** ni tofauti na wivu wa kibinadamu. Hilo ni sawa pale tunapozungumzia ghadhabu ya Mungu. Nia ya wivu Wake na ghadhabu Yake ni adilifu kabisa na ina sifa **kamili ya kutokuwa na ubinafsi. Anahusika na ulinzi wetu!** Anataka tuneemeka. Kupitia wivu Wake, **anataka kutuhifadhi** dhidi ya kuikimbilia miungu mingine. Anajua kwamba hilo litatuumiza tu. Miungu ya kisasa inaweza kuwa, mathalani: mwimbaji wangu ninaye mhusudu, gari langu, nyumba yangu, kazi yangu, hobi yangu – chochote ninachokipenda kuliko Mungu.

Kwa kuturuhusu tujue kwamba anatulinda kwa wivu, anataka kutuonesha kwamba uhusiano pamoja nasi una maana adhimu Kwake! Atasikitika sana kutupoteza.

Mungu wetu anataka "tudumishe unadhifu wa ndoa yetu ya kiroho." Hebu fikiria, endapo mume angemwambia mkewe

baada ya mwaka mmoja wa ndoa: "Japo tumeoana, kuanzia sasa nitakuwa mahali fulani siku mbili kwa juma." Inaeleweka, hakuna uwezekano wa mkewe kuliafiki hili!

Na Mungu pia hawezi kulikubali, pale ambapo hatudumishi "ahadi yetu ya ndoa." Yeye ni mwaminifu kwetu na anategemea hilo kutoka kwangu na kwako. (nadhiri za Ubatizo!) Anatamani kuona upendo wetu usiogawanyika. Ndiyo maana ujumbe wa Biblia ni bayana sana: **Iweni Wake kikamilifu,** au ruhusuni iwe hivyo!

## Upendo wa Mungu ni baraka kwa watu wote

Kuna baraka ya jumla kwa ajili ya kila mmoja. Kila mmoja hupokea baraka zinazoshabihiana na mwenendo wake. Mtu fulani anapofanya kazi kwa bidii, kikanuni hawezi kufa njaa. Mtu fulani anapoishi maisha ya uaminifu, atafurahia thamani ya watu wengi. Mtu fulani anapokuwa mwenye msaada, atathaminiwa. Baraka hizi za asili zinahusika kwa watu wote, bila kujali ni waumini au la.

Tunajua kwa Uzoefu – wa Biblia huthibitisha hili – kwamba Mungu huruhusu jua liwaangazie watu wema na wabaya, kwamba anaruhusu mvua iwanyeshee wenye haki na wasio haki na kwamba anaruhusu chakula kistawi kwa kila mmoja, ambapo kwa masikitiko hatuvigawi kwa uwiano sawia. Pamoja na hilo, Roho Mtakatifu humfuata kila mmoja ili kumhimiza asalimishe maisha yake kwa Yesu. Mungu anataka kuwaokoa watu wengi kadiri iwezekanavyo!

Mbali na baraka hizi asilia za jumla kwa watu wote, kuna **baraka maalumu, baraka kiungu** ambazo Mungu huweza kuwapatia **"watoto Wake"** tu. Hawa ni wale ambao wamesalimisha maisha yao kwa Yesu na kujitoa wakfu Kwake kila siku!

**Kila mtu hujiamulia mwenyewe,** ama anapokea tu baraka za jumla kutoka kwa Mungu au baraka za jumla **NA** baraka maalumu, za kiungu kutoka kwa Mungu. Daima upendo hufungamanishwa kwa mtu. Hakuna upendo bila uhusiano. Ni aina gani ya uhusiano unaofaa hapa? Biblia hulinganisha uhusiano wetu na Mungu kupitia Yesu Kristo na ndoa. Yesu

ni mwenye upendo mno na pia ni mshirika mwaminifu. Hivyo maisha katika utimilifu wa Mungu (Waefeso 3:19) hutegemea endapo nimemkabidhi Yesu maisha yangu. Kama nisipoidhamani nafsi yangu Kwake au sijakaa katika uhusiano huu, basi ninakuwa nakataa mvuto na upendo, na baraka za kiungu kwa wakati mmoja.

Tunaweza kusoma kwenye Biblia ili kujua baraka hizi maalumu ni nini:

- “Utunukaji Karama wa Kristo, huambatana na baraka zote, Roho Mtakatifu”
- “Maisha mapya pamoja na Kristo moyoni mwetu”
- “Kupata msamaha wa hatia yetu yote”
- “Kupata uzoefu na kukua katika matunda ya Roho: Upendo, furaha, amani, uvumilivu, ukarimu, wema, uaminifu, upole, kiasi – Wagalatia 5:22 – tabia yetu hubadilika na kukua.”
- “Uongozi wa Mungu”
- “Kupokea nguvu maalumu kimwili na kiroho”
- “Uhakikisho wa wokovu”
- “Malaika, anayeambatana nasi na kutusaidia”
- “Kupokea uzima wa milele.”

**Muumini hubarikiwa** maradufu (maridhawa) kwa baraka za jumla, na baraka maalumu, za kiungu: *“ili mweze kujazwa utimilifu wote wa Mungu.”* (Waefeso 3:19 NKJV); *“Maana katika Yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili. Na ninyi mmetimilika katika Yeye aliye kichwa cha enzi yote na mamlaka.”* (Wakolosai 2:9-10) Ni mpaka tupate uzoefu wa baraka hizi maalumu ndipo maisha yetu yatakuwa timilifu kama alivyokusudia Mungu. Ni maisha ambayo tunafikia hatua ya kujua na kuthamini vipengele zaidi na zaidi vya upendo wa Mungu.

Nataka kufunga somo hili la upendo wa Mungu kwa ombi kutoka kwa Paulo lipatikanalo katika Waefeso 3:16-19, KJV:

***Sala: "Kwamba awajalieni, kadiri ya utajiri wa utukufu Wake, mwimarishwe kwa nguvu katika utu wa ndani kupitia Roho Wake; kwamba Kristo aweze kukaa mioyoni mwenu kwa imani; kwamba ninyi ilhali mmekita mizizi na kujenga msingi katika upendo, mweze kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kina, na kimo; na kuujua upendo wake Kristo upitao ufahamu, ili mweze kujazwa na utimilifu wote wa Mungu AMINA"***

## Mawazo binafsi na mwongozo wa mjadala

1. *Kwa nini tuwe na hakika kwamba kweli Mungu ni upendo?*

   ______________________________________________

2. *Kwa nini ni muhimu sana kujua tabia ya Mungu? Ni athari zipi ziwawezekana kuwa na dhana potofu juu ya Mungu?*

   ______________________________________________

3. *Kuna tofauti gani iliyopo kati ya baraka za jumla na baraka maalumu, tukufu kutoka kwa Mungu?*

   ______________________________________________

4. *Kivipi "naweza kufahamu jinsi ulivyo upana, na urefu, na kina, na kimo; na kuujua upendo wake Kristo"? (Waefeso 3:17 NIV)*

   ______________________________________________

## Muda Wetu wa Maombi

- Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.
- Sali pamoja na mwanamaombi mwenzio…
  1. … kwa ajili ya moyo mwelekevu wa kutambua tabia ya Mungu.
  2. … kwa ajili ya moyo msafi na mtiifu.
  3. … kwa ajili ya upendo wa kiungu utubadilishao tuwe katika sura Yake.
  4. … kwa ajili ya baraka maalumu, za kiungu kutoka kwa Mungu.

Siku ya 7

SURA YA 2

# Njia Mahiri ya Mungu

Kutumika, kusaidia, kutoa, kubariki!
Kwa nini na kwa kusudi gani?
Utayari – mtazamo upatanao na moyo wa Mungu

## Ninamfuata nani?
## Ari ya kisasa au Neno la Mungu

Ni kwa mtazamo gani tunaiangalia mada “utumishi” – kwa mtazamo wa ulimwengu au ule wa kiungu? Mtu wa “asili” hutaka wengine wamtumikie, bila yeye binafsi kuwa wa radhi kuwa mwenye manufaa ya utumishi. Ni sawa na Mkristo wa “mwilini.” Mafarisayo na masadukayo wakati wa Yesu walikuwa na fikra hiyo hiyo (angalia Mathayo 23:4-7). Lakini Yesu anatuita tufanye kitu fulani tofauti: *“Naye aliye mkubwa wenu atakuwa mtumishi wenu.”* (Mathayo 23:11) Watu wengi hudhani kwamba mwenendo wa aina hii ni hasara. Lakini kinyume chake hasa ndiyo sahihi!

## Kusaidia Husaidia

Watoto wadogo hutaka “kuwasaidia” wazazi wao. Kwa nini ni vyema pale wazazi wanaporidhia hilo kwa furaha, japo mwanzo wa “msaada” huo husababisha kufanya kazi zaidi? Naam, mtoto hukua katika uzoefu wa uwezo wake na kiakili kupitia mwenendo wake wa “kusaidia” au “kutumika.” Anafurahia kila kitu anachoweza kufanya, hata kama matokeo ya awali kwa namna fulani ni ya ajabu mara nyingi. Kadiri mtoto anavyoweza “kusaidia” mara nyingi zaidi, ndivyo matokeo yatakavyokuwa bora zaidi. Na siku itakuja ambapo mtoto huyo ghafla atakuwa msaada halisi kwa wazazi wake. Mtoto anakuwa amejenga ujuzi. Na mtoto anaporuhusiwa kusaidia katika maeneo mengi mbalimbali, basi atakua na kufikia hatua ya mtu mwenye uwezo.

Nini kingetokea endapo wazazi hawakumruhusu mtoto huyu “asaidie”? Mtoto huyo angevunjwa moyo na ingekuwa vigumu zaidi kwake kujifunza kuyamudu maisha.

## Watendakazi wa Yesu – kwa nini na kwa kusudi gani?

Yesu, mfano wetu mkuu, alikuja duniani hapa: *“...kutumika, na kutoa nafsi Yake iwe fidia ya wengi.”* (Mathayo 20:28)

Kwa nini Yesu aliasisi huduma ya kutawadha miguu mara tu kabla ya *ubatizo wa mateso Yake*? Hadi hatua hii, wanafunzi Wake bado walikuwa hawajaelewa kwamba wangepaswa kuyaiga maisha ya Yesu – maisha ya utumishi usio na ubinafsi. “Katika chakula hiki cha Pasaka ya mwisho jioni, Yesu aliyarudia mafundisho Yake kwa kielelezo kilichogusa milele akili na mioyo yao.” (*Desire of Ages,* uk. 642.2 – egwwritings.org).

Inawezekana kwamba nasi vilevile bado hatujaelewa maana halisi ya kutawadha miguu?

Mtunzi wa Zaburi anatualika: *“Mtumikieni Bwana kwa furaha; Njoni mbele Yake kwa kuimba.”* (Zaburi 100:2). Kwa mtazamo wa haraka, tunadhani kwamba kutumika na furaha havishabihiani, sivyo? Fikiria tena jinsi watoto “wanavyotamani kusaidia.” Mtoto hupata uzoefu wafuraha pale anapoweza “kusaidia” au “kutumika.”

Mungu anajua kwamba utumishi ni mzuri kwa ajili yetu. E.G. White anafafanua juu ya hili: **“Hekima ya kiungu imeteua, katika mpango wa wokovu, sheria ya tendo na mwitikio, ikifanya kazi ya fadhila, katika matawi yake yote, iwe na baraka maradufu. Yule awapaye** wahitaji **huwabariki wengine, naye hubarikiwa hata kwa kiwango kikubwa zaidi.** Mungu angeliweza kutimiza lengo Lake katika kuwaokoa wadhambi bila msaada wa mwanadamu; lakini alijua **kwamba mwanadamu asingekuwa na furaha bila** kuhusika katika kazi kuu ambayo kwayo angekuwa akikuza sifa ya ukarimu na **kujikana nafsi. Ili mwanadamu asipoteze matokeo ya ukarimu yaletayo baraka, Mkombozi wetu aliunda mpango wa kumdahili awe mshirika Wake kazini.”** (*Testimony Treasures, vol. 1,* uk. 360.4-361.1)

Ni mawazo gani ya kustaajabisha ambayo yako kwenye nukuu hii? Hebu tuichunguze kwa kina zaidi:

- Kutenda mema kwa namna yoyote ni baraka maradufu: Pande zote mbili, kwa mtoaji na mpokeaji wa baraka.
- Katika mchakato husika, mtoaji hupokea baraka kubwa zaidi kuliko mpokeaji. Anapata uzoefu: kwamba kudumisha hali ya kujikana nafsi na kuwaonesha wengine ukarimu huinakisha tabia na kutufanya tuwe na furaha.
- Halikadhalika, mawasiliano mengi hufanya kwa watu kwa namna hii, ambapo kwa baadhi huweza kusababisha urafiki halisi.
- Kuwa mshirika wa Mungu kazini pia humaanisha kuwaongoza watu kwa Yesu. Hii huimarisha imani yetu na kuibua furaha ya kina ndani yetu.

Uzoefu kutoka Bolivia:

Kubarikiwa mara mbili kwa kutoa – Ni baraka za pekee ilioje ambazo nimepokea kwa kusoma kitabu hiki *(Hatua za Uamsho Binafsi)*! Kila asubuhi wakati wa muda wetu wa ibada, nawashirikisha wanafunzi wa shule yetu ya misheni dondoo husika. Wakati wa maandalizi na kuwasilisha, nabarikiwa maradufu kadiri yako. Katika ufalme wa Mungu, wakati wote hutendeka hivi: daima mtoaji hupokea zaidi ya mtoaji. (D. K. Bolivia / South America #9/132)

## Kutumika, Kutoa, Kusaidia!

Kwa vile siyo tu watu wa "asili" wasiopenda kutumika, bali hata Wakristo wa "mwilini," kijumla washiriki wengi wa kanisa wanapaswa kwanza kuandaliwa kwa ajili ya utumishi. Kujazwa Roho Mtakatifu ni muhimu sana kwa ajili ya badiliko hili, maana analeta mwenendo tofauti. Biblia inazungumzia kazi hii bayana kabisa: *"Naye [Kristo] alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu;* ***kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke****, hata mwili wa Kristo ujengwe."* (Waefeso 4:11-12)

Viongozi wanalo jukumu la kuwafundisha watu kuhusu maandalizi kwa ajili ya utumishi (Kristo aishiye moyoni mwako kupitia Roho Mtakatifu) na kuhusu maana na

utumishi (kwa ajili yetu sisi na wengine). Hii huchukulia kwamba wanadumisha maisha pamoja na Roho Mtakatifu, pamoja na kuwa mfano na kuwa na umahiri wa kuwasilisha mafundisho halimali katika maeneo fulani. Kwa jinsi hiyo, Mungu huwabariki viongozi na kanisa nalo hubarikiwa kupitia wao. Na kanisa litajengwa kwa utumishi wa washiriki ndani na nje ya kanisa. *Mbali na funguiliyotajwa mwanzoni, Mathayo 20:28, kuna mpangilio wa maandiko mengine ambayo hutuonesha kwamba kutumika, kutoa na kusaidia ni huduma zenye baraka:*

***"Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa;*** *kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwa-sukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa."* (Luka 6:38)

***"Mtu mmoja hutoa kwa hiari, lakini huongezewa hata zaidi;*** *mwingine huzuia isivyo haki, lakini hukabiliwa na umaskini. Mtu mkarimu atapata fanaka;* ***awanyweshaye wengine naye atanyweshwa.****"* (Mithali 11:24-25 NIV**)**

*"Amhurumiaye maskini humkopesha Bwana;* ***Naye atamlipa kwa tendo lake jema."*** (Mithali 19:17)

*"Lakini nasema neno hili, Apandaye haba atavuna haba;* ***apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu.*** *Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu."* (2 Wakorintho 9:6-8) Ni vema kusoma kutoka fungu la 6 hadi fungu la 15.

Hizi hapa pia nukuu mbili kutoka kwa E.G. White kuhusu mada ya utumishi:

"Wale wanaokataa **fursa ya ushirika pamoja na Kristo katika utumishi,** wanakataa mafunzo pekee yanayokuza ukamilifu kwa ajili ya kushiriki pamoja Naye katika utukufu Wake." (*Education,* uk. 264.3)

"Kweli ambayo haitekelezwi maishani, haikuzwi, hupoteza uwezo wake uletao uhai, dhamira safi huleta uponyaji. Baraka yake inaweza kudumishwa tu kadiri inavyoshirikishwa kwa wengine." (*The Ministry of Healing*, uk. 148.4)

## Kusimama bila kusogea ni Kupiga Hatua Kurudi Nyuma

**Kwa nini** washiriki wengi wa kanisa **hawana uzoefu ukuaji wowote wa kiroho? Kwa nini imani** ya wengi kwa kweli **hupungua** kadiri muda uendavyo? **Kwa nini** wengi **hawafurahii** tena **usomaji wa Neno la Mungu**? Na **kwa nini** wengi hawana tena **moto wa upendo wa kwanza**? Kuna jibu moja tu kwangu: Kwa sababu wanaishi kama Wakristo wa mwilini. **Kwa sababu wamepuuza uhusiano wao pamoja na Yesu**, matokeo hasa yote yaliyotajwa hapo juu hujitokeza! Uhusiano wa upendo wa kina pamoja na Yesu hutulinda dhidi ya ubinafsi na hutuhamasisha kuwatumikia wengine. Matokeo yake, sisi nasi tunabarikiwa!

Kimsingi, haimaanishi kwamba sisi ni hai kadiri iwezekanavyo kanisani, bali kwamba **matendo yetu yamejawa Roho**. Ili hilo liweze kutokea, Yesu hana budi kuishi mioyoni mwetu kupitia.

Kinachosikitisha, Wakristo hawajalielewa hili kikamilifu; wanadhani lazima wawe hai kanisani ili Mungu awakubali kama watoto Wake awali ya yote. Lakini ni kinyume chake hasa: **Mtoto halisi wa Mungu, hutoka na upendo na shukrani zake Kwake, hufurahia kufanya kitu fulani.** Wakati huohuo, maisha pamoja na Roho Mtakatifu yatamhamasisha pia. Mungu analo jukumu ama shughuli nyingi kwa ajili ya kila mtu. Tunapomwomba atutumie katika huduma Yake, ndipo atatuonesha jukumu ama majukumu yetu!

Ni muhimu kwamba aichunguze nafsi yake: Je mimi ni Mkristo aliyezaliwa mara ya pili? Hivi niko “ndani ya Kristo Yesu”? Ikiwa ndiyo, basi tutajua kwamba Yesu Kristo, tunayesalimisha maisha yetu Kwake kila asubuhi, anaishi ndani yetu na anaweza kutenda kazi kupitia sisi.

Lakini kama tumejibu hapa kwenye swali hilo hapo juu, basi tunapaswa mara moja tumwendee Yesu na kumwomba aingie maishani mwetu kupitia Roho Mtakatifu! Tumia muda wa kutosha kila siku kwa ajili ya kudumisha uhusiano wake pamoja na Yesu na Roho Mtakatifu! Kwa jinsi hiyo tunapokea mtazamo na mwenendo sahihi, tunaohitaji ili kudumisha upendo wetu wa

kwanza au kuurejesha, kufurahia kulisoma Neno la Mungu na kukua kiroho.

"Kuishi kwa ajili ya nafsi ni kuangamia. Tamaa, shauku ya kupata faida kwa ajili ya nafsi, huiondolewa nafsi uhai. Ni roho ya Shetani kupata, kuvutia kwenye nafsi. Ni roho ya Kristo kutoa, kujitoa kafara nafsi kwa ajili ya wengine. … Hivyo basi Yesu anasema, 'Angalieni, jilindeni na choyo, maana uzima wa mtu haumo katika wingi wa vitu vyake alivyo navyo.'" (E.G. White, *Christ's Object Lessons,* uk. 259.1-2**)**

Siku ya 8

## Sheria ya Utumishi – Suala Nyeti

Mara nyingi huwa hatutambui kwamba kauli katika kichwa hapo juu hakika ni ya kweli. E.G. White anafafanua:

"Vitu vyote mbinguni na duniani hutangaza kwamba sheria kuu ya maisha ni sheria ya utumishi. Baba wa milele anahudumia maisha ya kila kiumbe hai. Kristo alikuja duniani *"kama atumikaye."* (Luka 22:27) Malaika ni *"roho watumikao, wakitumwa kuwa hudumu wale watakaourithi wokovu."* (Waebrania 1:14) **Sheria ileile ya utumishi** imeandikwa juu ya vitu vyote kwenye asili. ... Kadiri kila kitu katika asili kinavyohudumia hivyo uhai mwingine ulimwenguni, chenyewe pia hujipatia mahitaji yake. *"Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa"* (Luka 6:38), ni somo ambalo limeandikwa si kwa uhafifu kwenye ulimwengu asili kuliko ilivyo katika kurasa ya Maandiko Matakatifu." (E.G. White, *Education,* uk. 103.2-3, egwwritings.org)

Baada ya maelezo haya, ningependa kuwasilisha mfano wa maisha ya kila siku, ambao hudhihirisha **sheria ya utumishi:**

Mtendakazi kwenye karakana ya seremala alitengeneza samani. Alipokea mshahara wa kila mwezi kutoka kwenye uongozi wa kampuni kwa ajili ya kazi yake. Mtendakazi huyu **"huitumikia"** kampuni hiyo, lakini pia **"anatunukiwa."** Kuna kutoa na kupokea katika pande zote mbili, kwa sababu: Ni kweli kwamba uongozi wa kampuni humpatia mtendakazi huyu fedha, kwa maneno mengine **"wanamtumikia"** yeye, lakini kwa upande mwingine, wao nao wanapokea **"tunu"** katika namna ya samani.

Hatimaye, siyo tu kwamba mtendakazi huyu anatunukiwa fedha, bali pia hupata uzoefu ridhaa na furaha ya kazi aliyoifanya vema. Na mtendakazi makini daima atajitahidi kufanya kazi bora kadiri iwezekanavyo. (Andiko katika Wakolosai 3:17 linahusika hasa kwa **mtendakazi Mkristo anayethamani mambo ya kiroho**: *"Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo,* ***fanyeni*** *yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa Yeye."* Na baada ya muda, maarifa ya mtendakazi huyu kuhusu uundaji wa samani utaendelea kukua na uwezo wake pia utaboreka.

Uongozi wa kampuni nao hupata uzoefu ridha na furaha na mapato yapatikanayo wanapouza samani zilizote-ngenezwa. Nao pia baada ya muda wakuza maarifa yao kuhusu utengenezaji wa samani na kuboresha mbinu zao za mauzo.

## Utumishi – Furaha au Mzigo?

Watu wengi bila shaka kabisa wanahusisha neno *utumishi* na neno *mzigo* kuliko *furaha*. Kwa nini hivyo? Ni bayana anahusiana na uzoefu binafsi uliotokana na utumishi.

Huu hapa mtazamo wa kuvutia:

"**Utumishi** wa Kristo siyo **wakuburuza nafsi iliyojisalimisha kikamilifu**.... Halitakuwa jukumu lisilopendeza kuwa mtii kwa mapenzi ya Mungu **pale tunaposalimisha nafsi zetu kikamilifu ili kuongozwa na Roho Wake**." (E.G. White, *Testimony Treasures, vol. 1,* uk. 357.2,3)

Hivyo, hutegemeana na uhusiano wetu pamoja na Kristo, juu ya namna tunavyotathmini utumishi. Na tena pia, mtazamo wetu wa ndani hutegemea endapo tumejazwa Roho Mtakatifu. (Warumi 8:5) Ni kwa kuendelea tu daima kumpokea Roho Mtakatifu ndipo Yesu anaweza kuishi dahari mioyoni mwetu. Yesu alisema Mwenyewe: *"Kaeni ndani Yangu, Nani ndani yenu."* (Yohana 15:4) Na anapokaa ndani yetu, ndipo tutaweza kutumika bila juhudi na hata hilo litatupatia furaha!

Ndiyo maana ni muhimu sana kuchukua hatua mbili muhimu kila siku:

- ▶ Kila asubuhi omba kwa imani (hususan kwa ahadi) kwamba Mungu akujaze Roho Mtakatifu. Na

- mwambie Yesu kwamba unaweka maisha yako yote chini ya mamlaka Yake. (The Desire of Ages, uk. 676)

Mungu anapotutumia kwa ajili ya utumishi Wake, anapotuongoza, ndipo atatupatia majukumu **aliyotuandalia.** Lakini siyo jukumu tu, lakini wakati huohuo uwezo unaohitajika!

(Mapendekezo ya usomaji: *Njia Salama*, sura ya 9: "Kazi na Maisha").

## Utumishi – Chini ya nira ya Yesu

Yesu alisema: *"Jitieni nira Yangu, mjifunze Kwangu; kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu."* (Mathayo 11:29)

Kwanza, hebu tubainishe neno "nira." Lina maana gani? Nira huwaunganisha maksai(ng'ombe wa kulima) wawili ili waweze kufanya kazi pamoja wakivuta mkokoteni ama plau. Yesu anataka kutuhimiza kwa taswira ya kufanya kazi kwa ukaribu wa pamoja Naye. Sisi ni kana kwamba tumefungamanishwa na Yesu. Anataka kutuunganisha kwa ajili ya utumishi wa pamoja. Hii ni fursa ilioje! Anatualika tujifunze kutoka Kwake, kwa sababu Yeye ndiye mahiri. Katika fungu la 30 yapo maneno haya yaletayo tumaini: *"kwa maana nira Yangu ni laini, na mzigo Wangu ni mwepesi.*" Fungu hili huniambia kwamba Yesu hatatuelemea "tunapojitia nira" pamoja Naye. Katika mchakato huo, Yeye hubeba wajibu, anabeba mzigo mkubwa zaidi wa kazi husika. Na kwa vile hilo liko hivyo, ndiposa anaweza kusema kwamba mzigo tunaopaswa kuubeba ni mwepesi.

## Utumishi na Kushuhudia

Morris Venden anaelezea tofauti kati ya *utumishi* na *kushuhudia:*

"Neno **utumishi** huelezea **mwenendo** wetu**,** wakati ambapo neno **kushuhudia** linahusiana na **vile tulivyo** na **yale tusemayo**. Kusudi la utumishi wetu kwa watu wengine ni kuwasaidia maishani mwao, ili wawe tayari kupokea habari njema za injili. Kwa utumishi wetu tunaweza kushuhudia kifanisi juu ya upendo wa Mungu kupitia silika na mwenendo wetu, na kusimulia

kuhusu Rafiki na Mwokozi wa pekee ajabu ambaye tumempata katika Yesu."

## Utumishi Maalumu: Ushuhudiaji

Katika Marko 5:1-20 kuna kisa cha kuvutia. Yesu alimponya mtu aliyepagawa pepo. Baada ya kuwekwa huru, mtu huyo alitaka kuendelea kukaa pamoja naYesu na wanafunzi Wake. Lakini Yesu hakumruhusu, Naye akampatia jukumu maalumu: *"...Enenda zako nyumbani kwako, kwa watu wa kwenu, kawahubiri ni mambo gani makuu aliyokutendea Bwana, na jinsi alivyokurehemu."* (Fungu la 19) Je mtu huyu aliyeponywa alifanya nini? *"Akaenda zake, akaanza kuhubiri katika Dekapoli, ni mambo gani makuu Yesu aliyomtendea; watu wote wakastaajabu."* (Fungu la 20)

E.G. White anafafanua (kwa mujibu wa Mathayo 8:28-34 walikuwepo watu wawili):

"... walisafiri kupitia Dekapoli, kila mahali wakitangaza uwezo Wake wa kuokoa, na kuelezea jinsi gani alikuwa amewaweka huru kwa kuwatoa pepo wachafu. **Kwa kuifanya kazi hii wangeweza kupokea baraka kubwa zaidi kuliko pale ambapo, kwa ajili ya manufaa yao wenyewe, wangebaki katika uwepo Wake.** Ni katika kufanya kazi ili kueneza habari njema za wokovu ndipo tunaletwa karibu na Mwokozi." (*The Desire of Ages*, uk. 339.4)

Watu hawa walioponywa walitenda jukumu lao kwa furaha. Kwa nini haikuwa mzigo kwao? Kwa sababu mioyo yao ilikuwa imejaa upendo na shukrani kwa Yesu. Kama kauli isemavyo: "Maana kinywa hunena yale ambayo moyo umeyajaza." Na siyo tu kwamba waliziambia familia zao kile ambacho Yesu alikuwa amewafanyia, lakini pia waliisimulia jamii yote ya ujirani wao. Kwa nini? Tunaweza kulipata jibu zuri kwenye kitabu kiitwacho *Njia Salama*: "...ukweli uokoao na utakasao hauwezi kufungiwa moyoni mwake. Iwapo tumevikwa haki ya Kristo na tumejazwa furaha ya Roho Wake akaaye ndani yetu, hatutaweza kutulia. **Iwapo tumeonja na kuona kwamba Bwana yu mwema, tutakuwa na kitu fulani cha kusimulia.**" (E.G. White, *Steps to Christ,* uk. 78.2)

Ndiyo, watu hawa walioponywa walikuwa na mengi ya kusimulia! Walikuwa wamejawa furaha ya kukombolewa kwao. Nao walitaka **kuelezea furaha yao kwa wengi kadiri iwezekanavyo.** Kwa jinsi hiyo walipata uzoefu wa nyongeza ya baraka: "...kwa sababu furaha tuwapatiayo watu wengine huurudia moyo wetu wenyewe." (Mithali ya Kijerumani)

## Watendakazi pamoja na Mungu – Watendakazi pamoja na Malaika

Malaika nao hushirikia kwenye utumishi huu:

"Wote wanaojihusisha katika huduma ni mkono wa msaada wa Mungu. **Wao ni watendakazi pamoja na malaika;** kwa usahihi zaidi, wao ni mawakala wa kibinadamu ambao malaika huwatumia ili kutimiza utume wao. Malaika hunena kupitia sauti zao, na hutenda kazi kupitia mikono yao. Na watendakazi wanadamu, kwa kushirikiana na mawakala wa kimbingu, wana manufaa ya elimu na uzoefu wako. Je kama njia ya elimu, ni "kozi gani ya chuo" inaweza kulingana na hii?" (E.G. White, *Education,* uk. 271.1)

Ama mama anawafundisha watoto wake katika jina la Yesu au endapo mtu fulani anaendesha mikutano ya injili, jambo la muhimu ni kwamba Kristo anatenda kazi kupitia Roho Mtakatifu ndani yetu.

Siku ya 9

## Utumishi ni Sehemu Muhimu ya Maandalizi Yetu Kwa Ajili ya Ujio wa Pili

Yesu alituachia taarifa ya thamani kuhusu Ujio Wake wa Pili katika Mathayo 24 na 25. Kwanza, alizungumzia ishara na kisha kuhusu namna ya ujio Wake. Japo Yesu alitupatia ishara za ujio Wake, bado litakuwa tukio la kushtukiza, kama mwizi wakati wa usiku. (Mathayo 24:43-44) Kwa sababu hali ndivyo ilivyo, Yesu alisema: ***"Kesheni basi; kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu."*** (Mathayo 24:42) Baada ya hapo Yesu alifafanua alichomaanisha kuhusu kukesha na kujiandaa, alipotumia mifano tofauti. Hebu tuiangalie mifano hiyo.

## Mielekeo Miwili ya Tabia kwa Wakili (Mathayo 24:45-51):

Hebu tuchukulie kwamba wakili anapewa jukumu la kuwahudumia waajiriwa wengine wakati mwajiri wake akiwa hayupo. Mwajiri anaporejea na kumkuta wakili **akiifanya kazi yake kwa bidii**, basi atampatia wajibu mkubwa zaidi mtu huyu anayetumainika.

Lakini kama wakili **hakuwa mtu wa kutumainika**, naye akadhani anao muda mwingi kabla mwajiri wake hajarejea na hivyo akapanga karamu nyingi na kujishughulisha katika unywaji badala ya kufanya kazi, basi ujio wa mwajiri wake utamshtukiza kabisa. Ndipo mwajiri huyo atamwadhibu wakili wake.

**Yesu anadhihirisha hapa kwamba ni muhimu kutenda majukumu ambayo Mungu ametupatia. Kwa jinsi hii, tunakuwa tunajiandaa kwa ujio Wake.**

## Makundi Mawili ya Wanawali (Mathayo 25:1-13):

Wanawali kumi walikuwa wakimngojea bwana arusi. Walikuwa na taa za mafuta, kwa vile ilikuwa giza. Watano miongoni mwao walikuwa na **busara** nao walikuwa na **mafuta ya ziada** kwa ajili ya taa zao. Watano wengine walikuwa **wapumbavu; hawakuwa wamechukua masarafu ya mafuta ya ziada**. Ujio wa bwana arusi ulichelewa zaidi ya vile walivyotegemea wote. Wote wakachoka na kusinzia. Wakati bwana arusi alipofika ghafla panapo usiku wa manane, wanawali watano wapumbavu hawakuwa mafuta ili kudumisha taa zao zikiwaka. Wanawali wenye busara wakaambatana na bwana arusi hadi kwenye ukumbi wa sherehe, ilhali wengine walikuwa wakingali wanajaribu kujipatia mafuta. Baadaye, walipobisha hodi mlangoni, hawakuruhusiwa tena kuingia.

**Yesu anadhihirisha hapa kwamba tunahitaji kujazwa Roho Mtakatifu kikamilifu ili tuweze kujiandaa vema kwa ajili ya ujio Wake. Wale "wasiokuwa na masarufu ya ziada" walipotea.**

## Kusimamia Fedha Iliyodhaminiwa (Mathayo 25:14-30):

Mfanyabiashara alitaka kusafiri, akawaita pamoja wajiriwa wake ili awakabidhi mali zake. Akiwa hayuko, kila mtu angepaswa kusimamia fedha husika aliyopewa. Waajiriwa wawili walitumia fedha kwa uangalifu na bidii, lakini mwajiriwa mmoja hakufanyia chochote kabisa fedha hizo. Mfanyabiashara huyo aliporejea, aliwatunuku waajiriwa wawili wenye bidii, ila akamwadhibu mvivu.

**Yesu anadhihirisha hapa kwamba tukiwa na mtazamo sahihi kwa Mungu tunapaswa kutumia karama zetu za kiroho pamoja na uwezo wetu wa asili katika kumtumikia Yeye. Yeyote afanyaye hivi hataweza kupotea!**

Nukuu kutoka kwa E.G. White kuhusu hili: "Talanta ambazo Kristo huzikasimisha kwenye kanisa Lake huwakilisha hasa karama na baraka zinazoakifiwa na Roho Mtakatifu. … Zinahusisha karama na vipawa vyote, ama ni vya kuzaliwa navyo au vile vya kujifunza, vya asili au vya kiroho. Vyote hivi havina budi kutumiwa katika huduma ya Kristo." (*Christ's Object Lessons*, uk. 327.1, 328.2)

## Hukumu ya Mwisho (Mathayo 25:31-46):

Yesu ajapo tena, atawagawa watu katika makundi mawili, kama ambavyo mchungaji huwagawa kondoo na mbuzi. Anawaweka kondoo **kulia** Kwake. Hawa **ndio wale "waliowatumikia" wanadamu wenzao,** walioonesha upendo wa kindugu kivitendo. Anawaweka wengine **kushoto** Kwake. Hawa **ndio wale ambao hawajawasaidia wengine,** mahali ambapo msaada ulikuwa unahitajika.

Yesu alisema katika fungu la 40: *"Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu Zangu walio wadogo, mlinitendea Mimi."*

**Yesu anatuonesha hapa: wafuasi Wake wa kweli kwa asili hutenda mema tu kwa ajili ya wanadamu wenzao. Imekuwa "asili" yao. Mara nyingi huwa hatatambui hili kabisa!**

Hivi haishangazi kwamba utumishi uliojawa Roho unajumu-

isha kukesha kwetu na maandalizi yetu kwa ajili Ujio wa Pili wa Yesu?

Kauli ya Yesu – kwamba tunapowatumikia wengine, tunamfanyia Yeye – inapaswa kuleta badiliko chanya katika mtazamo wetu juu ya huduma na hivyo uhusiano wetu pamoja na wengine. Hebu fikiri kwamba ungeweza kumwalika Yesu kwenye chakula au kumtembelea hospitalini au gerezani. Yesu alisema tunafanya hilo hasa pale tunapoonesha juhudi hii ya upendo kwa watu walio katika ujirani wetu. Ni fursa ya kustaajabisha ilioje tuliyo nayo ili kumwonesha Yesu upendo wetu! (Mwongozo wa Kujifunza Biblia, robo ya 3, 2019, somo la Agosti 22)

## Je tunalazimika (kuistahikimu) kupokea ujira wa mbingu?

**HAPANA!!!** Tunaokolewa kwa neema: *"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu."* (Waefeso 2:8-9)

Andiko hili husema wazi kwamba wokovu wetu hufanyikia upande wa Mungu kupitia neema na upande wetu kupitia imani. Paulo aliwaandikia Waefeso (kama ilivyonukuliwa hapo juu) kwamba waliokolewa kwa neema kupitia imani. **Tayari wokovu umefanyika: tuliokolewa mara ile tuliposalimisha nafsi zetu kwa Yesu kikamilifu.** Kwa mujibu wa Biblia, imani humaanisha (kudhamani)kukabidhi nafsi zetu. **Tunapodumu katika uhusiano huu wa dhamani, basi tunasalia tukiwa tumeokoka.** Na shauku yetu ya kutumika ni tunda – matokeo ya wokovu wetu.

Hebu tuangalie pia andiko katika Warumi 8:24: *"Maana tuliokolewa katika tumaini hili…"* (NKJV) Hii humaanisha nini? Hakika tumeokolewa, hata hivyo, Mungu hajatufunga Kwake. Tunaweza kujiondoa kwenye muunganiko huu wakati wowote. Biblia inasema kwamba mara tu kabla ya ujio wa pili, utakuwepo "uchunguzi" mbinguni ili kuona nani ana uhusiano pamoja na Baba Yake wa mbinguni na nani asiyekuwa nao (angalia Mathayo 22:1-14).

## Muhtasari wa kile ambacho Utumishi hutekeleza

Wanafunzi wa Kristo walijazwa Roho na kujisasafisha hupata kupitia utumishi wao furaha na nguvu, uwezo wao halimali na kiakili na kiroho huongezeka na tabia yao hujengwa kwa namna chanya kadiri ya mapenzi ya Mungu na kwa ajili ya maslahi yao bora. Hatua kwa hatua ubinafsi hupoteza nguvu yake. Maisha yangu huwa kivutio kwa watu wengine. Wanaweza kutambua mtindo wa maisha tofauti na wenye mvuto. Hii hujenga mazingira mazuri kwa ajili ya ushuhudiaji kuhusu kile ambacho Yesu amekifanya kwa ajili yangu na ndani yangu. Utumishi wangu huwasaidia wengine ili waweze kupata uzoefu wa maboresho ya maisha au ahueni. Anafurahia uzoefu Wake pamoja nami. Huipitisha kwenda kwa wengine na mara nyingi ongezeko mara dufu ufanyika. Nami nakuwa nimelindwa dhidi ya kudhoofika au kuipoteza imani yangu. Na nafasi kwamba mpokeaji atafungua moyo wake kwa ajili ya injili itaongezeka.

Sasa tunataka kuangalia mtazamo unaoweza kutuletea ahueni kuu katika maswali mengi maishani. Unahusiana na utayari wetu kumfuata Bwana Yesu katika kila kitu, ambayo ni pamoja na kutumika, kutoa, kusaidia na kubariki. Tukiwa na Mungu, haijalishi talanta (kutoa, kutumika, kusaidia) ni kubwa kiasi gani, badala yake hutegemea utayari wetu. Anapendezwa na kila anachoweza kutoa mtu, na wala hatudai kile tusichokuwa nacho. (2 Wakorintho 8:12)

Siku ya 10

## Utayari Wetu Una Maana kwa Mungu – Anataka Kutukirimia Kwayo

**Kwa nini ni muhimu sana kwetu kuwa tayari kufanya mapenzi ya Mungu?** Rahisi sana, kwa vile tungekabiliwa na hasara kubwa bila utayari huu. Tunahitaji kuliangalia hili kwa kina zaidi.

Kama ambavyo imetajwa tayari, kwa sababu ya asili yetu kibinadamu ya dhambi mara nyingi huwa hatuko radhi na hatuwezi kwa nguvu zetu wenyewe kufanya mapenzi ya Mungu.

Zingatia jambo lifuatalo: **Mungu anatupenda** kwa upendo usio na ubinafsi. **Anatutakia mambo bora. Anajua tabia yetu** na **hali yetu ya sasa.** Kwa vile anajua yote, **pia anajua kitakachotokea baadaye.** Tunapolizingatia hili, bila shaka ni jambo la maana sana wakati huohuo ni jambo lenye manufaa zaidi kufuata mapenzi Yake huku tukitegemea uwezo Wake. Yesu anasema katika Yohana 10:10: *"Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele."*

Anataka tupite kwenye njia bora kabisa – hususan iliyo-andaliwa vema kwa ajili ya silika yetu na wakati wa sasa. Ili aweze kutuongoza, lazima tuwe radhi. **Tunapoomba roho ya utayari, basi Yeye ataumba utayari ndani yetu. Hufanya roho yetu iwe radhi.** Kwa vile utu wa ndani hufanywa upya (huhawilinishwa) siku kwa siku (2 Wakorintho 4:16), halikadhila ni muhimu kila siku kuomba kukirimiwa roho ya utayari. Tunaweza kuomba kama ifuatavyo:

**"Bwana, nifanye niwe radhi kuwa tayari kwa ajili ya kila kitu unachotaka."**

Mungu anapendezwa sana tunapomruhusu atuongoze. Kwa Mungu, ni kama tu wazazi, wanaokuwa na furaha pale mtoto wao akitii kwa hiari.

## Kijumla, nini maana ya uradhi na jinsi gani hujidhihirisha?

**Uradhi** ni **mwenendo wa ndani wa uelekevu.** Ni mtazamo unaohitaji roho ya unyenyekevu na inayofundishika.

Nataka nisimulie kisa cha **mfano wa kukosekana kwa uradhi** wa kujifunza: Kinamhusu Dkt. Semmelweis. Mnamo mwaka 1840, Vienna ilikuwa kituo muhimu cha utabibu. Lakini kwenye wodi ya uzazi katika kliniki cha chuo, mwanamke mmoja kati ya sita, aliyemaliza kujifungua punde, alikufa. Mnamo mwaka 1840 wakati kijani daktari wa utabibu, Dkt. Semmelweis, alipochukua uongozi wa wodi hiyo aligundua hivyo hasa kwamba wanawake huao walikufa, ambao punde tu walikuwa wamechunguzwa na daktari ambaye ndipo tu ametoka kufanya otopsi au kumchunguza maiti. Katika kipindi hicho madaktari hawakunawa mikono yao baada ya kumchunguza maiti. Hivyo, Dkt. Semmelweis

kwanza akaamuru kwamba mikono ingepaswa kuoshwa baada ya kila otopsi na kisha baadaye anapomaliza kumchunguza kila mgonjwa. Matokeo yalikuwa na kustaajabisha sana: Kulikuwa na maboresho mara kumi 14! Kwa nadra mwanamke yeyote alikufa tena. **Lakini maprofesa na madaktari wa tiba walikuwa na kiburi kiasi cha kushindwa kukiri mafanikio haya!** Palitokea dhoruba ya maandamano kupinga hatua ya kunawa mikono "isiyo na mantiki." Mkataba wa ajira ya Dkt. Semmelweis haukuongezwa halafu sinki alizokuwa ameamuru zifungwe, zikavunjwa. Matokeo yake, kiwango cha vifo vya wanawake kikarudi vilevile kama ilivyokuwa awali. Dkt. Semmelweis aliondoka Vienna kwenda Budapest. Akiwa huko alirudia utaratibu wa mbinu yake. Lakini tena, watendakazi wenzake wakampinga**.**

## Bila Hekima ya Kiungu, Mara Zote Hakuna Uradhi Uliopo

Uzoefu wa Dkt. Semmelweis inaonesha ukweli kwamba tunaweza kutenda kwa upambavu kabisa kwa sababu ya kiburi na dharau, hata kama tuna uwezo mkubwa wa akili. Upumbavu ni kinyume cha hekima. Siku hizi, umuhimu mwingi huwekwa kwenye akili ya mtu na uwezo wake kufikiria. Neno hekima kwa kiasi fulani limesukumiwa mbali; lakini kwenye neno la Mungu, umuhimu mkubwa unafungamanishwa na hekima (angalia Mithali, sura ya 8 na 9). Biblia inasema kitu fulani cha kuvutia katika Zaburi 111:10: **"Kumcha Bwana ndio mwanzo wa hekima, Wote wafanyao hayo wana akili njema."** Hii huzungumzia hekima ya kiungu hapa. Na mtu fulani, ambaye maisha yake yanaongozwa na Mungu, yaani mtu mcha-Mungu, huonesha uelewa mzuri – angalau hilo ndilo lisemalo andiko hapo juu. Tungeweza kusema vivyo hivyo hasa kwamba mtu fulani anayeishi pamoja na Mungu anaenenda kwa akili! Hiyo ni kinyume kabisa na namna ambavyo watu wengi wanaenenda leo. Watu wa kisasa hudhani kwamba kuachana na Mungu na kuiacha dini ni uthibitisho wa uwezo wao mkubwa wa akili. Ghiliba(Kujidanganya) ilioje! Hufikia upeo katika Warumi 1:22: "Ilhali wakistamini kuwa wenye hekima, wakawa wapumbavu." (NKJV)

Hekima ya kibinadamu – pia huitwa falsafa – kama zilivyo kazi zote za wanadamu, ina mapungufu. Tunaweza kuiona hiyo tu katika ukweli kwamba wanafalsafa mahiri hupingana wao kwa wao katika dhana zao juu ya maana ya maisha, asili ya ulimwengu na nafasi ya wanadamu duniani. (More: Eta Linnemann, *Wissenschaft oder Meinung?* – Hänssler 1986)

Katika Biblia Mungu anasema yafuatayo kuhusu hekima ya mwanadamu: *"Nitaiharibu hekima yao wenye hekima; na akili zao wenye akili nitazipinga. Yu wapi mwenye hekima? Yu wapi mwalimu wa sheria? Yu wapi mwanafalsafa wa zama hizi? Je Mungu hakuifanya hekima ya dunia kuwa upumbavu?"* (1 Wakorintho 1:19-20 NIV) Inavutia kwamba andiko hili hutaja pia "walimu wa sheria." Leo tunawaita wanateolojia au wachungaji. Inawezekana kwamba wanafundisha *tu* kwa msingi wa akili yao kibinadamu na kwa sababu ya hii Mungu anawaita *wapumbavu*. Au wanapoichunguza Biblia kwa ufahamu wao wa kibinadamu, bila kuongozwa na Roho Mtakatifu, ndipo utafiti wanaorithisha una uwezekano pia kwamba ni wenye kutia mashaka.

Katika hitimisho: **Ni mtu yule tu, bila kujali anajihusisha na dini au la, aishiye maisha yaliyojawa Roho Mtakatifu ndiye mwenye hekima. Na mtu mwenye hekima tu ndiye atakuwa radhi kufanya mapenzi ya Mungu!**

## Kwa namna gani uradhi hujidhihirisha wenyewe au kwa namna gani roho iliyo radhi hujidhihirisha yenyewe katika maeneo ya kiroho?

Yesu alipoishi duniani hapa, alionesha uradhi huu. Alitufundisha kuomba katika Sala ya Bwana: *"mapenzi Yako yatimizwe."* Yeye Mwenyewe aliishi kwa mujibu wa kanuni hii pia. Hata wakati wa hali ngumu **kwenye Bustani ya Gethsemane, alionesha roho ya uradhi.** Mara tatu aliomba:

*"...walakini **si kama nitakavyo Mimi, bali kama utakavyo Wewe.**"* (Mathayo 26:39) Waumini huko Berea ni mfano wa uradhi wa jinsi hii. Walisikiliza mahubiri ya injili kutoka kwa Paulo wakiwa na roho ya uelekevu. Tunasoma katika Matendo 17:11 NKJV: *"Hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa*

*Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa* ***utayari wote****, wakayachunguza Maandiko kila siku, waone kwamba mambo haya ndivyo yalivyo."*

Tunapokuwa na roho ya uradhi kwa Mungu na neno Lake, ndipo tutachunguza kwa makini kila kitu tusomacho, tusikiacho na tuonacho. Taarifa hiyo inaposhahibiana na mapenzi ya Mungu, ndipo tunaweza kuikubali na kuitekeleza.

## Nini kinachoweza kumzuia mtu asiwe na mtazamo wa uradhi kwa Mungu?

Warumi 8:5 (NIV) inasema: ***"Wale waishio kwa kuufuata mwili, nia zao zimeelekezwa katika yale ambayo mwili huyatamani;*** *bali wale waishio kwa kumfuata Roho, nia zao zimeelekezwa katika yale ambayo Roho huyatamani."*

Leo tunazungumzia kuratibiwa kwa ajili ya hili au hilo. Matendo ya ***mtu wa asili na Mkristo wa mwilini*** huamuliwa kwa ubinafsi wao. Kiburi, dharau pamoja na uhakinifu kwenye ushirikina huweza kutuzuia tusiwe waelekevu kwa Mungu. Watu hawa hawatakuwa na mtazamo wa uradhi kwa Mungu wala hawatakubali mawazo mapya kutoka kwenye neno Lake.

Kwa upande mwingine, kila **Mkristo *wa kiroho*** kwa msaada wa Roho Mtakatifu atakuwa na mtazamo elekevu. Atazingatia kile kisemacho katika Warumi 12:2 GNT: *"Wala msifuatishe kanuni za dunia hii, bali mruhusuni Mungu awageuze utu wenu wa ndani kwa kufanya badiliko kamili la nia yenu. Ndipo mtaweza kujua mapenzi ya Mungu - yaliyo mema, yampendezayo, na makamilifu."*

## Hekima na Uradhi kupitia Roho Mtakatifu

Roho Mtakatifu ndiye atufanyaye tuwe na hekima na uradhi wa kutumika. Katika muktadha huu nataka kunukuu Matendo 6:3: *"Basi ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema,* ***wenye kujawa na Roho, na hekima****, ili tuwaweke juu ya jambo hili."* Huu ulikuwa uchaguzi wa kwanza ndani ya kanisa la Agano Jipya – uchaguzi wa mashemasi. Nini kilikuwa kigezo cha uamuzi kwenye uchaguzi huu? Walipaswa kuwa na sifa njema,

walipaswa kuwa na hekima na kujazwa Roho Mtakatifu. Na baada ya kile ambacho tumejadili, tunaelewa kwamba ni watu wa namna hiyo tu ndio wanaweza kutumika kwa moyo wote.

Kwa vile kila mmoja wetu anaitwa kwenye utumishi kwa mujibu wa Agano Jipya, kimawazo tunapaswa kuwa wenye hekima na kujazwa Roho Mtakatifu. Biblia hutupatia ushauri mzuri endapo tutagundua kwamba tunakosa hekima. *"Endapo yeyote miongoni mwenu anapungukiwa* ***hekima****, hana budi* ***kumwomba Mungu, atoaye kwa ukarimu*** *bila kutafuta dosari,* ***naye atapewa.****"* (Yakobo 1:5 NIV)

Nimepata uzoefu tena na tena ukweli wa maneno haya. Mungu anaahidi kujibu maombi yetu ya kukirimwa hekima. Jibu linaweza kuwa na namna mbalimbali: Wakati fulani napata uzoefu kwamba mara tu baada ya maombi yangu, ufumbuzi wa tatizo fulani hujitokeza akilini mwangu. Lakini mara nyingi huwa napata utambuzi ambao sikuwa nao hadi baada ya kuomba. Lakini nilipoendelea na kazi yangu katika imani kamili, mwishoni nilishangaa jinsi gani Bwana alivyokuwa amenisaidia – takriban bila kutambua. Kwa kweli Mungu anapenda kusaidia! Anataka kazi yetu, bila kujali ni ya namna gani, ilete matokea mazuri.

## Wale ambao hutenda mapenzi ya Mungu kwa hiari, watabarikiwa maridhawa!

Ninapoelewa kwamba Mungu **daima** anazingatia maslahi yangu bora mawazoni ikiwa ni pamoja na umilele, ndipo nitafanya mapenzi Yake kwa furaha. Mtu fulani anapotaka kututendea jambo fulani jema kutokana na nia sifa, kikanuni, huwa hatuna kipingamizi, sivyo? Na wale ambao mara nyingi wamedhahimu jinsi gani amewatendea mema, watajikabidhi kwa furaha chini ya uongozi wa Mungu. Ndiyo sababu Daudi aliweza kusema: *"Kuyafanya mapenzi Yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; naam, sheria Yako imo moyoni mwangu."* (Zaburi 40:8)

Katika hatua hii, ningependa kusisitiza tena kwamba Roho Mtakatifu ndiye aumbaye ndani yetu uradhi huu wa kutaka kuyafuata mapito ya Mungu. Na tunapomwomba Mungu kila

asubuhi atuongoze kwa Roho Wake, ndipo tutapata uzoefu wa mambo ya kushangaza! Kwa mfano, Dwight Nelson aliweza kupata uzoefu ufwatao baada ya kuanza kuomba **kila siku** kwa ajili ya Roho Mtakatifu:

"Mahubiri yangu yamepata uhuru na nguvu mpya. Uongozi wangu pamoja na timu yangu na watu wangu umeinuliwa kwenye kiwango kingine. Ghafla bilakupangwa (kile ambacho mwandishi mmoja hukiita uhusiano wa dhati) kunakuwa na ongezeko – ni kana kwamba mtu fulani anaratibu nyakati zangu za mchana na usiku, matukio yangu "fursa" ya mikutano na baruapepe na mazungumzo. Ni kana kwamba Roho Mtakatifu anaongoza binafsi saa zangu za kuamka (hata nyakati za kulala). Kwa kweli, nimefikia hatua ya kumjua Yeye kama Rafiki mpendwa binafsi na wa kweli hasa."

*Dwight Nelson ni mchungaji kiongozi wa Kanisa la Kumbukumbu ya Waasisi katika kampasi ya Chuo Kikuu cha Andrews huko Berrien Springs, Michigan, Marekani. (Nukuu kutoka Barua ya Sala Na. 143, Aprili 22, 2018 Huduma ya Maombi ya Konferensi Kuu)*

*Kila siku hunipatia fursa mpya ya uzoefu mpya wa mapenzi ya Mungu kwa ajili ya maisha yangu na kuongozwa na Roho Mtakatifu (2 Wakorintho 4:16). Uradhi niliokuwa nao jana wa kumfuata yeye siyo rahini kwamba nitakuwa mtii leo vilevile. Kwa hiyo, hebu tuombe* ***kila siku*** *kwamba tuweze kuwa radhi au tuendelee kuwa radhi kuyafanya mapenzi Yake:* ***"Baba uliye mbinguni, tafadhali nifanye niwe radhi kutenda kila kitu upendacho. Tafadhali, teka nyara fikra zangu ili zimtii Kristo."*** *(kwa mujibu wa 2 Wakorintho 10:5) Ombi kama hilo hushabihiana na mapenzi ya Mungu, na hivyo litajibiwa hakika (1 Yohana 5:14). Na pale tuombapo kwa jinsi hii, tunakuwa* ***watu tuupendezao moyo wa Mungu****. Tunajuaje hili? Liko kwenye Biblia katika Matendo 13:22: "...Nimemwona Daudi,...* ***mtu anayeupendeza moyo Wangu, atakayefanya mapenzi Yangu yote.****"*

*Je unataka kuwa mtoto, kijana, mwanamume au mwanamke unayeupendeza moyo wa Mungu?*

## Kuyatenda Mapenzi ya Mungu Huleta Uhuru

Mwanzoni, mtu huwa na mwelekeo wa kuamini kwamba hayuko huru, pale wanapopaswa kufanya mapenzi ya mwingine (kwa muktadha huu, mapenzi ya Mungu). Lakini tunahitaji kidogo kudadavua kuhusu neno uhuru. Hakuna **uhuru** kamili. Hata hivyo, tuna uhuru wa kuamua **kwa ajili ya Mungu au dhidi Yake**. Kwa vile Mungu ni upendo na uhuru huunda sehemu muhimu sana Kwake, napata uhuru na furaha ninapomfuata Yeye.

Nisipoamua kwa ajili ya Mungu, basi Shetani huwa mtawala wangu. Na wala yeye haruhusu uhuru wowote kwa watu; hutenda kazi kwa *nguvu*. Kila mraibu ni uthibitisho wa hili. Na pale mtu fulani anapotaka kuondoka kwenye himaya ya Shetani, ndipo atagunduau kwamba Shetani hatamruhusu aondoke hivihivi.

Kinyume chake, hakika Mungu anahuzunika pale tunapomwacha lakini hatumii kabisa shurti yoyote ili kutulazimisha tubaki Kwake.

Tunapozingatia haya yote, ni vema kukafahamu kwamba tanaweza tu kuishi maisha *huru* na *yenye furaha* tukiwa karibu na Mungu, na ni kweli, tunaposema: Kutenda mapenzi ya Mungu huleta uhuru!

## Kuwa Radhi Huzaa Matunda

Katika hitimisho, ningependa kuwasilisha mifano miwili jinsi ambavyo Mungu anaweza kututumia pale tunapojiweka chini ya mamlaka Yake. Na haijalishi iwapo tu maskini au matajiri, wadogo au wakubwa, wenye elimu au wasio na elimu.

Mfano wa kwanza ni kutoka kwenye Biblia. Tunaweza kuupata katika Yohana 6:5-13. Mvulana mmoja alimpatia Yesu kila kitu alichokuwa nacho; hakikuwa kingi – samaki wawili wadogo na vipande vitano vidogo vya mkate. Sasa, hakuwa na chochote kilichokuwa kimesalia kwa ajili yake mwenyewe. Na Yesu alifanya nini? Alitenda muujiza kiasi kwamba njaa ya wote waliokuwepo ilitoshelezwa. Kila mmoja – kwa muktadha huu, watu 5,000 na takriban idadi kama hii ya wanawake na watoto.

Tunaweza kuona: Tunapoweka nafsi zetu wenyewe au talanta zetu mikononi mwa Mungu, anaweza kutengeneza kitu fulani kikubwa zaidi kutokana nacho!

Mvulana huyu angeweza kula zaidi ya vile ambavyo alimpatia Yesu. Alichompatia, kwa namna fulani zilikuwa mbegu. Kwa mujibu wa kanuni ya chanzo na matokeo, **daima mavuno huwa mengi zaidi kuliko mbegu.**

Mfano wa pili ni uzoefu kutoka Ujerumani kuanzia mwaka 1994. Muumini mwenzangu alitoa DM 10,000 (kizio cha fedha nchini Ujerumani zamani) kwa ajili ya mradi fulani, uliokuwa sehemu ya utume ulimwenguni katika kujenga kanisa kwenye eneo jipya lenye idadi ya watu milioni huko Uzbekistani. Alinipigia mwaka mmoja baadaye na kuniambia kwamba kile kiasi cha DM 10,000 alichokuwa amehisani ilikuwa mirabaha kutoka kwenye kitabu alichokuwa ameandika. Na sasa ndipo tu amepata barua kutoka kwenye nyumba ya uchapishaji, ikisema kwamba hitaji la kitabu hiki ni kikubwa sana kiasi kwamba walikusudia kuchapisha toleo lingine. Ndipo tena akapokea cheki ya DM 10,000.

Akaendelea kueleza ni nadra kwamba toleo la pili la kitabu kisicho cha hekaya hata kiweze kuchapishwa. Ilikuwa dhahiri kwake: Mungu alikuwa ameweka mkono katika hili. Mungu alikuwa amemrejeshea DM 10,000 zake. Mwishoni mwa mazungumzo yetu kwa simu, ndugu huyu akasema: “Ukihitaji fedha tena kwa ajili ya kazi ya utume, tafadhali nifahamishe.” Siku moja muda huo ukafika. Nikampigia ndugu huyu. Jambo la kwanza alilosema ni hili: “Ndipo tu nilitaka kukupigia, ila umeniwahi. Mathalani, nilitaka kukutumia cheki, ambayo ungeitumia kwa makusudi ya utume.” Kisha aliendelea kusimulia kwa furaha kwamba wakati huohuo toleo la tatu la kitabu chake kilikuwa kimechapishwa na ndipo tu alikuwa amepokea cheki kutoka kwenye nyumba ya uchapishaji kwa mara nyingine. Ilikuwa nadra kwake kuliamini hili! Kisha nikamwambia kuhusu mradi wa utume wetu na kueleza kwamba tungehitaji tu fedha hiyo kwanza ndani ya majuma machache. Nilimwambia kwamba angetumia muda fulani kulifikiria hilo na kuamua endapo angependa kushiriki kwenye mradi husika. Alijibu: “Nakutumia cheki.” Ilifika siku inayofuata na ilikuwa ya DM 25,000! Tulipokutana kwa nasibu kwenye tukio fulani majuma machache baadaye, aliniambia: “Hivi ulijua kwamba tayari nilikuwa nimeiandika cheki hiyo ya DM 25,000 kabla hujanipigia?”

Hivyo, Mungu, kwa jinsi ya kustaajabisha hivi, aliweza kumbariki ndugu huyu na pia mradi wa utume! Andiko lililotajwa mwanzoni katika Luka 6:38 likawa uhalisia kwa ndugu huyu: *"Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwa-sukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa."*

Hebu Uzoefu huu utusaidie kumpenda Yesu kwa kina zaidi kuliko hapo kabla na kumtumikia kwa furaha, ilhali tukiwa tunajazwa Roho Mtakatifu.

***Ombi langu: "Baba uliye mbinguni, tafadhali nisamehe kwa kuwa na mtazamo ambao kiasi fulani au kwa ukamilifu wake ni potofu kuhusu utumishi, utoaji na kuwasaidia watu. Asante sana kwa kunibariki na wengine pia wakati huohuo, pale ninapotumika, ninapotoa na kusaidia. Wewe ulilipanga hili kwa umahiri! Tafadhali, nikirimie kila siku mtazamo sahihi wa moyo ili niweze kutenda kila kitu utakacho kutokana na moyo ukupendao Wewe na uliojaa furaha. AMINA."***

## Mawazo binafsi na mwongozo wa mjadala

1. *Ni mawazo gani mahiri ambayo Mungu amefunga-manisha na utumishi, kusaidia na utoaji? Je hili lina mantiki gani?*

   ____________________________________________

2. *Ni kwa kigezo gani ambapo utumishi siyo mzigo, badala yake ni furaha?*

   ____________________________________________

3. *Kwa nini ni muhimu kuwa na akili/weledi na hekima?*

   ____________________________________________

4. *Ni mtazamo gani tupaswao kuwa nao ili tuweze kuwa watu waupendezao moyo wa Mungu?*

   ____________________________________________

## Muda Wetu wa Maombi

- Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.

- Sali pamoja na mwanamaombi mwenzio…
  1. … kwamba uweze kuwatumikia wengine kwa furaha kama matokeo ya kuwa na Kristo moyoni mwako kwa imani.
  2. … kwamba Mungu aweze kukuonesha nani anauhitaji msaada wako.
  3. … kwamba uweze kulindwa dhidi ya kiburi na kujifikiria binafsi, kama unaweza kutenda mambo makuu kwa msaada wa Mungu.
  4. … kwa ajili ya moyo wa uradhi na furaha na ustahimilivu katika utumishi kwa Mungu na mwanadamu.

# Nani Atendaye Kazi: Mungu Kupitia Kwangu au Mimi Kwa Ajili ya Mungu?

Inahusisha maswali kadhaa muhimu sana:
Je namfanyia Mungu kazi kwa uwezo wangu wa kibinadamu?
Au Mungu anaweza kutenda kazi kupitia kwangu kwa uwezo Wake wa kiungu?

## Mfano Madhubuti katika Biblia: Musa

Mwanzoni, Musa alikuwa mfano wa mtu, aliyeishi kwa kujitumainia nafsi. Hata hivyo, baadaye akawa mfano bora wa mtu ambaye Mungu angetenda kazi kupitia kwake. Akiwa na umri wa miaka 40, alitaka kuwaweka huru watu wake kwa kutumia uwezo wake turufu wa kibinadamu. Hilo lilikuwa na athari mbaya tu. Miaka mingi baadaye Mungu aliweza kufanya mambo makuu kupitia kwake na yakawepo matokeo ya kiungu.

Katika Matendo 7:22-25 inaripoti kwamba: *"Musa akafundishwa hekima yote ya Wamisri, akawa hodari wa maneno na matendo. Umri wake ulipopata kama miaka arobaini akaazimu moyoni mwake kwenda kuwatazama ndugu zake Waisraeli. Akamwona mmoja akidhulumiwa, akamtetea, akamlipia kisasi yule aliyekuwa akionewa, akampiga huyo Mmisri.* ***Alidhani kwamba ndugu zake watafahamu ya kuwa Mungu anawapa wokovu kwa mkono wake,*** *lakini hawakufahamu."*

Musa alilazimika kukimbia na kuishi kwa miaka arobaini kama mchungaji wa kondoo huko Midiani. Hatimaye, alifikia hatua ya kujisalimisha kikamilifu. Ndipo Mungu akampatia mawazo, ambayo yameandikwa katika kitabu cha Mwanzo. Ni wakati huo tu ndipo Mungu alimwagiza Musa akawaweke huru Waisraeli. Hivyo, Musa kwa utii akaanza safari kwenda

Misri. Ghafla, akazuiwa na malaika. Ilikuwepo dhambi fulani iliyojulikana – dhambi ya kutowajibika. (Kutoka 4:24-26, *Patriarchs and Prophets,* uk. 255-256) Dhambi hii moja ilipaswa kushughulikiwa kwanza. Ndipo malaika angeweza kumlinda na **Mungu angeweza kutenda kazi kupitia kwake kwa uwezo Wake wa kiungu:**

Musa akawaongoza watu wake kutoka utumwani. Alitenda ishara na miujiza ya kustaajabisha kila mahali: huko Misri mbele ya Farao, kuivuka Bahari ya Shamu na kipindi cha miaka 40 huko jangwani. Hata Mungu alinena naye binafsi na kumpatia bamba za mawe alizoandikia amri kumi.

Alikuwa mmojawapo wa viongozi wakuu ulimwenguni kwa sababu Mungu aliweza kutenda kazi kupitia yeye. (Mapendekezo ya usomaji: *Wazee na Manabii*, sura ya 22: Musa)

## Je namfanyia Mungu kazi au Yeye anafanya kazi kupitia mimi?

Andiko letu la msingi ni Waefeso 2:10 NKJV:

*"Maana tu* ***ustadi wa kazi Yake****, tuliumbwa katika Kristo Yesu* ***tutende matendo mema****, ambayo tokea awali Mungu aliyaandaa ili tuenende kwayo."* (GNT): *"Ametuumba tuishi maisha ya mtendo mema, ambayo tayari ametuandalia tufanye."*

Hii huzungumzia **kazi mbili**!

## Kazi ya kwanza, Mungu hutenda kazi ndani yangu

Kazi ya kwanza atendayo Mungu ni **ndani yangu**. Haya ni maisha yangu mapya ndani ya Kristo. Yesu alisema: *"Njoni Kwangu ..."* (Mathayo 11:28) na *"...wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu…"* (Yohana 1:12)

Wale ambao wamekuja kwa Yesu na kumkubali kama Bwana na Mkombozi wake, hupokea mwaliko na ahadi nyingine: "*Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu."* (Yohana 15:4) Yesu anataka kuingia katika uhusiano thabiti na unaotuunganisha pamoja naye. Jinsi gani hili linatokea? Ni suala la hatua mbili za imani kila siku:

**Hatua ya kwanza:**

Waefeso 5:18 inasema: *"mjazwe Roho."* Au kwa maneno mengine: "mwendelee kujazwa Roho daima na mara kwa mara." (Joh. Mager: *Auf den Spuren des Geistes*, uk. 101). Hivyo, inahusiana na kuomba na kupokea Roho Mtakatifu. Kama vile ambavyo lazima gurudumu la kinu liwe kwenye maji yatiririkayo ili liendelee kuzunguka, nasi pia tunapaswa kubaki kwenye mto wa Roho Mtakatifu ili Mungu aweze kutenda kazi kupitia kwetu na kutukirimia maisha maridhawa. Lakini siyo kusudi la Mungu kwamba tuwe vyombo vya kuhifadhia Roho Mtakatifu. Hapana, anataka tuwe mkondo au mfereji ambao kupitia hapa anaweza kuwafikishia watu wengine upendo. (Angalia Luka 11:5-13).

**Hatua inayofuata:**

*"...itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana."* (Warumi 12:1)

Haya ni maisha ya kujisalimisha kikamilifu kwa Kristo. Maelezo bora na mafupi ya hatua hizi yanaweza kupatikana katika *The Desire of Ages,* uk. 676.2. Hutoa muhtasari:

- ▷ Roho Mtakatifu daima – na
- ▷ Kujisalimisha kikamilifu kwenye utumishi Wake.

Haya hapa maelezo mafupi kuhusu maana ya Roho Mtakatifu: "Lakini hadi **wamempokea Roho Mtakatifu**, vinginevyo hawawezi kuwasilisha ujumbe huu kwa nguvu. **Hadi wamempokea Roho, vinginevyo hawawezi kutambua kile ambacho Mungu anaweza kutenda kupitia kwao.**" (E.G. White, *Adv. Review and Sabbath Herald,* Juni 10, 1902).

Nukuu nyingine kuhusu kujisalimisha: "Yule atakayejikabidhi kikamilifu kwa Mungu ataongozwa kwa mkono wa kiungu… Kadiri anavyothamini masomo ya hekima ya kiungu, **utume mtakatifu utadhaminiwa kwake…**" *(The Acts of the Apostles,* uk. 283.3)

Sasa tunalo jibu la swali kuhusu jinsi tunavyoweza kuwa na muunganiko hai, endelevu pamoja na Yesu: kwa kuomba kila siku na kumpokea Roho Mtakatifu, pamoja na uhawilinishaji

wa kila siku wa kujisalimisha kwetu Kwake na kwa huduma Yake. Kila asubuhi, ni jukumu letu muhimu zaidi kutimiza hatua hizi mbili za kiroho. Kwa namna hii, **kazi ya Mungu ndani yangu** inadumishwa – yaani, maisha yangu mapya ambayo nimeyapokea kwa neema ya Mungu kupitia imani yangu, hudumisha kuwa hai.

## Kazi ya Pili – Kazi ya Mungu Kupitia Kwangu

Kwa msingi wa maisha haya mapya, Mungu hutenda kazi nyingine – kazi **kupitia kwangu**. Hebu tusome tena Waefeso 2:10: *"Maana tu kazi Yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo."* GNT: "Ametuumba kwa ajili ya maisha ya matendo mema, ambayo tayari ametuandalia tuyafanye."

Anasema kwamba matendo haya mema yameandaliwa na Mungu tangu awali. Ni wajibu wetu katika kuunganika Naye kutenda kazi hizi zilizoandaliwa.

Hivyo, katika mpango mkuu wa Mungu, ana mpango mwingine akisami kwa ajili yangu. Ameandaa majukumu fulani kwa ajili yangu. Kwa kukamilisha majukumu haya, tunakua katika imani na pia uwezo wetu halimali, wa kiroho na kiakili huimarika. Tunapata uzoefu wa furaha na nguvu ilhali tukitenda kazi kwa ajili ya ufalme wa Mungu na wakati huohuo tunaandaliwa kwa ajili ya ufalme wa Mungu kupitia utumishi huu. (Kwa maelezo zaidi kuhusu soma: E.G. White, *Education,* uk. 264)

Nehemia na jumuia nzima walipata uzoefu wa: ***"…furaha ya Bwana ni nguvu zenu."*** (Nehemia 8:10)

Ndiyo, kupitia kazi yao kwa ajili ya Mungu walipata uzoefu wa hili. Kwa kipindi cha siku 52 tu, kuta za Yerusalemu zilijengwa upya, kwa sababu watu hawakutishwa wala kuzuiwa kazi yao kutoka kwa maadui wao. Wakati wote Nehemia aliongoza njia kwa imani!

Na hicho ndicho tupaswacho kufanya vilevile. Kukumbuka kile ambacho tayari Bwana ametufanyia hutupatia msaada mkubwa, halikadhalika Warumi 8:31: *"Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu?"*

## Mungu huweka mipango madhubuti na ya muda mrefu

"Mungu hatuagizi tufanye kwa uwezo wetu wenyewe kazi iliyo mbele yetu. Ametuandalia msaada wa kiungu… Hutukirimia Roho Mtakatifu ili atusaidie katika kila adha." (E.G. White, *My Life Today*, uk. 37,4)

Kwa vile Mungu anamjua kila mtu na mustakabali ujao, pia anajua jinsi gani anavyoweza kututumia ipasavyo – ili kutimiza yaliyo bora kwa ajili yetu na ufalme wa Mungu.

Katika Yohana 7:37-39 tunasoma:

*"Mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe. Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake. Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho…"* (Hili linahusiana na kazi ya pili – ambayo Mungu anataka kufanya kupitia kwetu.)

Andiko hili la Biblia humaanisha ifuatavyo: Endapo kila siku tukizimisha kiu na shauku yetu kwa ajili ya Yesu, basi hatutakuwa tu na maji ya uzima kwa ajili ya nafsi zetu wenyewe, lakini pia Bwana atayafanya maji haya hai ndani yetu yawe chemchemi – maradufu – ili mito ya maji ya uhai yaweze kutiririka kutoka kwetu kwenda kwa wengine. Hii ni ahadi ya pekee ajabu!

Majukumu ambayo tumeaminishwa na Mungu yataamua kwa kiwango gani tunaweza kubadili mazingira yetu. Kwa vile hakuna yeyote aishiye kwa ajili ya nafsi yake mwenyewe, siyo tu kwamba matendo yetu hutuathiri sisi wenyewe, bali pia mazingira yetu. Na wakati mwingine ushawishi wa mtu mmoja hufika mwisho wa dunia.

Mungu anataka na anaweza kutenda mambo makuu kupitia kwetu, kama tukikuza uhusiano wa dhati pamoja naye:

"Yeyote anayekabidhi nafsi yake kwa Bwana kwa ajili ya huduma, bila kuzuia chochote, hupewa nguvu ya kufanikisha matokeo yasiyokadirika." (E.G. White, *Testimonies, vol. 7,* uk. 30.2).

Yeyote afanyaye hili ana ahadi katika Yohana 14:12 NKJV:

*"Hakika, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kazi kubwa zaidi kuliko hizi atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba."*

Kirai "kazi kubwa zaidi" humaanisha utandaaji angani hapa. Kwa nini tutaweza kutenda kazi kubwa zaidi kuliko Kristo? Maelezo ya Yesu yalikuwa: Kwa sababu Mimi naenda kwa Baba. Alimaanisha nini aliposema hivyo? Baada ya kupaa Kwake, alipokea mamlaka yote mbinguni na duniani kwa mara nyingine tena. Na Yesu anapoishi moyoni mwangu kupitia Roho Mtakatifu, ndipo anaweza kutekeleza haya "matendo makuu" kupitia kwangu. Hebu tumwangalie tena Nehemia, aliyekuwa mfano chanya katika Biblia.

## Je ujenzi upya wa kutaza za Yerusalemu lilikua wazo la Nehemia?

Nini kilichomhamasisha Nehemia, ambaye hakuwa bingwa wa ujenzi, ajenge upya kuta za mji wa Yerusalemu, japo alikuwa mbali sana huko Uajemi na alikuwa na cheo kikubwa? Tunasoma katika Nehemia 2:12: *"...neno hili alilolitia Mungu wangu moyoni mwangu, nilitende kwa ajili ya Yerusalemu..."* E.G. White anafafanua: "… wakati akiomba, mpango huu ulikuwa umeundwa akilini mwake [Nehemia]…" (*Southern Watchman*, Machi 29, 1904)

Kazi ile ya Yerusalemu halikuwa wazo la Nehemia, badala yake alitumwa na Mungu. Mungu alikuwa amempangia na kumwandalia kazi halisi.

Mungu alimbariki Nehemia kwa kiasi kikubwa! Mwishowe, kazi yake ilifanikiwa sana. Nehemia alipata uzoefu wa kile ambacho E.G. White aliandika katika *Testimony Treasures, vol. 3,* uk. 341.3: "Mungu ataifanya kazi husika iwapo tutamkabidhi nyenzo."

## Kikwazo au Mhamasishaji?

Mbali na Nehemia, nani mwingine alikuwa na mchango muhimu katika mafanikio haya? E.G. White aliandika: "Miongoni mwa watu wa kwanza kunasa roho ya Nehemia ya ari na juhudi walikuwa makuhani wa Israeli. Kutokana na nyadhifa za madaraka walizokuwa nazo, watu wangeweza kufanya mambo mengi zaidi katika kuzuia au kuendeleza kazi husika. Ushirikiano wao wa hiari tangu mwanzo kabisa ulichangia siyo kidogo katika mafanikio husika." (*The Southern Watchman*, Aprili 5, 1904)

## Moyo Usiogawanyika

Nehemia ni mfano katika Biblia wa mtu aliyejenga uhusiano wa dhati pamoja na Mungu katika maisha yake yote. Alimkabidhi Mungu maisha yake yote kwa moyo mkamilifu. Daima Mungu anawatafuta watu kama huyu. Tunasoma katika 2 Nyakati 16:9: *"Kwa maana macho ya Bwana hukimbia-kimbia duniani mwote,* ***ili ajionyeshe mwenye nguvu kwa ajili ya hao, waliokamilika moyo kuelekea Kwake****."* Hilo ndilo shartiasili – moyo usiogawanyika – ili nguvu ya Mungu iweze kutenda kazi kupitia sisi.

Kujisalimisha kikamilifu kwetu na maisha yetu pamoja na Roho Mtakatifu *(DA,* 676.2) hufanya iwezekane kwa Bwana kutenda kazi kwa nguvu kupitia sisi. Ni mpaka pale maisha yetu mapya yanapokuwa madhubuti – pale tunapokuwa na uhusiano endelevu na wakuaminika pamoja na Mungu – ndipo Mungu atatuamini katika kazi ambayo ameiandaa. Ni katika msingi wa kazi ya kwanza hai tu ndipo kazi ya pili – kazi kutoka kwa Mungu – inaweza kujengwa. Endapo maisha mapya (Yohana 3:1-17) bado hayajaanza au yamekoma, basi kazi yetu hufanyika tu kwa nguvu za kibinadamu ikiambatana na mapungufu na matatizo yote ya kibinadamu.

## Mfano Mwingine: Mfalme Asa

Kwa sehemu kubwa ya maisha yake, Asa alimwamini Mungu na kuufuata uongozi wake, lakini kuelekea mwishoni mwa maisha yake alifuata njia yake mwenyewe. Alionesha hili, mathalani, alipomwomba Ben-Hadad, mfalme Ashuru, msaada wa kijeshi badala ya kumwomba Mungu. Mungu alipomtuma Hanani mwonaji ili amwambie Asa athari mbaya ambazo matendo yake yangeleta, mfalme huyo akakasirika sana kiasi kwamba alimtupa mwonaji gerezani. Vilevile, miaka mitatu baadaye Asa alipougua, hakwenda kwa Mungu, bali alimwamini madaktari wake. Kwa vile Asa alikataa kumruhusu Roho wa Mungu amwongoze, Mungu aliuondoa msaada Wake. Tukilitafakari hili, Asa alikuwa mfalme mwaminifu kwa miaka 35 na alipata uzoefu kina kwa Mungu lakini miaka sita ya mwisho ya maisha yake alikuwa mfuasi wa Mungu mwenyewe kutiliwa

mashaka. Tunaweza tu kuomba: “Bwana, nisaidie nidumu kuwa mwaminifu katika njia Zako hadi mwisho wa maisha yangu!” (Angalia: 1 Wafalme 15:8-24 na 2 Nyakati 14-16).

Biblia anasema yafuatayo kuhusu Shetani: “*...audanganyaye ulimwengu wote...”* (Ufunuo 12:9) Mtume Paulo anatuambia: *“Kwa hiyo anayejidhania kuwa amesimama na aangalie asianguke.”* (1 Wakorintho 10:12) Tunataka kuangalia mfano mwingine – wakati huu kutoka katika historia ya Waadventista – kwa ajili ya ulinzi na onyo kwetu.

### Kuna athari gani kwenye kazi ya Mungu, wakati ambapo hatua kwa hatua ninapokengeuka katika imani, lakini nikasalia katika utumishi?

Pengine tunaweza kujiuliza wenyewe sasa: Hivi hata inawezekana kwa mtu anayemfanyia Mungu kazi asiongozwe tena na Roho Wake?

**Dkt. John Harvey Kellogg** alikuwa daktari mahiri sana na mtu mashuhuri katika kanisa letu Marekani. Baada ya miaka kadhaa mtu huyu mahiri alipuuza, mathalani, mashauri ya Mungu kuhusu kujenga na kuendesha sanatoriamu. Mungu akaruhusu Sanatoriamu ya Battle Creek iteketee kabisa kwa moto, kisha sanatoriamu mpya, iliyojengwa chini ya uongozi wa Kellogg, kutangazwa kufilisika. Kinachosikitisha, kwa wakati aliofanya kazi kama daktari kwa ajili ya kanisa, alianzisha dhana ngeni za kiteolojia, ambazo mwanzoni alizieneza kwa mdomo. Matokeo yake, aliwapotosha washiriki wengi wa kanisa. Baada ya muda, Kellogg alitaka kuchapisha kitabu kilichokataliwa na viongozi wetu kwa vile kilikuwa na mafundisho potofu. Kufuatia hilo, Kellogg akaamua kukichapisha kitabu hicho kwa gharama zake mwenyewe. Aliipatia nyumba yetu ya uchapishaji, *Review and Herald*, ambayo kwa wakati fulani ilikuwa ikichapisha machapisho ya watu wa nje, oda ya nakala 5,000. Nyumba ya uchapishaji ikaafiki. Mungu akaingilia kati moja kwa moja, akaruhusu nyumba hiyo ya uchapishaji iteketee kwa moto wa kutisha. Baada ya hapo, Kellogg akapeleka mswada wa kitabu chake kwenye nyumba ya uchapishaji ya nje ili uweze kuchapishwa.

Ni umilele pekee ndio utaonesha uharibifu kiasi gani alioufanya Kellogg dhidi ya kazi ya Mungu, hususan miongoni mwa vijana, hadi hatimaye alipoondoka kanisani kwa hiari yake mwenyewe. (Kwa taarifa zaidi angalia: Lewis R. Walton: "Omega", Review and Herald). Kwa muktadha huu, hatuhitaji hata kuuliza iwapo alimtendea Mungu kazi kwa nguvu zake au endapo Mungu aliweza kutenda kazi kupitia kwake.

Siku ya 13

## Kumfanyia Mungu kazi ni jambo moja, lakini Mungu kutenda kazi kupitia sisi ni jambo lingine

Katika kulihusianisha na hili, nataka kuwasilisha nukuu kutoka kwa Le Roy E. Froom: "Kumfanyia Mungu kazi ni jambo moja; lakini kumruhusu Mungu atende kazi kupitia sisi ni jambo lingine. Ni jambo kuachana na ulimwengu na kumfuata Kristo; ni jambo lingine kabisa kuwa mtu ambaye ndani yake Roho Mtakatifu hukaa ndani kikamilifu kwa wingi wa uwezo na neema. …Na Mungu hawezi kufanya jambo fulani la kimapinduzi *kupitia* watu hadi pale anapokuwa amefanya jambo fulani la kimapinduzi *kwa ajili ya* watu kupitia kumkaribisha Roho Mtakatifu ndani yao." (The Coming of the Comforter, Review and Herald 1928, uk. 119)

Hili linaweza kutokea maishani mwetu vilevile – kama ilivyomtokea Dkt. Kellogg – kwamba tunaamini tunapaswa kufanya hili au lile kwa ajili ya Mungu, bila kuongozwa na Roho wa Mungu. Wakati mwingine tunahitaji kujiuliza: Hivi namfanyia Mungu kazi kwa uwezo na mapungufu yangu ya kibinadamu, pengine hata kwa mamlaka ya wadhifa wa kiutawala, au Bwana anaweza kutenda kazi kupitia kwangu akitumia uwezo Wake wa kiungu usionakikomo na kutojilikana?

## Jinsi ambavyo Mungu anaweza kunitumia katika kazi ya pili hutegemeana na uhusiano wangu pamoja Naye

Kuhusiana na **waandishi wetu,** E.G. White aliandika:

"Maandishi yaliyoandikwa katika Roho wa Mungu malaika huyaidhinisha, na kuyahimiza kwa wasomaji. Lakini maandishi yaliyoandikwa wakati mwandishi haishi kikamilifu kwa ajili ya

utukufu wa Mungu, bila kujitolea kikamilifu Kwake, malaika hutambua upungufu huo kwa huzuni. Huondoka na wala hawahimizi wasomaji kwayo kwa sababu Mungu na Roho Wake hawamo ndani yake. Maneno ni mema ila yanakosa mvuto chanya wa Roho wa Mungu." *(PH 016,* 29.1 egwwritings.org).

Kwa sehemu kubwa, nini cha muhimu zaidi katika maandishi ya Kikristo? Yanapaswa kuandikwa chini ya mamlaka ya Roho Mtakatifu na mwandishi anapaswa kuishi kwa ajili ya utukufu wa Mungu, mathalani, katika kujisalimisha kikamilifu kwa Kristo na utumishi Wake. Mungu havutiwi kwa maudhui ya kustaajabisha kwenye makala fulani. Anafurahia zaidi mwenendo wa kiroho wa mwandishi aliyeandika ujumbe husika. Pale ambapo mwandishi aliandika chini ya mamlaka ya Roho Mtakatifu, ndipo Mungu anaweza kumhimiza msomaji kupitia Roho yuleyule naye msomaji anaweza kuja karibu na Mungu zaidi.

Hii ni sahihi pia kwa maeneo mengine yote, iwe katika huduma, ufundishaji, kusimamia mradi wa utume, uongozi wa kanisa, maisha ya familia, mafunzo ya mtoto au kitu fulani cha namna hiyo, kwamba "Siyo nguvu itokayo kwa wanadamu ndiyo hufanikisha kazi, bali ni nguvu ya wenye maarifa kutoka mbinguni wakitenda kazi pamoja na mawakala wa kibinadamu ndio huikamilisha kazi." (E.G. White, Christian Service, uk. 260.3)

Mungu anaweza tu kutumia mvuto Wake wa thamani kupitia sisi, pale tunapokuwa na uhusiano hai pamoja na Mungu. Kwa maneno mengine, endapo tunaishi kwa kujisalimisha kikamilifu au hatujajazwa Roho Mtakatifu kwa utoshelevu, ndipo baraka kuu huweza kupotezwa au uharibifu unaweza kusababishwa!

## Kulihubiri Neno la Mungu

Hebu tuzingatie uhusiano huu katika muktadha wa **kulihubiri Neno la Mungu**. Wachungaji wanapokuwa hawakujazwa kikamilifu Roho Mtakatifu, basi kamwe mahubiri yao hayatakamilisha kile ambacho Mungu anakusudia. Nukuu kutoka kitabu cha *Desire of Ages*, uk. 671.4:

“**Mahubiri ya neno la Mungu hayatafaa kitu bila uwepo endelevu pamoja na msaada wa Roho Mtakatifu…** Mtu anaweza kuwasilisha andiko la neno la Mungu, anaweza kufahamu amri na ahadi zake zote; lakini kama Roho Mtakatifu asipofikisha ukweli husika mahali pake, hakuna roho zozote zitakazoanguka kwenye Mwamba na kuvunjika. Hakuna kiwango chochote cha elimu, hakuna fursa zozote, hata zingekuwa kubwa kiasi gani, zinazoweza kuunda mkondo japo mmoja wa nuru bila ushirikiano wa Roho wa Mungu.”

Mungu na malaika hutenda kazi nasi tu pale tunapojazwa Roho Mtakatifu na kuishi maisha ya kujisalimisha kikamilifu kwa Kristo. Haijalishi sisi ni nani au nini tufanyacho, Mungu anatujulisha kupitia E.G., White: “Thamani ya kazi yetu inawiana na ukirimiwaji wa Roho Mtakatifu.” (*The Desire of Ages*, uk. 330.4) Na: “Siyo uwezo ulio nao sasa au utakaokuwa nao ndio utakupa mafanikio. Ni kile ambacho Bwana anaweza kukufanyia.... Anatamani akuwezeshe utegemee **mambo makuu** kutoka Kwake.” (*Christ Object Lessons*, uk. 146.4) (Mapendekezo ya usomaji zaidi: *Acts of the Apostles,* uk. 283-284)

Tutapata uzoefu wa nguvu za Mungu uanaotusaidia kwa wingi zaidi, kadiri tunapokuza ushirika kwa dhati pamoja Naye. “Hatutapata ushindi kwa idadi, bali kuisalimisha nafsi kwa kikamilifu kwa Yesu.” (*Sons and Daughters of God,* 279.2).

Kinachosikitisha, watu wengi, wakati fulani pamoja na mimi mwenyewe, huogopa au wana udhuru kuhusu kujisalimisha kikamilifu kwa Mungu. Wanadhani watakuwa watumwa. Mtazamo wa namna hii ni potofu kabisa. Biblia hulinganisha uhusiano na Kristo kama ndoa. Kristo ni mwenzi mahiri! Mtu fulani anapofunga ndoa, anaweza kutalakishwa kama akipenda. Sisi nasi tunaweza kujitenga na Kristo; tunakuwa watu tusiohusiana naye. Lakini sidhani vyovyote vile tunataka kufanya hilo, kwa sababu uhusiano na Kristo ndio uhusiano bora uwezekanao. Anataka kuwa na uhusiano pamoja nasi ambapo tumeunganishwa katika upendo na dhamani pamoja Naye. (Kwa maelezo zaidi kuhusu: *Kaeni Ndani ya Yesu*, sura ya “Kujisalimisha kwa Yesu”, tazama www. schritte-zur-persönlichen-erweckung.info).

## Uingiliaji kati wa Mungu unaweza kuwa wa kina zaidi kuliko stamani za kibinadamu

Mungu anataka kutenda mambo makuu na ya ajabu hata leo (Yeremia 33:3). Tunapoishi kiasi kwamba Mungu anaweza kutenda kazi ndani yetu na kupitia sisi, ndipo tutapata uzoefu tena na tena mambo ya kushangaza – mambo makuu na yastaajabishayo. Iko hivi: kile Mungu apangacho kufanya kupitia mimi, katika maeneo mengine zaidi ya uwezo na ustadi wangu. Na hili ni jambo jema. Huleta furaha na mshangao mkubwa na hukuza utegemezi na ushirikiano wetu pamoja na Mungu.

Hizi hapa nukuu mbili kutoka katika machapisho yetu kuhusu suala hili: "Omba neema na ufanisi wa Kristo, nawe hutaachwa ufanye kazi peke yako." (The Ellen G. White *1888 Materials*, 141.5).

"Yeyote anayekabidhi nafsi yake kwa Bwana kwa ajili ya huduma, bila kuzuia chochote, hupewa nguvu ya kufanikisha matokeo yasiyokadirika." (*Testimonies for the Church*, *vol. 7,* uk. 30.2).

## Muunganiko wa Maombi Endelevu

Tunapoishi kiasi kwamba Mungu anatenda kazi ndani yetu na kupitia sisi, basi tunahitaji muunganiko wa maombi endelevu pamoja Naye. Tunahitaji kuunganika na Yule anayetuandalia wajibu. Anaweza kutuongoza kwa namna bora kuikamilisha. Ni kama kuendesha ukiwa na kishanisi cha uongozaji. Mungu ametupatia ahadi kuu mno kuhusu kuunganika Naye: *"Niite, Nami nitakuitikia, na kukuonesha mambo makuu na adhimu usiyoyajua."* (Yeremia 33:3 NKJV; ahadi zaidi: Yohana 7:37; Yohana 14:12-14; Yohana 15:7; Yohana 15:16; Mathayo 18:19; 1 Yohana 3:22). Siyo tu kwamba Bwana anaahidi kujibu maombi yetu, bali pia kutuonesha mambo makubwa na adhimu. Anatupatia jibu la kiungu.

## Mashauri ya Kiungu

"Hebu yeyote asielemee uwezo wake aliopewa na Mungu katika juhudi ya kuiendeleza kazi ya Bwana haraka zaidi. Nguvu ya mwanadamu haiwezi kuiharakisha kazi; pamoja na

hii lazima iunganishwe nguvu ya wenye maarifa wa mbinguni… Mwanadamu hawezi kuifanya sehemu ya Mungu ya kazi. Mtu kama Paulo anaweza kupanda, na Apolo akamwagilizia, lakini Mungu ndiye aletaye ustawi na mavuno. Katika usahili na upole, mwanadamu anapaswa kushirikiana na mawakala wa kiungu, nyakati zote akitenda kwa ubora kadiri awezavyo, lakini akitambua daima kwamba Mungu ndiye Mtendaji Mahiri." (E.G. White, *7T 298.2,* egwwritings.org).

## Ni matokeo gani ambayo maisha ya Kristo yalisababisha hapa duniani?

Philipp Brooks alisema: "Hakika sijakosea nisemapo kwamba majeshi yote ambayo yamewahi kuandamana, manowari ya majini yaliyowahi kuundwa, mikutano yote ya bunge iliyowahi kufanywa na wafalme wote waliowahi kutawala, hawakugusa maisha ya watu duniani kama ilivyofanywa na maisha pekee ya Yesu." *(Letters to Andrew, Na. 2)*

Jinsi gani mwanadamu Yesu wa Nazareti aliweza kuwa na mvuto na ushawishi mkuu kiasi hicho? Yesu alituambia sababu kwa uwazi sana katika Yohana 14:10:

*"Husadiki ya kwamba Mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani Yangu? Hayo maneno niwaambiayo Mimi siyasemi kwa shauri Langu; lakini Baba akaaye ndani Yangu huzifanya kazi Zake."*

Akiwa kama mwanadamu Yesu aliweza kupata ushawishi mkuu kiasi hicho kwa sababu Baba alikuwa ndani Yake akitumia mvuto Wake wa kiungu.

Au hebu tumwangalie **mtume Paulo**. Jinsi gani Mungu kutenda kazi ya utume mkuu wa kustaajabisha kiasi hicho kupitia kwake? Tunaweza kulipata jibu katika Wagalatia 2:19-20: *"Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu...."* Alisalimisha uhuru na kujitawala kwake; Kristo aliruhusiwa kuyaongoza maisha yake.

Hii ndiyo sababu baadaye Paulo alisema yafuatayo kuhusu kazi kuu ajabu aliyoweza kuitenda:

*“Sitathubutu kuzungumzia chochote isipokuwa kile ambacho* ***Kristo*** *ametekeleza kupitia kwangu katika kuwaongoza wamataifa wamtii Mungu kwa kile ambacho nimesema na kutenda – kwa nguvu ya ishara na maajabu, kupitia nguvu ya Roho wa Mungu.”* (Warumi 15:18-19 NIV)

Jambo la msingi ni ***kuwa-ndani ya-Kristo***.

## “Kristo ndani yetu”

E.G. White alisema: “Ufahamu wa siri hii [Kristo ndani yetu] hutupatia ufunguo wa kila baraka nyingineyo. Huufungulia nafsi hazina za ulimwengu, uwezekano wa maendeleo yasiyo na ukomo.” (E.G. White, *Education*, uk. 172.1)

Yesu Kristo anataka kuishi ndani yetu. Kwa namna hii, anataka kutupatia maisha timilifu na kutenda kazi kupitia sisi, ama katika mambo madogo kabisa au mambo makuu. (Kwa maelezo zaidi kuhusu mada hii: *Kaeni Ndani ya Yesu* – sura ya “Yesu Anakaa Ndani Yako”, tazama www.steps-to-personal-revival.info)

John Wesley alitambua: “Mungu anaweza kufanya mengi zaidi akiwa na mtu mmoja ambaye ameadhimu [amesalimisha, amesabilisha] nafsi yake 100% kwa Mungu, kuliko awezavyo kutenda akiwa na umati wote wa wanadamu ambao wameadhimu nafsi zao 99% tu kwa Mungu.” (Joseph Kidder, *A Guide to a Spiritual Life,* Andrews University, PPP slide 14)

Neno la Mungu linatamka wazi katika Zekaria 4:6: *“Kile unachopanga wala hakitafanikiwa kwa nguvu za jeshi wala kwa uwezo wa kibinadamu; badala yake,* ***Roho Wangu atalikamilisha hilo!*** *Mimi, Bwana Mungu Mwenyezi, naahidi hili.”* (Zekaria 4:6 imefasiriwa kutoka kwenye sanifi ya Kijerumani, *Hoffnung für alle*)

Siku ya 14

## Mungu anaweza pia kutenda mambo makuu kupitia watoto na vijana

Mary Jones alizaliwa mnamo mwaka 1784 katika kijiji kidogo huko Wales. Alikulia katika familia ya ucha-Mungu ya Kimethodisti. Akiwa mtoto alipenda visa katika Biblia.

Baada ya kujifunza kusoma, alitamani sana kupata Biblia yake mwenyewe. Lakini zamani hizo Biblia zilikuwa aghali sana na wala hazikuwepo nakala nyingi. Katika siku za Jumapili, Mary aliruhusiwa kuisoma Biblia kwenye nyumba ya familia moja ya kitajiri iliyoishi takriban umbali wa kilomita nne. Ili amiliki Biblia yake mwenyewe, alianza kulipawa fedha kadiri alipoweza kwa kufanya kazi za suluba. Mathalani, siku moja alikusanya kuni na kuziuza, siku nyingine alifanya kazi ya kulea.

Ilimchukua miaka sita kutunza fedha za kutosha. Alipofikisha umri wa miaka 16, alitembea peku umbali wa kilomita 42 kutoka Langfihangel juu ya nyanda za milima hadi Bala, ili kununua Biblia kutoka kwa mchungaji mmoja huko.

Mchungaji Thomas Charles akamwambia kwamba alikuwa na Biblia mbili, lakini tayari zilikuwa zimeahidiwa kwa ajili ya watu wengine. Kwa masikitiko, asingempatia mojawapo. Mary alilia kwa uchungu! Alifadhaika sana. Ilhali akiwa ameudhika kiasi fulani, mchungaji akamuuliza kwa nini alikuwa analia. Alimwambia kwamba alikuwa akitunza fedha yake kwa ajili ya Biblia kwa miaka sita; aliposikia jambo hili alighairi na kumpatia Biblia moja. Akiwa na furaha tele, alianza safari yake kurudi nyumbani!

Mchungaji huyu aliguswa sana kiasi kwamba alisimulia uzoefu wake na Mary kwenye mkutano uliofuata wa *Jumuia ya Majarida ya Kidini.* "Hatuna budi kutafuta namna fulani ili kila mmoja huko Wales aweze kuinunua Biblia kwa gharama nafuu." Kuhusu hilo Robert William, mshirika wake akasema: "Kwa nini tusitafute njia kwa ajili ya ulimwengu wote?" Matokeo yake, jumuia ya kwanza ya Biblia ulimwenguni ilianzishwa (Jumuia ya Biblia Uingereza na Ughaibuni). Kufuatia mfano wao, jumuia za Biblia zaidi ya 140 zimeanzishwa hadi sasa.

Inashangaza kile ambacho Baba yetu ya mbinguni aliweza kufanya kupitia binti mmoja wa kawaida mtauwa! Hivyo, hebu tuzingatie maneno yafuatayo:

**Kamwe usidharau ushawishi wa mtu mmoja, pale ambapo utendaji wa Roho wa Mungu unapohusika kwa namna madhubuti. Pengine Mungu anakuita wewe kwa ajili ya wakati kama huu.**

(Usomaji unaoshauriwa: Esta 4:14-16 na pia: *Christian Service,* sura ya 26: Uhakikisho wa Mafanikio)

## Mungu Ameniandalia Kazi Pia

Kwa utukufu wa Mungu na pia kwa ajili ya kuwahimiza wasomaji, ningependa kuelezea jukumu ambalo Mungu alinipatia mnamo mwaka 2011/2012, bila hata kulitambua. Aliianzisha kazi ambayo ingegubika maisha yangu tena na tena. Kwa upande mmoja, nilpata uzoefu wenye changamoto kubwa, lakini kwa upande mwingine, vilevile nilpata uzoefu wenye ushindi mwingi na furaha kuu. Natambua vema kwamba kazi hii ambayo Mungu alinipatia, ni kazi Yake na inapaswa kubaki kuwa kazi Yake. Kila kazi ya mtu amruhusuye Mungu amtumie, ni ujenzi tu katika kazi kuu ya Mungu. Kwa sababu hii: "Ruhusu nuru yako iangaze kiasi kwamba utukufu utamrudia Mungu badala ya nafsi yako mwenyewe. ... Ruhusu nuru yako iangaze; jihadhari, ewe mtumishi wa Kristo, jinsi gani nuru yako iangazavyo. Kama inamulika kwenda juu mbinguni, ikidhihirisha ukamili wa Kristo, basi inaangaza vema. Kama inaelekea kwenye nafsi yako, kama unajidhihirisha mwenyewe, na unawavuta watu wakuhusudu wewe, ingelikuwa bora kwa ukae kimya kabisa: maana nuru yako hulenga kwenye mwelekeo mbaya." (E.G. White, *4T,* uk. 400.1, egwwritings.org)

## Mfano wa Kivitendo: Kueneza Machapisho ya Uamsho

Bila kutambua, Bwana alinianzishia kazi ya kusambaza machapisho ya uamsho. Hatua ya maendeleo ya vijizuu huni-onesha wazi kwamba mimi siye mwandishi husika, badala yake niliruhusiwa kuwa na bado ningali nyenzo mkononi mwa Mungu.

Ilianza hivi: Kupitia miguso minne tofauti, Mungu aliniha-masisha kuandaa mahubiri kadhaa kwenye mada ya maisha yaliyojawa Roho. Baada ya kuhubutu mojawapo ya mahubiri haya kanisani, ningeweza kuwapatia washiriki wote wa kanisa nakala tahiji ya hubiri. Nao waliwagawia marafiki zao nakala hizi. Hivyo, ndugu wawili viongozi wenye uzoefu wa kiteolojia

walipokea mahubiri yangu katika maandishi. Mmojawapo aliniandikia ifuatavyo mnamo Mei 1, 2012:

"Mahubiri yako juu ya *Hatua za Uamsho Binafsi* ni tunu kutoka mbinguni – kwanza kwa ajili yako kisha kupitia kwako kwa ajili ya wasomaji wote. … Japo hivi karibuni tumepokea vitabu kadhaa vya kivitendo na vya kina kiroho kanisani mwetu, mada ya *Hatua za Uamsho Binafsi* niya pekee. Katika namna iliyosheheni vilivyo na yenye maelezo ya kina, njia ya kujazwa Roho Mtakatifu imebainishwa. Yeyote asomaye hii hawezi kuepuka kufanya tathmini ya kiroho na kufanya uamuzi."

Wanateolojia wawili hawa walivutiwa sana kwa maudhui nao wakapendekeza kwamba nichapishe mahubiri haya katika vijizuu. Nililifikiria hilo ndipo nikahitimisha kwamba mahubiri hayo yangeunda tu kijizuu kidogo tu ambayo isingefaa kwa nyumba ya uchapishaji. Hivyo, sikufanya lolote kabisa juu ya hilo.

Lakini Mungu aliliona jambo hilo lote kwa namna tofauti. Kwa muda mrefu alikuwa na mpango. Na pia alijua jinsi gani ungefanikishwa.

Kupitia uongozi wa Mungu, muda mfupi baadaye nilipokea maulizo kutoka *Deutsch-Schweizerischen Vereinigung* (DSV – Konferensi ya Ujerumani-Uswisi) huko Zuriki. Wangependa kutahiji **mahubiri yangu kama kijizuu.** Nao walikuwa wakiomba ruhusa. DSV aliahidi kushughulikia vidokezo vyote vya kina (marekebisho, upangaji wa maandishi (usawiri), picha, kutahiji nukuu, nk.). Nilichelea kuliamini hilo! Chini ya uongozi wa Mungu toleo la kwanza la Kijerumani la *Hatua za Uamsho Binafsi* ilichapishwa mnamo Oktoba 2012 bila mipango yoyote kutoka kwangu.

Kabla ya kuanza kuchapisha, DSV iliwasilisha kwa konferensi na unioni zingine zinazozungumza Kijerumani pamoja na Unioni ya Austria pia. Konferensi ya Baden-Württembergische huko Kijerumani na Unioni ya Austria zikajiunga na mkakati huo na sasa nakala 9,200 zilikuwa zikihitajika.

Tulisonga mbele kwa imani thabiti na kuweka oda ya kuchapa nakala **10,000**. Hata hivyo, mchapaji alifanya kosa bila kukusudia na kuchapa nakala **13,500**. Tungefanya nini

sasa? Tulitumainia ahadi katika Warumi 8:28, ambapo inasema mambo yote hutenda kazi pamoja kwa ajili ya mema ya wale wampendao Mungu, hivyo tukakubali kutumiwa ziada hiyo.

Kinachoshangaza, nakala hizi 13,500 punde zikawa zimeisha nasi tukalazimika kuendelea kuchapisha nakala zaidi. Inastaajabisha, sivyo? Tangu wakati huo yamekuwepo matoleo 8 ya Kijerumani ya *Hatua za Uamsho Binafsi* pamoja na jumla ya nakala 45,000. Washiriki wengi wa kanisa ambao mioyo yao iliguswa kwa ujumbe husika walisaidia kusambaza vijizuu (broshua) hizi.

Je Maandiko yanasema nini kwa mara nyingine tena katika Waefeso 2:10 NIV: *"Maana tu kazi ya mikono Yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu ili* ***tutende matendo mema, ambayo Mungu alituandalia kwa usabiki ili tuyatende.****"*

## Bwana aliandaa mbinu nyingi kuu za usambazaji!

Mungu alihakikisha kwamba ujumbe huu umesambazwa kwa namna mbalimbali kwa watu wengi kadiri iwezekanavyo. Nimepokea na kuendela kupokea mialiko mingi makanisani ndani ya nchi na ng'ambo maombi yakiwa kuendesha semina ya *Hatua za Uamsho Binafsi*. (Inajumuisha saa nne: Kusimulia uzoefu mbalimbali siku ya Ijumaa, hubiri siku ya Sabato na saa mbili wakati wa mchana.)

Wakati huohuo, wapo ndugu wengine wanaosaidia kuendesha semina hizi. Wahubiri wengi ulimwenguni kote hutumia mada hizi katika mahubiri yao.

Mambo yafuatayo yalikuja kwa sababu ya uongozi wa Mungu, bila mipango yoyote kwa upande wangu: rekodi ya video, rekodi ya kusikiliza vitabu, usambazaji wa kitabu-e kupitia Amazon, pamoja na ufasiri katika lugha nyingi. Bwana aliniunganisha na wanandoa waliokuwa wameunda tovuti ya Kijerumani na Kiingereza. Kijerumani: www.schritte-zur-persönlichen-erweckung.info–Kiingereza: www.steps-to-personal-revival.info). Vijizuu(Brosha) zinaweza kusomwa mtandaoni, zinaweza kupakuliwa bila gharama au kutumwa kwa mtu mwingine – mathalani, *Hatua za Uamsho Binafsi*

katika lugha 40 na mfululizo uitwao *Kaeni Ndani ya Yesu* katika takriban lugha 20. Kwa pamoja zimetahijiwa nakala milioni 1.3 halafu na idadi isiyojulikana mtandaoni kutoka nchi 143 (hadi kufikia Agosti 2020).

Wasomaji wengi wamesimulia uzoefu wao. Unaweza kuzisoma kwa kuangalia kwenye “Erfahrungen” au “Shuhuda” (takriban 160).

Kutokana na shuhuda zaidi ya 500 za ana au maandishi ambazo nimepokea, vidokezo zaidi vimeongezwa kwenye vijizuu(brosha) hivi. Zinaonesha mahali ambapo *Hatua za Uamsho Binafsi* humfikisha mtu:

- Tunatambua bayana kwamba Roho Mtakatifu ni tunu ya thamani zaidi ambaye Yesu anatukirimia.
- Machapisho haya hufumbua macho yetu ili tufanye tathmini sahihi kuhusu hali yetu ya kiroho.
- Tunakuwa na ufahamu bora zaidi wa hatua mbili muhimu zinazopelekea tuwe na maisha ya kuvutia kiroho na uhakikisho wa wokovu.
- Tunapoomba kwa ahadi, maombi yetu hupata ubora mpya kabisa. Tunaomba kwa furaha, kwa ujasiri na kina zaidi. Kwa kuomba kwa ahadi, wengi hupokea uhakikisho kwamba wamempokea Roho Mtakatifu.
- Furaha yao kuu iliwafanya wawe mashuhuda na waliwashirikisha wengine na vijizuu(brosha), jambo lililoongeza furaha yao hata zaidi.

Naweza tu kustaajabu juu ya miujiza mikuu ya Mungu na kusema kwa furaha: *“Mfanyieni Bwana shangwe, dunia yote; Mtumikieni Bwana kwa furaha.”* (Zaburi 100:1-2) *“Kwa kuwa furaha ya Bwana ni nguvu zenu.”* (Nehemia 8:10)

Naliona jambo hili kwa namna hii: Bwana alinipatia jukumu la mwandishi na mratibu. Kutokana na kazi “yangu,” Mungu aliwapatia wengine wengi kazi ya pili yao wenyewe. Kazi hii ya pili inahusisha maombezi, ufasiri, urekebishaji, maombi, ufadhili wa kifedha, kuunda mpangilio, maandalizi ya utahijishaji, utahijishaji, kuanzisha miunganiko, misaada ya usambazaji, kuwasilisha shuhuda, kutengeneza (kusanidi) tovuti, nk. Ni jambo la pekee ajabu kwamba Bwana hulipatia kundi fulani jukumu. Kazi ya kuokoa ni ya thamani sana kuliko kama kila mtu angefanya kazi

peke yake. Mungu anataka kutuunganisha sisi kwa sisi. Nataka kuwasilisha shukrani zangu za dhati kwa ajili ya mawasiliano ya pekee ajabu kwa dada na kaka, ambao Bwana alifanya iwezekane. Baadhi walikuwa wa muda mfupi tu, wengine wa mrefu au mrefu sana. Kijumla, ni muhimu kwa hao wote waliohusika wajue: Kupitia neema ya Mungu, mimi ni mtendakazi-mwenza katika mpango mkuu wa Mungu. Natenda kazi, ama, Kristo hutenda kazi kupitia kwangu kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Nimeruhusiwa kupata uzoefu wa Mungu akitenda mambo makuu na yastaajabishayo. Mambo yanayoenda vizuri kabisa kuliko uwezo wetu, Naweza tu kumsifu na kumtukuza Yeye, nami nataka kuendelea kumtumikia kwa furaha!

**Mungu anataka kumtumia kila mmoja!** Kwa kweli, mara nyingi huwachagua wanyonge kabisa, ambao wana ahadi hii: *"...Uweza wangu hutimilika katika udhaifu."* (2 Wakorintho 12:9)

## Mara nyingi Mungu huwachagua wanyonge kabisa

Hudson Taylor, mmishenari mkuu na mashuhuri, ambaye kupitia kwake Mungu alianzisha Misheni ya China-Bara, aliwahi kusema, wakati mtu mmoja alipomsifu kwa ushawishi wake mkubwa katika kazi ya utume:

"Inaonekana kwangu kwamba Mungu aliitazama dunia nzima akimtafuta mtu fulani aliyekuwa dhaifu kiasi cha kuifanya kazi Yake. Hatimaye aliponipata mimi, akasema: 'Huyu ni dhaifu kabisa – ataifanya kazi hii.' Watendakazi wote mahiri wa Mungu walikuwa watu dhaifu waliomfanyia Mungu mambo makuu kwa sababu waliamini kwamba Mungu alikuwa pamoja na."

## Uzoefu

TAARIFA YA KUMSIFU MUNGU kutoka Osaka/Japani:

**Kufunga na kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Takriban papohapo...**

Sheri A.: Tulianza harakati ya kuanzisha kanisa katika eneo la Osaka huko Japani. Baada ya mwaka mmoja, bado hatukuwa na yeyote aliyehudhiria ibada au kupokea masomo ya Biblia. Tuliamua kujiunga na Siku 100 za Maombi, na hususan kufunga

na kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu mnamo mwezi Mei. **Takriban papohapo** Bwana aliwagusa wanandoa kwenye supamaketi moja waliokuwa wakitafuta kanisa, na kumtafuta Mungu. Punde walitaka masomo ya Biblia. Kwa sababu ya mlipuko wa maradhi, hawakuwa wakifanya kazi, hivyo tulifanya masomo ya Biblia kila siku, nao wakaanza kuhudhuria huduma za ibada. Pia, mmojawapo wa majirani zetu akaanza kuja kanisani. Hivyo, idadi yetu ilizidi maradufu siku ya Sabato, na kanisa hili dogo linakua! Mungu asifiwe!

Siku 100 za Maombi, Staanani ya Maombi (Siku ya 100)

Jumuia ya Huduma za Kichungaji ya Koferensi Kuu, Julai 4, 2020.

***Sala yangu: " Baba uliye mbinguni, tafadhali tusamehe sote mahali ambapo tumetenda kwa kujitumainia nafsi. Tujalie moyo mnyenyekevu uliosabilishwa Kwako kwa kujisalimisha kikamilifu. Tusamehe kwamba mara nyingi tumegemea tu matokeo ya wastani. Tafadhali tukirimie Roho Wako Mtakatifu kila siku! Tuwezeshe kutambua majukumu ambayo umetupangia katika wakati huu. Tafadhali tupatie uamsho na matengenezo halafu tutumie kwa ajili ya hatima kuu ya injili. Ni Wewe pekee ustahiliye heshima na utukufu. AMINA."***

## Mawazo binafsi na mwongozo wa mjadala

1. *Kuna tofauti gani kati ya mimi kumfanyia Mungu kazi au Mungu kufanya kazi kupitia kwangu?*

   ______________________________________________

2. *Kuna mifano gani ya Biblia iliyopo ya Mungu kumtumia mtu kwa ajili ya kazi kuu?*

   ______________________________________________

3. *Jinsi gani Paulo aliweza kutenda kazi ya utume kuu ajabu kiasi hicho?*

   ______________________________________________

   ______________________________________________

4. *Ni ahadi gani tulizo nazo zinazoonesha kwamba Bwana anataka kufanya mambo makuu kupitia sisi?*

   ______________________________________________

   ______________________________________________

## Muda Wetu wa Maombi

- Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.
- Sali pamoja na mwanamaombi mwenzio…

1. … ili kuona endapo mnatumika kwa uwezo wenu au endapo Mungu anatenda kazi kupitia ninyi katika uwezo Wake.
2. … kwa ajili ya hekima kutambua kanuni zinazodhirika katika mifano ya Biblia ya kusaidia na kutumikia.
3. … kwa ajili ya uhusiano sahibu pamoja na Mungu ili uwe nyenzo ya Mungu hasa.
4. … kwamba uweze kutambua ni wapi chini ya uongozi wa Mungu unaweza kusaidia katika mazingira yako na kanisani pako.

SURA YA 4

Siku ya 15

# Miaka Makini ya Mafunzo

## Kana umuhimu gani ambao ni mbinu bora katika kuwaongoza watu kuja kwa Yesu Kristo?

Kwanza, ningependa kusimulia uzoefu mwingi kidogo niliokuwa nao kama mchungaji katika uongoaji roho. Zilikuwepo sababu mbili mahususi zilizonihamasisha kuandika uzoefu mwingi: 1. Ili watu wengine wasifanye makosa yaleyale niliyofanya na 2. Ili wengine waweze kufaidika kutoka na uzoefu chanya.

Ili kumhamasisha kila mmoja, ningependa kueleza kwamba mimi – na ndugu wengine wawili – tuliitwa kutumika kama wachungaji bila mafunzo yoyote ya kiteolojia, kwa maneno mengine kama walei. Hii ilitokea kwa vile ulikuwepo upungufu mkubwa wa wachungaji wakati huo. Kabla ya hapo, nilikuwa nimejifunza mengi kwa kipindi cha miaka 22 ya kazi kanisani.

Maneno machache kuhusu historia yangu:

Natokea familia ya Kiadventista. Nilikuwa na umri wa miaka 17 nilipobatizwa. Nilikuwa kijana mwenye haya sana. Walakini, kamati ya uteuzi kanisani ilinipendekeza kama mwalimu msaidizi wa shule Sabato. Na kama ilivyokuwa kawaida wakati huo, sikuwa na ujasiri wa kutosha kujenga hoja tofauti. Nilishinda aibu yangu kidogokidogo kupitia kazi ya shule Sabato. Baada ya miaka kadhaa, nihudumu kama kiongozi wa shule Sabato, kiongozi wa vijana, kiongozi wa huduma za kichungaji na kiongozi wa kanisa. Kabla sijawa mchungaji, nilifanya kazi katika biashara kwa miaka 22. Maarifa niliyopata huko yalithibitisha kuwa yenye manufaa sana katika kazi yangu ya kichungaji. Wakati fulani, kampuni niliyoifanyia kazi ilinipatia fursa ya kupanua ujuzi wangu wa lugha ya Kiingereza huko Uingereza kwa mwaka mmoja. Kwa vile nilichagua shule yetu ya Kiadventista, Chuo cha Newbold, niliweza pia kuchukua

baadhi ya masomo ya Biblia. Hata hivyo, wakati huo sikujua muda si mrefu ningekuwa mchungaji.

Mke wangu mpendwa alikuwa msaada mkubwa wakati wa huduma yangu. Baba yake alikuwa mchungaji na mwalimu. Tayari alijua mambo mengi kutoka nyumbani kwao; lakini siyo hivyo tu, pia aliwahi kuwa msaada wa kivitendo(halimali) nyumbani kwao na kwenye kanisa mahalia. Ndipo Mungu akanipatia msaada zaidi kwa namna ya rafiki mwema na shemeji yangu – hawa wawili walikuwa wachungaji pia. Naam, naweza kusema kwamba Mungu aliniita katika jukumu tofauti kabisa, lakini alikuwa amehakikisha kwamba nilikuwa nimeandaliwa kwa namna nyingi na kwamba nilikuwa na msaada zinazohitajika.

## Ni kitu gani cha muhimu katika uongoaji roho?

Nilikuwa mchungaji nilipokuwa na umri wa miaka 38. Baadhi ya juhudi zangu kuu za kuwaongoa watu kwa ajili ya Kristo, mwanzoni zilileta matokeo duni tu. Kushindwa huku kulinifanya nichunguze kwa kina mbinu yangu. Na kwa msaada wa Mungu, taratibu nilitambua nilichohitaji kufanya kwa namna tofauti. Kadiri nilivyotekeleza maarifa haya mapya, matokeo yalikuwa chanya sana.

Yafuatayo ndiyo niliyojifunza:

Kama kanuni, ni vema kufuata mtiririko ufuatao:

- Kumtambulisha Yesu na kuwasaidia wengine wamkubali.
- Kuendesha kozi ya uanafunzi ili kuanzisha au kuimarisha uhusiano pamoja na Kristo, kusaidia ufahamu wao wa msamaha wa hatia na jinsi gani ya kuishi maisha katika nguvu ya Roho Mtakatifu.
- Baada ya hili, kweli msingi za Biblia zinaweza kuzingatiwa.
- Mtu anapofundishwa kwa jinsi hii, basi tunakuwa tunawasaidia wafanye maamuzi kwa ajili ya ubatizo na kanisa.

Kwa umbali gani unaweza kuambatana na mtu fulani kwenye mapito haya, mara zote hutegemea jinsi gani walivyo radhi kuitikia ushawishi wa Roho Mtakatifu.

Umbali ambao watendakazi pamoja na Yesu wanaweza kuambatana na wapendwa kwenye mapito haya, daima utatofautiana sana.

## Uzoefu wangu wa kwanza madhubuti

Nilipoanza kazi yangu ya kichungaji mnamo mwaka 1968, kampeni ya ulimwengu mzima ya *Biblia Yasema* ilianzishwa. Wale waliokuwa wakishiriki walienda nyumba kwa nyumba wakifanya tathmini ya mtazamo wa kidini. Baada ya uchunguzi huo, watu walipewa zawadi ya Biblia. Yeyote aliyevutiwa alipewa Biblia papohapo. Lakini masharti yalikuwa kwamba Biblia haikuwa yao kabisa hadi pale walipokuwa wamekamilisha masomo 24 ya Biblia. Wakati huo wakapewa masomo mawili ya kwanza na masomo haya yangekusanywa baada ya juma moja au mawili – kadiri yanavyohitajika – ili yasahihishwe na ndipo wangeachiwa masomo mawili yanayofuata.

Kwa bahati njema, kanisa, nililolisimamia wakati huo, likajiunga kwa moyo kwenye mradi huu. Kila Sabato jioni tulitoka na takriban watu 24 katika vikundi vya wawiliwawili katika msimu wote wa baridi wa mwaka 1968/69. Baada ya miezi michache, tulikuwa na watu 700 waliokuwa wakijifunza masomo haya. Shughuli hii ya utume ilikusudiwa kwa ajili ya maandalizi ya mkutano mkuu wa injili. Mfululizo huo wa mkutano wa injili uliendeshwa na mwinjilisti wa Konferensi Kuu, Andrew C. Fearing, kuanzia Aprili 1969. Ndugu fulani, Reinhard Rupp, mwinjilisti Unioni ya Kusini mwa Ujerumani, akaendeleza mfululizo wa hotuba hizo. Alifuatiwa na wazungumzaji wengine kadhaa walioendesha mihadhara kila Ijumaa, Jumamosi na Jumapili; kwa pamoja ilifanyika mihadhara 100. Kwa neema ya Mungu, ndani ya miaka miwili wahudhuriaji 32 wa mikutano ya injili, waliokuwa wamegundua mawasilisho haya kwa namna mbalimbali, walibatizwa. Nilitumia miongozo 10 ya kujifunza Biblia kutoka kwa Fordyce W. Detamore ili kuwasaidia watu wafanye maamuzi. (Leo, ningependekeza: Mark Finley, Ushawishi – Jinsi ya kuwasaidia watu wafanye uamuzi kwa ajili ya Yesu.)

Kinachosikitisha, alikuwepo mwanamke mmoja tu kutoka darasa la ubatizo, aliyekuwa miongoni mwa washiriki wetu 700 kwenye kampeni za Biblia Yasema. Tulijiuliza sababu ingekuwa ipi kwa ajili ya matokeo haya “duni.” Baada ya muda fulani, tuligundua yafuatayo: Tulijikita sana kwenye “kazi ya posta” na wala hatukufanya juhudi ya kutosha kutafuta mawasiliano

binafsi. Halikadhalika, tulisadikishwa kwamba miongozo ya kujifunza Biblia iligusia stahimani haraka kupita kiasi – kabla mtu hajaongozwa aje kwa Yesu. Na mpaka baadaye ndipo tulitambua kwamba kukosa kwetu Roho Mtakatifu kulichangia pia matokeo yetu "haba." Tulikuwa tumefanya angalau miito ya simu kwenye nyumba angalau 10,000 kama sehemu ya kampeni ya Biblia Yasema na licha ya juhudi zetu kuu, tuliweza kumleta kwenye ubatizo **mtu 1** tu kutoka katika **orodha ya watu 700**.

Nimeeleza kwa kina sana katika uzoefu mchache kwa sababu tu nataka kuwaepusha watu wengine zoefu kama hizi. Na ni rahisi sana kujifunza kutokana na uzoefu wa watu wengine kuliko kuzifanya wewe binafsi.

## Uzoefu wangu wa pili madhubuti

Kampeni yangu kuu iliyofuata ilifanyika mnamo mwaka 1971/72 katika kanisa tofauti. Kwa mara nyingine tena, tulienda nyumba kwa nyumba na kujitambulisha kwa watu tukifanya tathmini ya mawazo. Lakini wakati huu mara tu baada ya uchunguzi, tuliuliza **swali lililojaribiwa na kupimwa vilivyo kutoka kwenye kijitabu cha Kijerumani *Jitwalie Uzima*** (*Ergreife das Leben*): **"Tukichukulia kwamba ungekufa leo, hivi ungekuwa na uhakikisho wa uzima wa milele pamoja na Yesu Kristo?"**

Kama kanuni, hii ilisababisha usomaji wa papohapo wa kijitabu husika pamoja nao. Maudhui ni muhtasari mdogo wa mpango wa wokovu katika hatua nne na huhitimisha kwa ombi la kujisalimisha. Baadhi ya watu waliguswa sana kiasi kwamba walitupata anuani za wanafamilia wao na wakatuomba tuwatembelee na kupitia kijitabu husika pamoja nao vilevile.

Baada ya kukamilisha kusoma kijitabu hiki na watu wenye shauku, ndipo tulijifunza pamoja nao masomo matano yaliyochapishwa na idara ya vijana ya Konferensi Kuu kuhusu namna ya kuwaongoza vijana waje kwa Yesu. Na baada ya hapo tu ndipo takatumia mfululizo wa Biblia Yasema.

Kijumla, tulikuwa na washiriki 150 kwenye kozi ya Biblia Yasema.

Baada ya hapo, tulianzisha mfululizo wa mkutano mkubwa wa injili wa vipindi zaidi ya 52 jioni mzungumzaji akiwa

Mwinjilisti Kurt Hasel. Mwishoni mwa mawasilisho haya watu 13 walibatizwa; miongoni mwa hawa, **watu saba** walitoka kwenye **mawasiliano yetu ya 150**. Matokeo ya kampeni hii kubwa ya pili yalikuwa bora sana kuliko yale ya kwanza, ambapo tulifanikiwa kumbatiza mtu mmoja kutoka kwa washiriki 700.

Nimeeleza kwa kina sana katika uzoefu mchache kwa sababu tu nataka kuwaepusha watu wengine uzoefu kama hizi. Na ni rahisi sana kujifunza kutokana na uzoefu wa watu wengine kuliko kuzifanya wewe binafsi.

## Uzoefu wangu wa tatu madhubuti

Uzoefu yangu mkuu uliofuata katika makanisa mawili kwenye mji mkubwa mnamo mwaka 1973/74. Baada ya kufanya mihadhara sita ya injili pamoja na tabibu Dkt. Waldemar Maretz ili kuwatafuta watu wenye shauku, tuliwaalika kwenye kikundi cha kujifunza Biblia. Wageni saba na washiriki saba wa kanisa walihudhuria. Kwa pamoja, tulijifunza kwenye vijizuu (brosha) tisa kutoka katika *mfululizo wa uanafunzi*. Ulikuwa wasilisho juu ya uanafunzi uliojengwa kwenye Biblia na ulioandaliwa kwa umahiri, ambao pia ulijumuisha utangulizi juu ya *uinjilisti binafsi*. Katika mfululizo huu yalikuwepo masomo mawili kuhusu *Kuishi pamoja na Roho Mtakatifu.* Wasilisho hili lilikuwa limeandaliwa ili kusaidia kushughulika na matatizo ya msingi yafuatayo:

- Wakristo wengi hawana uhakika kuhusu uhusiano wao binafsi pamoja na Kristo.
- Wanaishi maisha yenye hali za fadhaa na kushindwa.
- Hawajui jinsi ya kuwasilisha kwa wengine imani yao kwa namna fanisi. [2]

Baada ya mfululizo huu wa wastani juu ya uanafunzi, tuliwaalika wageni hao saba kwenye mfululizo wa injili ya muda mrefu ambao ungedumu kwa vipindi zaidi ya 52 vya jioni. Mwishoni watu 13 walibatizwa, **watano** miongoni mwao walitoka kwenye **mawasiliano yetu saba.**

2 Mwandishi Dkt. William Bright – Matatizo hamali yalibainishwa kupitia utumiaji wa mbinu ya uchunguzi wa kina wa mitazamo ya watu.

Haya yalikuwa matokeo bora kabisa ambayo Mungu aliwahi kunipatia katika kazi ya namna hii. Hebu tulinganishe tena:

- 1 mmoja kutoka majina ya watu(mawasiliani) 700
- 7 mmoja kutoka majina ya watu(mawasiliani) 150
- 5 mmoja kutoka majina ya watu(mawasiliani) 7

Kama tuwezavyo kuona, mkakati ulioratibiwa vizuri huwa na mchango madhubuti katika kusaidia kuongoa watu waje kwa Yesu. Kumbuka: Yeyote anayekosea kufunga kishikizo cha kwanza kwenye jaketi, kamwe hatapatia hatua nzima. Mwishowe, atalazimika kufungua upya kila kitu na kuanza tena.

Yeyote asiyekuwa na "mwanzo" sahihi katika ufundishaji juu ya imani, kwa kawaida hawezi kutegemea matokeo mazuri. Na hatua zinazofuata vilevile hazina budi kupangiliwa vema tusikengeuke kwenye "uchochoro." hivi "vichochoro." hata vinaweza kuwa vya kuvutia, lakini havileti matokeo halisi – kuwaongoza watu waje kwa Yesu.

Baada ya uzoefu huu wa tatu, ambao ilikuwa chanya sana, daima nilianza kwa kujifunza wasilisho juu ya uanafunzi nikiwa na watu wapya wenye shauku. Kabla ya hili, au wakati mwingine mwafaka, ningeweza kupitia pamoja nao kijitabu kiitwacho *Jitwalie Uzima*. (Sura ya 7 kwenye kitabu hiki.) Ni baada ya hapo tu ndipo niliwasilisha mfululizo mkuu wa kujifunza Biblia.

Nilijifunza kwamba wanaofanya uamuzi kwanza kwa ajili ya Yesu wanahamasika zaidi, na mara nyingi huwa na nguvu kubwa zaidi katika kuyakubali na kuyatekeleza mafundisho ya Biblia.

Siku ya 16

## Uzoefu maalumu pamoja na vijana kanisani

Mnamo mwaka 1978 niliialika kamati ya vijana kutoka kanisa fulani huko Saarland ili kujifunza pamoja nao kutoka kwenye wasilisho la uanafunzi. Mwanzoni vijana hao walikuwa na mashaka fulani. Lakini hii ilibadilika haraka kadiri walipokuwa wafuasi wa Yesu wenye ujasiri na furaha kwenye somo hili. Tulipotaka kulishawishi kanisa ili kuendesha semina juu ya mada hizi, vijana waliwasilisha shuhuda za kuvutia. Halikadhalika Bwana alitumia wasilisho hili la uanafunzi ili kuwaongoza watu katika utekelezaji wa furaha wa imani.

Wakati nikifanya kazi huko Saarland, niligundua watu wangapi waliomba maombi ya kujisalimisha baada ya kupitia kijitabu kiitwacho *Jitwalie Uzima*. Walikuwepo watu 62 na 30 miongoni mwao walibatizwa. Nataka kumsifu na kumshukuru Bwana kwa ajili ya hili!

## Uzoefu zangu huko Bad Aibling katika mada ya uanafunzi na masomo ya Biblia

Kuanzia mwaka 1984 nilikuwa nasimamia makazi ya wastaafu huko Bad Aibling (Ujerumani). Kati ya 1985 na 1994 tuliendesha semina Maisha Bora kila msimu wa chipukizi na kipupwe. Wakati mwingine tuliipatia semina jina tofauti, hata hivyo, maudhui yalikuwa yaleyale. Kila wakati ulikuwa mfululizo wa vipindi 11-12 vya jioni. Kwa msaada wa Mungu, tuliweza kuwaongoa watu kwa ajili ya Kristo takriban katika kila semina. Baadhi ya wageni na waajiriwa kwenye makazi ya waliostaafu(ustajiri) nao walihudhuria semina hii mara mbili au tatu.

Kila jioni, semina ilikuwa na muundo ufuatao:

Kwanza, wasilisho la **dakika 30** lilifanywa juu ya **afya au familia** au kitu fulani kama ***Wakristo katika maisha ya kazi***.

**Sehemu kuu** ya huduma hiyo ya jioni ilitumika katika kujibu **maswali juu ya uanafunzi** (mfululizo wa vijitabu tisa). Tuliongeza mada zingine, kama vile *Umuhimu wa Kanisa Mahalia katika Maisha yetu ya Imani* na *Mivuto(Ghiliba) ya Ushirikina*. Baada ya hilo tungefanya mafunzo makuu ya Biblia kwa wale wenye shauku.

Kuanzia mwaka 1984 tuliwasilisha mafunzo stadi mbalimbali kwenye makazi yetu ya wastaafu: usimamizi wa ofisi, utunzaji wa nyumba, mapishi, usaidizi wa utabibu wa wazee (mwaka 1) na unesi kwa ajili wazee (miaka 3 madarasa yakiwa kwenye shule maalumu ya mafunzostadi).

Pamoja na hilo, tuna vijana watano wanaofanya huduma hanimu (mbadala wa utumishi jeshini).

Tunapowaajiri vijana tunawauliza endapo pia wangevutiwa na madarasa ya Biblia na madarasa ya afya mbali na mafunzo stadi. Tuliwaomba waelewe kwamba umuhimu(tunaadinasi)

wa nafasi chache za kazi mafunzni(uanagenzi) ni kwa ajili ya vijana ambao wangevutiwa na fursa nzima. Tulisisitiza kwamba wanapaswa kutuchagua tu endapo wanavutiwa na fursa yote kamili. Kuhudhuria madarasa ya mafunzo stadi, madarasa ya Biblia na madarasa ya afya lingekuwa suala la lazima kwenye kipindi cha mafunzo.

(Leo, ningejumlisha madarasa ya kijamii vilevile, kwa kutumia kitabu cha Mithali za Sulemani. Kitabu hiki kina ukamili wa Biblia kwa ajili ya maisha yetu binafsi na maisha yetu ya kazi. Siyo tu kwamba hubainisha mwenendo sahihi, lakini pia mashartiasili husika ya kitabia yanayohusiana na kumcha Mungu.)

Tuliwaambia vijana kwamba ni wajibu wao wenyewe kuhusu kile ambacho wangefanyia maarifa yao mapya ya imani na afya. Karibu waombaji wote waliamua kwamba walitaka kuja. Kwa namna ya kustaajabisha Mungu alitupatia mwanadada Mwadventista mahiri sana, aliyeendesha madarasa ya Biblia na madarasa ya afya na pia alisimamia semina nyingi za Biblia. Alipata mafunzo ya kichungaji na vile vile alikuwa na hati ya kufundishia utunzaji wa nyumba kwenye chuo cha ufundi cha wanawake.

Tulifurahi kwamba angalau mtu mmoja alibatizwa kila mwaka. Ilikuwepo miaka miwili ambapo katika kila mmoja tuliwabatiza watu saba – wengi wao walikuwa vijana waajiriwa. Hii ilikuwa njia bora ya kuwafikishia vijana imani yetu. Hivyo, kama taasisi tuliweza kusaidia kutimiza utume mkuu wa Kristo. Hivyo, ilikuwa njia sahihi na yenye mafanikio kwa sababu tuliwaongoza watu waje kwa Yesu kwanza.

## Uundaji wa Kikundi Kinacho saidia kwa ajili ya Utume Ulimwenguni

Katika mwaka 1994 kanisa huko Bad Aibling kikundi kinacho saidia kwa ajili ya utume ulimwenguni kama idara binafsi kanisani. (Taarifa huko Ujerumani kuhusu miaka 25-Shere za Kitimiza miaka hiyo, www.missionsbrief.de: 25 Jahrfeier). Mnamo mwaka 1990 Konferensi Kuu ilipitisha mpango wa utume ulimwenguni. Walihamasisha wazo la kukubali(unasabishaji)

ukanda wa watu milioni ambao haujafikiwa, kwa lengo la kuanzisha kanisa la kwanza hapo. Tulijitolea kama kanisa la Bad Aibling. Tuliombwa kuwasiliana na konferensi huko Tashkent-Uzbekistani. Tuliishia kuchukua fursa ya kusimamia "ukanda wa watu milioni" ambao haujafikiwa huko Navoiy nchini Uzbekistani. Kwa sababu ya baraka za Mungu, tuliweza kuanzisha kanisa huko lenye washiriki takriban 200. Pamoja na hilo, kituo cha kanisa kilijengwa.

Kazi ya utume isiyotarajiwa iliibuka kutoka kwenye mianzo hii hafifu chini ya uongozi wa Mungu na neema Yake. Tulijifunza mengi wakati tukifanya kazi pamoja na viongozi wetu na usaidizi wa utume. Bwana hubariki ushirikiano wa pamoja. Yafuatayo yalitokea:

- Kuanzia mwaka 1994 **makanisa yalianzisha na waasisi** (wamishenari walei wa kudumu). **Shule ya utume ya walei** ilianzishwa kwa ajili ya mafunzo ya waasisi huko Navoiy-Uzbekistani. Katika kipindi cha miaka minne tu wamishenari walei 42 walifunzwa; 41 miongoni mwao walianza kufanya kazi kama wamishenari walei wa kudumu. Kupitia juhudi zao **"kanda 10 zenye watu milioni" huko Uzbekistani zilifikiwa.** Katika kila moja ya maeneo haya, makanisa ya vikundi vilianzishwa. Kwa sababu ya shughuli zake, **watu zaidi ya 500 walibatizwa.** Baada ya uzoefu huu wa kustaajabisha, kikundi chetu saidizi huko Bad Aibling kilianza kuendesha miradi miwili huko Turkmenistani kuanzia mwaka 2001/2002. Kisha mwaka 2006 miradi mitatu huko India iliongezwa. Ellen White alisema yafuatayo kuhusu kazi ya utume binafsi na ughaibuni:
- "Washirki wetu wa kanisa wanapaswa kupata **shauku ya kina** katika **utume nyumbani na ughaibuni**. Baraka kuu zitawajia kadiri wanavyofanya juhudi za kujitoa nafsi ili kupandikiza kweli makini kwenye eneo jipya. **Fedha zilizowekezwa katika kazi hii zitaleta matokeo tele**." *(Testimonies for the Church, vol. 9,* uk. 49.3)

  "Kazi ya umishenari wa nyumbani utazidi kuendelezwa kwa kila namna pale ambapo roho ya ukarimu, ya kujikana

nafsi, na kujitoa nafsi itakapodhihirishwa kwa ajili ya ustawi wa utume ughaibuni; **maana ustawi wa kazi nyumbani hutegemea kwa kiasi kikubwa, ikiongozwa na Mungu, fanaka rejeshi ya kazi ya uinjilisti ifanyako katika nchi za mbali**." (*Testimonies for the Church, vol. 6,* uk. 27.5)

Tulipata uzoefu wa ukweli wa nukuu hizi! Hii "fanaka rejeshi" kwa upande wetu ilikuwa:

▶ Kuanzia mwaka 1999 makanisa yalianzishwa huko Ujerumani kupitia wachungaji, washiriki wa kanisa na waasisi. Makanisa yaliyoshiriki kwenye kazi ya utume ughaibuni huko Uzbekistani kwa takriban miaka 8-10 (kuanzia mwaka 1995), walianzisha makanisa tanzu katika kipindi hiki **tu**:
- Kanisa huko Bad Aibling – katika mji wa Feldkirchen Westerham
- Kanisa huko Lindau – katika mji wa Wangen, huko Lindenberg halafu pamoja na kanisa hili tena huko Isny
- Kanisa huko **Überlingen** – katika mji wa Pfullendorf na huko Markdorf

Makanisa yaliyoshiriki kwenye kazi ya utume ughaibuni yenyewe yalikuwa yameanzishwa takriban miaka 100 kabla. Ni pale tu yalipopata uzoefu "fanaka rejeshi", uliotokana na kazi ya utume ughaibuni, ndipo walipoendelea katika "kazi yao ya utume nyumbani".

Majukumu mengine muhimu yakafuata:

Kuanzia mwaka 1994 jarida la utume Missionsbrief lilichapishwa. Kusudi lake ni kuhabarisha na kuhamasisha katika maeneo ya uanzishaji makanisa, kazi ya utume nyumbani na ughaibuni, uamsho na maisha ya kiroho. (Usambazaji: nakala 13,000 kwa ajili ya makanisa huko Ujerumani, Austria na Uswisi.)

▶ Mnamo mwaka 2003 shule ya misheni huko Navoiy-Uzbekistani ilifungwa kwa amri ya serikali. Kwa msingi wa matokeo madhubuti ya shule hii – ndani ya miaka minne 41 waasisi/wamishenari walei waliingia kwenye kazi ya utume muda wote – tuliwasiliana na asasi ya Kimataifa ya Vituo Kungani huko Marekani na kuweka mapendekezo

ya kuanzisha taasisi ambayo ingesaidia kujenga shule za wamishenari walei ulimwenguni – msisitizo ukiwekwa kwenye uinjilisti wa afya. Baada ya mashauriano, mnyororo wa maombi wa watu 150 ulianzishwa na walihimizwa waombe hadi tupate ubayana wa jambo hili – endapo Mungu alitaka tuwe na taasisi ya namna hiyo. Baada ya muda mfupi, ilikuwa dhahiri kabisa kwamba Mungu wetu mkuu alitaka taasisi ya namna hiyo. Hii ilipelekea uanzishwaji wa **L.I.G.H.T.- Lay Institute for Global Health Training (Taasisi ya Walei ya Afya Ulimwenguni)** yenye makao yake makuu huko Wildwood/Marekani.

Kusudi: utumishi/mashauriano/msaada katika uanzishaji wa shule ndogo za uinjilisti wa afya ulimwenguni (mafunzo yakidumu kwa miezi 6-12) na kuendesha kozi za uinjilisti wa afya muda wa mwezi mmoja. **Leo, LIGHT ni amilifu katika nchi zaidi ya 100.** Takriban **watu 5,000-6,000** wamefanya mafunzo ya afya ya miezi 6-12 kwenye **shule za misheni** zinazoshirikiana na LIGHT na zaidi ya **watu 24,000** wamefanya mafunzo ya kina ya majuma manne (hadi kufikia mwisho mwa mwaka 2019).

- Tangu mwaka 2012 **uhamasishaji wa machapisho ya uamsho** pamoja na wasilisho madhubuti la Siku 40 kutoka kwa Dennis Smith. Hili ni somo bora la kiroho na kiinjilisti ambalo nimewahi kuona. Tuliratibu ufasiri na usambazaji wa *Vitabu vya Siku 40, juzuu ya 1-5* kutoka kwa Dennis Smith, pamoja na *Hatua za Uamsho Binafsi*, *Kaeni Ndani ya Yesu* na *Washirika wa Yesu Waliojazwa Roho* kutoka kwa Helmut Haubeil. Pamoja na hilo, tovuti zifuatazo zimeanzishwa: www.schritte-zur-persönlichen-erweckung.info na Global Mission.
- Kuanzia mwaka 2014 **ilianzishwa tovuti** www.gotterfahren.info, ili watu wanaotafuta waweze kupata maisha maridhawa katika uhusiano binafsi pamoja na Mungu. Tovuti hii huendesha kwa ushirikiano na Taasisi ya Tumaini la Biblia huko Ujerumani, Austria, Uswisi na Luxembourg. Taasisi hizi huwahudumia watu wanaotafuta ambao huwasiliana nao. Tovuti hii iliundwa

kwa ushirikiano na Ilja Bondar kutoka Advedia. Tovuti hii hutembelewa mara 3,000 hadi 5,000 kwa mwezi.

Kwa neema ya Mungu, hadi sasa nimeweza kusaidia kikundi hiki kwa ajili ya miaka 25. Naweza tu kurudia tena na tena kumshukuru na kumsifu Mungu wa pekee ajabu kwa ajili ya uongozi Wake pamoja na uzoefu mwingi tuliopata kwa fadhila. Pamoja na hilo, naweza tu kumshukuru Bwana na Mkombozi wetu mpendwa, Yesu Kristo, kwamba alinikirimia maisha timilifu katika taluma yangu na katika ustaafu. Nikiwa na furaha tele, nimeweza kuwa sehemu ya kazi ya Mungu ya uamsho ulimwenguni katika siku za mwisho za historia ya ulimwengu!

*"Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Basi, ndugu zangu wapendwa, mwimarike, msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana siku zote, kwa kuwa mwajua ya kwamba taabu yenu siyo bure katika Bwana."* (1 Wakorintho 15:57-58)

Hebu tumtumikie Bwana wetu wa pekee ajabu, tukiwa na Yesu Kristo mioyoni mwetu na tukiwa tumejazwa nguvu ya Roho Mtakatifu. Tunataka kumshuhudia Kristo katika maneno na matendo yetu – kumpa Mungu heshima, kwa ajili ya wokovu na baraka ya wanadamu wenzetu na kwa ajili ya ukuaji wetu wenyewe kama wafuasi wa Yesu, kwa ajili ya furaha na utimilifu wetu wenyewe.

***Sala ya Shukrani: "Baba uliye mbinguni, nataka kukusifu na kukushukuru kwa ajili ya uongozi wako adhimu. Asante kwa vile kanisa letu mahalia lilikuamani Wewe na lilikuwa radhi kujitolea na kuchukua hatua fulani katika utume ulimwenguni. Nataka kukushukuru kwa ajili ya watu wote waombao, watoao, na wasaidiao. Asante kwa ajili ya hao wote walioshiriki – waasisi, makanisa, ofisi za utawala na huduma saidizi. Ulituongoza ili tuweze kusaidia katika wokovu wa watu. Tafadhali endelea kuwa pamoja nasi na pia kazi yetu ya utume! Asante kwamba tuliweza kudhahimu "fanaka rejeshi"! Sasa tunakuomba kwa ajili ya uamsho na matengenezo ulimwenguni kote! Naam, tunataka utangazwaji mkuu wa mwisho wa injili ufanyike sasa, ili Yesu aweze kuja tena hivi karibuni! Baba, sifa na utukufu viwe Vyake milele na milele! AMINA."***

## Uzoefu

### *Mwenyekiti wa nchi yenye vizuizi huko Asia*

"Naomba kwamba kitabu hiki kiweze kubadilisha kazi yetu yote ya utume. Mimi ni mwenyekiti wa Fildimisheni. Ndipo nimemaliza usomaji wangu wa kwanza wa kitabu hiki *Hatua za Uamsho Binafsi*. Nasikitika kwamba sikujua kuhusu kitabu hiki hapo awali, lakini nashukuru kwamba sasa Mungu amenionesha kitabu hiki.

Kwa kweli, nilipokea kitabu hiki kama zawadi kutoka kwa rafiki fulani. Sikutegemea mengi sana, lakini mara tu nilipokifungua kitabu hiki, kilianza kugusa maisha yangu ya kiroho. Hivyo usiku wa jana nilituma faili za pdf za kitabu hiki kwa wafanyakazi wetu wote, na kuwaomba wakisome pamoja na wanafamilia wao. kuanzia leo, nitakisoma tena pamoja na mkewe wangu, na pia nitakituma kitabu hiki kwa wanangu na mkwe wangu. Wakati nikielezea kitabu hiki kwa wafanyakazi wetu, nilitambua kuwa fasiri yake katika lugha zetu mbili kuu iko njiani. Naomba kwamba kitabu hiki kiweze kubadili kazi yetu ya utume. Tutakichapisha katika lugha zetu ili washiriki wetu waweze kubarikiwa kwa uwepo wa Roho Mtakatifu maishani mwao. Sababu ya kuandika baruapepe hii ni kuomba hisani yako, kama unaweza kuja na kuzungumza kwenye makimbi la familia ya watendakazi wetu. Kama unaweza kuja na kuwaongoza wafanyakazi wetu, basi litakuwa jambo adhimu hasa.

Naomba kwamba Bwana wetu aendelee kukutumia pamoja na kitabu chako ili kuleta uamsho katika kanisa Lake." (H.J. EE090220 #148)

**Washiriki wetu zaidi ya elfu kwenye saa ya maombi mtandao wakitumia kitabu cha "Kaeni Ndani ya Yesu"** Naishi katika mji wa Curitiba-Paraná, Brazili. Mwaka uliopita kanisa letu lilisambaza kitabu, *Hatua za Uamsho Binafsi*. Ni kitabu cha pekee ajabu. Tayari nimekisoma mara tatu. Tayari nimeandaa mahubiri matatu kuhusu ujumbe huu. Nilifuraha sana kwamba rafiki fulani alinialika katika saa ya maombi: kila siku saa 11 alfajiri. Kikundi hiki cha maombi kinajifunza kutoka kwenye kitabu cha pili, "Abiding in Yesu". Kupitia vitabu hivi viwili, ndugu zaidi ya elfu sasa ni wanakikundi katika

saa moja ya maombi kila siku. Miujiza na shuhuda hujitokeza miongoni mwetu. Nilipojiunga na darasa hili mwezi mmoja uliopita, tulikuwa wanafunzi 200. Kila siku Mungu anawaleta ndugu wengine zaidi kwenye kikundi chetu wamtafutao Roho Mtakatifu na kujiandaa kwa ajili ya marejeo ya Kristo. Watu wengi wanajiunga kutoka nchi zingine kupitia ZOOM. Sasa, baada ya mwezi, tayari tu washiriki zaidi ya 1000 na kikundi hiki kinazidi kukua na kukua zaidi. Mungu ashukuriwe. Wachungaji watano huongoza darasa hili, ambalo limewakifishwa kwa ajili ya kumtafuta Roho Mtakatifu. Darasa hili linatujenga sana. Nakushukuru kwa moyo wangu wote kwa ajili ya vitabu hivi juu ya Roho Mtakatifu. Umenipatia mtazamo mpya kuhusu Mungu na Roho Mtakatifu. Asante sana kwa ajili ya kila kitu. (L.T.G. EE11112020 kutoka Brazili 170)

## Mawazo binafsi na mwongozo wa mjadala

1. *Ni hatua zipi husaidia katika uongoaji roho? Zaidi ya yote, nini apaswacho kujifunza mtu ili ajue na kupenda?*

   ______________________________

   ______________________________

2. *Ni jambo gani lenye umuhimu wa pekee wakati wa kuwasilisha injili, na lipi linapaswa kuepukwa?*

   ______________________________

   ______________________________

3. *Kwa nini mada hii ya uanafunzi ni muhimu na ya lazima sana?*

   ______________________________

   ______________________________

4. *Nini uwezacho kujifunza kutokana na uzoefu uliotajwa hapa?*

   ______________________________

## Muda Wetu wa Maombi

- Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.
- Sali pamoja na mwanamaombi mwenzio…
  1. Ili kupata ufahamu bora wa tabia ya Mungu kupitia Yesu na kubadilishwa uwe katika sura Yake.
  2. Kutambua njia sahihi ya kuwafikishia watu injili.
  3. Kuwa na kudumu kuwa wanafunzi waaminifu wa Yesu.
  4. Ili kupata uzoefu katika kazi yako uitendayo pamoja na Mungu itakayoimarisha imani yako.

Siku ya 17

SURA YA 5

# “Nitawafanya Kuwa Wavuvi wa Watu”

Nini kinachomfanya Yesu amvutie kila mmoja kwa njia ya pekee?
Kwa nini anataka tuwaongoze watu wengine waje Kwake?
Kwa nini na kwa jinsi gani Yesu hutufanya kuwa wavuvi wa watu?
Nawezaje kuwa shuhuda fanisi kwa ajili ya Yesu?

## Ni kwa namna gani Yesu ni mwenye umuhimu wa pekee kwa kila mmoja? Nini ambacho Yesu hunifanyia, ambacho hakuna yeyote awezaye kufanya?

Yesu aliteseka kwa ajili yangu, akafa kwa ajili yangu na kufufuka tena. Alikuwa hana hatia(msalihi) lakini hata hivyo alikufa kwa ajili ya hatia yote ya maisha yangu. Hii ni ishara kuu zaidi iliyopo ya upendo. Na japo anatawala ulimwengu mzima, anaisha kwa ajili yangu. Nataka kumshukuru kwa ajili ya upendo Wake wa pekee ajabu kwa ajili yangu. Akiwa Mkombozi na Kuhani wangu Mkuu, anatetea hazina Yake adhimu ya neema kwa ajili yangu. Anafanya mbadilishano mkuu nami: hujitwalia hatia yote ya maisha yangu. Alilipa gharama yake msalabani. Hunipatia haki Yake. Hivyo, naweza kuishi bila mzigo wa hatia.

Huvunja nguvu ya dhambi maishani mwangu kiasi kwamba **silazimiki** kutenda dhambi. hunilinda dhidi ya dhambi na malaika walioanguka. Hutupatia maisha maridhawa na huibadili tabia yangu iwe bora hatua kwa hatua; hunipatia talanta zinazoniwezesha kumtumikia Yeye. Huniweka huru dhidi ya majeraha na utumwa. Huniongoza maishani mwangu na kunipatia nguvu ya kuamini upendo wa Mungu na kuzifuata sheria Zake. Aliniandikia barua ya upendo kupitia neno Lake, ambalo hunipatia msingi imara kwa ajili ya maisha yangu na ushauri mwema kwa ajili ya wakati wa sasa na milele. Kwa kawaida, ningeshutumiwa kwa hukumu ya Mungu kama

matokeo ya hatia. Kwa vile Yesu ni mwombezi wangu na anatetea haki Yake kwa ajili yangu, nimesamehewa hatia zangu zote. Bila Yeye ningelazimika kusimama mbele hukumu nikiwa mstakiwa. Hata sasa hunipatia maisha timilifu. Na wakati wa ufufuo au wakati wa kubadilishwa kwangu, maisha haya yataendelea katika uzima wa milele wenye utukufu. Yesu ni wa pekee. Hakuna yeyote aweza kuichukua nafasi Yake.

## Ushirika pamoja na Yesu ni uhusiano wa thamani zaidi uliopo

Tunapotafakari kwa muda kitambo, itakuwa dhahiri kwamba dhamani yetu ya kujisalimisha kwa Yesu hutuongoza kuingia katika urafiki wa karibu na usio kifani pamoja Naye. Je una rafiki mwaminifu zaidi kuliko Yesu? Mtu fulani angeweza kubadilisha uhusiano huu wa kina? Je uhusiano wa upendo wa kina pamoja na Kristo umekuwa msingi wa maisha timilifu kwako? Namshukuru Yesu kila siku kwamba hunidhamani na kunipenda – kwamba hata niko katikati ya upendo Wake. Namuuliza: Ruhusu urafiki wetu daima uimarike halafu nidumishe katika upendo huu.

Pale uhusiano wako binafsi pamoja na Yesu unapokuwa kitu cha thamani zaidi maishani mwako, basi nini jambo bora kabisa unaloweza kumtendea mtu mwingine?

## Ni upi msaada wa thamani zaidi niwezao kumpatia mtu fulani? Yapi manufaa makubwa zaidi ambayo kwayo naweza kuelekeza mawazo yao?

Je kuna chochote cha thamani zaidi kwa ajili ya wapendwa wako, jamaa, marafiki na watu mnaofahamiana? Je unataka kuwasaidia wapate urafiki kama huo muhimu na bora? Ni jambo zuri kabisa unaloweza kumfanyia mwingine. Yesu alisema: *“Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.”* (Yohana 10:10) na *“Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima.”* (1 Yohana 5:12) Kwa neema ya Mungu, tunaweza kuwaelekeza wengine njia ya kuyaendea maisha mapya na uzima wa milele. Hii ni furaha kuliko nyingine yoyote! Ni nadra kupata

uzoefu mwingineo wa kiroho unaosisimua na kukirimu kama “tamashani ya kushuhudia kuhusu Yesu” – vile Kristo alivyo na kile anachomaanisha kwangu.

Nikiwa mfanyabiashara kijana, nilijifunza kutokana na machapisho yahusuyo mafanikio kwamba: “Kila mtu huruhusu nafsi yake iguse wengine(ishawishiwe) kwa ajili ya manufaa yake mwenyewe.”

Mara nilipojizoeza hili katika mauzo ya huduma za usafirishaji, nilipata mafanikio makubwa.

Katika maisha ya imani, ni muhimu kwamba wanadamu wenzetu waweze kuona matokeo mema ya uhusiano wetu pamoja na Yesu maishani mwetu. Mfikirie mtu aliyepagawa pepo ambaye Yesu alimponya. Yesu alimwambia: *“Enenda zako nyumbani kwako, kwa watu wa kwenu, kawahubiri ni mambo gani makuu aliyokutendea Bwana, na jinsi alivyokurehemu.”* (Marko 5:19)

## Kipi kigezo muhimu zaidi?

Kama nataka kuwaonesha watu wengine njia ya kuja kwa Yesu, basi napaswa kwanza mimi binafsi niwe nimempata na kuunganika kwa ukaribu pamoja Naye. Biblia huiita hii “kuwa ndani ya Kristo.” Hii imetajwa mara 170 kwa namna tofauti katika Agano Jipya. Bwana anataka tuwe na utambuzi bayana kuhusu uhusiano wetu pamoja Naye. *“Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele…”* (1 Yohana 5:13) Je nina uhakikisho wa wokovu leo? Hivi nina hakika kwamba nimeokolewa – siyo mwishoni mwa maisha yangu, bali sasa? Robert Folkenberg alisema: Hakuna uhakikisho, hakuna utume. Tunaweza tu kushuhudia kisadikifu kuhusu wokovu wetu kupitia Kristo pale tunapojua kwamba tumeokolewa.

## Shauku ya Yesu

Yesu anataka kuwafikishia watu wengine upendo Wake – mathalani kupitia Wakristo waliojazwa Roho Mtakatifu. Anataka kuwavuta wanaume, wanawake na watoto waje Kwake kupitia sisi. Anataka kunifanya mimi na wewe tuwe mfereji wa upendo Wake. Anataka kuwafanya watu wawe watahiniwa wa Ufalme wa Mungu kupitia mimi na wewe.

## Unaionaje shauku ya Yesu?

Pengine hujawahi kamwe kumwongoza mtu fulani aje kwa Yesu. Lakini nina hakika kwamba ungependa kufanya hivyo. Je tatizo linaweza kuwa wapi? Zinaweza kuwepo sababu mbili.

1. Je unajua jinsi ya kuishi maisha nadhifu, yenye ushindi, yaliyojawa Roho?
2. Je unajua jinsi ya kuwashirikisha wengine imani yako kuhusu Yesu kwa namna ufanisi?

Sikulijua hilo kwa muda mrefu…

Hali yetu ni sawa na ile aliyokuwa nayo Petro. *"Tweka mpaka kilindini, mkashushe nyavu zenu mvue samaki. Simoni akajibu akamwambia, Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu; lakini kwa neno Lako nitazishusha nyavu. Basi, walipofanya hivyo walipata samaki wengi mno, nyavu zao zikaanza kukatika."* (Luka 5:4-6) Wengi wanaweza kuthibitisha: Hatujavua chochote. Lakini tukiwa na Kristo mioyoni mwetu kupitia Roho Mtakatifu, tunaweza kutupa nyavu zetu tena.

## Jinsi gani tunaweza kuwa wavuvi wa watu?

Yesu alimwambia Petro na Andrea – na inatuhusu sisi sote vilevile: *"Nifuateni, Nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu."* (Mathayo 4:19) Kwa mujibu wa fasiri nyingine: *"Njoni pamoja Nami, nitawafundisheni kuwavua watu."* (GNT) Tunaitwa kumfuata Yesu katika uwezo na chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Naye anawajibika katika kuwafanya "wavuvi wa watu" kutoka kwangu na kwako. Alisema: *Nitawafanya kuwa wavuvi wa watu*. Yeye ndiye hulifanya hilo, siyo mimi wala wewe. Yeye ni mjuzi, nami ni mwanafunzi.

## Jinsi gani Yesu aliwafanya wanafunzi Wake wawe wavuvi wa watu?

Sasa nitawasilisha sehemu ya shuhuda nilizopokea kutoka kwa watu baada ya kuanza kujilisamisha kila siku kwa Yesu na kuomba wakirimiwe Roho Mtakatifu. Tafadhali zingatia kwa kina jinsi Yesu alivyoweza kuwafanya wavuvi wa watu.

- ▶ Baada ya *Siku 40* za maombi, mchungaji aliandika: “Washiriki wa kanisa, waliokuwa wakiogopa kuzungumza na wageni, ghafla wakazungumza na watu kwa hiari.” Je hatua ya badiliko ilikuwa ilikuwa nini? Maisha katika Roho Mtakatifu. (#532, 1)
- ▶ Katika kipindi cha kutwa, Roho wa Mungu hushuhudia tena na tena kwenye roho yangu kwamba mimi ni mtoto wa Mungu na kwamba nina uhakikisho wa uongozi Wake. Furaha niliyo nayo kutoka kwenye uzoefu huu mpya wa Ukristo hububujika kutoka ndani yangu na imewahamasisha baadhi ya washiriki wa kanisa nao pia wasome kijitabu hiki. (#532,37)
- ▶ Matokeo ni ya kustaajabisha sana kwa sababu hamasa mpya na furaha ya ndani havipiti bila kutambulika. Katika kipindi hiki nimepata uzoefu mwingi sana. Pia nilitafuta fursa mbalimbali ili kupitisha kile kilichoenea ndani yangu. (#532,38)
- ▶ Pale ninapoweza kueleza habari za Yesu Kristo, ndipo ninajawa furaha kuu. (#532, 46)
- ▶ Nilizoea kuchukulia kazi ya utume kama wajibu. Sasa imekuwa shauku yangu kuzungumza na watu kuhusu Yesu. Siyo tu kwamba Yesu ameamsha hitaji hili ndani yangu, lakini pia amenipatia fursa nyingi. Nataka kumsifu na kumtukuza Mungu kwa ajili ya hili. (#532,48)
- ▶ Ni jambo la pekee ajabu kupata uzoefu jinsi Roho Mtakatifu anavyonionesha na kunifundisha vile Yesu anipendavyo na namna anavyoshughulika na wapotevu. Sasa naweza kuzungumza kwa uhuru kuhusu Yesu, kwa asili kabisa kiasi kwamba karibu kila mtu anasikiliza. Roho Mtakatifu huratibu fursa za kukutana na mazungumzo mara nyingi katika kiwango cha kina, kiasi kwamba naweza tu kustaajabu. Sasa, natamani kwamba kila mmoja aliye karibu nami angeweza kudhahimu kile ninachopata. (#532, 54)
- ▶ Awali, Roho Mtakatifu aliniongoza mara mojamoja ili kushuhudia. Sasa hutokea kila siku. Wala sihitaji “kuandaa hotuba,” kwa sababu Mungu hinipatia maneno sahihi kwa vile ndiye hasa ajuaye moyo wa mtu huyo mwingine. (#532,57)

Uzoefu huu wote uilikuja baada ya watu hawa kuanza kuomba kwa imani wakirimiwe Roho Mtakatifu na kumpokea. Pamoja na hilo, walisalimisha maisha yao kwa Yesu kila siku na walikuwa tayari kutumika. Nadhani kwamba tunaweza kuona kwenye shuhuda hizi jinsi Yesu anavyoweza kuanza kuwafanya wavuvi wa watu kutoka kwetu. Analifanya hilo kwa kuishi ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu. (Angalia kijitabu: *Kaeni Ndani ya Yesu*, sura ya: Yesu Akaaye Ndani Yenu.) Maisha pamoja na Roho Mtakatifu hubadili mtazamo wetu juu ya utume na hutupatia uwezo wa msingi na furaha kwa ajili ya hilo.

## Juhudi Binafsi

Ellen White aliandika: "Juhudi na shauku pekee, binafsi kwa ajili ya marafiki na majirani zako zitafanikisha mengi zaidi kuliko inavyoweza kukadiriwa. … Nenda kwa majirani zako [marafiki, watu unaofahamiana nao] mmoja baada ya mwingine, halafu wakaribie hadi mioyo yao inapokuwa imeguswa kwa shauku na upendo wako usio na ubinafsi. Huzunika pamoja nao, waombee, tafuta fursa mbalimbali za kuwatendea mema." (E.G. White, *Review and Herald*, Machi 13, 1888) Ni nadra kupata uzoefu mwingineo wa kiroho ambayo hutufanya kupata furaha tele na ridhaa kama uzoefu wa kuwaambia wengine kuhusu Kristo na kuwaongoza waje Kwake. (Maelezo zaidi kuhusu hili baadaye.)

## Ni kwa Vigezo Vipi Ndipo Naweza Kuwaongoza Watu Waje kwa Yesu?

Siku ya 18

Sasa, tunataka kujifunza kuhusu vigezo ambavyo huyafanya maisha yetu na ushuhuda wetu kwa ajili ya Yesu uwe na ufanisi. Tunataka kudumisha dondoo hii iwe rahisi kadiri iwezekanavyo. Tunapofuata hili, ndipo maisha yetu huwa maridhawa nasi tutamletea Mungu matunda katika njia nyingi mpya.

***Sala: Hebu tuombe kila siku: "Bwana, nifanye niwe radhi kuwa tayari kwa ajili ya kila kitu unachotaka. Tafadhali, amsha ndani yangu shauku ya kuwaongoa watu waliopotea waje Kwake. AMINA."***

## Uhusiano pamoja na Kristo

Tunapokuwa "ndani ya Kristo", ndilo sharti muhimu zaidi tayari limetimilika. Ni muhimu sana kwamba tunaiweka wakfu nafsi zetu kwa Yesu kila asubuhi – pamoja na kila kitu tulicho nacho na na vile tulivyo. Halikadhalika, tunapaswa kuomba kila siku tujazwe Roho Mtakatifu; tunapaswa kuomba kwa uhakika na kwa namna bora tukitumia ahadi. Kwa namna hii, Yesu Kristo anaishi ndani yetu, aliyesema: *"Kaeni ndani Yangu, Nani ndani yenu…akaaye ndani Yangu Nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote."* (Yohana 15:4-5) Neno la Mungu hutualika kujichunguza nafsi: *"Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe. Au hamjijui wenyewe, kwamba Yesu Kristo yu ndani yenu? Isipokuwa mmekataliwa."* (2 Wakorintho 13:5) Mungu anataka tujue hali yetu kiroho. Je ni wakati gani tunakosa sifa au tunakosa umahiri? Umahiri wetu hutegemezwa na Kristo ndani yetu pale tunapokuwa tumejawa Roho Mtakatifu. Kwa mantiki hiyo, kukosa umahiri huonesha kwamba hatuna Kristo "mioyoni" mwetu na kwamba hatukujazwa Roho Mtakatifu. Biblia huiita hali hii kuwa watu wa mwilini (kuishi kwa nguvu za kawaida za kibinadamu bila Roho Mtakatifu, au bila kujazwa vilivyo na Roho Mtakatifu). (1 Wakorintho 3:1-4; Warumi 8:1-17) Gari haliwezi kufanya kazi bila mafuta, Mkristo naye hawezi kutenda kazi bila Roho Mtakatifu. *"Lakini mtapokea nguvu* [umahiri, pekee]*, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi Wangu…"* (Matendo 1:8)

Sasa, tunataka kuangalia kwa ufupi, lakini kwa makini dondoo nyingine ya ziada. Nataka kurudia: unapofuata hili, utapata maisha timilifu nawe utamletea Mungu matunda katika namna mpya. Pengine utaacha "nyavu" za kazi yako ya sasa na kujihusisha katika kuwaongoa watu kwa ajili ya Yesu kupitia Yesu.

## 1. Kujisalimisha kwa Kristo

Je nimeadhimu kikamilifu maisha yangu kwa Yesu Kristo? Hivi ninajisalimisha Kwake kila siku pamoja na kila kitu nilivyo na nilicho nacho? Kujisalimisha kwangu kuna umuhimu gani?

(Kwa maelezo ya kina zaidi tazama *Kaeni Ndani ya Yesu*, sura ya 2 Kujisalimisha hadi Yesu na sura ya 3 Yesu Akaaye Ndani Yenu.)

**Kujisalimisha kikamilifu kwetu kwa Yesu Kristo ni kiini** cha wokovu kwa ajili ya maisha mapya (Yohana 3:1-21), kwa ajili ya ushindi dhidi ya dhambi (Warumi 8:1-4), kwa ajili ya kujazwa Roho Mtakatifu (Waefeso 3:16-17) na kwa ajili ya uhakikisho wa wokovu.

Roho Mtakatifu ni karama ya Yesu adhimu zaidi kwa wanafunzi Wake. Roho Mtakatifu ni karama iletayo karama zingine zote pamoja nayo. "Lakini kama ilivyo kila ahadi nyingineyo, hukirimiwa kwa masharti. … Wanamzungumzia Kristo na kuhusu Roho Mtakatifu, lakini hawapokei manufaa yoyote. **Hawaisalimishi nafsi** iongozwe na kutawaliwa na mawakala wa kiungu." (E.G. White, *The Desire of Ages,* uk. 672.1) Wengi hawajasalimisha nafsi zao kwa Mungu – mara nyingi kwa kutojua – nao huyaratibisha maisha yao wenyewe. Hii inaweza kuwa chanzo cha kukosa Roho Mtakatifu. Ndiyo maana kipengele hiki kina sehemu itwayo: Kujitoa kikamilifu(Kujiadhimu) kwa Yesu Kristo.

"Wale wamwaminio Kristo kama asemavyo katika neno Lake, na kusalimisha nafsi zao chini ya uangalizi Wake, maisha yao ayaratibishe Yeye, watapata amani na utulivu(stahamani). Hakuna lolote la ulimwengu linaloweza kuwahuzunisha Yesu anapowafanya wawe na furaha kwa uwepo Wake. Katika ridhaa kamilifu kuna pumziko kamilifu." (E.G. White, *The Desire of Ages,* uk. 331.2)

## Kwa nini kujisalimisha?

Kujisalimisha imeelezewa bayana kitabu kiitwacho *Njia Salama*: "**Mungu ana shauku ya kutuponya, kutuweka huru.** Lakini kwa vile hili huhitaji badiliko letu kamili, ubadilikaji(uhawilinishwaji) wa asili yote, lazima *tusalimishe nafsi zetu Kwake kikamilifu…*

**Mungu huweka mbele yetu kimo cha baraka ambacho ana shauku kutufikisha kupitia neema Yake**. Anatualika tujikabidhi Kwake ili aweze kutenda mapenzi Yake ndani yetu. Inabaki kuwa wajibu wetu kuchagua endapo tutawekwa huru kutoka kwenye

kifungo cha dhambi, ili kushiriki tukufu pekee wa wana wa Mungu.” (E.G. White, *Steps to Christ,* uk. 43.2-43.4)

Kujisalimisha kwetu kwa Mungu huleta baraka zisizokadirika. Mungu anatuita tujisalimishe kwa sababu anataka kutuponya na kutuweka huru. Kutoka kwenye nini? Yesu anaporuhusiwa kuyaongoza maisha yetu, ndipo anaweza kutuweka huru dhidi ya ukatili wa ubinafsi wetu, mathalani, husuda, hasira, ukuu, ulafi, uraibu, ghadhabu, kiburi, majivuno, kufa moyo, adhali changamani, nk. Kumbuka: Kila mtu ni tatizo kuu la nafsi yake mwenyewe. Wewe ni tatizo kuu nafsi yako mwenyewe. Ni Mungu pekee ndiye awezaye kutuongoza katika uhuru halisi. Lakini mfinyanzi anaweza tu kufinyanga udongo ulioko mikononi mwake. Ndiyo sababu Mungu anahitaji tujisalimishe.

## Ahuweni na Kukombolewa kupitia Kujisalimisha

Kwa namna hii, Mungu anahitaji pia kutuweka huru kutoka kwenye nguvu ya dhambi (Warumi 8:1-4) na kutupatia uongozi na ulinzi wa kiungu (1 Yohana 5:18). Pamoja na hilo, kujisalimisha huyafanya maisha yetu yawe rahisi zaidi. E.G. White alisema: “Usalimishwaji wa nguvu zetu zote kwa Mungu hurahisisha kwa kiasi kikubwa sana tatizo la maisha. Hudhoofisha na kufupisha mapambano elfu dhidi ya tamaa za moyo wa asili.” (*My Life Today*, uk. 6.6, egwwritings.org)

## Sharti la Lazima: Kujazwa Roho Mtakatifu

Yesu anatupatia maagizo muhimu ili tuwe mashuhuda Wake: *“Lakini mtapokea nguvu [kwa mashariti, uwezo], akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi Wangu... hata mwisho wa nchi.”* (Matendo 1:8) Yesu **aliwaamuru** wanafunzi Wake wangojee ili wajazwe Roho Mtakatifu kabla hawajaanza kazi yenye uhai(amilifu) kwa ajili Yake (Matendo 1:4). Hii huonesha kwamba Roho Mtakatifu ni sharti la muhimu sana kwa ajili ya ushuhudiaji wetu. Yesu yumo ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu. Anatuwezesha kushuhudia. *“Maana pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote.”* (Yohana 15:5) Yesu alisema: *“Nao wakamshinda* [joka] *kwa damu ya Mwanakondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao*

*hawakupenda maisha yao hata kufa."* (Ufunuo 12:11) Tutakuwa washindi: kwa damu ya Mwanakondoo – kafara Yake kwa ajili yetu huwa fanisi kupitia dhamani yetu ya kujisalimisha kwa Yesu – na kwa neno la ushuhuda wao – kwa kuwaambia wengine kile ambacho Yesu ametufanyia. Hawakuyapenda maisha yao hadi kufa, hutuonesha kwamba maisha yaliyosalimishwa kwa Kristo yalidumishwa hadi mwisho wa maisha yao. Kujisalimisha humaanisha kuishi kwa ajili ya Yesu (2 Wakorintho 5:15).

## Kujisalimisha – imeelezewa kwa kina

Lengo kuu la 'Kujisalimisha kwa Yesu' limefafanuliwa kwa kina katika kitabu cha pilil cha mfululizo uitwao *Hatua za Uamsho Binafsi*. Kitabu hiki kinaitwa *Kaeni Ndani ya Yesu*. Sura ya pili: "Kujisalimisha kwa Yesu". Inapendekezwa sana kusoma upya sura hii.

## 2. Kujazwa Roho

Yesu alisema katika Yohana 15:4 NIV: "*Bakini ndani Yangu, kadiri ambavyo Mimi pia nabaki ndani yenu."* Ama Yesu anadumu ndani yangu, hilo hutegemeana na mimi mwenyewe. Anatuonesha wazi kabisa yapi matokeo ya kukaa ndani ya Kristo: *"Akaaye ndani Yangu Nami ndani yake, huyo **huzaa sana**; maana pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote. Mtu asipokaa ndani Yangu, **hutupwa nje** kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea. Ninyi mkikaa ndani Yangu, na maneno Yangu yakikaa ndani yenu, **ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa.** Hivyo hutukuzwa Baba Yangu, kwa vile mzaavyo sana; nanyi mtakuwa wanafunzi Wangu."* (Yohana 15:5-8)

## Nakaaje ndani ya Jesus Kristo?

Tuna maelezo adhimu kuhusu maneno ya Yesu "kaeni ndani Yangu" katika *The Desire of Ages*. Humaanisha:

- *kuendelea daima kumpokea Roho Wake* (hivyo, kuomba kila kukirimiwa Roho Mtakatifu na kumpokea.)
- *maisha ya kujisalimisha kikamilifu katika utumishi Wake*

(Kwa sababu hii, tuanajitoa upya(tunahawilinisha) kila asubuhi hatua yetu ya kujisalimisha.) (E.G. White, *Desire of Ages*, uk. 676.2 egwwritings.org)

## Njia ya Furaha ya Kweli

Ufumbuzi huu wa kiungu wenye vipengele viwili ni njia ya maisha ya furaha. Kwa nini? Yesu alieleza: *"Hayo nimewaambia, ili furaha Yangu iwe ndani yenu, na furaha yenu itimizwe."* (Yohana 15:11)

Kristo anaishi ndani yetu kupitia hatua hizi mbili (kuendelea kumpokea Roho Wake pamoja na maisha yaliyosalimishwa kikamilifu kwenye utumishi Wake) na ni njia ya furaha kamilifu. Ni njia ya furaha ya kweli.

## "Kila Siku" ndiyo siri

Yesu alisema katika Luka 9:23 kwamba uanafunzi wetu ni suala la kila siku. Na 2 Wakorintho 4:16 hutaja kwamba mtu wa ndani anahawilinishwa siku kwa siku. Tunapaswa kuomba kila tujazwe Roho Mtakatifu (Luka 11:13 na Waefeso 5:18 katika Kiyunani: endelea kuomba) na kila siku tunapaswa kujitoa upya (kuhawilinisha) kwa hatua yetu ya kujisalimisha kwa Yesu Kristo. Nadhani hili ndilo lengo kuu la ibada yetu ya asubuhi kwa kila mmoja wetu. Yesu anataka kuambata nasi mchana kutwa (angalia Mathayo 6:33). Je unaomba ukitumia ahadi, ili upate uhakika wa kumpokea Roho Mtakatifu? (1 Yohana 5:14-15; Marko 11:24; 2 Petro 1:3-4)

## Maelezo ya Kina kuhusu Maisha Yaliyojazwa Roho

Ningependa kumrejesha yeyote ambaye angependa kusoma kwa kina kuhusu mada hii, kwenye kitabu kiitwacho *Hatua za Uamsho Binafsi*, hususan sura isemayo "Je Matatizo Yetu Husuluhika?" Huonesha kwa nini kujisalimisha kila siku kwa Yesu na kuomba kila siku kukirimiwa Roho Mtakatifu ni muhimu na lazima. Pia unaweza kusoma sura isemayo "Ufunguo wa Uzoefu wa kivitendo" kwenye kitabu hichohicho, ambayo huonesha jinsi ya kuomba kwa kutumia ahadi ili kupata

uhakika kwamba maombi yetu kwa ajili ya Roho Mtakatifu yamejibiwa.

Siku ya 19

## 3. Sala ya Maombezi
## Jinsi Gani Naweza Kufanya Sala ya Maombezi Iliyojazwa Roho?

***Kwa nini tuwaombee watu wengine?***

E.G. White anasema:

"Kwa maombi mengi, lazima ujitaabishe kwa ajili ya roho, maana hii ndiyo njia pekee ambayo kwayo unaweza kuifikia mioyo." (*Evangelism*, uk. 341.3) Hivyo, sala ya maombezi iliyojazwa Roho ndiyo njia pekee ya kuifikia mioyo ya watu.

Mchungaji fulani aliandika: Uzoefu mwingine una-mhusu dada mmoja mwenye asili ya Ujerumani na Urusi. Alishiriki katika kipindi cha maombi ya Siku 40 naye akaanza kuwaombea majirani zake wazungumzao Kirusi. Alipomwambia mojawapo wa majirani zake kwamba alikuwa akimwombea, dada huyo alishangaa sana, akasema kwamba alikuwa akilitafuta kanisa linaloshika Sabato kama isemavyo Biblia. Dada huyu na majirani wengine kadhaa wakaja kwenye mikutano ya injili. Wawili miongoni mwao wakabatizwa. (#532,19)

- Mwanamaombi mwenzangu alipiga hatua nyingi sana katika imani yake! Maombi ya kina huwa mazoea pale yanaporudiwa kwa kufuata utaratibu wa Siku 40. Kesho, angalau watu watatu miongoni mwa watano tuliokuwa tukiwaombea, watakuja kwenye Sabato ya wageni. (#532, 30)
- … Tulijadili tulichokuwa tumesoma kisha tukawaombea watu watano maalumu. Tulipata uzoefu usiowakawida. Kijana mmoja, tuliyekuwa tukimwombea, alianza kuwa na shauku ya imani na akaanza kuuliza maswali kuhusu Mungu. Ndugu wa mwanamaombi mwenzangu alipata uzoefu wa baraka za Mungu pale tatizo fulani liliposuluhisha ghafla. Niliweza kuzungumzia imani pamoja na mfanyakazi mwenzangu, japo nilikuwa nimedhani haliwezekani kabisa. Mungu alitubariki maridhawa. (#532,53)
- Dada mmoja alisema baada ya maombi ya Siku 40:

> "Baada ya maombi ya kina, Roho Mtakatifu alitenda kazi hasa kwa mume wangu, akamwongoza kurejea kanisani baada ya miezi mingi ya kutohudhuria. Mungu anaweza kutenda mambo makuu!" (#532, 4 D)

Uzoefu huu hutuonesha kwamba maombi yaliyojazwa Roho hutupatia matokeo ya sala nyingi na maombezi yaliyojibiwa.

## Yesu alifundisha Sala ya Maombezi

Yesu alisimulia mfano kuhusu rafiki ajaye usiku wa manane, wakati akizungumzia mada ya sala ya maombezi (Luka 11:5-8). Rafiki huyu anampokea mgeni asiyetarajiwa jioni sana. Hana chochote cha kumlisha mgeni wake. Hivyo, anaharakisha kwenda kwa jirani yake na kumwomba mkate. Ana uhakika mkamilifu kwamba rafiki yake atamsaidia. Na kwa kweli, anapata mkate. Yesu alibainisha wazi kwamba sisi hatuna chochote. Hatuna budi kumwendea Rafiki yetu wa kiungu ili tuweze kupokea mkate wa uzima kwa ajili ya wapendwa wengine. Kisha Yesu akasema: *"Nami nawaambia, Ombeni, nanyi mtapewa…"* (Luka 11:9) Kwa kauli hii, anatuelekeza kwenye wito Wake mkuu, halani na wa upendo na – kwamba tunapaswa kwa gharama zote kuomba tukirimiwe Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu ni muhimu sana vilevile kwa ajili ya sala yetu ya maombezi.

## Omba katika Roho Mtakatifu/Omba katika Jina la Yesu

Neno la Mungu hutualika "kuomba katika Roho Mtakatifu." (Yuda 20) Hivyo basi, tunapaswa kuomba tukiwa tumewezeshwa na Roho Mtakatifu. Hilo ni sawa na kuomba katika jina la Yesu. Tunaomba katika jina la Yesu, tunapoishia kwa kujisalimisha kikamilifu Kwake na tuko radhi kumfuata Bwana wetu katika kila kitu. Kuna ahadi kuu kwa ajili ya sala ya aina hii:

- ▶ *"Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba."* (Yohana 14:12)

- *“Nanyi mkiomba lolote kwa jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lolote kwa jina Langu, nitalifanya.”* (Yohana 14:13-14)
- *“Ninyi mkikaa ndani Yangu, na maneno Yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa.”* (Yohana 15:7)
- Tunapoomba pamoja na mwanamaombi, ndipo tunapata ahadi ya nyongeza kutoka kwa Yesu katika Mathayo 18:19: *“Tena nawaambia, ya kwamba wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lolote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba Yangu aliye mbinguni.”*
- “*Bwana… hapendi mtu yeyote apotee, bali wote wafikilie toba.”* (2 Petro 3:9)
- *“Mtu akimwona ndugu yake anatenda dhambi isiyo ya mauti, ataomba, na Mungu atampa uzima kwa ajili ya hao watendao dhambi isiyo ya mauti. Iko dhambi iliyo ya mauti. Sisemi ya kwamba ataomba kwa ajili ya hiyo.”* (1 Yohana 5:16)

Ahadi za nyongeza kwa ajili ya watoto na jamaa zetu:

- *“Naam, Bwana asema hivi, Hata jeshi la wafungwa wake aliye hodari watapokonywa mikononi mwake, na mateka yake aliye jabari wataokoka; kwa maana nitateta na yeye atetaye nawe, Nami nitawaletea wana wako wokovu.”* (Isaya 49:25)
- *“Wakamwambia, Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako.”* (Matendo 16:31)

Tunaweza kupata katika Vitabu vya *Siku 40 juzuu ya 1, 2 na 3* vya Dennis Smith kwenye ‘utangulizi na muhtasari’ ahadi zingine zaidi kwa ajili ya sala ya maombezi: Angalia Kiambatisho A: Ahadi kwa ajili ya Sala ya Maombezi

## Neno la Mungu husimama imara zaidi kuliko milima

Kristo anapokuwa ndani yetu nasi tukaomba kwa kutumia ahadi, ndipo tunaweza kuwa na hakika kwamba Bwana anajibu maombi yetu. Hili pia linahusika katika maombi yetu:

*"Ndivyo litakavyokuwa neno Langu, litokalo katika kinywa Changu; halitanirudia bure, bali litatimiza mapenzi Yangu, nalo litafanikiwa katika mambo yale niliyolituma."* (Isaya 55:11)

*"Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno Yangu hayatapita kamwe."* (Yesu katika Mathayo 24:35)

## Orodha ya Maombi

Je unataka ndugu, marafiki na jirani zako wampate Kristo? Basi unapaswa kuanzisha orodha ya maombi kisha uwaombee mara kwa mara. Tumaini katika uhakika wa neno la Mungu kisha tumia ahadi.

## Napaswa kuwaombea mara nyingi kiasi gani?

Wakristo wengi makini wana orodha ndefu ya sala ya maombezi. Wakati fulani huwa napata hisia kwamba maombi yetu yanaweza kuwa purukushani tunapojaribu kuwaombea wote kila siku. Najiuliza: Hivi isingekuwa vema zaidi kuombea idadi ndogo kila siku – pengine hata mara kadhaa kutwa – na kisha kuwaombea wengine mara moja au mara kadhaa kwa juma, ili tuweze kuwasilisha kwa kina mbele ya Mungu shida na mahitaji yao?

## Napaswa kuwa na watu wangapi kwa ajili ya maombi maalumu?

Dennis Smith[3] na Josef Kidder[4] hupendekeza kwamba tunapaswa kuwaombea watu watano ambao hawajafikiwa. Tunapaswa kuanzisha mawasiliano pamoja nao na kukuza urafiki wetu. Joseph Kidder anasema: "Daima nimewahimiza washiriki wa kanisa kuomba mara kwa mara kwa ajili ya watu watano, kutimiza mahitaji yao katika namna ya msaada wa kirafiki, na kuwapenda. Kama matokeo ya aina hii ya maombi, nimewashuhudia watu wengi wakimpokea Yesu kama Bwana

3 Dennis Smith, 40-Days (book one) – Prayers and Devotions to Prepare for the Second Coming, katika kitabu hiki: Sehemu ya Pili: The Holy Spirit and Prayer, uk. 47

4 S. Joseph Kidder, … und sie wächst doch! Vier entscheidende Faktoren für das Wachstum von Gemeinden (Lüneburg 2014), S. 101, 131, 124, 136 – Kiingereza: The Big Four – Secrets to a Thriving Church Family, 2011 R&H

wao. Kwa nini usiwaombee watu watano, kama nifanyavyo, kisha shuhudia kile ambacho Mungu atafanya kwa ajili yao?”

## Wakati gani napaswa kumweleza mtu fulani kuwa namwombea?

Siku ya 20

Ni wakati gani tunapaswa kumwambia mtu fulani husika kwamba tunamwombea? Kuna mitazamo kadhaa kwenye jambo hili. Baadhi hupendekeza kumwambia tangu mwanzo. Wengine hupendekeza kumwambia baada ya kumwombea kwa majuma matatu au manne.

Tunapaswa kumwambia kwamba kanisa letu (kikundi cha maombi, kikundi cha malezi) kimepanga majuma sita kwa ajili ya muda maalumu wa maombi. pamoja na hili, tumehimizwa kuwaombea watu watano. “Na ningependa kukuombea. Je una mahitaji maalumu kwa ajili ya afya yako, familia au kazi, ninayoweza kuyaombea?”

## Sala ya Maombezi na Uhuru

Tatizo lingine la kuzingatia: Kamwe Mungu hamshurutishi wala kumghilibu mtu tunapomwombea. Bwana amempatia kila mtu uhuru, Naye huheshimu hilo kabisa. Lakini – nimepatauzoefu mimi binafsi pamoja na mke wangu mpendwa katika mazingira tofauti jinsi ambavyo Bwana alituelekeza upya kwa midokezo tofauti. Tulikuwa na mawazo mapya. Ghafla tukawa radhi kufanya kile ambacho hatukutaka kufanya hapo kabla. Tunaweza kusoma katika Matendo 16:14 kuhusu mwanamke mfanyabiashara aitwaye Lidia huko Filipi jinsi ambavyo *“moyo wake ulifunguliwa na Bwana, ayatunze maneno yaliyonenwa na Paulo.”*

Ni wajibu wetu kuomba kwamba watu wengine wampate Kristo na kuwaelekeza Kwake. Ni Mungu pekee awezaye kuzalisha imani mioyoni mwao kupitia Roho Mtakatifu na kubadili fikra na maisha yao. Lakini jambo moja tupaswalo kukumbuka: kwa kawaida, mtu aliyejazwa Roho tu, yule aombaye, ndiye anaweza kutegemea kujibiwa maombi yake kwa ajili ya wokovu wa ndugu zake au watu wengine.

## Sala ya Maombezi Zilizojibiwa

Nina shuhuda nyingi sana ambapo washiriki wa kanisa hueleza kuhusu majibu ya maombi baada ya kuanza kuomba katika Roho Mtakatifu na kuishi katika muunganiko wa karibu pamoja na Yesu. Mifano:

- Mzee mmoja kutoka familia ya Kiadventista alihudhuria kanisa pamoja na ibada zingine za kanisa mara kwa mara. Baada ya miaka mingi, hatimaye aliamua kubatizwa. (#532,4 O.)
- Watu wawili ninaowapatia masomo ya Biblia, wameikubali Sabato. (#532,4 M.)
- Mungu hakutuacha tungoje. Alitupatia majibu adhimu kwa maombi yetu katika kipindi cha Siku 40. Mtu fulani tuliyekuwa tukimwombea kwa dhati, alianzisha mahusiano mapya na kanisa baada ya kutohudhuria kwa muda mrefu. Ulikuwa wakati wa furaha kuu. (#532, 13)
- Kijana mdogo wa mama huyu alikuwa na matatizo mengi kanisani na hivyo wakati wa Siku 40 za maombi, yeye pamoja na mwanamaombi mwenzake walimwombea yeye hasa. Matokeo yalikuwa kwamba mwanawe alibadilisha maisha yake na kuanza kujiandaa kwa ajili ya ubatizo. (#532,16)
- Mtu fulani ambaye hakuwa radhi kusamehe, akugua akili, akapoteza kazi yake na kupata mawazo ya kujiua. Ndoa yake ikaharibika pia. Hali hii ilidumu zaidi ya mwaka. Alirejeshwa kupitia maombi na aliweza kupata nasihi makini ya kichungaji. Wanamaombi wawili wa Siku 40 za maombi walimwombea kila siku. Hatua ya badiliko ilikuja baada ya miezi miwili. Aliweza kusamehe halafu akaungana tena na mkewe na watoto, furaha yake ya maisha imerejea na anaweza kufanya kazi tena. (#532,17)

Shuhuda tatu za kina hueleza jinsi ambavyo mivutano ya miongo mingi na kutotaka kuhusiana vyovyote vile vilisuluhishwa kwa sababu ya sala ya maombezi wakati wa Siku 40. (mengine zaidi tembelea: www.steps-to-personal-revival.info: – Shuhuda: Na. 3/40, 4/52, 7/84 a und 7/84 b.)

Hebu Mungu atende kazi kwa kina zaidi mioyoni mwa watu unaowaombea.

## Nadumishaje Mawasiliano?

*Vitabu vya Siku 40* vya Dennis Smith vina ushauri wa thamani kwa ajili ya kudumisha mawasiliano, chini ya kipengele kisemacho "utangulizi na muhtasari."

Anasema: Orodha ifuatayo hukupatia mapendekezo kadhaa ya kile uwezacho kufanya kwa ajili ya watu husika kwenye orodha yako ya maombi ili wahisi kwamba wao ni muhimu kwako. Ongeza mawazo mengine katika orodha husika kadiri Mungu anavyokuongoza. Pia tuliongeza mapendekezo kadhaa. Unaweza kuipata orodha hii katika Kiambatisho B: Mapendekezo ya namna ya kuwafikia watu.

## Lengo Letu:

Ili kuwa baraka kwa wengine kupitia maombi yetu, kupitia kielelezo chetu, kufahamiana kwetu pamoja na kuwasilisha mapendezo yafaayo na machapisho, ili tuweze kufurahia maisha timilifu na kujiandaa kwa ajili ya ujio wa pili wa Yesu hivi karibuni. Chini ya uongozi wa Mungu, tunataka:

- Kuwahimiza watu ambao hawamtafuti Mungu waanze kumtafuta.
- Kuwaongoza watu wamtafutao Mungu, ili waje kwa Yesu.
- Kuwapatia changamoto watu ambao wamempata Yesu, ili waweze kujisalimisha kwa kina zaidi.

Kuna kila chapisho bora kabisa kwa ajili ya kusudi hili. Tutayaangalia machapisho haya katika sura ya 9: Msaada wa Kivitendo (Awini Halimali).

Hebu Bwana atupatie neema ya kuwa wavuvi wa watu kupitia ukaaji ndani (stakamani) wa Roho Mtakatifu na kupitia mafunzo Yake. *"Nifuateni, Nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu."*

"Kote kutuzunguka wapo vijana ambao hawajatubu wala kuongoka, tunafanya nini kwa ajili yao? Wazazi, katika ari ya upendo wenu wa kwanza, hivi mnajibidiisha kwa ajili ya uongofu wa watoto wenu, au mmegubikwa na mambo ya maisha ambayo

hamfanyi juhudi za za dhati kuwa watendakazi pamoja na Mungu? Je mnathamini kazi na utume wa Roho Mtakatifu? Hivi mnatambua kwamba Roho Mtakatifu ni wakala ambaye kupitia Kwake tunapaswa kuzifikia roho za wale wanaotuzunguka?" (E.G. White, *Selected Messages, book 1,* uk. 190.1)

Shuhuda fanisi humaanisha:

**Kwa maombi nachukua hatua ili niweze kuzungumza kuhusu Kristo katika nguvu ya Roho Mtakatifu – namwachia Mungu matokeo.** [5]

## Uamsho husababisha kazi ya Utume

"Roho Mtakatifu atawajilia wote waombao mkate za uzima ili kuwapatia majirani zao." (E.G. White, *Testimonies for the Church, vol. 6,* uk. 90.1)

5 Wirksames Zeugnis –Wie macht man das? (Neuhausen-Stuttgart, 1971), uk. 33

## Mawazo binafsi na mwongozo wa mjadala

1. *Nini ambacho Yesu ananitendea, ambacho hakuna yeyote awezaye? Kwa nini ni manufaa makubwa kabisa yaliyopo pale ninapomwonesha mtu fulani njia ya kuja kwa Yesu?*

   ______________________________________________

   ______________________________________________

2. *Tunawezaje kuwa wavuvi wa watu?*

   ______________________________________________

3. *Je "kujisalimisha kwa Yesu" humaanisha nini? Huonekanaje kivitendo?*

   ______________________________________________

4. *Ni mbinu zipi wezekani za kudumisha orodha ya majina unazoweza kutekeleza katika mazingira yako?*

   ______________________________________________

   ______________________________________________

## Muda Wetu wa Maombi

- Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.
- Sali pamoja na mwanamaombi mwenzio…
  1. Kwamba Mungu awasaidie mtambue zaidi kile ambacho Yesu humaanisha kwetu.
  2. Kwamba Mungu aweze kuwafanya wavuvi wa watu waliojazwa Roho.
  3. Kwamba Mungu aweza kuwaonesha jinsi mwezavyo kujisalimisha binafsi kwa Yesu.
  4. Kwa ajili ya ujasiri na hekima ya kutambua fanaka ya jinsi ya kudumisha mawasiliani na kuwa baraka katika mazingira yenu.

## Uzoefu

**Suluhu ndani ya jamuia nzima**
**Uzoefu wa kanisa lingine huko Guadeloupe/Karibiani**

"Uzoefu wa pili tumeupata pamoja na jumuia nyingine kwenye mtaa wetu. Mtangulizi wangu alisema, 'Unahitaji ujasiri mwingi kwa ajili ya kanisa hili kwa sababu unaenda katika mgodi halisi!' Tulitambua kwamba mivutano ilikuwa mikubwa sana. Ilikuwepo migogoro, migawanyiko, majeraha na kutosameheana. Milipuko na hisia zisizotawalika na mashambulizi binafsi zilifunika jumuia nzima kwa wingu jeusi. Ilikuwa simanzi kuona jinsi gani washiriki wa kanisa walikuwa wamenaswa kwenye utando wa kutosamehe nao hawakutambua kwa wasingeweza kupata ufumbuzi kwa uwezo wao wenyewe. Baada ya vikundi vya nyumba mbalimbali kuanzishwa, kijizuu (brosha) kiitwayo *Hatua za Uamsho Binafsi* ilisambazwa ili kusomwa kwenye vikundi hivi. Washiriki walionesha mwitikio chanya na walishukuru sana kwa ajili ya kijizuu (brosha) hiki, kiliyokuja kwa ajili yao. Hapa, pia, washiriki binafsi walianza kufanya huduma ya siku 10 za maombi na kufunga. Hatimaye, shauku iliibuka kuifanya pamoja kama kanisa. Huduma ilifanyika tena saa kumi kamili alfajiri. Mwanzoni, hawakuwepo watu wengi, lakini taratibu walikuja wengi zaidi na likawepo angahewa adhimu, la amani, la kiroho. Mtu angeweza kutambua kwamba Mungu alikuwa akitenda kazi. aliliandaa kanisa kimuujiza kwa ajili ya hatua ya mwisho iliyokuwa ngumu sana kwalo: hatua kwa ajili ya msamaha wa kweli. Mwishowe, "ukuta" ukaanguka na mtu mmoja baada ya mwingine akaomba msamaha hadharani. Wengine walikuwa wakizungumza moja kwa moja na kuombana msamaha na watu fulani waliokuwa wamezozana nao. Walikumbatiana. Machozi yakatiririka. Nyuso za huzuni zikawa na furaha tena halafu upendo ukarejea mioyoni mwao. Daima ni tukio la pekee kupata uzoefu na kuona. Mungu pekee ndiye awezaye kuwaongoza watu kupitia Roho Wake Mtakatifu. Kuna tumaini kwa ajili ya maeneo ya migodini." (B. & F. H. #84b Guadeloupe)

Mshiriki wa kanisa kutoka Ujerumani Kusini aliandika:

Mimi na rafiki yangu hivi sasa tunajisomea mara ya tatu kitabu kiitwacho *Siku 40 za Maombi na Ibada ili Kujiandaa kwa ajili ya Ujio wa Pili*, sambamba na kijitabu kiitwacho *Hatuza za Uamsho Binafsi*. Kabla hatujagundua chapisho hili, uzoefu wa imani yetu na maisha ya maombi havikuwa kama ilivyokuwa hapo awali. Tulikuwa na shauku ya kurejesha upya "upendo wetu wa kwanza." Tumeupata! Tunamshukuru Mungu kwa mioyo yetu yote. Inastaajabisha sana jinsi gani Mungu wetu mwenye upendo anavyojibu maombi na kudhihirisha namna Roho Wake atendavyo kazi – ndani yetu na kwa watu tuwaombeao." M. S.

Siku ya 21

SURA YA 6

# Kwa Nini Tunapaswa Kuwaongoza Watu Waje kwa Yesu Kwanza?

Sababu nzuri za utaratibu sahihi:
Sababu 10 kwa nini tuwaongoze watu waje kwa Yesu kwanza, kabla hatujawafundisha kuhusu itakidi za Biblia.
Mtiririko: Kwanza Yesu, kisha uanafunzi na Roho Mtakatifu, itakidi za Biblia, ubatizo, mafunzo

### Marudio

Mada iliyopita ilihusu maneno ya Yesu: *"Nifuateni, Nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu."* (Mathayo 4:19) Yesu anatualika tuwe wanafunzi Wake. Anataka kutufundisha tuwe wavuvi wa watu. Anataka kutufundisha binafsi. Tusingeweza kuomba kiongozi mahiri kuliko yeye. Ni furaha tunapokuwa wanafunzi wa Yesu na pale uwezo wetu unapokuzwa. Kiini cha mafunzo: Yesu mwenyewe atakuza uwezo huu kupitia sisi na ndani yetu. Sharti ni utayari wetu kumfuata Kristo. Jinsi gani?

1. Kwa kusahimisha maisha yetu Kwake kila siku – pamoja na kila kitu tulivyo na tulicho nacho – na
2. Kuomba kila siku kwa imani (kuomba kwa kutumia ahadi – 2 Petro 1:4) kwa ajili ya Roho Mtakatifu.

Hatupaswi kufikiri kwamba "uwanafunzi" wetu utakamilishwa siku moja. Ipo kauli isemayo: "Mtaalamu ni yule avumbuaye kitu fulani. Msafiri ni yule awezaye kufanya kitu fulani. Mwanafunzi ni kila mtu." mmtaalamu na msafiri pia wanapaswa kuendelea kujifunza. Nasi pia hatutakoma kamwe kujifunza kuhusu sayansi ya kuokoa roho.

## Ni jambo gani kuu na bora zaidi tuwezalo kumtendea mtu fulani?

Hakika tutatambua zaidi na zaidi kwamba uhusiano wetu binafsi na wa karibu na Yesu ndio uhusiano wa thamani zaidi tunaoweza kuwa nao, Yesu anataka kutupatia “maisha maridhawa” sasa katika maisha haya (Yohana 10:10). Baada ya ujio Wake wa pili, atatukirimia uzima wa milele – katika ufalme mtukufu wa Mungu (Yohana 3:16). Hakuna mbadala wa uhusiano huu makini. *“Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima.”* (1 Yohana 5:12) Pale furaha ya uhusiano huu inapotutosheleza na tunapokuwa tumepata uzoefu wa thamani pamoja na Yesu, ndipo tutatambua kwamba huu ni **uhusiano wa thamani usiokuwa na mbadala kwa ajili ya wanadamu wenzetu.** Jambo kuu na bora kabisa tunaloweza kumfanyia mtu fulani ni kumsaidia kupata uzoefu wa urafiki huu wakina. Uhusiano huu ni wa thamani zaidi kuliko dhahabu.

## Jinsi gani tunakuwa wavuvi wa watu?

Tunakuwa mashahidi wa Yesu anapoishi mioyoni mwetu kupitia Roho Mtakatifu. Katika sura iliyopita, tuliona katika uzoefu binafsi jinsi gani shauku yetu kwa ajili ya wengine huamshwa madhubuti pale Kristo anapoishi ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu. Tunataka kusikia shuhuda mbili zingine:

Mtu fulani aliandaa baada ya kuomba kila siku kwa ajili ya Roho Mtakatifu kwa muda fulani:

“Tumegundua kwamba maombi yetu yameleta tofauti maishani mwetu. Na tusingehifadhi hili kwa ajili yetu wenyewe. Kila fursa tuliyopata, tulihisi msukomo wa kuli-zungumzia. Ni muhimu kwangu kuwahamasisha watu wengine wapate uzoefu kama huu. Matokeo yalionesha utayari mkubwa. Baadhi ya washiriki wa kanisa waliambukizwa ari yetu.” (#432,13)

Mtu mwingine aliandika:

“Kufuatia hilo, mwanawe alibadili maisha yake, akaanza kujiandaa kwa ajili ya ubatizo. Niliambukizwa ari yake mama huyu na sasa ninamwombea mwanamaombi mwenzangu na nimeanza kuvisoma vitabu hivi viwili.” (#432,16)

### Ni kazi gani maishani tuliyo nayo mimi na wewe?

Je inahusisha kuwaongoza watu waje kwa Yesu? Inasema yafuatayo kwenye kitabu kiitwacho *Utumishi wa Mkristo:* "Uokoaji roho unapaswa kuwa kazi ya maisha ya kila mmoja anayemkiri Kristo." (E.G. White, *Christian Service,* uk. 10.1)

Yesu Mwenyewe alitupatia utume, aliposema: *"Kama Baba alivyonituma Mimi, Mimi nami nawapeleka ninyi."* (Yohana 20:21) Pamoja na hilo, tunazijua amri Zake: *"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote."* (Mathayo 28:19) *"...Nanyi mtakuwa mashahidi Wangu..."* (Matendo 1:8) *"...zaidi ya hayo nitakutoa uwe nuru ya Mataifa, upate kuwa wokovu Wangu hata miisho ya dunia."* (Isaya 49:6)

Wengi wamepambana katika uelekeo huu. Wakati mwingine kwa mafanikio, mara nyingi bila mafanikio. Tunapaswa kukiri kwamba wengine wetu tumepuuza sana kutelekeza utume wa Yesu. Tunapaswa kufanya tathmini aminifu hapa. Wengi wanahitaji kukiri kama alivyofanya Petro: *"...tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu."* (Luka 5:5) Je matokeo yananiridhisha? Hivi nilitimiza vigezo tulivyojadili kwenye sura iliyopita? Je pengine tatizo lilisababishwa na ukosefu Roho Mtakatifu? Hivi hatupaswi kujibu kama alivyofanya Petro: *"... lakini kwa neno Lako nitazishusha nyavu."* (Luka 5:5)

### Vigezo vya kuwa Wavuvi wa Watu

Tunataka kudurusu kwa ufupi vigezo hivi:

- Je nimesalimisha kikamilifu maisha yangu kwa Yesu? Hivi nataka kumtii Yeye na Neno Lake katika kila kitu? Je nimehawilinisha kila siku uhusiano wangu pamoja Naye kupitia kujisalimisha kikamilifu?
- Wakati nikiifanya kazi hii, hivi nilikuwa nimejazwa Roho Mtakatifu? Je niliomba kila siku kwa imani ili nikirimiwe Roho Mtakatifu na kumpokea? (Ni bora zaidi kuomba kwa kutumia ahadi, tazama 2 Petro 1:4.)
- Je nilimwombea kwa juhudi mtu husika kabla sijafanya kitu fulani kwa ajili yake?
- Hivi nilitafuta mawasiliano binafsi na kuonesha shauku halisi katika maisha ya mtu huyo? (Mapendekezo ya

jinsi ya kufanya hili yanapatikana katika Kiambatisho B: "Mapendekezo ya namna ya kuwafikia watu" na katika Vitabu vya Siku 40, juzuu 1 na 2 vya Dennis Smith)



## Mbinu Yenye Baraka Maridhawa

Katika sura hii na inayofuata, tutaangalia mbinu ambayo imepimwa kwa mapana kivitendo. Hutupatia ujasiri mpya kwa mara nyingine tena kuendelea katika jina la Yesu.

Kwanza kabisa, tunataka kuomba mara kwa mara kila siku:

**"Baba uliye mbinguni, nifanye niwe radhi kutenda kila kitu unachotaka Wewe. Tafadhali umba ndani yangu shauku ya kusaidia kuuongoa ulimwengu uliopotea uje Kwako."**

Ndiyo, kwa neema ya Mungu, Yesu anaweza kuwaongoza watu waje Kwake kupitia mimi na wewe. Hutekeleza hili kupitia wanafunzi waliojazwa Roho, ambao huishi mioyoni mwao kupitia Roho Mtakatifu. Usichukulie kama mzigo kazi hii ya kuwahudumia wengine. Kanuni yetu ituongozayo inapaswa kuwa:

**Nachukua hatua kupitia maombi ili niweze kushuhudia kuhusu Kristo kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu. Namwachia Mungu matokeo.**

Kamwe kazi yetu haitakuwa mzigo tukiwa na mtazamo huu. Badala yake, itakuwa fadhila kumtendea Yesu kazi. Ni kazi ya pekee ajabu pale tunapoweza kuwaongoza watu waje karibu na Yesu au wajisalimishe Kwake kikamilifu. Hili ni jambo bora na muhimu kabisa tunaloweza kuwafanyia watu wengine.

## Kwa Nini Tuwaongoze Watu Waje Kwa Yesu Kwanza?

Kwa nini tunapaswa kuwaongoza watu waje kwa Yesu kwanza kabla hatujajadili misingi ya Biblia? Katika hatua hii, ningependa kusisitiza tena jinsi ilivyo muhimu sana kwa ajili ya kazi yetu kwamba tuwe ndani ya Kristo – kwamba Kristo yumo mioyoni mwetu kupitia Roho Mtakatifu (Waefeso 3:16-17). Biblia huiita hali hii ya kiroho *"kuwa ndani ya Kristo"* au *"Kristo ndani yenu"* (Wakolosai 1:17) na pia *"kuzaliwa mara ya pili"* (Yohana 3:3) au *"kuzaliwa na Mungu"* (1 Yohana 5:18).

Nataka kusisitiza kwa mara nyingine tena kile ambacho E.G. White alifupisha kwa umahiri kuhusu maneno ya Yesu katika Yohana 15:4:

> **"*'Kaeni ndani Yangu, Nami ndani yenu.'* Hii huumaanisha:**
> - **Kuendelea kumpokea Roho Wake daima,**
> - **Maisha ya kujisalimisha kikamilifu kwenye huduma Yake."***(Desire of Ages,* uk. 676.2, egwwritings.org)

Kila asubuhi tunaweza kumpokea Roho Mtakatifu tunapoomba kwa imani (Wagalatia 3:14). Tunampokea kwa namna maridhawa pale tunapoamini kwamba *hata tukingali tunaomba,* tayari tunakuwa tumempokea (1 Yohana 5:14-15; Marko 11:24). Baadhi ya watu wana tatizo juu ya hili. Lakini ni kweli: Kadiri tunavyoomba kwa maneno ya jumla, kwa kawaida huwa tunatumaini kwamba tumempokea Roho Mtakatifu. Lakini katika suala hili, "kutumaini" hakutoshi. Ndiyo maana napendekeza: omba kwa kutumia ahadi ili ujue kwamba hakika umempokea Roho Mtakatifu. Kuomba kwa kutumia ahadi huimarisha imani yetu yote. Tafadhali, kama inahitajika, soma tena kitabu kiitacho *Hatua za Uamsho Binafsi*, hususan sura isemayo "kuwa na matumai" hakutoshi ndio maana napendekeza: kuomba kwa ahadi." Sura hii hujadili kwa kina mada ya kuomba kwa ahadi. Kuomba kwa ahadi kunapendekezwa bayana kabisa katika 2 Petro 1:4: *"Tena kwa hayo* [maarifa kuhusu Yesu na uhusiano sahibu pamoja Naye] *ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu…"*

Dondoo ya pili "maisha ya kujisalimisha kikamilifu kwenye huduma Yake" inaweza kufanikishwa kila siku, pale tunapoomba kwa bidii na kwa uaminifu: "Baba uliye mbinguni, naisalimisha Kwako nafsi yangu pamoja na kila kitu jinsi nilivyo na vyote nilivyo navyo."

## Kwa Nini Tunapaswa Kuwaongoza Watu Waje Kwa Yesu Kwanza Kabla ya Kuwafundisha Misingi ya Biblia?

Unapokosea kufunga kifungo cha kwanza, basi kasoro hutokea. Kudumisha mpangilio sahihi mara zote huleta manufaa.

Huwarahisisishia sana wapendwa hawa, unaotaka kuwaongoza waje kwa Yesu, hatua ya kuwa Wakristo. Pamoja na hilo, huimarisha furaha yetu, nguvu na maisha yetu kwa ujumla wake.

1. **Tunataka kuwaongoza watu waje kwa Yesu kwanza kwa sababu hatutaki kumpendekeza yeyote mapito yasiyo-wezekana.**

   Kwa kawaida, mpendwa fulani tunayetaka kumwongoza aje kwa Kristo, haishi katika nguvu ya Roho Mtakatifu. Tunapomfundisha mtu fulani misingi katika Biblia, basi tunaona na kutumaini kwamba atakuzikubali na kuzitekeleza. Lakini kwa kawaida mtu huyu ambaye bado hajajazwa Roho Mtakatifu, anakosa hamasa na nguvu. Kimsingi, bado hajawa mtu wa kiroho. Biblia inasema katika Warumi 8:7 yafuatayo kuhusu mtu wa namna hiyo: *"...maana hawaitii sheria ya Mungu,* ***na kwa kweli wala hawawezi kuitii.****"* (GNT)

   Kama tungewafundisha misingi ya Biblia wakati huu, basi tungekuwa tu tunawajengea wapendwa hawa "mlima" wasioweza kuukwea. Hapo tungekuwa tunawaongoza kwa Wakristo wa mwilini, yaani kuishi maisha ya Ukristo kwa uwezo wao wenyewe. Mtu huyu ana nguvu na uwezo wa kawaida tu wa kibinadamu alionao. Lakini mtu fulani anapokuwa amempokea Kristo na amejazwa Roho Mtakatifu, basi anakuwa na hali bora zaidi kwa ajili ya kuzikubali na kuziishi misingi ya Biblia.

   Katika hatua hii, ningependekeza usomaji wa kitabu kiitwacho *Hatua za Uamsho Binafsi*, sura isemayo "Nini kiini cha matatizo?" na kipengele kisemacho "Kipi kizuizi kikuu katika Ukristo wa mwilini?"

   "Jinsi utii wa furaha unavyoweza kuwa" imefafanuliwa katika kitabu kiitwacho *Kaeni Ndani ya Yesu*, sura isemayo "Utii Kupitia Yesu."

2. **Tunataka kuwaongoza watu waje kwa Yesu kwanza kwa sababu bila Kristo wanakuwa wamepotea.**

   *"Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima."* (1 Yohana 5:12) Yesu alisema: *"Mimi ndimi Njia, na Kweli, na Uzima; mtu haji kwa*

*Baba, ila kwa njia ya Mimi."* (Yohana 14:6) Biblia inasema bayana: *"Wokovu hupatikana kupitia Kwake pekee; duniani kote hakuna mwingine yeyote ambaye Mungu ametupatia awezaye kuokoa."* (Matendo 4:12 GNT)

**3. Tunataka kuwaongoza watu waje kwa Yesu kwanza kwa sababu wanapata uzoefu kurejesha upya kwa thamani kupitia Kwake.**

Yesu hutupatia hapa maisha mapya na yenye thamani na baada ya kuja tena, atatufanya tuwe washirika wa uzima wa kiungu milele. *"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya…"* (2 Wakorintho 5:17) *"Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele."* (Yohana 10:10) Paulo aliomba: *"…ili mweze kujazwa utimilifu wote wa Mungu."* (Waefeso 3:19 NKJV) *"Maana katika Yeye* [Yesu] *unakaa utimilifu wote wa Uungu, kwa jinsi ya kimwili; Nanyi mmetimilika katika Yeye…"* (Wakolosai 2:9-10 NKJV)

**4. Tunataka kuwaongoza watu waje kwa Yesu kwanza kwa sababu anatupatia uhuru wa kweli.**

Yesu alisema: *"Basi Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kwelikweli."* (Yohana 8:36) Yesu hutuweka huru tuondokane na hatia. Hii humaanisha kwamba tunaweza kuishi bila mzigo wa hatia. Hutuweka huru tuongokane na ukatili wa ubinafsi wetu, mathalani, tuondokane na upotovu wa asili yetu ya kale (kinyongo, husuda, hasira, kiburi, adhali changamani, kutoridhika, mashaka, upuuzi, nk.), tuondokane na uraibu na mifangamano yoyote na ushirikina, nk.

Neno fulani kuhusu kuwekwa huru kutoka kwenye asili yetu ya zamani ya upotovu. Naamini kwamba kuomba **kila siku** ili kuwekwa huru kutoka kwenye silika hii, ni muhimu kwa sababu 2 Wakorintho 4:16 inasema: *"...lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku."* Mtume Paulo alisema kuhusu nafsi yake mwenyewe: *"...ninakufa kila siku."* (1 Wakorintho 15:31) Na Martin Luther anadhaniwa kusema kwamba alimzamisha Adamu wa kale, lakini "Oh mpendwa, jamaa huyo anaweza kuogelea." Ninaomba kila siku kuwekwa huru nikitumia ahadi katika Yohana 8:36. Kwa

sasa, siwezi kusema iwapo hili ni lazima wakati wote au kwa kipindi fulani.

Hata hivyo, tunaweza kuwekwa huru kabisa kiasi cha kuondokana na utumwa wa mambo ya nje kama vile kuvuta sigara na pombe,[6] kupitia ombi moja. Mtu fulani anapokuwa amewekwa huru ndipo majaribu mapya hunyemelea kote kumzunguka. Hii ndiyo sababu ni muhimu kumwongoza mtu aliyewekwa huru afanye mahusiano ya dhati pamoja na Yesu, adumishe maisha katika nguvu ya Roho Mtakatifu. Hii ndiyo sababu pia kwa nini, kwa mfano, watu walio kwenye vituo visivyojulikana vya uraibu kama vile *Alcoholics Anonymous*, wanafundishwa kuyasalimisha maisha yao kwa Mungu kila siku ili waendelee kuwa huru.

Kumbuka kuwa nguvu za dhambi huvunjwa katika maisha yetu(Warumi 8:1-2; Wagalatia 5:16). Yesu anatulinda dhidi ya dhambi. Shetani hawezi kutugusa (1 Yohana 5:18). Yesu anatuhitaji kuwajulisha wengine kile alichotufanyia sisi.

"... alipo Roho wa Bwana, hapo ndipo penye uhuru." (2 Wakorintho 3:17 NKJV)

**5. Tunataka kuwaongoza watu waje kwa Yesu kwanza kwa sababu upendo wa Mungu unatuhimiza.**

Roho Mtakatifu humjaza upendo wa Mungu Mkristo aliyezaliwa mara ya pili (Warumi 5:5) na husukuma mioyo yao ipate shauku ya kuwaambia wengine kuhusu Yesu. *"Basi tukiijua hofu ya Bwana, twawavuta wanadamu... Maana, upendo wa Kristo watubidisha ...tena* [Kristo] *alikufa kwa ajili ya wote, ili walio hai wasiwe hai tena kwa ajili ya nafsi zao wenyewe, bali kwa ajili yake Yeye aliyekufa akafufuka kwa ajili yao."* (2 Wakorintho 5:11, 14-15)

Tunakirimiwa Roho Mtakatifu kwa sababu mbili:

1. Kwa ajili ya ubadilishwaji wa tabia zetu - Biblia huita hii tunda la Roho (Wagalatia 5:22; 1 Wakorintho 13:1-7).
2. Na kuwa mashahidi kwa ajili ya Yesu. *"Lakini mtapokea nguvu* [pia uwezo]*, akiisha kuwajilia juu yenu Roho*

6 Angalia Victory over Tobbaco & Alcohol www. Steps-to-personal-revival.info: Letters toAndrew Na. 5 – Nyenzo za kimishenari.

*Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi Wangu."* (Matendo 1:8) – Hii ndiyo sababu tunapokea karama za kiroho.

Siku ya 23

**6. Tunataka kuwaongoza watu waje kwa Yesu, ili tusije kushutumiwa kwa hukumu ya Mungu.**

Je ni muhimu kweli kujumuisha ujumbe wa hukumu? Ujumbe wa hukumu unatupatia changamoto: Jikabidhi nafsi yako kwa Yesu ili usije kushutumiwa katika hukumu ya Mungu.

Biblia inasema:

*"Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya."* (2 Wakorintho 5:10)

*"Mhofuni Mungu na kumtukuza, maana saa ya hukumu Yake imekuja; mwabuduni Yeye…"* (Ufunuo 14:7 NKJV)

Awamu ya kwanza ya hukumu – hukumu kabla ya ujio wa pili – tayari ilianzishwa mnamo mwaka 1844 kwa mujibu wa Danieli 8:14. Kiasili, watu walioishi nyakati za kale ndio wanaochunguzwa kwanza. Na kuanzia wakati huo, uchunguzi unaelekea kwenye kesi za nyakati za mwisho.

*"Basi, kwa vile ikaliko ahadi ya kuingia katika raha Yake,* ***hebu tuhofuni,***[7] *vinginevyo mmoja wenu asije akaonekana ameikosa."* (Waebrania 4:1 NKJV).

Andiko hili linatuhimiza kutafakari: hivi nimeokolewa? Na *"Basi tukiijua hofu ya Bwana,* ***twawavuta wanadamu…****"* (2 Wakorintho 5:11) Hofu juu ya Mungu na ufahamu wa hukumu ujayo vinapaswa kutuhamasisha kuwa na shauku ya kuwaokoa watu wengine.

E.G. White anawasilisha maelezo makini sana ya neno "hofu":

"Bwana angependa watu Wake wamwmani Yeye na kukaa katika upendo Wake, lakini hilo halimaanishi kwamba hatutakuwa na hofu wala mashaka. Baadhi huonekana kudhani kwamba endapo mwanadamu ana hofu kamili(salidi) kuhusu hukumu za Mungu, basi huo ni uthibitisho kwamba ana uhaba

---

7 Si lazima ihusiane na ustahivu (kicho) hapa, badala yake ni hofu, mashaka. NKJV: "Hebu tuhofuni;" RSV: "Hebu tuhofuni"

wa imani; lakini hii siyo kweli. **Hofu sahihi ya Mungu, katika kuamini vitisho Vyake, huzalisha matunda aminifu ya haki, kwa kuifanya nafsi itetemekayo imkimbilie Yesu.** Wengi wanapaswa kuwa na roho hii leo, na kumrejea Bwana kwa majuto ya unyenyekevu, maana Bwana hajawasilisha vitisho vingi kiasi hicho, hajatangaza hukumu kali katika neno Lake, ili tu virekodiwe, lakini humaanisha asemacho. … Paulo anasema, *'Basi tukiijua hofu ya Bwana,* ***twawavuta wanadamu****.' …*" *(R&H,* Okt. 21, 1890, par. 6)

Jinsi gani tunaweza kupata uwiano wa kauli mbalimbali kuhusu hofu? Mfano, tuna ujumbe huu katika 1 Yohana 4:18: *"Katika pendo hamna hofu."*

Ninapofikiria Warumi 5:5, basi natambua: *"...pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi."* Kristo huishi ndani ya mioyo yetu kupitia Roho Mtakatifu. Anapokuwa mioyo mwetu na kudumu humo, ndipo anatuwakilisha katika hukumu. Anasema katika Yohana 5:24: *"Amin, amin, nawaambia, Yeye alisikiaye neno Langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani."*

Vidokezo viwili zaidi vya ufafanuzi juu ya andiko hili: "Kuamini" ni hatua ya lazima. Wakati fulani nilichunguza yafuatayo kwenye mtandao: "Kuamini kwa mujibu wa Biblia." Maana manne zilijitokeza. Katika Biblia, usadikifu humaanisha: "Kujitoa nafsi," "kuufungia uwepo wake kwa mtu mwingine," "kumtawakali mtu mwingine" na "kuwa mtiifu kwa mtu mwingine." Humaanisha uhusiano huu wa imani pamoja na Yesu. Maisha ya kila mtu binafsi yatachunguzwa katika hukumu ya Mungu. Lakini, kwa ajili ya wamwaminio Yesu, kwa wale walio ndani ya Kristo, hakuna hukumu kwa sababu Yesu huibeba hatia yao.

Hii hutuonesha kwamba haitoshi kuzungumza tu kuhusu upendo wa Mungu – ingawa kiasili ni lengo letu kuu. Tunapaswa pia kudokeza kwamba siku moja Mungu atamwajibisha kila mtu. Hatupaswi kuucha ujumbe wa hukumu. Lakini ni muhimu kuuwasilisha kwa hekima. Wakati huohuo, tunapaswa kubainisha

wazi kwamba kufuatia hukumu, uovu wote utakoma na hivyo kila mgogoro, kila ugonjwa na kila hisia ya maumivu itatoweshwa. Haitakuwepo tena maumivu ya kisaikolojia(shakawa) wala mauti! Pamoja na hilo, tunapaswa kudokeza kwamba kila mmoja anayeishi akiwa ameunganika kwa ukaribu na Kristo, hana sababu ya kupata hofu kuhusu hukumu ya Mungu. Mungu anamwahidi kumwachilia huru hukumuni kila mtu aliye ndani ya Kristo.

Katika kampeni za Urusi wakati wa VVII, yafuatayo yalitokea: askari wa Kijerumani walikuwa mstari wa mbele kwenye mahandaki na walijua kwamba walikuwa mkabala na Warusi. Kikosi cha jeshi la Wajerumani kikajiunga nao na kwa muda kitambo hawakutambua wapi mstari wa mbele ulikokuwa. Wangeweza kwenda mchana hadi mikononi mwa askari wa Warusi endapo askari wa Kijerumani handakini asingepaza na kusema, “simama!” Ni wakati huo tu ndipo walipotambua hatari waliyokuwemo. Wajerumani mahandakini walitaka kuwaokoa wenzao.

Sisi nasi tunapaswa kuwaonya wanadamu wenzetu juu ya hukumu ya Mungu na tunapaswa kuwaonesha ufumbuzi wa tatizo hili. Tunawaambia watu kwa upendo kwamba itakuwepo hukumu. Ndipo wanakuwa na nafasi ya kujilinda wenyewe. Kama tungezuia hili tusiwaambie, basi siku moja wangeweza kutushutumu vikali. Ni wajibu wetu kuwaonesha wanadamu wenzetu mbadala ili waweze kufanya maamuzi mazuri.

### 7. Kwa sababu kushuhudia kwa ajili ya Yesu vilevile ni msaada kwetu

Kuzungumza kuhusu Yesu hutusaidia sisi pia. Wale wanaozungumza kuhusu Yesu wanakua katika imani. Kuzungumza kuhusu Yesu huwa na mrejeo mwema kwa ajili yangu. Tutagundua jinsi gani hili hutuhamasisha ili tuwe na maisha ya maombi ya kina na kuendelea kutafuta mawazo mapya katika neno la Mungu.

Tunapozungumza kuhusu Yesu katika nguvu ya Roho Mtakatifu, basi tunakuwa tunapanda upendo, furaha na amani. Kwa mujibu wa kanuni ya kiungu ya kupanda na kuvuna, tunavuna kile ambacho tumepanda. Tutavuna hata zaidi. Kwa

kawaida mavuno ni ongezeko la mbegu. Yesu alisema katika mfano wa mpanzi: mara thelathini, mara sitini, mara mia (Marko 4:20). Mfano, tunapopanda upendo, tunavuna upendo, lakini daima huwa zaidi ya kiasi tulichopanda awali. *"Lakini nasema neno hili, Apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu. Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu. Na Mungu aweza kuwajaza kila neema kwa wingi, ili ninyi, mkiwa na riziki za kila namna siku zote, mpate kuzidi sana katika kila tendo jema."* (2 Wakorintho 9:6-8)

**8. Kwa sababu tunaweza kuwa mabalozi wa Mungu kwa kubeba ushuhuda wa Yesu.**

Ni fadhila kuu kuwa balozi wa Mungu. *"Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu."* (2 Wakorintho 5:20) Kila balozi huchukulia kuwa heshima kuu kuiwakilisha nchi yake, rais wake au mfalme wake. Tukiwa kama wanafunzi wa Yesu, sisi ni mabalozi wa Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana. Hii ni heshima ya juu zaidi tunayoweza kuipata.

**9. Kwa sababu Roho Mtakatifu hutupatia uwezo wa kiungu na mamlaka.**

E.G. White alifafanua juu ya Matendo 1:8: *"Yesu anasema, 'Mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi Wangu.'* Ni muungano wa Roho Mtakatifu na ushuhuda wa shahidi halisi ndiye anayepaswa kuuonya ulimwengu. Mtendakazi wa Mungu ni wakala ambaye kupitia kwake mawasiliano ya kimbingu hufikishwa kwetu, na Roho Mtakatifu hulipatia neno la kweli mamlaka ya kiungu." *(RH,* Aprili 4,1893, par. 9) Hapa, neno "nguvu" humaanisha: uwezo, uwezeshaji, uidhinishaji. Humaanisha kwamba Roho Mtakatifu hutuwezesha na kutuidhinisha sisi ili tuwe mashahidi wa Yesu. Hivi tumefikiria vya kutosha kuhusu ukweli kwamba tunapokea uwezo na mamlaka kutoka kwa Roho Mtakatifu?

**10. Tunataka kuwaongoza watu waje kwa Yesu kwa sababu Kristo ametupatia utume wa kufanya hili.**

Yesu alisema katika maneno ya maagano:

*"Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, Mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."* (Mathayo 28:18-20) Tunayaita maneno ya Yesu Utume Mkuu.

Je Yesu anategemea tuutii utume Wake? Tafadhali kumbuka kwamba utii wetu kwa imani hutarajiwa. Una vipengele vitatu:

1. Uamuzi wangu
2. Hatua zangu za maandalizi
3. Mungu hutekeleza

Hebu tumwangalie Danieli kama mfano (Danieli 1:8-9):

1. Danieli aliazimu moyoni mwake. Danieli alifanya uamuzi.
2. Hatua zake za maandalizi: Nini alichofanya binafsi? Aliomba pamoja na marafiki zake kuhusu hali tata. Pamoja na hilo, alifikiria nini kingine angeweza kufanya. Matokeo: Aliwasilisha ombi kwa msimamizi mkuu.
3. *"**Basi Mungu** alimjalia Danieli kupata kibali na huruma machoni pa huyo mkuu wa matowashi."* (Fungu la 9)

Utayari wangu kuwa mtiifu mara nyingi huja kwanza: Hivi nataka kuutii utume wa Yesu? Baada ya kufanya uamuzi chanya, basi naanza hatua za maandalizi zilizo ndani ya uwezo wangu. Namwombea mtu husika, natafuta mawasiliano na kudumisha mawasiliano binafsi.

(Kristo anapoishi mioyoni mwetu kupitia Roho Mtakatifu, ndipo atatusaidia hatua kwa hatua.)

Mungu anataka kuwaongoza watu hawa wapate wokovu! Atatenda kazi mioyoni mwao.

Pengine hata zipo sababu zingine zaidi kwa nini tunataka kuwaongoza watu waje kwa Kristo. Katika hitimisho, tunataka kukumbuka kile ambacho waongoaji wengi wa roho wamejifunza:

Nataka kuwa bayana tena kwamba mafunzo, nyenzo na mbinu hazifai kitu kabisa endapo tusipotenda katika mamlaka na nguvu ya Roho Mtakatifu.

Na sasa linakuja swali kuu:
**Jinsi gani naweza kuzungumza kuhusu Yesu?**
Kuna mbinu za mazungumzo na njia nyingi mbalimbali za kutumia wakati wa kuzungumza kuhusu Yesu. Njia **mojawapo**, ambayo imejaribiwa na kupimwa ni kuanza na kijitabukazi. Kwenye sura inayofuata, tutajadili kwa kina matumizi ya kitabukazi hiki.

Sura yetu inayofuata ni:
**Jinsi gani tunaweza kuwaongoza watu waje kwa Yesu?**
Zipi sababu 12 nzuri za kutumia kitabukazi? Ni uzoefu upi utendaji wakivitendo tunaoweza kufuatisha? Naweza kufanya kazi kwa kutumia kitabukazi kilichojaribiwa na kupimwa?

Kwa sasa, tunataka tu kuipitia haraka. Dondoo makini kwa wengi wetu ni kupata njia sahihi ya kuanza mazungumzo. Nawezaje kuzungumzia imani kwa namna ya kawaida na halisia? Ni swali gani la ufunguzi ambalo kwa ustadi na hulenga huelekea kwenye wazo kuu

- ▶ Nawezaje kumtambulisha mtu fulani kwa Yesu na kumwonesha muhtasari rahisi wa mpango wa wokovu?
- ▶ Nawezaje kufanya utambuzi wa kiroho ili mtu husika ajue mahali anakosima na wapi anataka kwenda katika wakati ujao? Hii ni muhimu kwangu ili niweze kumpatia (awini) uungaji mkono mahususi.
- ▶ Nawezaje kumsaidia mtu fulani ambaye tayari anataka kumkubali Yesu?

Mungu shukuriwe kwamba yapo majibu mazuri kwa maswali haya. Yote yako kwenye kijizuu (brosha) kiitwayo, “Jitwalie Uzima.” Yeyote anaweza kujifunza kutumia kijizuu (brosha) hiki. Kwa kweli, mbinu hii imetumiwa kwa miaka mingi ulimwenguni – kwa mafanikio makubwa! Ni muhimu kwamba watu wengi zaidi waitumie kwa ajili ya wokovu wa wengine na kwa ajili ya furaha ya wasaidizi.

Tunataka kumshukuru Bwana kwa moyo wetu wote kwamba anatufanya tuwe radhi na tupate uwezo wa kuwaongoza wengine waje kwa Yesu vilevile.

***Sala: "Baba uliye mbinguni, nifanye niwe radhi kutaka kila kitu unachotaka Wewe. Tafadhali, amsha shauku ndani yangu ili kusaidia katika jukumu kuu la kuongoa ulimwengu uliopotea uje Kwako. Asante, Bwana Yesu, kwamba utaniongoza kwa Roho Wako mwema. AMINA."***

## Mawazo binafsi na mwongozo wa mjadala

1. *Je tunapaswa kufuata mtiririko gani tunapotaka kuwa wavuvi wa watu wenye ufanisi?*

   ______________________________________________

   ______________________________________________

2. *Je kuna masharti gani ya kuwa mvuvi wa watu?*

   ______________________________________________

   ______________________________________________

3. *Taja sababu chache kwa nini tunapaswa kuwaongoza watu waje kwa Yesu kwanza kabla hatujawafundisha itakidi za Biblia.*

   ______________________________________________

   ______________________________________________

4. *Ni kipi ukionacho cha thamani katka kanuni ifuatayo? Kwa njia ya maombi, nachukua hatua ya kushuhudia kuhusu Yesu katika nguvu ya Roho Mtakatifu. Namwachia Mungu matokeo.*

   ______________________________________________

   ______________________________________________

## Muda Wetu wa Maombi

- Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.
- Sali pamoja na mwanamaombi mwenzio…
  1. Ili kuweza kumshuhudia Yesu kwa namna halisi.
  2. Ili Mungu anifanye niwe tayari kutenda kwa furaha kila kitu anachotaka.
  3. Ili kuelewa kwa nini ni muhimu sana kuwaongoza watu waje kwa Yesu kwanza.
  4. Kwa ajili ya hekima ya kuweza kutathmini vema kile ambacho watu ninaowasiliana nao wanahitaji kiroho.

Siku ya 24

Siku ya 26

SURA YA 7

# Tunawezaje Kuwaongoza Watu Waje Kwa Yesu?

Kupitia kusoma pamoja somo la Biblia
kwa kutumia mwongozo uitwao Barua kwa Andrea Na. 13.
Jitwalie uzima kupitia uhusiano binafsi pamoja na Mungu

Kwanza tunazingatia hatua mbili muhimu katika sura ya 7 na 8. Kisha katika sura ya 9 mpangilio ambao kwao tunaweza kwa kawaida kutumia *Barua kwa Andrea*.

## Kwa nini ni vema kutumia kijitabu cha mwongozo?

Mwinjilisti Mwadventista Eiden K. Walter aliniandikia: “Kadiri nihusikavyo, sitaki kutumia hatua hizi – kuwaongoza watu waje kwa Yesu – bila kijitabu hiki cha mwongozo. Kina manufaa. Humpatia mtu kujiamini anayeanza na hutumika kwa kusudi kivitendo(halimali) zaidi.

**Manufaa kumi na mbili za kijitabu cha mwongozo ni:**

1. Kina jumbe kuu za injili.
2. Siyo tu kwamba msomaji ana mwongozo mbele yake kwa ajili ya kurekebisha kauli binafsi, ambazo aghalabu huweza kupotosha, lakini pia ana injili katika muktadha wake. Ni muhtasari rahisi wa mpango wa wokovu.
3. Muundo mzuri huifanya injili iwe rahisi zaidi kueleweka. Siyo tu kwamba mwenzako katika mazungumzo ana kitu fulani cha kusikiliza, lakini pia ana kitu fulani cha kutazama wakati huohuo (kielelezo sauti na kuona).
4. Hutusaidia kubaki kwenye mada na kuongoza mazungumzo.
5. Huanza kwa namna chanya, yaani, kwa upendo wa Mungu kwa ajili yetu.

6. Hupelekea katika utekelezaji kwa namna ya asili wa kile kinachosikiwa.
7. Yapo mapendekezo kwa ajili ya ukuaji na huonesha umuhimu wa ukuaji wa kanisa.
8. Unaweza kuwa makini(kustamakani vema) zaidi kwa mtu unayezunguza naye kwa sababu unajua kile unachotaka kusema.
9. Hukusaidia kuanzisha mazungumzo kuhusu maswali ya imani. Mfano, unaweza tu kusema: Nimegundua mwongozo wenye muhtasari wa jumbe kuu za Biblia. Je unafahamu tayari?
10. Pia huwasaidia wale ambao bado hawajaifahamu Biblia, katika kuielezea injili kwa wengine na kuwaongoza kufanya uhusiano binafsi pamoja Kristo.
11. Unaweza kumpatia mtu husika baada ya kufanya mazungumzo yenu. Unapaswa kufanya hivyo pia! Watu wengi hutunza kwenye Biblia yao.
12. Wakati huohuo, mshiriki ambaye ameongozwa kwa Kristo hujifunza jinsi ya kuwaonesha wengine njia ya kumwendea Kristo.

Hata kuna sababu zingine zaidi. Jaribu hilo baada ya kuomba kisha ziweke katika utekelezaji. Kujifunza kwa uzoefu ni bora kuliko kusoma. Kama inawezekana, dhamiria kwamba “Kamwe sitaweza kujadili na yeyote hatua hii muhimu bila kuwa na mwongozo huu.”

## Zoefu chache zilizochaguliwa:

**Uzoefu 1:** “Niliweza kufanya mazungumzo mara moja tu na meneja wa miaka 40. Kwa kuanza, niliuliza swali kuu namba 1, naye akawa radhi tupitie pamoja kijizuu (brosha) husika. Kinachosikitisha, hakuwa radhi kumkubali Yesu siku hiyo. Hata hivyo, wakati wa kuagana, akasema: ‘Nataka kukushukuru kwa dhati sana. Kwa mara ya kwanza maishani mwangu, najua imani ya Ukristo ikoje.’ Wakati huo, mwanamama huyu bado hakuwa tayari. Lakini angalau alijua njia ya kumwendea Yesu baada ya mazungumzo yetu na angeweza kuipitia njia hiyo wakati

wowote ujao. Kwa kweli, nilimwachia kijitabu cha mwongozo kiitwacho *Jitwalie Uzima*.”

**Uzoefu 2**: “Wakati wa safari kutoka Bagdadi hadi Mossul huko Iraki, nilikuwa kwenye behewa moja la kulala pamoja na mwanafunzi wa Iraki. Tuliweza kuwasiliana kwa Kiingereza. Baada ya swali la kwanza, alitaka kujua pia jinsi ambavyo angepata uhakikisho. Mwishowe, alikuwa tayari kwa ajili ya ombi la kujisalimisha kwa Yesu Kristo. Nilikuwa nimemweleza nini kingejumuishwa kwenye ombi hilo nami nikamuuliza endapo alitaka kuomba ombi hilo. Alisema angeomba kwa kufuatisha mistari hiyo, lakini kwamba asingekumbuka kila kitu. Ningepaswa kutamka sentensi moja baada ya nyingine, naye angenifuatisha. Hivyo ndivyo nilifanya. Nilimtakia baraka tele za Mungu katika mapito haya ya kumwendea Yesu nami nikaelekeza mawazo yake katika ukweli kwamba kuna kanisa la Kiadventista katika mji wa nyumbani kwao huko Bagdadi.”

**Uzoefu3:** “Wakati wa safari yangu ya kwanza kwenye kanisa jipya mtaani, nilipata kumjua mshiriki wa kanisa mwema pamoja na mwanawe mwenye umri wa miaka 17. Kijana huyo alikuwa amelemaa kutokana na kemikali ya thalidomaidi. Baada ya swali la ufunguzi, wote walikuwa radhi na wenye shauku katika kuisoma pamoja nami kijizuu (brosha) cha *Jitwalie Uzima*. Wote wawili walikuwa tayari kuyasalimisha maisha yao kwa Yesu katika sala. Kijana huyo alibatizwa wakati fulani baadaye. Katika baadhi ya shuhuda zake kwa hadhara, kwa furaha alidai (alistamini) kwamba maisha yake kama mlemavu yamepata mawanda mapya kabisa kupitia Yesu.”

**Uzoefu 4:** “Wakati mwingine, nilizungumza na bwana fulani mwenye umri wa miaka 38 aliyekuwa amemwoa Mwadventista. Alikuwa mvutaji sigari aliyekithiri (sigara 70 kwa siku) na hakuwa na uwezo wa kuacha kuvuta sigara. Nilimweleza jinsi ambavyo angekuwa huru halahali na kikamilifu kwa msaada wa Mungu kupitia maombi na kudai ahadi za Mungu. Na ndicho kilichotokea. Muda mfupi baadaye, alinidhihirishia tatizo lingine zaidi: alikunywa chupa 10-14 za bia kwa siku. Sasa alitaka kuacha kunywa pombe pia. Tuliomba tena na Bwana akampatia ukombozi kamili akaondokana na pombe. Wakati uliofuata

nilipokutana naye, tulipitia naye kijizuu cha *Jitwalie Uzima*. Alikuwa mwelekevu kwa maswali na mawazo husika. Baada ya kuomba pamoja naye sala ya kujisalimisha, nilimuuliza: 'Tukichukulia kwamba ungekufa usiku wa leo, ungeokolewa?' Akajibu: 'Hakika.' Mkewe alipigwa butwaa. Kisha mumewe akaeleza: 'Yesu alijibu ombi langu la kwanza na kuniweka huru dhidi ya tumbaku, katika sala yangu ya pili aliniweka huru nikaachana na pombe, na kwa vile nimemwalika maishani mwangu, ameingia maishani mwangu. Hivyo, nimeokolewa.' Alikuwa sahihi. Ndipo akaanza kufanya ibada ya asubuhi pamoja na mkewe mpendwa. Alikuwa tayari kwa ajili ya masomo ya Biblia na punde akabatizwa. (Unaweza kupata maelezo yote ya kina kuhusu wokovu huu katika *Barua kwa Andrea, Namba 5: "Ushindi dhidi ya Tumbaku na Pombe."* Mbinu hii inaweza kutumiwa ili kukabili uraibu mwingine vilevile.)"

**Tafadhali chukua kifungasho cha Seti-Anzilishi na kusoma barua asili iitwayo *Barua kwa Andrea Na. 13 "Jitwalie Uzima."*** Nyenzo hii ya thamani ambayo imethibitishwa ulimwenguni kote (yenye vichwa vya somo tofauti) hutumiwa wakati wa kumwongoza mtu fulani aje kwa Yesu. Katika Sura ya 9 "Msaada wa Kivitendo," utapata taarifa za msingi kuhusu Seti-Anzilishi na mawasilisho mengine ya *Barua kwa Andrea*.

Baada ya kuusoma *Barua kwa Andrea Na. 13,* tafadhali rejea kwenye kitabu ili uendeleze usomaji katika Sura ya 7. Sura hii kuhusu *Barua kwa Andrea Na. 13* imeandaliwa kama mwongozo halimali ili kutumika kwa watu unaowasiliana nao. Pamoja na hilo, una ufafanuzi katika msisitizo na maswali unayoweza kutumia ili kumwongoza mtu fulani aje kwa Yesu. Maswali haya yatawasaidia kufanya uamuzi.

***Soma Barua kwa Andrea Na. 13 "Jitwalie Uzima"***

Baada ya usomaji huu, tafadhali rejea kwenye hatua hii kitabuni. Asante!

**Je swali gani la ufunguzi linaweza kutumika kistadi na kihalani ili kuhamasisha usomaji wa *Barua kwa Andrea***

***Na. 13 "Jitwalie Uzima"* pamoja na rafiki, ambalo huweza kupelekea kujenga uhusiano binafsi kwa Mungu?**

Nauliza:

*"Je naweza kukuuliza swali muhimu sana?"*

Wakati wote kila mmoja hujibu Ndiyo. Hata kama tulizungumzia mambo tofauti kabisa, daima niliweza kuingia kwenye wazo kuu kwa kutumia swali hili.

Kisha nauliza:

**Swali kuu namba 1:**

*"Tuchukulie kwamba ungekufa leo – kwa shambulio la moyo, ajali, nk.! Je ungekuwa na uhakikisho wa uzima wa milele pamoja na Yesu Kristo?"* – Kwa kawaida jibu ni *"Hapana,"* wakati mwingine *"Natumaini"* na kwa nadra *"Ndiyo!"* Kamwe huwa sitoi maelezo yoyote juu ya majibu haya.

Ni pale tu ambapo mtu fulani alijibu *"Ndiyo"* ndipo niliendelea kuuliza **swali kuu namba 1a.** Kisha nikasema:

**Swali kuu namba 1a:**

*"Je naweza kukuuliza swali lingine?"* Wakati wote huwa napata ridhaa yao, halafu ningeuliza:

*"Tuchukulie kwamba Mungu akuulize: Kwa nini unaamini unaweza kwenda mbinguni?"*

Jibu husika huonesha ikiwa mtu huyo anategemea kuhesabiwa haki kwa matendo au kuhesabiwa haki kwa imani. Pia huwa sitoi maelezo yoyote kuhusu jibu hili. *Barua kwa Andrea* huonesha kwamba tunaokolewa kwa neema ya Mungu kupitia imani.

**Swali kuu namba 2:**

*"Je unataka kupata uhakikisho huu?"* Hili wakati wote lilijibiwa kwa ukubalifu.

*"Je una dakika chache za kusoma pamoja nami kitu fulani juu ya mada hii?"*

Endapo jibu lilijibiwa kwa ukubalifu – ambayo ni kawaida – **ndipo ningewasilisha *Barua kwa Andrea* namba 13 ili tusome pamoja.** (Chukua nakala zakutosha endapo kuna watu wengi.)

Wakati wa kusoma pamoja, tunaweza kuwasaidia watu kutafakari kwa kuwauliza maswali. Lakini kama inawezekana,

hatupaswi kuuliza maswali mengi zaidi ya haya yaliyooneshwa hapa. Mara nyingi huwa tunazunguza sana na kuvurugwa kwayo.

Katika ibara zifuatazo, kila kitu ambacho kimeandikwa kwa mkono ni kile ambacho ningesema kama nyongeza. Napendekeza ukiandike kwenye nakala ya kijizuu chako. Ndivyo nifanyavyo. Tafadhali zingatia kwamba hii ni nyenzo yenu muhimu sana ya kuwaongozea watu waje kwa Yesu. Ni *Waraka pekee kwa Andrea* ambayo tunataka kuiandaa kwa makini sana.

**Sasa tunaanza kusoma pamoja na rafiki yetu**

"Hebu tuanze kusoma:"

## Jitwalie Uzima – Kupitia uhusiano binafsi pamoja na Mungu Barua kwa Andrea Na. 13

Siku ya 25

"Tunarudia tu swali letu muhimu. Nililitoa hapa. Alinivutia sana "

Siku ya 27

Mpendwa Andrea,[8]

Je naweza kukuuliza moja kwa moja swali muhimu sana?

**Tuchukulie kwamba ungekufa leo (kwa shambulio la moyo, ajali, nk.!) Je ungekuwa na uhakikisho wa uzima wa milele pamoja na Yesu Kristo? Usibaki gizani! Taarifa tano zitakusaidia kulipata jibu.**

Yeyote anayetafuta uhusiano pamoja na Mungu atafanya ugunduzi wa maisha yote:

### 1. Mungu ananipenda!

*"Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma Mwanawe pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa Yeye. Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba Yeye alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu."* (1 Yohana 4:9-10)

Ndiyo sababu Mungu ana mpango kwa ajili yangu. *"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali*

8 Jina hili lilichaguliwa ili kutukumbushia Andrea katika Biblia aliyemwongoza Petro nduguye aje kwa Yesu (Yohana 1:40-42).

*awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika Yeye.”* (Yohana 3:16-17)

Yesu anaahidi: *“...Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.”* (Yohana 10:10)

**Mungu ananikirimia mambo makuu:**

- Maisha maridhawa na yenye maana – sasa
- Uzima wa milele – baadaye

Kwa nini kukarimiwa na Mungu hakupewi uthibitisho mwingi? Nini sababu inayopelekea uhalisia huu mchungu?

## 2. Tumejitenga na Mungu!

Tangu mwanzo, wameitwa ili wafanye ushirika pamoja na Mungu. Walikuwa na uhusiano binafsi pamoja na Mungu. Kwa utashi wao huru, walijitenga na Mungu. Walidhani wangeweza kujitegemea kwa njia hii. Na hivyo, uhusiano wa karibu na Mungu ukapotea.

Biblia huuita uamuzi huu wawanadamu “dhambi.” Hivyo, haijalishi inajidhihirisha pengine kama uasi makusudi au usiowa kukusudia wa kumtojali Mungu.

**Dhambi hututenga na Mungu.**

Biblia inaeleza dhambi ni nini:

*“Lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso Wake msiuone, hata hataki kusikia.”* (Isaya 59:2)

*“Yeyote atendaye dhambi ana hatia ya kuvunja sheria ya Mungu, kwa kuwa dhambi ni uvunjaji wa sheria.”* (1 Yohana 3:4 GNT)

*“Kila lisilo la haki ni dhambi…”* (1 Yohana 5:17)

Wengi hutambua kwamba maisha yao hayana maana yoyote. Ndiyo maana hupambania maisha yenyewe maana. Lakini kwa namna gani? Bila Mungu?

Hata hivyo, maisha ya staha na heshima, mawazo kwa ajili ya kuuboresha ulimwengu au mafanikio ya kidini hayatambui ufa kati yetu na Mungu. Dhambi, pamoja na athari zake zote, haiondolewi kwa juhudi hizi zote.

Lipi jibu la Mungu kwa juhudi hizi zote za mwanadamu?

## 3. Jesus Kristo alikufa kwa sababu ya dhambi zangu!

Mauti Yake ililipa gharama za dhambi zangu:

*"Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, Na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona."* (Isaya 53:5)

*"Kristo Yesu ndiye aliyekufa; naam, na zaidi ya hayo, amefufuka katika wafu, Naye yuko mkono wa kuume wa Mungu; tena ndiye anayetuombea.*" (Warumi 8:34)

Yesu Mwenyewe alisema: *"Mimi ndimi Njia, na Kweli, na Uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya Mimi."* (Yohana 14:6)

Mungu alinifanyia, kile ambacho siwezi kufanya kwa ajili yangu mwenyewe: Aliingiliakati(Alihinikiza) ufa wa utengano kati yangu na Yeye. Hii ilitokea wakati Mwana wa Mungu alipokufa kwa ajili ya dhambi Zangu.

*"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo."* (Matendo 4:12)

Tunaweza kupata uhusiano binafsi pamoja na Mungu kupitia Yesu.

Haitoshi kujua tu ukweli huu. Mungu anangojea mwitikio. Unaweza kuwa kitu fulani kama hiki:

## 4. Namkubali Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wangu

*"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu."* (Waefeso 2:8-9)

Kumkubali Yeye humaanisha:

- ▶ Kuishi pamoja Naye katika uhusiano binafsi,
- ▶ Imani na kumtegemea(dhamani katika) Yeye.

*"Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake…"* (Ufunuo 3:20)

**(Stamani) Uwezekano wa aina Mbili:**




**(Ubinafsi) Fikra yangu kama kiini cha maisha yangu.**
(Ubinafsi) Fikra yangu hutawala.
Matokeo ni, mathalani, shauku ya uhalili, mashaka, wahaka, hatia, hangaiko la ndani, nk.




**Yesu Kristo kama kiini cha maisha yangu.**
Yesu Kristo huniongoza. Manufaa, miongoni mwa mambo mengine: *amani, uhakika, msamaha, upendo*

**Jibu langu kwa maswali yafuatayo ni muhimu sana:**

- ▶ Je ni kielelezo gani kinachoonesha maisha yangu?
- ▶ Yanahusiana sana na kielelezo cha juu ama cha chini?

(Pengine tunaweza kusaidia kwa kusema:)
"Hebu tuangalie tena vielelezo husika."
(Tulia kidogo baada ya hapo kisha uliza:)
"Kwa sasa, hivi ni kielelezo cha kushoto au kulia kinacho-husika zaidi?"
(Hatutoi maoni kuhusu jibu lake, badala yake tunasema:)

"Hebu tuendelee kusoma:"

- ▶ Hivi ninapenda maisha yangu yaonekaneje?
- ▶ Ni kielelezo gani unachotazamia katika siku zijazo?

(Sasa tunaweza kuuliza:)
"Ni kielelezo gani unachotazamia katika siku zijazo?"

(Hatutoi maoni kuhusu jibu lake, badala yake pengine tunaweza kusema:)

"Hebu tuendelee kusoma:"

- ▶ Nini ambacho kingeweza kunizuia nisimkubali Kristo maishani mwangu sasa?

(Baada ya kutulia kidogo, tunaweza kuuliza:)
"Nini ambacho kingeweza kukuzuia usimkubali Kristo maishani mwako sasa?"
(Kwa kawaida jibu: "Hamna kitu…")
(Hatutoi maoni kuhusu jibu lake, bali endelea kusoma:)

"Hebu tuendelee kusoma katika ukurasa wa 4:"

Tafadhali soma ukijumusha na sala.

(Lakini tafadhali zingatia kwamba unapaswa kuisoma sala hii taratibu na kwa ufasaha sana.)

## Jinsi gani naweza kumkubali Yesu Kristo maishani mwangu?

Naweza kufanya uamuzi leo, sasa, kwa ajili ya Yesu Kristo. Ni rahisi sana kuzungumza na Yesu. Biblia huiita hii **"Sala."** Sala yangu inaweza kuwa kwa hii:

***Pendekezo la Sala: "Bwana Yesu Kristo, nataka kukushukuru kwamba ulikufa na kufufuka tena kwa ajili yangu. Mimi ni mdhambi, tafadhali nisamehe. Tafadhali, njoo maishani mwangu sasa. Siwezi kujiokoa. Siwezi kuufanyia kazi ya malipo uzima wa milele. Ndiyo maana nakuamini. Niweke huru dhidi ya nguvu ya uovu. Nipatie nguvu ya kukufuata Wewe. Naisalimisha nafsi yangu Kwako pamoja na kila kitu nilicho nacho na vile nilivyo. Naukubali uzima wa milele. Sijauulipia; lakini nakushukuru kwa ajili ya karama hii. AMINA."***

**Je unaweza kusema 'Ndiyo' kwa sala hii?**

Hebu nipendekeze kusoma kwa makini tena. Swali ni kwamba: Je hilo hukubaliana na utashi wako? Kumbuka: utashi wako ni mahali pa Mungu kutua maishani mwako.

"Nitaisoma hii tena kwa sauti ili uamue kama unaweza kusema Ndiyo kwa sala hii."

Sasa, tafadhali soma sala hii mara ya pili kwa sauti taratibu na kwa ufasaha.

## Usomaji Mara ya Pili

Baada ya usomaji huu wa pili, uliza: "Je unaweza kusema Ndiyo kwa sala hii?"

Baada ya kutulia kidogo, wakati ambapo tunapokea ukubali, ama kwa neno au ishara za uso, tunaendelea.

Napendekeza kwamba tuombe/uombe sala hii kwa sauti sasa.

"Kabla ya hilo, hebu tusome sentensi inayofuata:"

Kama ni Ndiyo, basi nataka kujisalimisha binafsi Yesu Kristo kwa maneno ya sala hii iliyopendekezwa. Atasikia sala yangu.

"Endapo ni sawa kwako, hebu tupige magoti." Ni bora kupiga magoti katika sala kama hiyo. (Lakini siyo lazima iwe hivyo.)

## Sala

Baada ya kuomba pamoja, unaweza kusema:

"Hongera kwako! Bwana wetu mpendwa ameisikia sala yako. Tutaendelea tu kusoma hadi mwisho ili kuona nini maana ya jambo hili kwa kina."

Siku ya 28

## 5. Maisha yangu mapya pamoja na Yesu Kristo

Sasa nimempokea Yesu Kristo maishani mwangu. Nataka kuendelea katika njia hii pamoja Naye. Nachukulia kwa dhati ahadi za Mungu kwenye neno Lake.

Maisha mapya hayajengwi katika hisia, badala yake hujengwa katika taarifa za kweli katika Neno la Mungu:

*"Yeyote ambaye amejiunga na Kristo ni kiumbe kipya; hali ya kale imepita, hali mpya imekuja."* (2 Wakorintho 5:17 GNT)

Baadhi wanaweza kutegemea hisia ya kusisimua baada ya sala hii. Mhandisi mmoja alisema kwa fadhaa:

"Nimempatia Yesu Kristo ahadi yangu kufuatia sala hii ya kujisalimisha. Lakini nakosa hisia zinazowasiliana."

Umeyasalimisha maisha yako kwa Yesu Kristo. Sala yako ya kujisalimisha iliunda **ukweli mpya** kwa sababu Mungu na neno Lake hutumainika. Utambuzi ufuatao ni muhimu katika muktadha huu: **Taarifa hizi za kweli hazitegemei hisia zetu.** Kweli hizi ni halali kabisa bila hisia zozote. Hazitegemeani na hisia zangu.

Mfano: Siku yako ya kuzaliwa iko katika siku fulani maalumu. Lakini huna kabisa hisia za siku ya kuzaliwa! **Ukweli ni:** siku yako ya kuzaliwa iko katika siku hii – hata kama huna hisia zozote za siku ya kuzaliwa.

Unajua jedwali la kuzidisha. Mfano: 2 x 2 = 4; au 4 x 4 = 16. **Jedwali la kuzidisha ni ukweli** – wala huhitaji kuhisi hilo. Hisia hazina maana hapa. Hisia siyo geji ya taarifa za kweli!

> ***Mhandisi alifarijika alipotambua:***
> ***"Nimesema Ndiyo kwa Yesu Kristo. Hivi sasa mimi ni Mkristo – hata bila hisia zinazowasiliana***

***(shabihiani). Kinachosikitisha, kamwe mama yangu hakunieleza kanuni hii rahisi.”***

## Nini kipya au kimebadilika maishani mwangu?

1. Kristo ameingia maishani mwangu. (Ufunuo 3:20; Wakolosai 1:27)
2. Kristo husamehe hatia yangu. (Wakolosai 1:14; 1 Yoh1:9)
3. Mimi ni mali ya Mungu – mimi ni mtoto Wake. (1 Yoh 3:1)
4. Maisha yangu sasa yana maana ya kina. (Yohana 10:10; 2 Wakorintho 5:14-15,17)
5. Kristo hunisaidia kufuata mafundisho Yake. (Yohana 14: 15; 15:10-11)
6. Najiandaa kufanya agano pamoja na Kristo kupitia ubatizo. (Marko 16:16)
7. Kristo hunipatia uzima wa milele. (1 Yohana 5:12)

Yesu anaahidi: *“Nimekuja ili mweze kupata uzima – uzima katika utimilifu wake wote.”* (Yohana 10:10b GNT)

## Maisha ni ukuaji, kutuama ni kurudi nyuma.

Ndiyo sababu:

- ▶ Sijitazami nafsi yangu, bali namtazama Yesu Kristo.
- ▶ Nategemea ukombozi wa Mungu, siyo mabadiliko ya hisia zangu.
- ▶ Nadumisha muunganiko wa karibu pamoja na Bwana wangu.
- ▶ Nadumisha maisha ya maombi.
- ▶ Nasoma kila siku kwenye Biblia yangu – Neno la Mungu
- ▶ *Ninafanya ushirika wa mara kwa mara na Wakristo wenye nia sawa.*
- ▶ Namkiri Yesu Kristo katika mazingira yangu.
- ▶ Najiandaa kwa ajili ya ubatizo.
- ▶ Natazamia ujio wa pili wa Bwana wangu

Umeanza maisha mapya pamoja na Yesu Kristo. Nina furaha kwa ajili yako. Nataka kulinganisha uamuzi wako na ahadi ya ndoa. Ahadi ya ndoa hufanyika katika faragha. Muda mwafaka hufuatia hatua hii ya miadi. Mnafikia kufahamiana vema,

mnajifunza kupenda na kuamaniana zaidi, na mahusiano mapya huwa ya kina zaidi. Muda unapowadia ambapo mnataka kuwa pamoja milele, basi ndoa hufuata. Harusi pamoja na Kristo ni sawa na ubatizo wa Biblia.

*"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa."* (Marko 16:16)

Pengine ungesoma waraka wangu wote mara kadhaa kwa sababu nimejaribu kuandika muhtasari wa msingi wa uhusiano wetu na Mungu kupitia Yesu Kristo.

## Jinsi gani naweza kumjua Yesu Kristo vema zaidi?

Namna ileile tunayotumia kumjua mtu yeyote, asiyekuwepo. Kwa mazungumzo (miito ya simu). Kwa muktadha huu, tunaiita "sala." Kwa kusoma habari kuhusu wao. Inapendekezwa sana kusoma vitabu vya injili (Mathayo, Marko, Luka, Yohana) katika Agano Jipya ya Biblia. Hizi husimulila kuhusu maisha ya Yesu. Hutupatia muhtasari mzuri. Pamoja na hilo, usomaji wa Biblia kwa kuzingatia mada unapendekezwa – kwa ajili ya vidokezo vya kina zaidi. Kuna kozi za Biblia kwa njia ya barua zitolewazo bure katika nchi yoyote.

Kiasili, sasa ni suala la kufurahia na kudumisha uhusiano wetu mpya wa dhamani pamoja na Yesu Kristo. Yesu Kristo ametupatia msaada adhimu kwa ajili ya kusudi hili: maisha katika nguvu ya Mungu. Natazamia kuwasilisha mengi zaidi kuhusu hili katika waraka wangu unaofuata. (Maisha katika Nguvu ya Mungu – jinsi gani?)

Yesu ana shauku ya kudumisha uhusiano wa dhati na kudumu pamoja nawe. Alisema: *"Kaeni ndani Yangu, Nani ndani yenu."* (Yohana 15:4)

Sasa, nimemwalika Yesu Kristo aingie maishani mwangu kwa sala hii. Naamini kwamba atadumisha ahadi Zake maishani mwangu: *"Kamwe sitamfukuza yeyote ajaye Kwangu."* (Yohana 6:37 GNT)

*"Lakini tukiziungama dhambi zetu kwa Mungu, atadumisha ahadi Yake na kutenda haki: atatusamehe dhambi zetu na kutusafisha udhalimu wetu wote."* (1 Yohana 1:9 GNT)

Neno la Mungu hunipatia uhakikisho: *“Yeyote aliye na Mwana anao uzima huu; yeyote asiye na Mwana wa Mungu hana uzima huo.”* (1 Yohana 5:12 GNT)

Helmut na Kurt rafiki yangu
(Helmut Haubeil na Kurt Hasel)

**Mwisho wa nakala ya mazoezi ya Jitwalie Uzima**

## Hatua ya Kwanza katika Mwelekeo Sahihi

Moyo wako utajawa furaha kuu, pale mpendwa fulani anapoomba sala ya kujisalimisha katika *Barua kwa Andrea* namba 13. Lakini kumbuka kwamba hii ni hatua ya kwanza tu, lakini hatua muhimu sana, katika uelekeo sahihi. Bado angali hajawa tayari kubatizwa (kwa kawaida), lakini pengine yuko tayari kwa ajili ya masomo ya uanafunzi au masomo ya Biblia.

Mwisho wa waraka huu hufanya iwe rahisi sana kupendekeza usomaji wa Biblia wa ziada. Na bila shaka litakubaliwa kwenye mazingira haya chanya.

**Hapana kwa sala**

Ikiwa mtu husika asiposema Ndiyo kwa sala husika, ndipo unaweza kusema:

“Umepata kijizuu (brosha) na unaweza kusali sala hii baadaye ukipenda. Lakini tunaweza kukamilisha kuisoma pamoja sasa.”

Kama hana vizuizi vyovyote, basi mnaweza kukamilisha kukisoma kijizuu (brosha) pamoja. Ndipo, tunaweza kuirejea baadaye na kupendekeza kwamba asome tena kijizuu (brosha) hicho ili kujenga uhusiano binafsi pamoja na Kristo. Ikiwa hutaki kutumia kijizuu (brosha) katika jaribio lako la pili, basi tumia kitini kiitwacho *Njia ya Uzima wa Milele* (angalia pia kiambatisho C mwishoni mwa kitabu au www.steps-to-personal-revival.info – *Barua kwa Andrea)*. Kinahusika na mada hiyohiyo, lakini kwa mtiririko tofauti wa mawazo. Kimejumuishwa kama Z1 katika Seti-Anzilishi. Rafiki yetu hata hatambui kwamba tunarudia juhudi zetu za kumwongoza aje kwa Yesu. Ni muhimu kwamba tupate uelewa bayana kwa ajili ya hatua hii katika sala halafu tusonge mbele katika sala.

**Maneno ya Faraja**

Kijitabu hili kilikuwa na bado kingali nyenzo bora kwa ajili yangu. Nadhani nimepitia kijitabu hiki na watu 400 hadi 500 kwa kipindi cha miaka kadhaa. Sehemu kubwa ya hatua hii ilifanyika katika mazungumzo ya ana-kwa-ana na katika mkutano wa kwanza. Wengi wao wakawa wafuasi wa Yesu. Wakati mwingine watu wananiuliza tunapokutana mwanzoni niwatembelee jamaa au marafiki zao na kuwafikishia ujumbe huu. Ni msaada makini kwa ajili ya sehemu ya kwanza ya kukutana. Hupelekea kufanya Masomo ya Uanafunzi au masomo ya Biblia au kutoa somo pamoja. Kuna machapisho mengi sana mazuri yaliyopo sasa kwa ajili ya awamu zingine za kutembelea

Katika sura ya 9 naonesha jinsi ninavyoweza kusonga mbele katika kumtambulisha Yesu baada ya hatua chache za ziada za maandalizi.

**Dondoo za Kiutendaji**

Huweza kuwa msaada mkuu kama ukiandika maswali kutoka hapo juu (yaliyo kwenye msisitizo) kwenye nakala ya kijizuu chako mwenyewe.

Kama ukipenda, unaweza kufanyia mazoezi utaratibu mzima ukiwa na rafiki fulani au mwanafamilia ili upate kujiamini (staamani). Na kama hujisikii kumsaidia maswali mwanadarasa, basi someni pamoja bila maswali yoyote au ahirisheni hadi wakati mwingine. Au liombeeni jambo kwa dhati kisha mpatie mtu huyo asome peke yake.

Ikiwa mtu fulani anataka kuachana na tumbaku na/au pombe au aina yoyote ya uraibu, tumia *Barua kwa Andrea* ***namba 5: "Ushindi dhidi ya Tumbaku na Pombe. Jinsi gani unaweza kuwa huru kabisa dhidi ya uraibu mbalimbali, kwa msaada wa Mungu?"*** Kwenye ukurasa 127 kwenye Uzoefu wa 4 ni mfano mfupi. – Ni muhimu kumwongoza kwa Yesu mtu aliyewekwa huru kwa kutumia ama ***"Jitwalie Uzima"*** au/na ***"Njia ya Uzima wa Milele"*** ili aweze kuyapinga majaribu. Inahusu hatua ya kuepuka kurudia uraibu.

## Njia ya Uzima katika Nguvu ya Mungu, kuishi katika Roho Mtakatifu

Tunatumia *Barua kwa Andrea* **Na. 14.**

Hatua inayofuata, ambayo ni muhimu zaidi baada ya kumkubali Yesu maishani mwetu, inapaswa kuwa, kama inawezekana, kujifunza Biblia kwa kutumia *Barua kwa Andrea* **namba 14:** *"Kuishi katika Nguvu ya Mungu – Jinsi gani?"* (inapatikana kwenye kitabu hiki sura ya 8)

Kwa namna hii, mpendwa huyu anaweza kuongozwa katika maisha ya kudumu katika Kristo. Hapa, wala huhitaji kuuliza maswali mengi sana kwa sababu maswali sahihi yamejumuishwa kwenye mada husika.

Kwa kweli inapendekezwa kurudia *Barua kwa Andrea* **Na. 13** (au *"Njia ya Uzima wa Milele"* – maelezo zaidi juu ya hili yanakuja hivi punde) na *Barua kwa Andrea* Na. 14 kwa ajili ya vidokezo vingine zaidi. Omba kwamba Roho Mtakatifu aweze kukuongoza katika hatua yenu inayofuata.

Endapo hatua mbili zimefanyika (sala kwa mujibu wa sura ya 7 na maendeleo chanya maishani kupitia nguvu ya Mungu kwa mujibu wa sura ya 8), basi huo ni msaada mkubwa kama ukipendekeza baadaye asome kitabu kiitwacho *Hatua za Uamsho Binafsi* na kisha *Kaeni Ndani ya Yesu* au mngeweza kujifunza pamoja. (Angalia ofa za kitabu husika mwishoni mwa kitabu hiki.)

## Uzoefu
## Mtihani kabla ya uchapishaji

"Niliwaomba wanateolojia wawili wafanye tathmini. Jibu la kwanza lilikuwa (katika nukuu):

Kazi yako katika *Hatua za Uamsho Binafsi* hakika ni tunu kutoka mbinguni, "Mahubiri yako juu ya *Hatua za Uamsho Binafsi* ni tunu kutoka mbinguni, kwanza kwako kisha kupitia kwako kwa ajili ya wasomaji wote. Japo hivi karibuni vimekuwepo vitabu kadhaa halimali na vya kina kiroho kanisani mwetu, *Hatua za Uamsho Binafsi* visivyo vya kawaida. Katika namna iliyosheheni vilivyo na yenye maelezo ya kina, njia ya utimilifu imebainishwa na Roho Mtakatifu. Yeyote akisomaye hawezi kuepuka kufanya tathmini yake ya kiroho na kufanya uamuzi."

Barua pepe Mei 1, 2012 – Ndugu wote wawili wanapendekeza kuchapishwa.

**Kutoka Kanisa la Ludwigsburg**– “Mimi na mume wangu tulikuwa tukijifunza kitabu kiitwacho *Siku 40 Na 1* na tulipata uzoefu wa baraka kuu binafsi kwa kuomba pamoja. Baadaye, tuliratibu mikutano ya maombi mara mbili kwa juma kanisani Ludwigsburg na kusoma kitabu hiki pamoja na washirki wetu wa kanisa. Kwa namna bayana kabisa, tulipata uzoefu wa uongozi na baraka za Mungu na miujiza tele! Mungu alituburudisha na kuliamsha kiroho kutano letu la kanisa: washiriki ambao hapo awali kamwe hawakuweza kuzungumza na watu, ghafla wakakutana na wageni. Tulipoungana kwenye maombi, Mungu alitushikamanisha pamoja kama kutano. Kuomba kwa ajili ya watu 5 kipindi cha siku 40 kulileta matokeo yasiyo ya kawaida – Mungu alitenda kazi kwa nguvu kuu juu ya watu hao. Mara kadhaa watu wanakuja kwenye huduma kanisani mwetu katika Sabato kutoka mtaani. Mojawapo ya familia hizo sasa hupokea mafunzo ya Biblia. Waligundua juu ya Sabato kupitia video kwenye mtandao na kupitia kitabu kiitwacho *Pambano Kuu* nao walikuwa wakilitafuta kanisa kwa muda fulani.” K.a.C.S. (imefupishwa) Web T1

**Sala Changamfu ya Maombezi** – “Mwanzoni, nilisoma kitabu chote cha (*Siku 40 Na 1*). Sasa kwa vile napitia masomo ya maombi haya pamoja na mwanamaombi mwenzangu, natambua kwamba ni ya thamani zaidi kuliko nilivyodhani awali! Nilipata majibu ya maswali ambayo nisingeweza kuyasuluhisha mwenyewe. Namshukuru Mungu pia kwa ajili ya mwanamaombi mwenzangu anayeshiriki kwa wazi na kwa nguvu nyingi. Nilivutiwa na kitabu hiki tangu kurasa za kwanza. Hatupaswi tu kumwombea mtu fulani, lakini pia tumhudumie mtu huyo kwa upendo. Hili huifanya Sala ya Maombezi iwe hai. Najuta kwamba kamwe sikuiona sala ya maombezi kwa namna hii hapo awali. Imani hai, changamfu! Nashawishika kwamba maombezi ni muhimu kwa yule aombaye kama ilivyo tu kwa yule aombewaye.” Web T6

## Mawazo binafsi na mwongozo wa mjadala

1. *Je jibu langu lingekuwa lipi kwa swali la ufunguzi, endapo mtu fulani angeniuliza?*

2. *Kwa nini ni vema kujifikiria kuwa katika hatua zifuatazo za injili? (1. Mungu ananipenda! 2. Tumejitenga na Mungu! 3. Yesu Kristo alikufa kwa sababu ya dhambi zangu!)*

3. *Kwa nini maswali (kwenye dondoo ya 4- Namkubali Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wangu) hunisaidia kutambua nafasi yangu binafsi kiroho? Hilo linachochea nini baadaye?*

4. *Jinsi gani mtu anaweza kumkubali Yesu Kristo maishani mwake?*

5. *Nini huwa kipya katika kufikiri, kuhisi, kuzungumza na kuamua, unapojisalimisha kwa Yesu?*

6. *Kumkubali Yesu kupitia sala ya kujisalimisha ni hatua ya kwanza katika uelekeo sahihi. (Linganisha na ahadi na ndoa). Jinsi gani mpendwa huyu anavyoweza kufikia hatua ya kumjua Yesu vema? Tunawezaje kumsaidia hapa?*

## Muda Wetu wa Maombi

- Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.
- Sali pamoja na mwanamaombi mwenzio…
  1. Kwa ajili ya uhakikisho kwamba wewe ni mtoto wa Mungu na hivyo umeokolewa.
  2. Kwa ajili ya utambuzi ili kuona palipo na vikwazo maishani mwangu vinizuiavyo kujisalimisha kikamilifu kwa Yesu.
  3. Kwa ajili ya furaha ya kuishi maisha yako pamoja na Kristo.
  4. . . . kwamba unaweza kuambatana na watu wakiwa katika mapito yao ya kumwendea Yesu.

SURA YA 8

# Tunawezaje Kuwaongoza Watu Waishi Katika Nguvu ya Mungu?

## Kupitia kujifunza somo la Biblia pamoja kwa kutumia Barua kwa Andrea Na. 14 – Maisha katika nguvu ya Mungu – kwa namna gani?

Hapa ningependa kupendekeza kwamba uende kwenye Seti-Anzilishi na kusoma barua asili Na. 14: “Maisha katika nguvu ya Mungu – jinsi gani?” – Tafadhali, njoo katika hatua hii baadaye ili uendelee. Hii kuwa ya thamani kwako kwa uhusiano wako binafsi pamoja na Roho Mtakatifu na itakuwezesha kuifahamu nyenzo hii makini. Asante sana kwa uelewa wako.

Hakuna maelezo maalumu yanayohitaji hapa, isipokuwa kama mwenzetu ana swali. Hata hivyo, tunaweza kuulizwa maswali pale tunapodhani ni muhimu. Endapo mtu fulani anataka kufahamu kwa kina zaidi katika suala hili muhimu, basi hatuna budi kuwarejesha kwenye *Hatua za Uamsho Binafsi* (uk. 205) au tujifunze pamoja naye.

Mpendwa Andrea![9]

Nililazimika kuendesha maziko ya mwanadada daktari. Niliomba Biblia yake ili nipate rejea kadhaa kwa ajili ya kulifanya wasilisho hilo liwe binafsi zaidi. Nilipata mahali ambapo alikuwa ameandika: “Nataka uzima tele!” Alikuwa akitaka kile hasa ambacho Yesu pekee anaweza kutukirimia:

*“...Mimi nalikuja ili wawe na* ***uzima****, kisha wawe nao* ***tele.”*** (Yohana 10:10)

Yesu anataka tupate uzoefu wa maisha haya mapya sasa na tuendeleze maisha haya mapya kama uzima wa milele katika ufalme wa Mungu atakapokuja tena.

9 Jina hili lilichaguliwa ili kutukumbushia Andrea katika Biblia aliyemwongoza Petro nduguye aje kwa Yesu (Yohana 1:40-42).

Changamoto sasa ni jinsi gani tunaweza kupata hamasa na nguvu kwa ajili ya uhusiano wenye furaha na udumuo katika maisha pamoja na Yesu.

Ulinganisho ufaao: Gari lisilo na mafuta. Kuna shuluhisho za aina mbili tu: kulisukuma gari hili au kutafuta mafuta. Ni pale tu gari linapokuwa na mafuta ndipo linaweza kutimiza kusudi lake.

***Maisha ya Ukristo bila nguvu ya Mungu yanaweza kulinganishwa na gari bila mafuta.***

Hivyo: Nawezaje kuishi katika nguvu ya Mungu? Yesu aliwaambia wanafunzi Wake:

*"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu..."* (Matendo 1:8)

Hilo linafanyikaje? Ni wapi tunaweza kupata taarifa za kina zaidi? Hii ni ibara ya pekee kwenye Biblia, ambapo Bwana wetu mpendwa Yesu kwa upendo na kwa dhati anatuhimiza tuombe kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Hili hapa andiko husika – Luka 11:9 -13:

*"Nami nawaambia, **Ombeni**, nanyi mtapewa; **tafuteni**, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa. Kwa kuwa kila **aombaye** hupokea; naye **atafutaye** huona; naye **abishaye** atafunguliwa. Maana ni yupi kwenu aliye baba, ambaye mwanawe **akimwomba** mkate, atampa jiwe? Au **akimwomba** samaki, badala ya samaki atampa nyoka? Au **akimwomba** yai, atampa nge? Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je, Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao **wamwombao**?"* (Luka 11:9-13)

Je unatambua kitu fulani? Yesu alitumia kitenzi "omba" mara sita kwenye ibara hii; kisha anabadilisha neno "omba" mara mbili na kuingiza kwa neno "tafuta"—kitenzi amilisi—kisha mara mbili tena kwa kitenzi "bisha"—pia kitenzi amilisi. Hivi hii haituoneshi bayana kwamba tunapaswa kuchukua hatua? "Omba" ya mwisho iko katika kitendo endelevu katika Kiyunani. Hii ina maana kwamba hatupaswi kuomba mara moja tu, badala yake tuendelee kuomba daima. Siyo tu kwamba Yesu anasisitiza juu ya uharaka wa kuomba, bali pia anatarajia tuendelee kufanya hivyo daima. Hii hutuonesha kwamba Yesu amesadikisha kwamba tunakosa kitu fulani muhimu sana. Ni

wazi anavuta usikivu wetu uelekee kwenye ukweli kwamba tunamhitaji Roho Mtakatifu na kwamba tu wategemezi Kwake.

Yesu anatuonesha kwa ustadi – kwa kuvirudia vitenzi mara kwa mara na kufanya malinganisho – hitaji letu kuu zaidi: tunapaswa kuomba daima kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Hili ni jambo la pekee. Linahusiana na karama turufu ya Mungu – karama iletayo karama zingine zote katika msafara wake. Hii ndiyo karama adhimu ambayo Yesu aliwapatia wanafunzi Wake na ndiyo uthibitisho bayana wa upendo Wake.

*Kila siku itakuwa tamashani kwetu, pale tunapotambua uhalisia wa maisha yaliyojazwa Roho Mtakatifu na daima kukabidhi nafsi zetu kwenye uongozi Wake.*


## Biblia huzungumza kuhusu makundi matatu tofauti ya watu kwa muktadha wa uhusiano wao na uhusiano na Mungu:

Jiulize: Niko kwenye kundi gani? Na – hivi nataka kuwa kwenye kundi gani?

**A. Mtu wa Asili**

Huyu ni mtu ambaye bado hajamkubali Kristo.

*“Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni.”* (1 Wakorintho 2:14)




**Maisha yatawaliwayo na Fikra yangu (ubinafsi)**

E = Ubinafsi, nafsi yenye ukomo inatawala


† = Kristo nje ya maisha yake

• = Maeneo ya maisha yatawaliwayo na ubinafsi na mara nyingi husababisha mfarakano na fadhaa

**B. Mtu wa Kiroho**

Huyu ni mtu ambaye amempokea Kristo na anaongozwa na Roho Mtakatifu.

*“Lakini mtu wa rohoni huyatambua yote…”* (1 Wakorintho 2:15)



**Maisha yaongozwayo na Kristo**

† = Kristo yu katika enzi ya maisha


E = Ubinafsi umepinduliwa(umetushwa)

• = Maeneo ya maisha yaliyoko chini ya uongozi wa Mungu asiye na ukomo na hukua katika upatanifu na mpango wa Mungu

## C. Mtu wa Mwilini

Huyu ni mtu ambaye amemkubali Kristo, lakini mara nyingi hupitia uzoefu wa kushindwa kwa sababu anajaribu kuyaishi maisha ya Ukristo kwa nguvu zake mwenyewe, badala ya kuishi katika uwezo wa Roho Mtakatifu.

*"Lakini, ndugu zangu, mimi sikuweza kusema nanyi kama na watu wenye tabia ya rohoni, bali kama na watu wenye tabia ya mwilini, kama na watoto wachanga katika Kristo. Naliwanywesha maziwa sikuwalisha chakula; kwa kuwa mlikuwa hamjakiweza. Naam, hata sasa hamkiwezi, kwa maana hata sasa ninyi ni watu wa tabia ya mwilini. Maana, ikiwa kwenu kuna husuda na fitina, Je si watu wa tabia ya mwilini ninyi; tena mnaenenda kwa jinsi ya kibinadamu?* (1 Wakorintho 3:1-3)



**Maisha yatawaliwayo na Fikra yangu (ubinafsi)**

E = Ubinafsi, nafsi yenye ukomo inatawala

† = Kristo maishani mwake, lakini hayuko kwenye enzi

• = Maeneo ya maisha yatawaliwayo na ubinafsi na mara nyingi husababisha mfarakano na fadhaa.

Tunataka kuliangalia suala hili muhimu katika hatua nne. Tutaangalia kwa kina zaidi hali ya watu wa kiroho na wa mwilini.

## 1. Mungu anataka tuwe na maisha timilifu na yazaayo matunda.

Yesu alisema: *"Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele."* (Yohana 10:10)


*"Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi,* ***akaaye ndani Yangu Nami ndani yake,*** *huyo huzaa sana; maana pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote."* (Yohana 15:5)

*"Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi."* (Wagalatia 5:22-23)

*"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi Wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi."* (Matendo 1:8)

**Mtu wa kiroho**

Baadhi ya silika zilizo sifa za maisha ya kudumu pamoja na Mungu:



- "Kristo ni ndiye kiini
- "Mamlaka kupitia Roho Mtakatifu
- "Maisha ya maombi fanisi
- "Kulielewa neno la Mungu
- "Kumwamini Mungu
- "Kumtii Mungu
- "Kuwaongoza watu wengine waje kwa Kristo

*Upendo/ Furaha/ Amani/ Uvumilivu/ Utuwema/ Fadhili/ Uaminifu/Upole/Kujitawala*

Matokeo ya silika hizi maishani mwetu hutegemea ukomavu wetu katika Kristo katika kiwango cha muunganiko wetu pamoja Naye na pia endapo tutamdhamani kikamilifu maeneo yote ya maisha yetu.


Mtu fulani ambaye ndipo tu anaanza kuielewa kazi ya Roho Mtakatifu, hapaswi kuvunjika moyo pale anaposhindwa kuzaa matunda mengi kama Mkristo aliyekomaa, ambaye kwa muda mrefu ameufahamu ukweli huu.

**Kwa nini Wakristo wengi hawapati uzoefu wa maisha haya timilifu?**

## 2. Nani ambaye hawezi kupata uzoefu wa maisha ya Ukristo timilifu na yazaayo matunda?

**Mtu wa Mwilini**

Baadhi au silika zote zifuatazo huwapambanua Wakristo wa mwilini, wasiomwamini Mungu kikamilifu.




- “Kutojua karama za kiroho alizo nazo
- “Kutoamini
- “Kutotii
- “Upendo haba kwa Mungu na wengine
- “Maisha hafifu ya maombi
- “Shauku duni katika Biblia

*Mawazo machafu/Husuda/Hatia/Hofu zisizohitajika/ Kuvunjika moyo/Tabia ya ukosoaji/Fadhaa/Kukosa malengo/Ushupavu wa sheria (dhana kwamba wanapaswa kupokea malipo fulani kutoka kwa Mungu)*

(Mtu fulani anayedhani ni Mkristo halisi, lakini hudumu kutenda dhambi, anapaswa kujichunguza kwa mujibu wa 1 Yohana 2:3, 3:6, 3:9 na Waefeso 5:5 ili kuona kama ni Mkristo kweli.)

**Dondoo ya tatu hutuonesha ufumbuzi pekee wa tatizo hili…**

Siku ya 30

## 3. Yesu ametuahidi maisha timilifu na yazaayo matunda. Ni matokeo ya kujazwa Roho Mtakatifu, pamoja na uongozi na mamlaka ambayo Roho Mtakatifu hutupatia.

Maisha yaliyojazwa Roho ni maisha ambayo ndani yake Kristo anashikilia uongozi. Kristo huyaishi maisha Yake ndani yetu na hutenda kazi ndani yetu na kupitia sisi kwa uwezo endelevu wa Roho Mtakatifu. (Yohana 15)

**A.** Kwa mujibu wa Yohana 3:1-8, mtu anakuwa Mkristo kupitia utendaji wa Roho Mtakatifu. Wakati wa kuzaliwa kwetu kiroho, tunapokea maisha mapya kupitia Kristo.

Tunaambiwa katika Yohana 14:17 kwamba Roho Mtakatifu hudumu karibu nasi na ndani yetu.

Tunapaswa kuzingatia:

Tulipokea maisha yetu ya asili wakati wa kuzaliwa. Tulipewa kwa kusudi kwamba yangehifadhiwa katika kipindi chote cha uhai wetu. Kwa nje, huhifadhiwa kwa hewa, maji, chakula, nk. Ndivyo ilivyo hasa katika ulimwengu wa kiroho kama katika ulimwengu wa asili. Tunapokea maisha yetu ya kiroho – Biblia huiita hiyo *“kuzaliwa mara ya pili”* (Yohana 3:3), pale tunapojisalimisha kikamilifu kwa Kristo na kulithibitisha hili kupitia ubatizo wa Biblia kwa muda mwafaka (Matendo 2:38; Yohana 1:12; Yohana 14:16-17). Ili maisha haya ya kiroho yaweze kuhifadhiwa, huhitaji kudumu pamoja na Roho Mtakatifu, sala, Neno la Mungu, nk.

**B.** Roho Mtakatifu ni chanzo cha maisha timilifu (Yohana 7:37-39).

**C.** Roho Mtakatifu alikuja kumtukuza Kristo. (Yohana 16:1-15) Mtu fulani anapokuwa amejazwa Roho Mtakatifu, ndipo huwa mfuasi mwaminifu wa Yesu Kristo.

**D.** Kristo alituahidi nguvu ya Roho Mtakatifu katika maneno Yake ya mwisho kabla hajapaa mbinguni, ili tuwezeshwe kuwa wanafunzi na mashahidi Wake (Matendo 1:1-9).

**Jinsi gani mtu anaweza kujazwa Roho Mtakatifu?**

## 4. Tunajazwa Roho Mtakatifu kwa imani.

**Ndipo tunaweza kupata uzoefu wa maisha maridhawa na yazaayo matunda, ambayo Kristo ametuahidi.**

Hatuwezi kulipia vitu maridhawa vya Mungu – ni karama. Tunaipokea kupitia imani – kwa kumwamini Mungu.

Unaweza kupata uzoefu wa hali ya kujazwa Roho Mtakatifu sasa, mathalani:

**A.** Unapokuwa na shauku halisi ya kujazwa na kuongozwa na Roho Mtakatifu (Mathayo 5:6; Yohana 7:37-39).

**B.** Omba kwa imani ili kujazwa Roho Mtakatifu, kwa maneno mengine, kuamini kwamba Yesu Kristo atajibu maombi yako.

Yesu alisema:

*“Aniaminiye Mimi, kama vile Maandiko yalivyonena, mito*

*ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake. Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho…”* (Yohana 7:38-39)

*“…tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani.”* (Wagalatia 3:14)

Mungu ameturahisisha kumwani Yeye kwa kutukirimia ahadi halisi. Anasema katika 1 Yohana 5:14: *“Na huu ndio ujasiri tulio nao Kwake, ya kuwa,* ***tukiomba kitu sawasawa na mapenzi Yake, atusikia.”***

Wale wanaoomba kwa mujibu wa mapenzi ya Mungu – fungu linayofuata inasema:
*“Na kama tukijua* [kwa sasa] *kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba.”* (1 Yohana 5:15)

Fasiri nyingine (NIV) inasema:
*“Na kama tunajua kwamba anatusikia – chochote tuombacho – tunajua kwamba tuna kile ambacho tumemwomba.”* Hii humaanisha kwamba sala zinazopelekana na mapenzi ya Mungu zinajibiwa mara hiyo, tunapozileta mbele ya Mungu, hata mara nyingi hatuhisi chochote. Hizi zinaweza kujitokeza baadaye.

**Mfano:**
Mtu fulani anaomba kuwekwa huru aachane na tumbaku. Ombi lake hujibiwa kwa imani wakati ule anapotamka hitaji lake. Saa chache baadaye, anatambua kwamba haendelei tena kutamani tumbaku. (Maelezo zaidi ya kina yanapatikana katika *Barua kwa Andrea* Na. 5 juu ya *“Ushindi juu ya Tumbaku na Pombe.”* Tazama katika www.steps-to-personal-revival.info – *Barua kwa Andrea)* Kuomba kwa ahadi pia kumeelezewa kwa kina katika *Hatua za Uamsho Binafsi*, Sura ya 5 – tazama tovutile ileile).

Yesu anasema katika Marko 11:24: *“Kwa sababu hiyo nawaambia, Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea* [hakika]*, nayo yatakuwa yenu.”*

**C.** Mungu ametupatia ahadi katika Luka 11:9-13 kwa ajili ya kumpokea Roho Mtakatifu. Tayari tumeliangalia hili

mwanzoni mwa waraka huu, hivyo tu fungu la 13: *"Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je, Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?"*

Jinsi gani ya kuomba kwa imani ili kujazwa Roho Mtakatifu.

Sala kwa kutumia ahadi huimarisha dhamana yetu katika kupewa hilo, na wakati huohuo ni fursa ya kuelezea imani yetu. Ifuatayo ni sala inayopendekezwa:

***" Baba uliye mbinguni, nakuja Kwako katika jina la Yesu. Siwezi kukufuata kwa uwezo wangu mwenyewe. Unajua jitihada zangu zinazoshindwa. Nakuomba kwa dhati unipatie nguvu ya kuishi kadiri ya mapenzi Yako. Uliniamuru: "mjazwe Roho!" (Waefeso 5:18) Niko radhi kujazwa. Nakuomba tafadhali lifanye hili liwe halisi sasa, kwa sababu umeahidi kwamba una shauku ya kutupatia Roho Mtakatifu kuliko vile ambavyo akina baba duniani walivyo na shauku ya kuwapatia watoto wao vitu vyema (Luka 11:13). Nataka kukushukuru kwamba tayari umenijaza, kwa sababu umeahidi kwamba ninapoomba kadiri ya mapenzi Yako, ndipo najua kwamba tayari ninacho kile nilichokiomba (1 Yohana 5:14-15). Tafadhali niongoze na kunitumia leo kadiri ya mapenzi Yako. AMINA."***

Je ombi hili linapelekana na shauku zako? Ikiwa ndivyo, basi lifanye hili kuwa ombi lako sasa. Napendekeza kwamba uombe sala hii kwa sauti na kuamani kwamba Mungu amekujaza sasa Roho Mtakatifu.

## Uhakikisho kwamba umejazwa Roho Mtakatifu

Je umemwomba Mungu akujaze Roho Mtakatifu? Kwa msingi wa mamlaka gani unaweza kujua endapo umejazwa Roho Mtakatifu? (Kwa sababu Mungu na neno Lake huamanika: Waebrania 11:6; Warumi 14:22-23.)

Hisia siyo muhimu. Ahadi za Mungu katika neno Lake ndiyo muhimu hasa – siyo hisia zetu. Mkristo huishi kwa imani, ikimaanisha kwa kuamini na kumtegemea Mungu na neno Lake.

Kielelezo kifuatacho kinapaswa kuonesha uhusiano kati ya taarifa yakinifu (Mungu na neno Lake), imani (kumwmini Mungu na neno Lake) na hisia (matokeo ya imani na utii) (Yohana 14:21).




Treni inaweza kusafiri ikiwa na mizigo au ikiwa tupu. Ni jambo lisilofikirika kuhusu mizigo kuvuta kichwa cha treni. Vilevile, Wakristo hawategemei mhemko na hisia zao, bali wanaweka matumain yao (imani) katika kumtegema Mungu na ahadi katika neno Lake.

Siku ya 31

## Jinsi gani ya kuishi katika Roho Mtakatifu

Mkristo anaweza tu kuwa na maisha yaliyojawa Roho Mtakatifu kwa imani (mtegeme Mungu na ahadi Zake). Kwa kufanya hivyo, tunapaswa kuzingatia kile ambacho 2 Wakorintho 4:16 inasema:

*"...lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku."*

Hii ndiyo sababu inashauriwa kwamba tufikishe maisha yetu kwa Mungu kila asubuhi na kwa imani tumwombe – hususan pamoja na ahadi – ili tuweze kubadilishwa na Roho Mtakatifu. Unapoishi siku kwa siku huku ukimtumainii Kristo, ndipo yatuatayo yatatokea:

**A.** Maisha yako yatazidi kuzaa matunda tele ya Roho (Wagalatia 5:22); tabia yako inaendelea kufanana na ile ya Kristo (Warumi 12:2; 2 Wakorintho 3:18).

**B.** Maisha yako ya maombi na usomaji wa neno la Mungu vitakuwa na maana zaidi.

**C.** Utapata uzoefu wa nguvu Yake ya kupinga majaribu na dhambi.

Neno la Mungu linasema:

*“Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo…”* (1 Wakorintho 10:13)

*“Nayaweza mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu.”* (Wafilipi 4:13)

*“Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu Zake.”* (Waefeso 6:10)

*“Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi.”* (2 Timotheo 1:7)

*“Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. Kwa sababu sheria ya Roho* [Roho Mtakatifu] *wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti.”* (Warumi 8:1-2)

*“Twajua ya kuwa kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi; bali yeye aliyezaliwa na Mungu hujilinda, wala yule mwovu hamgusi.”* (1 Yohana 5:18)

**D.** Utapata uzoefu wa Mungu unaposhuhudia (Matendo 1:8).

## Upumuaji wa Kiroho

**Kwa imani unaweza kuendelea kupata uzoefu wa upendo na msamaha wa Mungu. Inapobainika kwako kwamba Mungu haridhii kitu fulani (mtazamo au tendo fulani) maishani mwako, japo unaishi pamoja Naye na kwa dhati unataka kumfuata, basi ungama dhambi yako, mathalani, kosa fulani, moyo wa kutofanya suluhu, nk. Kisha mshukuru kwamba amekusamehe dhambi zako kwa sababu Kristo alikufa msalabani. Uukubali upendo na msamaha Wake kwa imani na kuendelea kuishi katika ushirika pamoja Naye.**

Unapotenda dhambi – tendo la kutotii – basi jizoeze kufanya upumuaji wa kiroho.

Upumuaji wa kiroho (kutoa hewa chafu na na kuvuta hewa safi) ni zoezi la imani, ambalo kwalo unaweza kupata uzoefu wa upendo na msamaha wa Mungu.

**1. KUTOA HEWA**

Ungama dhambi yako kwa jina; kubaliana na Mungu kuhusiana na hukumu ya dhambi yako kisha mshukuru kwa ajili ya msamaha Wake (1 Yohana 1:9 na Waebrania 10:1-25). Maungamo hujumuisha toba – badiliko la mtazamo au matendo.

**2. KUVUTA HEWA**

Salimisha tena kwa Kristo hatamu ya maisha yako halafu omba tena kwa imani kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Amini kwamba ataendelea kukuongoza kama alivyoahidi katika Luka 11:13 na 1 Yohana 5:14-15.

**Maelezo haya yanapokuwa yenye msaada, basi tafadhali gawa nakala yake au msomee mtu fulani. Uwe na furaha kuu katika maisha yako mapya katika uwezo wa Mungu.**

Nakutakia kila la heri na baraka,

Helmut na rafiki yangu Kurt

(Helmut Haubeil na Kurt Hasel).

## Mawazo binafsi na mwongozo wa mjadala

1. *Kwa nini maisha ya Ukristo bila uwezo wa Mungu yanaweza kulinganishwa na gari bila mafuta?*

2. *Ni mwaliko gani wa upendo aliotupatia Yesu ili tuweze kujazwa nguvu ya Roho Mtakatifu? Nini tupaswacho kufanya? ( "Omba" ya mwisho katika Luka 11:13 iko katika njeo endelevu katika Kiyunani: hiyo ina maana kwamba kuendelea kuomba, kuomba daima)*

3. *Ni makundi gani matatu tofauti yaliyopo kwa kuzingatia uhusiano uliopo kwa Mungu? Ni kundi gani ulilomo?*

4. *Jinsi gani mtu fulani anaweza kujazwa Roho Mtakatifu?*

5. *Neno la Mungu linasema: "...utu wa ndani badilishwa kuwa mpya siku kwa siku." (2 Wakorintho 4:16) Nini kinatokea pale tunapoomba kila siku tukirimiwe Roho Mtakatifu?*

6. *Jinsi gani unaweza kuwaongoza watu wapate maisha yaliyojawa nguvu ya Mungu?*

## Muda Wetu wa Maombi

- Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.
- Sali pamoja na mwanamaombi mwenzio…
  1. Kwamba utaishi katika uwezo wa Mungu na kwa ajili ya hekima ili kuwahimiza wengine wafanye hivyo.
  2. Kwamba sifa za mtu wa kiroho ziweze kukua ndani yako.
  3. Kwamba uweze kuelewa nini maana ya kuishi katika Roho Mtakatifu na kwamba uweze kuliwasilisha hili kwa wengine kisahihi.

Siku ya 32

SURA YA 9

# Msaada wa Kivitendo Kusaidia Kuwaongoza Wapendwa Wamwendee Yesu

Barua kwa Andrea (BA) ili kuwaongoza watu waje kwa Yesu Mfululizo wa Video ili kufundishia imani
Nawezaje kujitafutia binafsi kanisa la kweli?

"Kila nafsi ambayo Kristo ameiokoa inaitwa kutenda kazi katika jina Lake kwa ajili ya kuwaokoa waliopotea. … Kila ana wajibu wake wa kufanya … Kwa muda mrefu Mungu amengoja roho ya utumishi itamalaki kwenye kanisa zima, ili kila mmoja awe akimtendea kazi kadiri ya uwezo wake." *(Christian Service,* uk. 10.6, 11.6, 11.7) Mungu wa upendo katika hekima Yake amepanga kuwafanya waliopotea wawe wataradhia wa mbingu na hivyo kushamirisha ukuaji na furaha ya watendakazi-wenza waliojazwa Roho. Hivi hatutaki kuwaonesha wapendwa hawa njia ya kwenda mbinguni?

## Barua kwa Andrea (Ba) Ili Kuwaongoza Watu Waje kwa Yesu

Hizi zimeibuka takriban miaka 30 ya utumishi wangu katika kukidhi mahitaji ya sasa – zilizochukuliwa kutoka kwenye huduma ili zitumike katika huduma. Hivyo, nazipendekeza kwa dhati kwa ajili ya mawasiliani wetu wa utume. BA 13 *"Jitwalie Uzima"* na BA 14 *"Maisha katika Nguvu ya Mungu – Jinsi gani?"* zilikuwa zikitumika ulimwenguni kote kwa majina mengine kabla ya kuzijumuisha. Nilipata uzoefu mwingi sana kwa hizi barua. Sitaki tena kuifanya huduma bila hizi.

Barua kwa msomaji:

"Sasa, pia nawasilisha *Barua kwa Andrea* katika mfumo wa kitabulahani. Zinapokelewa vema. Hii ndiyo sababu kwa

mara nyingine tena nimeagiza nakala 30. *Barua kwa Andrea* hunisaidia mimi binafsi kuielewa Biblia vizuri zaidi. Kwa vile nimekuwa nikijifunza Biblia kwa mwaka tu, ninashukuru zaidi kwa ajili ya kila dondoo kutoka kwenye Neno la Mungu.

Hivi karibuni, nipokea simu kutoka kwa rafiki fulani ambaye punde alikuwa amepokea CD ya sauti ya *Barua kwa Andrea*. Aliniambia kwamba aliguswa sana na neno la Mungu kiasi kwamba sasa alitaka kubadili mtindo wake wa maisha. Pia anataka kulitembelea kanisa siku ya Sabato. Mume wangu naye amesikiliza CD hii na kusema: Nimevutiwa sana na barua hizi – kuanzia ya kwanza hadi ya mwisho." (R. A. # 159)

**Mada hizi zinafaa sana katika kuanzishia orodha ya watu wa kuwasiliana,** kwa mfano, tunapotaka kujenga uhusiano pamoja watu watano ili kuwasaidia kwenye safari yao kuundea ufalme wa Mungu. *Barua kwa Andrea* zinaweza kutumiwa kwa namna mabali mabali. Tunaweza kuzitumia kama masomo ya Biblia ili kuzisoma, tunaweza kuwapatia watu kama zawadi ili wajisomee wenyewe. Katika Kijerumani tunaweza kuwapatia wengine kama MP3 au CD sauti ili kusikilizwa pamoja au kusikiliza wakati wa kuendesha au wakati wa shughuli za kawaida.

**Kwa nini niliziita** *Barua kwa Andrea*? Kwa nini ziko katika mfumo wa barua pamoja na salamu "Mpendwa Andrea*"? *Nyota hii inaelezewa chini ya ukurasa wa kwanza wa kila barua: "Andrea, sawa na Andrea wa Biblia katika Yohana 1:40-42." Sababu – Andrea alimwongoza Petro nduguye akaja kwa Yesu.

Maandishi haya mafupi yanapaswa kusaidia kuwaongoza watu waje kwa Yesu. Wataalam wa utangazaji husisitiza kwamba barua hupolewa vema. Huruhusu kuwasiliana na watu kwa namna isiyo rasmi na wapokeaji hupata hisia ya kusemeshwa kwa namna binafsi.

**Kijerumani:** Mada 17 zinapatikana katika namna tatu tofauti: kama barua binafsi, kama kitabu *Mdhahimu Mungu Kupitia Barua kwa Andrea,* pamoja na vitabulahani vya MP3 na CD. Pia zinapatikana bila malipo kwa ajili ya kompyuta, tableti na simumilisi kwenye **www.schritte-zur-persönlichen-**

**erweckung. info** – *Andreasbriefe.* Natumaini kwamba mikakati ya namna hii itaanzishwa katika lugha zingine.

**Kiingereza:** Nini kilichopo? Barua, zilizotajwa kwenye kitabu hiki, tayari zimefasiriwa katika Kiingereza. Tafadhali tembelea **www.steps-to-personal-revival-info** – *Letters to Andrew.*

Barua binafsi au Seti-Anzilishi nzima nayo inaweza kupakuliwa bila malipo au ikatumwa kwa wengine.

Kiambatisho D kina maelezo mafupi kuhusu maudhui ya barua zote 17. Hii hukupatia muhtasari wa haraka.

## Jinsi gani tunapaswa kuanza na mawasiliani yetu binafsi?

**BA 4 – Kubashiri kwa Pascal: Je Mungu Yupo au la? Uwezekano ukoje?**

Ni vema kuitumia barua hii kwa ajili ya orodha ya majina ya awali. Mada hii huonesha kutoka kwenye pembe isiyo ya kawaida kwamba imani ya Ukristo inatamanika kwa kila mmoja. Miongoni mwa barua zote, hii *Barua kwa Andrea* ndiyo hutazamwa mara nyingi zaidi kwenye mtandao. Hapa tunawasilisha maelezo mafupi ya maudhui ili kukupatia taarifa:

Kijumla, ubashiri huu unaitwa "Ubashiri wa Pascal." Blaise Pascal alifikia hitimisho kwamba kila mtu mwenye busara alipaswa kuamua kwa ajili ya Yesu Kristo hata kama uwezekano wa usahihi wa mafundisho ya Ukristo ulikuwa 50:50 tu. Dkt. Viggo Olson, Daktari mashuhuri mpasuaji na mpinzani mshupavu wa imani, alikutana na kauli za Blaise Pascal. Yeye pamoja na mkewe walipambana kufa na kupona dhidi ya imani ya Kikristo. Lakini baada ya masomo ya kina alikuwa Mkristo thabiti. Lazima kila mtu afanye uamuzi. Mtu ana budi kuyajenga maisha yake ama katika dhana kwamba mafundisho ya Ukristo ni ya kweli au kwenye dhana kwamba ni ya uongo. Yeyote asiyeingia katika ubashiri huu, moja kwa moja huweka ubashiri kwenye uwezekano kwamba mafundisho ya Ukristo ni ya uongo.

Ningependekeza **BA 1** baada ya hapo:

**BA 1 – Imani ya Kikristo Yajaribiwa**

Kila kitu hujikita katika kujibu kwa uaminifu maswali matatu. Nimepitia njia hii mara mamia na nimerudia mara kadhaa na kupata uzoefu chanya pamoja na mshangao.

1. Je yupo Mungu hai, ajuaye yote na mwenye uwezo wote, awapendaye wanadamu?
2. Hivi Yesu wa Nazareti ni mkombozi kweli aliyetumwa na Mungu?
3. Je Biblia au Maandiko Matakatifu kweli yaliandikwa na watu walioongozwa na mamlaka ya Mungu au ni zalisho tu la wanadamu?

Kuna majibu ya kuridhisha kabisa kwa maswali haya ya msingi. Jihakikishie mwenyewe. Pengine hukuwa unafahamu utangulizi huu hadi sasa.

Kwa vile namba 1 inahusika na unabii 1 tu, daima niliongeza BA 8 au niliipitia baada ya hii. Mafunuo matatu mengine ya unabii yamebainishwa katika BA 8. Kwa namna hii, tunaweza kuwaongoza watu katika imani imara mwanzoni au tukahimiza imani iliyopo sasa katika Mungu, Yesu na Biblia.

**BA 8 – Mafunuo ya unabii kuhusu Yesu Kristo**
**Uwezekano wa Utimizwaji 1:1017**

Hii *Barua kwa Andrea* hususan huimarisha tumaini katika Yesu wa Nazareti kuwa Mkombozi wa kiungu, na pia ukweli kwamba Biblia imevuviwa na Mungu. Matukio mbalimbali ya unabii na utimizwaji wake kuhusu maisha ya Yesu vimelinganishwa. Vidokezo nane huonesha kwa nini utimizwaji wa matukio haya ya unabii hauwezekani kwa mtazamo wa kibinadamu.

Sasa ni fursa nzuri kumtambulisha Yesu.

**BA 2 – Upekee na Usioleza Kulinganishwa: Yesu wa Nazareti**

Mhusika mkuu zaidi katika historia ya ulimwengu– upekee usioweza kulinganishwa. Ni matokeo gani aliyokuwa nayo Yesu? Kwa nini Yesu ni wapekee kiasi hicho? Kwa nini maisha yake yaliacha mguso wa kudumu kiasi hicho, kuliko mhusika mwingine yeyote? Yesu alisema Yeye ni nani? Nini walichosema

mashuhuda, historia inasemaje? Nini ambacho wenye mashaka halisi waligundua walipochunguza ukweli wa mambo?

Sasa hakika rafiki yetu yuko tayari kujifunza kuhusu Biblia na mpango wa wokovu.

**BA 3 – Nini taanani kuu ya Biblia?**

Mpango wa Mungu wa ukombozi unabainishwa kwa namna fupi na ya ari kwenye hii *Barua kwa Andrea*. Nini ambacho mtu anapaswa kufanya ili kupokea utimilifu wa maisha na uzima wa milele? Utafiti mkubwa ulionesha kwamba 98% ya watu waliohojiwa, walikuwa na mtazamo potofu kuhusu nini ilikuwa taanani kuu ya Biblia. Barua hii huonesha wazi kwamba ukombozi ni karama ya Mungu na haiwezi na wala haihitaji kustahikimishwa. Ni shanani pale ukweli huu unapokuwa bayana kwa mtu fulani!

Mada muhimu zaidi katika mfululizo huu kwa ajili ya awamu ya mwanzo ni:

**BA 13 – Jitwalie Uzima kupitia Uhusiano Binafsi pamoja na Mungu**

Tukichukulia kwamba ungeweza kufa leo (shambulio la moyo au ajali). Je una uhakikisho sasa wa uzima wa milele pamoja na Yesu Kristo? Usibaki gizani! Mambo matano ya kweli yatakusaidia kulipata jibu. Yeyote anayechunguza uhusiano wake pamoja na Mungu, atafanya ugunduzi wa maisha yake yote!

Tafadhali kumbuka kwamba Sura ya 7 ni mwongozo kivitendo wa kutumia BA 13 *"Jitwalie Uzima."*

Kwa vile mambo mengi hutegemea huu, ni muhimu kwamba tutumie muda hasa kwa ajili hii. Mambo mawili ni muhimu sana: Kwamba tumeisoma barua yote mara nyingi na kwamba tumeomba kwa dhati na tunaendelea kuwaombea watu hao wote tutakaofahamiana nao, ambao tunataka kuwaonesha njia ya kumwendea Yesu.

Barua hii anaweza kupewa mtu huyo aisome, lakini ni bora **bayana** na yamguso na hufaa zaidi hasa kuisoma pamoja ili sisi binafsi tuweze kuambatana nao katika safari yao kwenda

kwa Kristo. Napendekeza kuitumia barua hii katika awamu ya mwanzoni ya mawasiliano na kuomba kwa ajili ya wakati mwafakawa kukabidhi kijitabu husika au wakati gani wa kuisoma Biblia pamoja, kwa sababu ni msaada mkubwa sana pale mtu anapokuwa akimtafuta Yesu. Hatulazimiki kumshurutisha ajisalimishe, badala yake tunamsaidia katika mchakato huu.

Endapo katika jaribio la kwanza, rafiki yetu hayuko tayari kwa ajili ya sala ya kujisalimisha, basi tunapaswa, baada ya muda mfupi pamoja na ombi binafsi, kuiwasilisha pamoja na Z1 *Njia ya Uzima wa Milele*, ambayo huelekea kwenye lengo lilelile kwa maneno na mawazo mengine tofauti kidogo.

*Kaeni Ndani ya Yesu,* Sura ya 2: Jisalimishe kwa Yesu, inapendekezwa kwa ajili ya msaidizi na pengine pia kwa ajili ya rafiki husika kwa ajili ya taarifa za kina juu ya mada husika.

Ni jambo la thamani hasa kujifunza jinsi ya kuishi katika nguvu ya Roho Mtakatifu. Kwa hiyo:

**BA 14 – Maisha katika Nguvu ya Mungu – Kivipi?**

"*…Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele*." (Yohana 10:10) Yesu anataka tupate uzoefu wa maisha haya mapya sasa na kuyaendeleza baada ya Ujio Wake wa Pili kama uzima wa milele katika ufalme wa Mungu. Hii *Barua kwa Andrea* inahusu jinsi tunavyoweza kupata hamasa na nguvu kwa ajili ya uhusiano wenye furaha na linganifu wa maisha pamoja na Yesu.

**BA 5 – Ushindi dhidi ya Tumbaku na Pombe**

Tunatumia uzoefu huu mkuu pale ambapo kuna utumwa kupitia uraibu na pia tunapotaka kufundisha kuomba kwa ahadi.

Dereva wa lori mwenye umri wa miaka 39 alitaka kuacha mazoea ya kuvuta sigara. Alikuwa akivuta sigara 60-70 kwa siku, na hakuna chochote alichojaribu kilikuwa kimemsaidia. Hivyo nilimuuliza: "Je ungependa kujua jinsi gani, na kwa msaada wa Mungu unaweza kuwa huru dhidi ya uvutaji sigara, haraka, na bila maradhi ya kujiondoa?" Ndiyo, hakika. Alitaka kujua. Nilimweleza kwamba sikuwa na uwezo wa kumsaidia,

ningeweza tu kumwonesha njia ya kumwendea Mungu; Yule aliye tayari kabisa kusaidia. Adolf aliikubali msaada wa Mungu naye akawekwa huru papohapo na kikamilifu. Siku 14 baadaye, aliomba kwamba Mungu amweke huru pia dhidi ya unyaji wa bia – chupa 10-14 kwa siku. Mungu alimweka huru dhidi ya uraibu huo pia, na daktari wa Adolf alishangazwa kwa maboresho ya ghafla katika afya yake. Mwaka mmoja baadaye, kwa fedha alizokuwa ameweka kaba, Adolf hata aliweza kuchukua likizo kwenda Marekani pamoja na mkewe na mabanti wake.

## Seti-Anzilishi – Barua kwa Andrea Ili Kuwaongoza Watu Waje kwa Yesu

Tumeongeza *Seti-Anzilishi Barua kwa Andrea* kwenye kitabu hiki. Kwa nini neno *Seti-Anzilishi?* Kutoka kwenye *Barua 17 kwa Andrea* zile zinazoweza kutumika ili kuanzishia uhusiano zimechaguliwa. Barua hizi ni daraja kutoka kwenye nadharia hadi vitendo. Tafadhali kumbuka manufaa 12 ya kijitabu husika, ambayo yametajwa mwanzoni mwa sura ya 7. Bahasha ina nakala moja ya barua zote zinazohitajika Nr. 1, 2, 3, 4, 5, 8, 13, 14 na Z 1. Mwonekano ulisanifiwa na maudhui yanayovutia vitakupendeza. Utafurahi kumgawia mwingine. Unahitaji seti moja kwa ajili ya kila mtu unayetaka kumwongoza aje kwa Yesu. Bahasha husika imekusudiwa kwa ajili ya maelezo: lini nilitoa namba fulani na vidokezo vingine. Anuani ya uagizaji kwa ajili ya Seti-Anzilishi zingine imetajwa katika ukurasa wa 202. – Barua hizi zinaweza pia kupakuliwa bila malipo kwenye www.steps-to-personal-revival.info:*Letters to Andrew*, au kutumwa kwa mtu fulani. Mawasilisho yote 17 ya *Barua kwa Andrea* yako katika Kiingereza na yatapatikana mwishoni mwa mwaka 2020. *"Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo."* (1 Wakorintho 15:57)

### Masomo ya Uanafunzi

Endapo Yesu akikubaliwa (BA13) ni muhimu kuimarisha uhusiano huu. Kwa ajili ya kusudi hili, unaweza kutumia kitabu cha pekee *Steps kwa Kristo* (hupatikana kwa majina kadhaa tofauti) cha E.G. White. Kina sehemu kuu mbili: Jinsi gani naweza kuja

kwa Kristo? Jinsi gani naweza kukaa ndani ya Kristo? Hupatikana katika lugha yoyote (kimetafsiriwa katika lugha 150).

Ikiwa maisha katika Roho Mtakatifu yameanza, kisha ni muhimu pia kuimarisha uhusiano huu. Hili hufanywa vema kwa kujifunza kijizuu (brosha) cha *Hatua za Uamsho Binafsi*. (angalia Ofa za Kitabu, uk. 203)

Baada ya masomo haya ya uanafunzi, unaweza kuchagua vipengele mwafaka kutoka kwenye mawasilisho yafuatayo ya *Barua kwa Andrea*. Ni vema pia kusonga mbele katika hatua ya kawaida ya mfululizo wa kujifunza Biblia au kutazama mfululizo wa injili kwenye video ambamo kweli muhimu za Biblia zinawasilishwa. (maelezo zaidi katika Kiambatisho F)

## Nini maudhui ya mawasilisho mengine tisa ya Barua kwa Andrea?

Mawasilisho mengine ya *Barua kwa Andrea* yaliyosalia yanaweza sasa kutumiwa kwa busara yako. Tafadhali tazama Kiambatisho D kwenye uk. 193 mwishoni mwa kitabu hiki. Kipengele hiki kina maelezo mafupi ya maudhui ya kila barua, hivyo unaweza kujifahamisha haraka.

**BA 6 – Unajuaje yaliyopo kwenye mustakabali ujao?** (Danieli 2)

**BA 7 – Uzuiaji au uponyaji?** (Utangulizi wa Ujumbe wa Afya)

**BA 9 – Mafunuo ya unabii kuhusu miji minne** (Huimarisha imani katika Biblia)

**BA 10 – Yesu na Sabato** (Hii ni somo langu la kwanza la Biblia kuhusu Sabato. Siyo la makabiliano, hupunguza nishaha na kujenga mguso wa awali wa kuidhamani Sabato.)

**BA 11 – Nini alichosema Yesu kuhusu Yerusalemu, Ujio Wake wa Pili na mwisho wa ulimwengu?** (Nini tuwezacho kujifunza kutokana na “hukumu ndogo” iliyotokea mnamo mwaka 70 B.K.?)

**BA 12 – Ishara ya Yesu Kurejea** (Je tunakabili hatua kuu ya mageuzi au – … ule mwisho?)

**BA 15 – Manufaa kutokana na kusoma Biblia – Kivipi?** (Hebu tuangalie mapito ambayo wengi wameyafurahia wakati wakiisoma Biblia.)

**BA 16 – Jinsi gani naweza kudhahimu upendo na msamaha wa Mungu?** (Mungu hataki nibebe mzigo wowote wa zamani na nihofie wakati ujao, bali niishi katika urafiki pamoja Naye leo na kuimarishwa kwa nguvu Yake.)

**BA 17 – Je una kitu fulani dhidi ya mtu fulani?** (Jinsi gani naweza kusamehe na kusahau? Msamaha huwaweka huru watu wa pande zote mbili)

Hebu nipendekeze kwamba ujifahamishe vema katika *Barua kwa Andrea* kwenye maswali husika ili uweze kuyawasilisha kwa furaha na usadikisho.

**Darasa la Biblia**

Endapo kanisa lako lina **darasa la Biblia kwa watu wenye shauku au waliobatizwa hivi karibuni,** kisha masomo ya Biblia yanaweza kufanyikia hapa au huweza kuwa nyongeza ya usomaji wa Biblia kila juma. Hujikita kwenye maswali juu ya uhusiano binafsi na Mungu na uanafunzi, pamoja na kweli za msingi. Darasa hili, ambalo huitwa darasa la Biblia la mchungaji katika nchi nyingi, ni la manufaa makubwa. Niliendesha darasa hilo katika makanisa yangu yote. Ndipo tunapaswa kuzungumzia ubatizo baada ya darasa hili na kumsaidia rafiki yetu ajisalimishe kwa Yesu kupitia ubatizo na kujiunga na kanisa Lake kama mshiriki hai. (Maelezo zaidi katika sura ya 10)

## Video kwa Ajili ya Kufundishia Imani

Leo nyenzo nzuri hasa kwa ajili ya kufundishia na kukuzia imani katika Mungu na neno Lake, kama hakuna mwalimu aliyepo. Ili kufundisha injili, tafadhali tafuta mifululizo ya mikutano ya injili yenye kweli za Biblia zote muhimu. Mfululizo

wenye mawasilisho 20-30 ni bora. Katika Kiambatisho F utapata maelezo mafupi ya tovuti 15 na kila unachoweza kupata hapo. Kurasa hizi zina thamani kwa watoto, vijana, watafuta-ukweli na waumini wa muda mrefu. Kingine kilichotajwa pia ni tovuti kutoka katika Ujumuishwaji Timilifu wa Mshiriki wa Konferensi Kuu. Hii ina vidokezo vya Uinjilisti, Usambazaji wa Machapisho na mifululizo mbalimbali juu ya Afya na Siha, Kisukari, Utengamano kutoka kwenye Mfadhaiko na Shule ya Mapishi. Katika Kiambatisho F utapata hazina ya tovuti zenye manufaa.

Kwenye www.steps-to-personal-revival.info unaweza kupata:

– Video 7 za mahubiri ya *Hatua za Uamsho Binafsi* za Helmut Haubeil
– Kitabulahani *Hatua za Uamsho Binafsi,* Mzungumzaji: Mike Fenton
– Video 3 za mahubiri ya *Jinsi ya kubatizwa kwa Roho Mtakatifu* za Dwight Nelson

**Kujipatia Marafiki kwa ajili ya Mungu: Furaha ya Kuwasilisha Utume Wake**

(Mwongozo wa Kujifunza Biblia wa Shule Sabato kwa Watu Wazima – Sanifi Kuu Robo ya 3, 2020)

Mwandishi mkuu, Mark Finley, anasema katika utangulizi:

"Mmojawapo wa marafiki zao aliwasilisha wazo hili, 'Kimsingi utume ni kazi ya Mungu. Anatumia rasilimali zote za mbinguni ili kuiokoa sayari yetu. Kazi yetu ni kushirikiana naye kwa furaha katika kazi Yake ya kuwaokoa watu waliopotea.' Ilionekana kana kwamba mzigo wa mbinguni uliondolewa mabegani pangu." Hilo ndilo kusudi la kitabu hiki. Ningependekeza: Tunza Mwongozo wa Kujifunza Biblia wa Shule Sabato wa robo ya 3 ili uweze kuangalia maelezo mengine ya kina kadiri yatakapohitajika. Uhifadhi pamoja na kitabu hiki.

## Jinsi Gani Naweza Kulitafuta Mwenyewe Kanisa La Kweli?



Utafutaji wa kanisa la kweli ni somo makini sana katika Biblia kwa ajili ya wataradhia wa ufalme na pia kwa ajili ya washiriki wa kanisa.

Je hivi bado kungali na kanisa la kweli? Kwa vile Yesu alilizungumzia kama kanisa Lake, ningechagua kuliita kanisa la Yesu Kristo. *"Wala milango ya kuzimu haitalishinda* [kanisa Langu]*."* (Mathayo 16:18) Maneno ya Yesu hutuonesha kwamba kanisa Lake lingalipo leo. Kwa hiyo, tunaweza kulitafuta na kulipata.

Uzoefu fulani unatupatia kielelezo: Dada watatu, ambao kila mmoja alikuwa muumini wa kanisa tofauti, walimuuliza mchungaji: "Je kanisa lipi ni sahihi?" Akawauliza maswali matatu, ambayo waliyajibu kwa uhakika. Baada ya hapo aliwaambia jinsi gani wangeweza kusuluhisha tatizo hilo wao wenyewe kwa uchunguzi mfupi wa Biblia. Walikamilisha uchunguzi huu wa Biblia kisha wakajiunga na kanisa moja.

**Kwa nini mtu anapaswa kugundua hili yeye mwenyewe?** Je huwezi kumuuliza tu mtu mweye utaalamu? Au kuyauliza mkanisa mojamoja ama vikundi? Hilo ni jambo la asili. Lakini karibu kila mojawapo hudai kuwa kanisa la kweli, japo kijumla yana mafundisho tofauti kabisa. Hivyo, kwa namna hii hatutaweza kufanikisha lolote. Ingelikuwa vema kuufuata mfano wa wakazi wa (Uyunani). Biblia hutaja mwenendo wao kuwa mwelekevu:

*"Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo."* (Matendo 17:11)

Huu ni ushauri mzuri! Kipindi hicho zamani watu huko Berea walisikiliza kwa shauku mahubiri ya Paulo. Lakini waliichunguza Biblia kila siku kwa ajili yao wenyewe ili kuona kama yalikuwa ni kweli. Hii ndiyo sababu napendekeza pia kufanya jambo husika tunapokabiliwa na swali kuhusu kanisa sahihi la Yesu. Uchunguzi mfupi wa Biblia ni njia nzuri ya kutumia.

Lakini kwanza, hebu tuyaangalie maswali matatu aliyoyauliza mchungaji. Maswali haya ni viegezo-awali muhimu kwa ajili ya uchunguzi mafanikio kwa swali hili.

**1. Je unaamini kwamba Yesu Kristo aliifundisha na kutenda maishani Mwake?**

Yesu alisema:

*"Mimi ndimi Njia, na Kweli, na Uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya Mimi."* (Yohana 14:6) *"Na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi…"* (Mathayo 28:20)

Petro alisema:

*Yeye hakutenda dhambi yoyote; alikufa kwa ajili ya dhambi zetu.* (1 Petro 2:22-24)

*"…Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuate nyayo Zake."* (1 Petro 2:21)

Tunapaswa na tunataka kuufuata mfano Wake katika mambo yote. Ndiyo sababu Yohana alisema:

*"Yeye asemaye ya kuwa anakaa ndani Yake, imempasa kuenenda mwenyewe vile vile kama Yeye alivyoenenda."* (1 Yohana 2:6)

Naamini kwamba Yesu aliifundisha kweli na kuidhihirisha kweli ya kiungu na kwamba maisha Yake yote yalikuwa mfano kwa ajili yetu. Kila Mkristo wa kweli analiamini hili. Hili ni sharti la kwanza kwa ajili ya kusudi letu. Je unaamini hii vilevile?

**2. Je unaamini kwamba kanisa la kweli la Yesu linapaswa kukubaliana na mafundisho na mfano wa Yesu?**

Je kanisa la Yesu leo – baada ya miaka 2,000 – bado linapaswa kuafikiana na Yesu? Hivi haikuwepo hatua yoyote ya maendeleo? Nini ambacho Yesu Mwenyewe alisema?

Yesu alisema:

*"…Maandiko hayawezi kutanguka."* (Yohana 10:35)

Hapa, Yesu alikuwa akirejelea Agano la Kale. Kiasili, hii inahusika na Biblia nzima ikiwa ni pamoja na Agano Jipya. Kwa mujibu wa Yesu, Maandiko hayawezi "kutanguka." Unapotangua kitu fulani, basi unapata vipande vingi. Hapa Yesu anawasilisha dhana kwamba hatuwezi kwa hiari kuikubali sehemu moja na kuikataa sehemu nyingine. Yohana alisema katika kufikia mwafaka na Yesu: *"Kila apitaye cheo, wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana*

*pia."* (2 Yohana 9) Huu ni ukanusho wa wazi wa mchakato wowote endelevu wa mabadiliko ya mafundisho ya Biblia. Kile ambacho Mungu amedhihirisha kupitia Mwanawe (Waebrania 1:1) hakiwezi na wala hakipaswi kufanyiwa maboresho na wanadamu.

Mtume Paulo alisema: *"Lakini ijapokuwa sisi* [mitume] *au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe. Kama tulivyotangulia kusema, na sasa, nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na alaaniwe."* (Wagalatia 1:8-9)

Hata mitume au malaika hawana haki ya kuibadili injili ya Yesu Kristo. Kwa hiyo, hakuna mwingineyo anayeweza kufanya hivyo pia. Hivyo, tumethibitisha: Kanisa la Yesu leo linapaswa kuafikiana na Yesu Kristo na neno Lake.

Je nawe pia unaliamini hili?

**3. Je uko tayari kujiunga na kanisa la Yesu sasa utakapolipata?**

Kwa nini utayari huu ni muhimu sasa kabla uchunguzi haujaanza?

Yesu alisema:

*"Mtu akipenda kuyatenda mapenzi Yake, atajua habari ya yale mafunzo, kwamba yatoka kwa Mungu…"* (Yohana 7:17)

Yesu alikuwa akisema: Yeyote atakaye kuyafanya mapenzi ya Mungu, atayatambua pia. Mungu atawasaidia wale wenye shauku ya dhati ya kujua na kutenda mapenzi Yake, kuujua ukweli na hivyo pia kulijua kanisa la Yesu. Ahadi ya kiungu inasema: "[Mungu] *Huwawekea wanyofu akiba ya mafanikio kamili…"* (Mithali 2:7 NIV) – Mungu ameahidi msaada wa Roho Mtakatifu kwa wale ambao ni watiifu Kwake (Matendo 5:32). Ameahidi kutuongoza katika kweli yote (Yohana 14:26 na Yohana 16:13). Hakika kabisa, hii hujumuisha ukweli kuhusu kanisa Lake. Kitabu adhimu kuhusu maisha ya Yesu kinasema: "Wale wanaojisalimisha hivyo kwa Mungu, wakiwa na shauku aminifu ya kuyajua na kuyafanya mapenzi Yake, ukweli hudhihirishwa kwao kama nguvu ya Mungu kwa ajili ya wokovu

wao." (E.G. White, *The Desire of Ages,* uk. 455.3) Je uko tayari kujiunga na kanisa la Yesu utakapokuwa umelipata?

## Sasa, jinsi gani naweza kugundua mwenyewe lipi kanisa la kweli la Yesu?

Ipi njia rahisi. Chunguza injili ya Mathayo. Inayo takriban kurasa 40. Haina mafundisho yote ya Yesu, ila inajumuisha mengi husika. Unaweza kupenda kupigia mstari/kudhulisha mafungu mbalimbali kuhusu mafundisho Yake, mfano Wake na kile alichosema kuhusu Yeye. Nilifanya uchunguzi huo kama ifuatavyo:

Nilitumia daftari lenye pambizo kwenye pande mbili za ukurasa na kuligawa kama ifuatavyo:

Niliandika sura na fungu kwenye pambizo ya kushoto.

Niliandika katika nusu ya pili ya kushoto ya safu kuu sentensi au sehemu ya sentensi kutoka kwenye Biblia, iliyokuwa na fundisho au mwenendo mfano wa Kristo.

Niliandika katika nusu ya pili ya kulia ya safu kuu ni ufundisho gani iliyokuwa kwenye sentensi hii.

Kwenye pambizo ya kulia, nilitengeneza safu kwa kila moja ya makanisa hayo niliyotaka kuyachunguza (mfano safu ya Kanisa Katoliki, Kanisa la Kiinjili, Kanisa la Waadventista, na Kanisa la Kibaptisti).

Niliweka alama ya kumjulisha kwenye safu ya kila kanisa lilivyoona fundisho hilo husika.

Mwishowe, kanisa lililokuwa na alama ya kumjulisha kwa ajili ya kila fundisho, liliafikiana na mafundisho ya Yesu. Hili ndilo kanisa la Yesu ninalotaka kujiunga nalo.

| Ibara ya Bilia | Ibara ya Bbilia | Fundisho | Makanisa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Katoliki | Kiinjili | Waadiventista | Wabaptist |
| Mathayo 1:1 | Kitabu cha ukoo wa Yesu Kristo. | Hii ni historia na wala siyo visabuni au hekaya. | + | + | + | + |
| Mathayo 1:18 | Mariamu alionekana ana mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu. | Muujiza wa kuzaliwa kupitia bikra | + | | + | + |

Mara nyingi nimetumia sura au kipande cha sura katika Mathayo kwenye masomo ya Biblia au kama somo la nyongeza nusu saa kabla ya somo la Biblia. Shauku katika somo hili daima ilikuwa kubwa sana. Wakati fulani mtu mmoja aliwahi kuniambia: “Hadi nafika sura ya nne, niligundua siko kwenye kanisa sahihi.” Utatambua kwamba utagundua sehemu tu ya ukweli mara ya kwanza ufanyapo hili – kama itakavyokuwa pia kwa marafiki zako. Lakini hilo halijalishi. Kila wakati nilipofanya uchunguzi huu niligundua kweli zingine zaidi na zaidi. Uchunguzi huu ni wenye msaada mkubwa kwa ajili ya watafuta-ukweli katika kufanya uamuzi kwa ajili ya kanisa la Yesu.

Hebu Mungu wetu wa pekee ajabu akubariki katika huduma yako.

## Mawazo binafsi na mwongozo wa mjadala

1. *Ni nyenzo zipi halimali zilizopo kwa ajili ya kusaidia kuwaleta watu kwa Yesu?*

   ______________________________

2. *Jinsi gani unaweza kuendelea na muwasiliani binafsi ili kuamsha shauku yake kwa Yesu?*

   ______________________________

3. *Ni maswali gani uwezayo kutumia ili kuwafanya watu wafikirie kuhusu kama wana uhusiano na Kristo au wanataka kuimarisha uhusiano wao pamoja Naye?*

   ______________________________

4. *Ni maswali gani uwezayo kuwauliza watu wanaotafuta kanisa la kweli?*

   ______________________________

## Muda Wetu wa Maombi

- Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.
- Sali pamoja na mwanamaombi mwenzio…
  1. Kwa ajili ya hekima kujua nini cha kusema au kumpatia watu wengine ili mioyo yao iwe tayari kupokea ujumbe wa Mungu.
  2. Kwa ajili ya maandalizi sahihi ya kazi ya kimishenari.
  3. Kwa ajili ya upendo kwa wengine, ambao ni muhimu ili kuifikia mioyo yao.
  4. Kwa ajili ya uzoefu pamoja na Mungu katika kutenda kazi kwa ajili ya wengine.

Siku ya 34

SURA YA 10

# Mwanzo Mpya Kiroho– Kimishenari Katika Hatua Tatu

Jinsi gani watu binafsi na makundi, makanisa na konferensi mbalimbali huweza kupata uzoefu huui?

## "Roho Wangu atalitimiza hilo!"

*"Kile unachopanga wala hakitafanikiwa kwa nguvu za jeshi wala kwa uwezo wa kibinadamu; badala yake, Roho Wangu atalikamilisha hilo! Mimi, Bwana Mungu Mwenyezi, naahidi hili."* (Zekaria 4:6 efasiriwa kutoka kwenye sanifi ya Kijerumani "Hoffnung fuer Alle")

Ninashukuru sana kwamba Bwana wetu ametudhihirishia wazo hili kupitia uzoefu mwingi mndogo wa kivitendo. Hakuna aliyepanga chochote katika uelekeo huu.

Tutaanza na uzoefu kielelezo.

### Uzoefu kutoka kanisa moja katika Decatur, Alabama, Marekani:

"Mnamo mwezi Aprili mwaka 2019 Mungu aliliongoza kanisa lake lijikite kwenye maombi na kujisalimisha kwa Yesu mara tu kabla mfululizo wa mkutano wa injili. Hili lilifanyika kwa lengo la kupata mafanikio makubwa zaidi katika juhudi zao za kimishenari.

…Mwelekeo wa kanisa letu ulitasilishwa baada ya Mchungaji Robert Meneses kuitembelea familia yake huko Ureno mwanzoni mwa mwaka huo. Wakati akiwa huko, shangazi yake alimpatia kijitabu cha Kiingereza na Kireno kiitwacho *Hatua za Uamsho Binafsi* cha Helmut Haubeil. Wakati huohuo, mkewe, Elida, ambaye ni mratibu wa maombi kanisani, alisoma

katika jarida la *Ministry* (jarida la kimataifa la kichungaji) ushuhuda wa mchungaji kuhusu uzoefu kwenye kitabu hiki. Baada ya kujisomea kitabu hiki, alivutiwa kwamba kanisa lingepaswa kukisoma vilevile. Hivyo aliondoka na kitabu hicho kwenda kwenye kikundi cha maombi Sabato asubuhi, lakini kinachoshangaza sana mshiriki mwingine wa kanisa alisimulia kwamba rafiki yake mmoja alikuwa amempatia mrejesho chanya wa kitabu husika.

Wakati wa maandalizi yao kwa ajili ya mikutano ya injili, kanisa lilifanya shughuli kadhaa mpya. Walianza kuomba pamoja kila Sabato asubuhi kanisani kwa dakika 30. Walipashana taarifa kwenye buletini ya kanisa ili kuhamasisha maombi, uamsho na kazi ya Roho Mtakatifu. Waliendesha semina kwa video inayohusu Roho Mtakatifu kanisani Sabato mbili mfululizo nyakati za jioni. Baada ya semina, nakala za kitabu *Hatua za Uamsho Binafsi* ziligawanywa kwa washiriki na wakaomba kuvisoma katika kipindi kinachofuata cha majuma sita.

Baada ya hilo, walishiriki katika mkakati wa 'Siku Kumi za Maombi' kutoka Konferensi Kuu. Washiriki wa kanisa walitumia muda huu kukutana kanisani na kuombea uamsho na Roho Mtakatifu. Katika Sabato iliyofuata, waliendesha huduma kuu maalumu ya 'sifa na maombi.'

Brian Danese, kiongozi wa uanzishaji makanisa katika Konferensi ya Majimbo ya Guba, akaja na kuendesha semina ya wikendi. Baadaye, kanisa likaanza kujifunza kwenye kitabu cha *Kitabu ch Siku 40: Maombi na Ibada ili Kujiandaa kwa Ujio wa Pili* katika vikundi vya watu wawiliwawili. Kwenye Sabato asubuhi, klipu fupi za video kutoka kwa Dennis Smith, mwandishi wa vitabu vya *Siku 40*, zilioneshwa wakati wa matangazo.

Walifuata mapendekezo kwenye kitabu hiki kwamba kila mtu angepaswa kuwaombea watu watano ambao hawajafikiwa. Kisha wakakutana na wapendwa hawa au washiriki wa zamani wa kanisa. Idadi kubwa ya ubatizo ilitoka kwenye kundi hili ambalo washiriki wa kanisa walikuwa wamelichagua binafsi kuliombea na kulihudumia.

Nyongeza: 'Hatujui hasa ni washiriki wa kanisa waliohudhuria. Lakini hebu fikiria – pale ambapo washiriki 10 wa kanisa kila mmoja anawaombea na kudumisha mawasiliano na watu watano, hiyo ingekuwa watu 50; washiriki 50 wa kanisa wao wangekuwa na watu 250. Hii huunda mzunguko wa thamani wa watu wenye shauku kwa ajili ya mikutano ya injili au vikundi vya kuhudumia.'

Wakati mfululizo wa masomo ya mkutano ya injili ulipoanza mwezi Aprili, kanisa lilipitia uzoefu wa uamsho na uhusiano wa kina zaidi pamoja na Yesu. Wakati wa mihadhara kutoka kwa Robert Meneses, washiriki wa kanisa waliweza kuimarisha mahusiano yao na wageni, na Roho Mtakatifu akatenda kazi mioyoni mwao. Baada ya mfululizo wa mihadhara, wapendwa kumi walimkabidhi Yesu maisha yao kupitia ubatizo na baadaye watu wengine kumi. Kanisa huchukulia matokeo haya kama ushuhuda wa nguvu ya moambi."

(Imechukuliwa kutoka kwenye ripoti ya Elida Meneses, *Southern Tidings,* Sept. 2019, uk. 20 – Unioni Konferensi ya Kusini, Marekani EE EPM171119 #146)

Mbinu hii ya umishenari wa kiroho hutenda kazi ya kuongoa roho kwa neema ya Mungu ulimwenguni kote, pia katika nchi zilizowazi, kwa sababu nguvu ya Roho Mtakatifu haina mipaka. Katika nchi zenye utayari zaidi, ni msaada mkubwa kumwimarisha mtu mpya na pia kwa ajili ya mwanzo mpya wenye furaha kwa washiriki wa kanisa wasiohai. Huko Burundi kwa pamoja washiriki wa kanisa 320 walirejea kwa sababu ya ushawishi wa kitabu *Hatua za Uamsho Binafsi*. Walibatizwa tena na kuingia kanisani mnamo Mwezi Machi 2017.

## Hatua Tatu za Mwanzo Mpya

Kanisa hili lilichukua hatua tatu zifuatazo:

**Hatua ya 1: Mwanzo Mpya – Uhamasishajii wa maisha ya kiroho**

Mwanzo mpya wa kiroho kupitia usomaji wa kina wa kitabu *Hatua za Uamsho Binafsi.*

**Hatua ya 2: Uhamasishaji wa Mahusiano – Ndani na Nje**

Wajifunza kwa kutumia kitabu *Siku 40: Maombi na Ibada ili Kujiandaa kwa Ujio wa Pili cha* Dennis Smith ili kuimarisha maisha yao ya kiroho. Walianzisha huduma ya maombezi na kuwafikia watu watano ambao hawajafikiwa.

**Hatua ya 3: Kuwasilisha Injili**

Kwa muktadha huu, waliendesha mikutano ya hadhara. Lakini hili linaweza pia kufanyika katika masomo binafsi ya Biblia au kwenye vikundi vidongo nyumbani binafsi au kwa video.

**Kutazama kwa kina zaidi kuhusu hatua hizi tatu**

Sasa, tanataka kuangalia kwa kina zaidi hatua hizi tatu ili tuweze kuzitekeleza kivitendo.

## Hatua ya 1: Mwanzo Mpya – Ushamirishaji wa Maisha ya Kiroho

Kuza ukuaji wa maisha yako ya kiroho – rejea kwenye upendo wako wa kwanza – kwa msaada wa kitabu *Hatua za Uamsho Binafsi.* (Kitabu hiki kinapatikana katika lugha zaidi ya 40.) Zaidi ya shuhuda 500 huonesha kwamba:

- ▶ Roho Mtakatifu ni karama kuu zaidi ambayo Yesu angeweza kutukirimia.
- ▶ Kitabu hiki hufumbua macho yetu na kutusaidia kufanya tathmini binafsi na sahihi ya hali yetu kiroho.
- ▶ Hutusaidia kuelewa vema zaidi hatua mbili za msingi ambazo huyafanya maisha yetu ya kiroho yavutie na kutupatia uhakikisho wa wokovu.
- ▶ Tunapata uzoefu kwamba kuomba kwa ahadi huyapatia maombi yetu ubora mpya kabisa. Tunaomba kwa furaha kuu zaidi, uhakika, na kina. Kwa kuomba wakitumia ahadi, wengi wamepokea uhakikisho wa kukirimiwa Roho Mtakatifu.
- ▶ Katika furaha yao kuu, wamekuwa mashuhuda na wamegawa vitabu, na matokeo yake furaha yao imeongezeka hata zaidi.

Kuna uzoefu wa zaidi mara 160 katika Kiingereza na Kijerumani kwenye: www.steps-to-personal.revival.info

Toleo jipya kabisa la kitabu hiki kimegawanywa katika sehemu 14. Unaweza ama kusoma kitabu hiki kwa kipindi cha majuma sita au ukakisoma mara tatu katika wakati huu ili kupata manufaa makubwa zaidi. Uzoefu mkuu zaidi kwa kawaida hupatikana tu baada ya usomaji wa mara kadha na kutekeleza kile kinachosomwa. Utafiti wa elimu umeonesha kwamba ni lazima kusoma au kusikiliza mada muhimu mara sita hadi 10 ndipo mtu huyo aielewe vema. Jaribu hilo angalau mara moja. Karibu uzoefu wote mnzuri hutoka kwa watu ambao wameshughulika na mada husika mara kadhaa na kwa moyo wao wote. Watu wenye haraka hawapati manufaa yoyote.

Ni fursa nzuri kujifunza kwa kutumia usomaji wa *Siku 10 za Maombi* 2021 kabla au baada ya kujifunza *Hatua za Uamsho Binafsi*.

Kwenye matangazo kuhusu *Siku 10 za Maombi* (ANN: Okt. 24, 2020) Konferensi Kuu (GC) iliandika: "Mwaka ujao programu ya Siku 10 za Maombi itaendeshwa chini ya dhima 'KUTAFUTA UAMSHO' na lengo litakuwa katika umuhimu wa kupata uzoefu wa uamsho binafsi na furaha ya kujisalimisha kikamilifu kwa Mungu katika kila kipengele cha maisha... – Masomo ya kila siku yaliandikwa na Mchungaji Helmut Haubeil... "

Masomo haya, kwa namna fulani, ni sanifi fupi ya mfululizo wa kijitabu kiitwacho *Hatua za Uamsho Binafsi.*

Nakusudia kuiomba GC ruhusa ya kuongeza siku 1o za maombi 2021 kwenye tovuti yetu www.steps-to-personal-revival.info: 10 Days of Prayer. Hapo masomo yanaweza kupakuliwa au kusambazwa wakati wowote. Mtu fulani anataka kuyatumia. Pia tutataja kitabu husika na sura kila siku, ili watu wafaidi kutokana na usomaji wa ziada. (Vitabu hivi hupatikana katika lugha nyingi kwenye tovuti.) Uimarishaji huu wa kiroho utapelekea kupata nguvu na furaha.

Siku ya 35

## Hatua ya 2: Uhamasishaji wa Mahusiano – Ndani na Nje

**Kwa Nje**

Mwongozo bora na tumainifu kwa ajili ya Siku 40 za maombi ni *Kitabu cha Siku 40, juzuu ya 1: Maombi na Ibada ili Kujiandaa*

*kwa Ujio wa Pili,* cha Dennis Smith (R & H). Kitabu hiki kimegawanyika katika sehemu tano zenye masomo maneno kila moja:

- Ubatizo wa Roho Mtakatifu;
- Ubatizo wa Roho na maombi;
- *Ubatizo wa Roho na uinjilisti;*
- Ubatizo wa Roho na kudumu ndani ya Kristo;
- Ubatizo wa Roho na ushirika.

Dondoo zifuatazo zimechukuliwa kutoka *kitabu cha Siku 40, Na. 1,* uk. 5-6, utangulizi – umechukuliwa ili:

Usomaji wa Siku 40 na ibada ya maombi imekusudiwa kuliandaa kanisa la Mungu kwa ajili ya ujio wa pili wa Kristo, pamoja na kuwafikia wengine katika maandalizi kwa ajili ya tukio hilo tukufu.

Maandalizi haya huanza na washiriki wa kanisa walioradhi kujiadhimu kwa ajili ya Siku 40 za maombi na usomaji wa kiibada ili kujenga uhusiano binafsi wa karibu na Yesu Kristo, na kuwafikia watu watano ambao Bwana amewaweka moyoni mwao ili kuwaombea kila siku.

Yesu alisema, *"Wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lolote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba Yangu aliye mbinguni"* (Mathayo 18:19). Kuna nguvu kuu katika maombi ya pamoja, na kuna faraja na nguvu ya kiroho katika ushirika wa Kikristo. Inapendekezwa kwamba umtafute mwanamaombi mwenzako kwa ajili ya ushirika na kuomba pamoja naye. Shirikishaneni kile ambacho mmesoma siku hiyo kisha mwombe pamoja, ama kwenye simu au ana kwa ana, kila siku wakati wa Siku 40 za maombi na kujifunza.

Ili kupata manufaa makubwa zaidi, napendekeza kwamba mwatafute watu kadhaa ili wajiunge nanyi katika kutumia kitabu cha maombi. Ingekulikuwa vema kukutana kila juma kama kundi ili kushirikishana na kuomba pamoja. Mchague mmoja katika kikundi hicho awe mshirika mwanamaombi mwenzako. wanandoa wamerejesha ripoti ya baraka maalumu pale walipojifunza pamoja. Wanandoa fulani waliandika: "Usomaji na kuomba pamoja vimetuongoza katika ukaribu na umoja wa kina kiasi ambacho hatukuwakupata uzoefu kamwe hapo

kabla." Kila mshiriki kwenye kikundi atafanya hivyo ili aweze kupokea baraka kuu zaidi wakati wa siku 40 … Wale walio kwenye orodha yako ya maombi wanaweza kuwa wanafamilia yako, marafiki au wafanyakazi wenzio. **Ukurasa wa orodha ya maombi kila siku umejumuishwa kwa kusudi hili katika Kiambatisho E.**

**Kwa Nje**

**Maombezi maalumu kwa watu watano**

Wakati wa siku 40 utawaombea watu hawa watano kila siku na kuwafikia. Kuna mapendekezo ya jinsi ambavyo unaweza kumfikia mtu fulani na jinsi ya kumfahamisha kwamba utakuwa ukimwombea kwa siku 40 na wakati huohuo umwombe kile ambacho angependa ukiombee kwa niaba yake. Unaweza kupata maelezo husika katika Kiambatisho A na B mwishoni mwa kitabu hiki. Kwa nini maombi?

Maombi ni nguvu madhubuti zaidi duniani. Ni lazima kwa ajili ya ukuaji wa mtu kiroho na pia ni njia fanisi zaidi ya kuwafikia wengine kwa ajili ya Kristo. Kuhusu maombi na ukuaji wa Mkristo kiroho, Ellen White aliandika:

"Maombi ni pumzi ya nafsi. Ni siri ya nguvu ya kiroho. Hakuna njia nyingine ya kupata neema inayoweza kuwa mbadala halafu afya ya kiroho ikahifadhiwa. Maombi huuleta moyo katika muunganiko halahali na Chemchemi ya uzima na kuimarisha kano na mshipa wa uzoefu wa kiroho. Puuza zoezi la maombi, au jihusishe kwenye maombi mara mojamoja, hapa na pale, kadiri ifaavyo, nawe utapoteza mshikamano wako kwa Mungu. Nadhiri ya kiroho upoteza uhai wake, uzoefu wa kiroho hukosa afya na nguvu." (*Gospel Workers*, uk. 254)

Bi. White pia alitambua ulazima wa maombi katika kuwaongoza wengine kwa Kristo: "Kwa maombi mengi, lazima ujitaabishe kwa ajili ya roho, maana hii ndiyo njia pekee ambayo kwayo unaweza kuifikia mioyo." (*Evangelism,* uk. 341) "Bwana atasikia maombi yetu kwa ajili uongofu wa roho." (*Messages to Young People,* uk. 315)

Kadiri unavyozingatia kwa maombi njia zilizopendekezwaa (angalia Kiambatisho B) ili kuwafikia wale unaowaombea,

siyo tu kwamba utakuwa unawaombea, lakini pia utakuwa ukijibidiisha ili kuwaleta karibu zaidi na Kristo pamoja na kanisa Lake. Mungu atabariki juhudi zako unapowaombea, na kujishughulisha kwa ajili ya wale walio katika orodha yako ya maombi. Siyo tu kwamba atakutumia ili kuwaongoa wengine waje kwa Kristo; nawe atakuta uje karibu Naye. Ellen White alielewa baraka hii maradufu alipoandika:

"Kadiri unavyofanya kazi ili kujibu maombi yako mwenyewe, utagundua kwamba Mungu atajidhihirisha kwako. … Anza sasa na kupanda juu zaidi na hata juu zaidi. Yathamini mambo ya mbinguni kuliko mivuto na ushawishi wa duniani. … Jifunze jinsi ya kuomba; jifunze jinsi ya kuwasilisha ushuhuda bayana na farisi, Naye Mungu atatukuzwa ndani yako." (*The Upward Look*, uk. 256)

"Maombi yao ya ustahimilivu yataleta roho kwenye msalaba. Katika kushirikiana na juhudi zao na kujitoa nafsi, Yesu ataigusa mioyo yao, akitenda miujiza katika uongoaji wa roho." (*Testimonies for the Church*, *vol. 7,* uk. 27)

**Kwa nini siku 40?**

- Musa alitumia siku 40 katika Mlima Sinai pamoja na Mungu
- Ninawi ilipokea siku 40 za "neema" pale Yona alipouita mji huo kwenye toba
- Yesu alijiandaa kwa ajili ya huduma kwa siku 40.
- Yesu alitumia siku 40 pamoja na wanafunzi Wake kabla ya kupaa mbinguni.

**Nini ambacho wanafunzi hao walipaswa kungojea?**

Baada ya ufufuo Wake, Yesu aliwaambia wanafunzi Wake kwamba wangepaswa kungoja ili wapokee ubatizo wa Roho Mtakatifu kabla hawajaenda kuitangaza injili ulimwenguni: *"Hata alipokuwa amekutana nao aliwaagiza wasitoke Yerusalemu, bali waingoje ahadi ya Baba, ambayo mlisikia habari Zake Kwangu; ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache. Basi walipokutanika, wakamwuliza, wakisema, Je Bwana, wakati huu ndipo unapowarudishia Israeli ufalme? Akawaambia, Si*

*kazi yenu kujua nyakati wala majira, Baba aliyoyaweka katika mamlaka Yake Mwenyewe. Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi Wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi."* (Matendo 1:4-8)

Japo walikuwa wametumia kipindi kilichopita cha miaka mitatu na nusu kila siku wakiwa pamoja na Kristo na walikuwa wameona na kushiriki katika huduma ya miujiza, hawakuwa tayari kumshuhudia. Walipaswa kungoja ili wapokee ubatizo (ujazo) wa Roho Mtakatifu, tukio lililofanyikia siku ya Pentekoste, ndipo wangewezeshwa kuliko wakati mwingine wowote uliopita ili kumshuhudia Kristo: *"Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja. Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka."* (Matendo 2:1-4) Je mpangilio ulikuwa upi: maombi, upokeaji wa Roho Mtakatifu, kuihubiri injili kwa furaha. (Angalia pia Matendo 4:31.)

**Baraka Maradufu**

Kwa kuchagua kushiriki katika Siku 40 za kujifunza na kuomba, unaingia katika mshangao wa ajabu na wenye baraka pamoja na Bwana. Utapata uzoefu wa uhusiano wa kina zaidi pamoja na Kristo, nawe utamwona Bwana akikutumia ili kuwavuta wengine waje karibu Naye katika maandalizi ya ujio Wake hivi karibuni. Kadiri unapofanya ushirika na mwanamaombi mwenzio pamoja na wengine wanaoshiriki katika Siku 40 za maombi na ibada ya kujifunza, utapata uzoefu wa kina na upendo wa Kikristo pamoja na waumini wenzako. Hii itakuwa na mchango muhimu katika ukuaji wako binafsi kiroho.

Ili kupata fanaka maridhawa katika uzoefu huu, inapendekezwa kwamba hili liwe jambo la kwanza ufanyalo asubuhi. Inaweza kuhitaji kuamka mapema kidogo, lakini juhudi husika zinatuzwa! Ukimwomba Bwana akuamshe ili uweze kuwa na wasaa bora moja Naye, atasikia na kulijibu ombi lako. Kuhusu maisha ya maombi ya Yesu Ellen White aliandika:

“Kila siku alipokea ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu. Katika saa za alfajiri ya siku mpya, Bwana alimwamsha kutoka kwenye usingizi Wake, na nafsi na midomo Yake iliakifishwa kwa neema, ili aweze kuwakirimia wengine. Maneno Yake mapya alipewa kutoka kwenye maskani ya mbinguni, maneno ambayo angeyanena wakati mwafaka kwa waliochoka na waliodhulumiwa.” (*Christ's Object Lessons*, uk. 139)

Kristo atafanya hivyo kwa ajili yako, kama ukimwomba. Anatamani sana kukuweka wakfu kwa njia ya Roho Mtakatifu katika maandalizi ya kila siku mpya.

**Kigezo Muhimu: Washiriki wa Kanisa Kuhusika Katika Kazi ya Utume**

Huduma hii kwa ajili ya wanadamu wenzetu ni njia ya furaha kuu na ukuaji binafsi katika imani, na huwaongoza watu kwenye wokovu katika Kristo. Hivyo kuna mapende-kezo kadhaa zaidi:

**Mwombe Mungu kuhusu mtu unayetaka kumwombea.**

Wakati wa siku hizi 40, unaitwa ili kuwaombea watu watano kila siku. Mwombe Mungu akuongoze katika kuwachagua watu hawa.

**Wachague watu watano unaotaka kuwaombea.**

Pengine kwenye orodha yako una jamaa, marafiki, wafanya-kazi wenzio, majirani, watu mnaofahamiana, washiriki wa kanisa wa zamani au wasioamilifu unaotaka hususan kuwahu-dumia katika kipindi cha siku 40 kwa kuwafikia au kuwaalika mathalani kwenye tukio maalumu kanisani – watu watu walio katika janibu halahali.

**Wafikie watu watano ambao umewachagua.**

Kama unataka, unaweza kuwafikia haraka – muda mfupi kabla ya kuanza zile siku 40. Wengine huomba siku 20 au 30 kwa ajili ya watu hawa kisha wafikie na kuwaambia kwa nini na jambo gani ulilokuwa ukiliombea na kuwaalika kwenye Sabato ya wageni kanisani, ambayo hufanyika mwishoni mwa siku 40 yenye programu maalumu. Tunajiandaa wenyewe kupitia maombi kabla ya kuwafikia watu hawa.

**Jinsi gani tunaweza kujifunza kuhusu mahitaji ya watu tunaofahamiana nao?**

Tunaweza kumwambia mtu tunayefahamiana naye: "Kanisa letu limepanga muda maalumu wa maombi kwa majuma sita. Tumehimizwa kuwaombea idadi fulani ya watu katika wakati huu. Ningependa kukuombea. Naweza kujua ni mahitaji gani ya maombi uliyo nayo kuhusu afya, familia au kazi?"

Mshukuru kwa ajili ya fursa hii na kumpatia ama *Barua kwa Andrea namba 4 Unasibu wa Pascal – Je Mungu Yupo*? *Au hayupo*? Au kama Sabato ya wageni inafanyika hivi karibuni, basi mwalike halafu jitolee kumchukua au kukutana naye kwenye mlango wa kanisa.

**Andaa taarifa:** Jina, namba ya simu, baruapepe, anuani, mahitaji ya maombi, uchunguzi na jinsi gani mawasiliano yalivyofanyika.

**Waombee watu hawa kila siku.**

Hii ni fursa nzuri ya kudai ahadi. Utapata "Ahadi kwa ajili ya Huduma ya Maombezi" katika Kiambatisho A.

**Jinsi gani tunaweza kuonesha shauku yetu?**

Tunataka kuonesha shauku kwa watu hawa watano. Unaweza kupata dondoo kwa ajili ya hili katika Kiambatisho B: Mapendekezo ya jinsi ya kuwafikia watu. Pendekezo muhimu ni kuwasilisha chapisho liletalo faraja, hasa vijizuu vya Biblia vinavyovutia. Hii ndiyo sababu tuna *Barua kwa Andrea*. Katika sura ya 9 ukurasa 157 huonesha kile ambacho kwa kawaida ni bora ili kuvitumia. Kama umejiandaa kwa ajili ya kuwasiliana na huyu kupitia maombi ya kina, kwa kawaida vijizuu hivi vinaanguka juu ya udongo wenye rutuba moyoni.

Tunaambiwa: "Nimeoneshwa kwamba hatukuwa tukifanya wajibu wetu katika usambazaji usiokoma wa machapisho mdogo. Kuna roho nyingi zenyeuamini ambazo zingeletwa kuipokea kweli kwa njia hii pekee. … Majarida haya madogo yenye kurasa nne, nane, au kumi na sita, yanaweza kugawiwa kwa malipo kidogo, kutokana na fedha iliyokusanywa kwa hisani ya wale wenye mzigo wa kazi moyoni." *(1T* 551,552 na *ChS* 151.2 egwwritings.org)

**Mwongozo wa Mafunzo ya Siku 40 kwa Viongozi**

Mwongozo wa mafunzo wa Siku 40, pamoja na mikutano ya injili mwishoni, hupatikana kutoka kwa Dennis Smith. Mwongozo unapatikana bure kwenye: www.40daysdevotional.com

**Sabato ya Wageni**

Mwishoni mwa siku 40 siku maalumu ya wageni hupangwa kanisani au katika kikundi cha huduma. Hii haina budi kuandaliwa vyema kwa maombi.

Katika Sabato ya wageni, wageni hualikwa kwenye mikutano ya injili, ambayo huanza ndani ya siku chache au ndani ya juma kanisani au kwenye kikundi cha huduma.



## Hatua ya 3: Kuwasilisha Injili

Hii huweza kufanyika kwa masomo ya Biblia mikutano ya injili katika vikundi vya huduma au makanisa au kama ni mpango wa konferensi, huweza kufanyia mikutano yote kwenye konferensi wakati mmoja. Konferensi na hata unioni au nchi nzima imeendesha mamia au maelfu ya mikutano ya injili wakati mmoja kupitia wahubiri wa ukanda husika pamoja na wale kutoka ughaibuni.

(Tunaita harakati hii ya injili "Ujumuishwaji Timilifu wa Mshiriki." https://tmi.adventist.org)

**Mawasilisho ya Video ya kufundishia imani**

Tunarudia: Leo tunazo nyenzo nzuri hasa kwa ajili ya kufundishia na kujenga imani katika Mungu na Neno Lake, endapo hakuna mwalimu aliyepo. Ili kufundisha injili, tafadhali tafuta mawasilisho ya injili yenye kweli za Biblia zote muhimu. Mfululizo wenye mawasilisho 20-30 ni bora. Katika Kiambatisho F utapata maelezo mafupi ya tovuti 15 na kila unachoweza kupata hapo. Kurasa hizi zina thamani kwa watoto, vijana, watafuta-ukweli na waumini wa muda mrefu. Kingine kilichotajwa pia ni tovuti kutoka katika Ujumuishwaji Timilifu wa Ushiriki wa Konferensi Kuu. Hii ina vidokezo vya Uinjilisti, Usambazaji wa machapisho mbalimbali mifululizo juu ya Afya na Siha, Kisukari, Utengamano kutoka kwenye Mfadhaiko na

Shule ya Mapishi. Katika Kiambatisho F utapata hazina ya tovuti zenye manufaa.

**Kazi nyingine kabla au baada ya mikutano ya injili: Kozi ya Uanafunzi**

Ni muhimu sana kwamba washiriki waliobatizwa hivi karibuni washiriki kwenye kozi ya uanafunzi. Kitabu chetu adhimu, Hatua za Ushindi (*The Steps to Christ)* Ellen White, huweza kupendekezwa ulimwengu mzima. (Kinapatikana kwenye nyumba zetu za uchapishaji kwa majina mbalimbali.) Ni kitabu chetu kilichofasiriwa zaidi na hupatikana katika lugha takriban 150. Kitabu hiki kimegawanywa katika sehemu kuu mbili na kina sura 13. Sehemu hizi mbili ni "Jinsi gani naweza kuja kwa Kristo?" na "Jinsi gani naweza kukaa ndani ya Kristo?" Kiasili, mtu anaweza kusoma kitabu hiki peke yake, lakini huweza pia kusomwa katika vikundi vidongo, kwenye kikundi cha mjadala kwa watu wenye shauku au vijana au katika Darasa la Biblia la Mchungaji.

**Darasa la Biblia la Mchungaji**

Kikundi hiki maalumu cha mjadala ni mpango wenye thamani kubwa na hutumika kama darasa la ubatizo. Lakini hatutumii neno hili. Kikundi hiki hujifunza kwa kwa usaidizi wa maswali maalumu mafunzo ya Ukristo binafsi (yani, kwa Hatua za Kumwendea Kristo) na kweli msingi za Biblia. Kistahabu, darasa hili liko kwenye chumba tofauti. Mshiriki pekee wa kanisa wanaohudhuria darasa hili ni wale wanaomsandikiza mgeni. Wale wanaosandikiza mgeni huwa makini zaidi wakati wa kuuliza maswali au wanapowasilisha maelezo. Kikundi hiki huongozwa na mchungaji au mwalimu mwengine anayefaa. Katika nchi nyingi, darasa hili linaitwa **"Darasa la Biblia la Mchungaji,"** kwa sababu linaongozwa na mchungaji inapowezekana. Watahiniwa wa ubatizo (vijana na marafiki wa kanisa) wana fursa ya kufundishwa kutoka kwenye neno la Mungu mara moja kwa juma pamoja na usomaji wao wa Biblia wa kawaida kila juma. Katika nchi nyingi darasa hili la Biblia ni mojawapo ya mbinu fanisi kabisa za kuwaongoa watu kwa ajili ya Yesu. Kikundi hiki ni uinjilisti wakati wa huduma ya kanisa.

**Sabato ya Utume**

Akina baba zetu wa imani walikuwa na ufumbuzi wa kivitendo zaidi katika maeneno mengi. Mojawapo ulikuwa Sabato ya utume. Mara moja kwa mwezi – kawaida Sabato ya kwanza katika mwezi – Sabato ya utume ilifanyika katika kila kanisa. Wazo la msingi lilikuwa kwamba lile la uhamasishaji kwa ajili ya kazi ya utume ulihitaji "mafuta" daima. Umuhimu wa Sabato ya utume kila mwezi ni kuamsha na kudumisha ari ya utume. Huhitaji uangalifu katika neno na tendo. Ama mtu au kundi tawakafu linapaswa kubeba wajibu wa kuiandaa Sabato. Aina hii ya Sabato taratibu itakuwa furaha kuu na mchakato wa lazima. Maneno ya msingi: filamu fupi ya utume, nyimbo mpya za utume, uzoefu wautume, habari njema, kisa cha watoto cha utume, hubiri la utume, huduma ya utume au utembeleaji kwa kusudi la utume.

**Hatua zinazofuata ni zipi?**

Inapendekezwa kurudia programu hii ya hatua tatu mara kwa mara. Katika mara ya kwanza, idadi fulani ya washiriki wa kanisa watadhahimu faraja kutokana na ujumbe huu na mara ya pili kundi lingine litajiunga nao katika maisha ya furaha na yazaayo matunda. Kila wakati watafuta-ukweli wapya watakuja. Na ni jambo la thamani kwa washiriki waliobatizwa hivi karibuni. Nao pia wana shauku ya kuona marudio yakifanyika. Na jukumu letu la kuwaongoza watu kwa Kristo linapaswa kufanyika kisahiwifu. Tunahitaji kufanya marudio kwa vile tunaishi katika nyakati faridi na zenye shughuli nyingi. Ni lishangazwa kusoma mambo mawili katika nukuu ifuatayo:

"Katika kila kanisa wanapaswa kufunzwa vilivyo kiasi kwamba watatoa wao muda ili kuongoa roho zije kwa Kristo.… Mabadiliko ajanabi na tasihili hivi karibuni yatatokea, na watu wa Mungu hawana budi kukirimiwa Roho Mtakatifu, ili kwa hekima ya mbinguni waweze kukabili changamoto za kizazi hiki." (3TT 69)

Vitabu vilivyotumika kwenye mkutano wa kwanza wa injili huweza kutumiwa tena Lakini kitabu *Kaeni Ndani ya Yesu* cha Helmut Haubeil kinapaswa pia kuzingatiwa kwa sababu husaidia

kujeng uhusiano wa karibu pamoja na Kristo. Kimegawanywa katika sura zifuatazo za kujifunza:

- Karama ya Yesu ya Thamani Zaidi
- Kujisalimisha kwa Yesu
- Yesu Akaaye Ndani Yako
- Utii kupitia Yesu
- Imani Adinati kupitia Yesu

Uwezekano mwingine ni *kitabu 2 cha Siku 40: Maombi na Ibada ili Kuhuisha Uzoefu Wako na Mungu* cha Dennis Smith. Kuna mawasilisho manane kwa kila mada: Watu wenye uzoefu wa kushangaza, Watu wamngojeao Mungu, Mungu wetu jalali, Uzoefu mgumu lakini yenye ulazima, Watu walio tayari kumlaki Yesu.

Vitabu hivi viwili hukamilishana na kitabu cha kwanza miongoni mwa vile *vitabu vya Siku 40* na *Hatua za Uamsho Binafsi* na vimejengwa hapa.

**Ni uzoefu upi ambao watu wamekuwa nao?**

Uzoefu wa pekee wa kutoka kwenye kanisa moja huko Cologne-Kalk/Ujerumani na jinsi lilivyokua kutoka washiriki 17 hadi 65 katika kipindi cha miaka 4 tu kwa sababu walitumia na kurudia mbinu hii kila mwaka, huelezewa kwa kina katika www.steps-to-personalrevival.info, Testimonies 2/19.

Matokeo hutegemeana na vile ambavyo Roho Mtakatifu anaweza kutenda kazi kupitia sisi. Tunalenga katika taarifa hii ya uzoefu wa nchi zinazo kataa taratibu za kidini:

- Marekani – Decatur, Alabama: Imesimuliwa mwanzoni mwa sura hii: watu 15 walibatizwa
- Uswisi – Tessin: watu 15 walibatizwa kupitia vikundi vya Siku 40.
- Tajikistani – Dushanbe: watu 46 walibatizwa kwa mwaka kupitia injili ya Siku 40.
- Uingereza: watu 22 walibatizwa kupitia kazi zinazolenga uamsho wa kiroho.

**Uzoefu wa Mwisho**

Mchungaji alishuhudia kwamba alipotambua hali yake ya kutokuwa na nguvu, aliamua kusoma vilivyo mada ya Roho

Mtakatifu kwenye Biblia: “Hatimaye nilichunguza maandiko 273 katika lugha asili ambayo moja kwa moja huzungumza juu ya kazi ya Roho Mtakatifu, nami nilipata nukuu zaidi ya 2,000 kwenye maandishi ya Ellen White kwenye mada hii.”[10]

Naweza kuuliza: Hivi hilo bila shaka lolote halikuwa kusudi la Mungu kwa ajili ya siku ya mwisho lililomfanya amvuvie Ellen White ili amtaje Roho Mtakatifu zaidi ya mara 2,000? Je anataka kulipatia kanisa Lake la mwisho nguvu, mamlaka na ushindi? Hivi anataka kutuleta kwenye mstari wa hitimisho kwa namna hii?

The mchungaji aliendelea kusimulia kwamba Yesu alimuuliza maswali matatu:

“Je unawapenda watu Wangu?”

“Hivi unaihubiri injili kila juma ukiwa na shauku kwa ajili ya roho zilizopotea?”

“Unatafuta sifa kutoka kwa wanadamu?”

Machozi yakaanza kunichuruzika wakati nikiiungama dhambi yangu.

Mwaka huo watu 37 walimkabidhi Yesu maisha yao. Katika miaka iliyofuata tangu usiku huo, mamia ya watu wamefanya maamuzi kwa ajili ya Kristo. Bwana Yesu asifiwe milele!”[11]

**Nini hatua ya kwanza ya uamsho?**

Mungu wetu wa pekee ajabu analijibu swali hili binafsi katika 2 Nyakati 7:12-14:

*“Bwana akamtokea Sulemani usiku, akamwambia, Nimesikia uliyoyaomba. ... ikiwa watu Wangu… [1] watajinyenyekesha, na [2] kuomba, na [3] kunitafuta uso, na [4] na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao.”*

**“Watajinyenyekesha”**

… hili ni agizo la kwanza katika mfululizo wa masharti manne katika ujumbe huu kutoka kwa Mungu. Kabla

10 *Seeking God's Spirit,* Januari 8. – 18.,2020, Siku ya 4, uk. 36 – www.tendaysofprayer.org)

11 ditto, uk. 37, Tumetaja mawazo makuu tu.

hatujaambiwa kuomba au kutafuta au kughairi, tunaambiwa kuzinyenyekesha nafsi zetu. … Kwa kawaida huwa tunatega sikio bovu kwenye tatizo hadi kunapotokea mlipuko wa nyuklia, ndipo tunalazimika kusikiliza. … Ni dhahiri kwenye filamu iitwayo 'Titanic' kwamba nahodha wa meli hiyo na mabaharia wake hawakutaka kusikia tahadhari za uwanda wa barafu waliokuwa wakiuelekea.

Sisi wanadamu mara nyingi huwa hatusikilizi hadi tunapokuwa tumechelewa kabisa. Kwa nini? Kwa sababu ni nadra kwamba tunapenda kile tunachosikia – hususan kama kile tunachosikia hutupatia changamoto ya kubadili mawazo, mwenendo wa maisha, mtazamo, au tabia." [12]

Hivi hatupaswi kumwomba Yesu kila siku atukirimie moyo wa unyenyekevu ili aweze kutenda "mambo makuu na yastaajabishayo" kupitia sisi?

**Ushauri na Maombi: Tufanyie nini hatua hizi tatu?**

Tunataka kutumia muda kwa ajili ya maombi na tafakari ili kupata mawazo tangulizi ya namna tunavyoweza kutimiza mapendekezo katika sura ya 10 *Mwanzo Mpya Kiroho na Kimishenari katika Hatua Tatu* (angalia maswali kwenye ukurasa unaofuata).

Zahama ya kirusi-korona kimekuwa na athari juu ya maisha yetu ambayo kamwe hatukuwahi kuamini inawezekana. Tunapowaalika majirani zetu katika kikundi cha huduma ili kujadili "Njia za Kuboresha Mfumo-kinga Wako," ndipo tunaweza kuzungumzia maana ya uhusiano binafsi pamoja na Mungu (Zaburi 91) na kuhusu njia nane za afya (Mwanzo Mpya) au Fanaka za Mwanzo Mpya. Lengo linapaswa liwe kuwaonesha wengine manufaa, ambazo hawana bado. Hebu Bwana akubariki katika tafakari na maombi yako.

---

12 Randy Maxwell, Kama Watu Wangu Wakiomba (Pacific Press 1995), uk. 72.

## Mawazo binafsi na mwongozo wa mjadala

1. *Ni hatua zipi muhimu kwa ajili ya mwanzo mpya wa kiroho?*

   ______________________________

   ______________________________

2. *Andika majina ya watu watano unaotaka kuwaombea kwa namna mahususi.*

   ______________________________

3. *Kwa maombi, zingatia ni majukumu yapi uliyo nayo kwa ajili ya kuendesha masomo ya Biblia/ vikundi vya malezi na/ au mikutano ya injili.*

   ______________________________

   ______________________________

4. *Ni uzoefu upi ambao vikundi/watu wengine wamekuwa nazo? Tazama Uzoefu huu kwa kina zaidi.*

   ______________________________

   ______________________________

## Muda Wetu wa Maombi

- Wasiliana na mwanamaombi mwenzio ili mjadili mada husika.
- Sali pamoja na mwanamaombi mwenzio…
  1. kwa ajili ya mwanzo mpya kiroho – binafsi na kanisani kwako.
  2. kwa ajili ya watu watano uliowaandika.
  3. ili kutambua stamani gani ulizo nazo binafsi na kama kikundi/kanisa ili kufanya kazi kwa ajili ya Mungu na pamoja Naye.
  4. kwa ajili ya uzoefu, ambapo Mungu ameliongoza kanisa lako.

Siku ya 37

## Kujazwa Roho Upya Kila Siku!

### Wengine wana nini cha kusema kuhusu ulazima wa kuomba daima ubatizo wa Roho Mtakatifu?

**Konferensi Kuu ya Waadventista Wasabato:** “Ubatizo wa Roho siyo tukio la mara moja; tunaweza kupata uzoefu huu kila siku. Tunahitaji kumsihi Bwana kwa ajili ya ubatizo huo kwa sababu huipatia kanisa nguvu ya kushuhudia na kutangaza injili. Ili kufanya jambo hili, lazima tuendelee daima kusalimisha maisha yetu kwa Mungu, tukae katika Kristo kikamilifu, na kumwomba hekima ya kugundua karama zetu (Yakobo 1:5).”[13]

**Carlos Steger:** “Ubatizo wa Roho Mtakatifu humaanisha kutawaliwa kikamilifu na Roho, kujazwa Roho kikamilifu (Waefeso 5:18). Huu siyo uzoefu wa mara moja tu, bali kitu fulani kinachohitaji kuendelezwa daima.”[14]

**Frank Hasel:** “Wakati ambapo Roho hukirimiwa kwa kusikia kunakotokana na imani (Wagalatia 3:2) na hupokelewa kupitia imani (Wagalatia 3:14) wakati wa ubatizo wetu (Tito 3:5-6), tunapaswa kutafuta ujazo wa Roho Mtakatifu kila siku. Hatuwezi kuishi kwa kutegemea uzoefu fulani thabiti tuliokuwa nao mwaka uliopita au mwezi uliopita au hata jana. Tunahitaji ujazo wa Roho wa Mungu kila siku, maana kila siku huja na changamoto zake.”[15]

**Johannes Mager:** “Kwa mujibu wa hii, kujazwa Roho Mtakatifu siyo uzoefu wa mara moja, bali ni mchakato endelevu na unaojirudia. Mkristo si kama chombo ambacho kimejazwa

---

13 Seventh-day Adventistis Believe - A Biblical Exposition of 27 (28) fundamental doctrines, Copyright by the Ministerial Association General Conference of Seventh-day Adventists, Chapter 17, Spiritual Gifts and Ministries, uk. 213.2 – www.Carenage Seventh-day- Adventist-Church Trinidad and Tobago, 16.8.2020

14 Adult Bible Study Guide – Standard Edition – July 17, 2014, Principle Contributor: Carlos Steger

15 Adult Bible Study Guide – Standard Edition – January 30, 2017, Principle Contributor: Frank Hasel

mara moja tu, badala yake anapaswa kuiruhusu nafasi yake ‘ijazwe tena’. … Kujazwa Roho Mtakatifu, tunakopokea wakati wa ubatizo wetu, kunaweza kupotezwa pale ambapo utimilifu tuliopewa haudumishwi. Kama umepotezwa, basi unaweza kupokelewa tena.”[16]

**David Wolkwitz:** “Kwanza kabisa, tutaonesha jinsi gani ilivyo muhimu kujazwa Roho. …Mwishowe utagundua kuwa kujazwa huku ni wazo kuu la agano jipya. Nasi tunataka kutambua ushawishi wa Mungu, anayetaka tupokee baraka hii siku baada ya siku.”[17]

**Ekkehardt Müller:** “Pamoja na hilo, lazima ikumbukwe kwamba kujazwa Roho Mtakatifu hufuatia kuzaliwa upya, lakini siyo mchakato unaotenda kazi moja kwa moja(kitarasili). Uhusiano huo hauna budi kuhawilinishwa kila siku.”[18]

**Dennis Smith:** “Wazo lingine muhimu ni kwamba ujazo wa Roho unapaswa kurudiwa upya kila siku. Paulo alisema katika 1 Wakorintho 15:31 ‘*ninakufa kila siku*. Kuifia nafsi na kujazwa Roho Mtakatifu ni uzoefu wa kila siku. Wala siyo uzoefu wa ‘mara moja tu.’ Paulo alisema kwamba ‘*utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku*’ (2 Wakorintho 4:16). Tunahitaji upya wa ujazo wa Roho kila siku katika maisha yetu. Paulo anatupatia changamoto akitumia maneno ‘*mjazwe Roho’* (Waefeso 5:18). Kitenzi katika fungu hili kiko katika kitendo endelevu, ikimaanisha katika Kiyunani kwamba tunapaswa kulifanya hilo kila siku. Kwa kujazwa Roho, ndipo muumini anaongozwa Naye.” [19]

---

16 Auf den Spuren des Heiligen Geistes, Advent-Verlag (Lüneburg 1999), S. 101

17 Der Weg zu einer kraftvollen Erweckung (Hrsg. Abteilung Heimatmission, Gemeinschaft der Siebenten-Tags-Adventisten in Nordrhein-Westfalen), S. 102, 103, ohne Datum. Abschnitt “Lasst euch erfüllen” (Waefeso 5,18)

18 Die Lehre von Gott (Seminar Schloss Bogenhofen 2019), S. 224

19 10 Days – Prayers and Devotions to Experience the Baptism of the Holy Spirit, Dennis Smith 10 Tage – Translated from the German Version: Andachten und Gebete zur Erfahrung der Taufe mit dem Heiligen Geist. (Konrad Print & Medien, Rudersberg/Württemberg), S. 48

**Ellen G. White:**

– “Ili kupata ubatizo wa Roho kila siku, kila muumini anapaswa kuwasilisha dua yake kwa Mungu.”[20]

– “hata Kristo katika maisha Yake duniani alimtafuta Baba Yake kila siku ili kupata masarufu mapya ya neema inayohitajika.”[21]

“Kupitia mbinu za ujuzi wa kudanganya adui, akili za watu wa Mungu huonekana kutoweza kutambua na kujitwalia ahadi za Mungu. … Nguvu ya Mungu hungojea maombi na upokeaji wao.”[22]

## Uamsho!

### Nini ambacho wengine wanasema kuhusu uamsho? Nini maana ya uamsho?

Je tunaweza kufanya kitu fulani juu ya hilo?

**Ellen G. White:** Nini maana ya uamsho? “Uamsho humaanisha kufanya upya wa maisha ya kiroho, uhuishaji wa nguvu za akili na moyo, ufufuaji kutoka kwenye mauti ya kiroho.”[23]

**Mark Finley:** Je tunaweza kufanya kitu fulani juu ya hilo? “Uamsho hautokei pale tunaposoma tu habari zake, bali pale tunapotekeleza vipengele vya Biblia vihusuvyo uamsho.”[24]

**D. Martin Lloyd-Jones:** “Mungu anapoleta uamsho, ndipo anaweza kutimiza mambo mengi kwa siku moja kuliko kipindi cha miaka 50 ya majaribio yetu ya uratibu.”[25]

**Charles G. Finney:** “Uamsho siyo lingine zaidi ya mwanzo mpya wa kumtii Mungu (Ufunuo 2:5) [Kuurejea upendo wako wa kwanza].”[26]

---

20 Acts of the Apostles, p. 50.2, Das Wirken der Apostel (Saatkorn, Hamburg 1976), S. 52, [50, 51]

21 Acts of the Apostles, uk. 56.1, Das Wirken der Apostel (Saatkorn, Hamburg 1976), S. 57, [55, 56]

22 Testimonies to Ministers and Gospel Workers, uk. 174.2

23 Selected Messages Book 1, 1SM, 128.1

24 Belebe uns neu (Advent-Verlag Lüneburg, 2011), S. 25 (Revive us again, PPPA 2010)

25 Vollmacht (Franke, Marburg 1984) S. 105

26 Ch. G. Finney, Über Geistliche Erweckung (Harfe-Verlag, Aarburg 1976), S. 5

**Dennis Smith:** “Kujazwa Roho Mtakatifu huwapatia Wakristo Walaodikia nguvu inayohitajika kwa ajili ya uamsho wa kiroho pamoja na nguvu ya kushuhudia. Yesu alijua jinsi gani umwagwaji wa Roho Mtakatifu ungekuwa muhimu kwa Wakristo wa awali wakati wa Pentekoste. Alisema: ‘Nimekuja kutupa moto duniani; na jinsi gani natamani endapo ungekuwa umewashwa tayari!’ (Luka 12:49, NKJV) Na jinsi gani Wakristo Walaodikia wanaweza kudhahimu ujazo wa Roho Mtakatifu pamoja na uamsho? Kwa namna hiyohiyo kama ilivyo daima – kwa kuomba na kudai ahadi za Mungu.” [27]

**LeRoy E. Froom:** “Mungu hawezi kufanya lolote la kimapinduzi pamoja na watu kabla hajafanya lolote la kimapinduzi kwa ajili yao, kwa njia ya Roho Mtakatifu kuingia maishani mwao.”[28]

---

27 40-Days of Prayers and Devotions to prepare for the second coming, 40 Tage-Andachten und Gebete zur Vorbereitung auf die Wiederkunft Jesu (Wien 2012), S. 103

28 Das Kommen des Heiligen Geist (Edelstein 1995), S. 100

# Baraka

**"Kukaa ndani ya Kristo humaanisha:**
**"kumpokea Roho Wake daima,**
**"maisha ya kujisalimisha kikamilifu**
**"kwenye huduma Yake."** (E.G. White, The Desire of Ages, uk. 676.2)

Hebu ujumbe huu utusaidie ili kila siku tuombe na kupokea Roho Mtakatifu kupitia kudai ahadi katika maombi, na uweze kutusaidia ili kila siku tujisalimishe kikamilifu kwa Yesu na huduma Yake, ili tuweze kuishi maisha ya kuzaa matunda kwa ajili ya heshima Yake na furaha yetu.

Napendekeza kwamba ujifunze kwa makini Yohana 15:1-17. Yesu anatuonesha mfano wa Mzabibu na matawi:

| | |
|---|---|
| Fungu la 2 | Matawi yasiyokuwa na matunda yatakatwa na kuteketezwa!<br>Matawi yazaayo matunda yatapogolewa ili yazae matunda mengi zaidi! |
| Fungu la 4 | Ni pale tu tunapokaa ndani ya Yesu ndipo tunazaa matunda! |
| Fungu la 5 | Yeyote akaaye ndani ya Yesu, huzaa matunda tele! |
| Fungu la 8 | Mungu hutukuzwa kwa matunda tele! |
| Fungu la 16 | Kazi yetu ni kujaa matunda! |

***Sala: "Baba uliye mbinguni, tunakuomba kwamba tuweze kuzaa matunda kila siku kwa heshima Wako kupitia ushirika pamoja na Yesu na Roho Mtakatifu. Tafadhali tusaidie ili tujazwe upendo Wako ili tuweze kukutumikia kwa kuwatumikia wanadamu wenzetu. Tuongoze katika maombezi yetu na wawasiliani wetu binafsi. Tupatie maisha yenye hamasa na ushindi kwa heshima na utukufu Wako, kwa ajili ya wokovu na baraka ya wanadamu wenzetu pamoja na wokovu na furaha yetu wenyewe. AMINA."***

# Mapendekezo

**Ushauri muhimu:** Soma kitabu hiki au ibara ama sura muhimu zaidi kwako – kama inawezekana – mara sita mfululizo. Utafiti wa elimu umeonesha kwamba tunapaswa kusoma au kusikia mada fulani ihusuyo maisha yetu mara sita hadi kumi ndipo tuweze kuielewa vizuri.

Angalau jaribu hilo. Matokeo yatakushawishi. Nimepokea shuhuda nyingi za ari na shukrani kuhusu maisha mapya ya watu katika Roho Mtakatifu. Karibu yote miongoni mwa shuhuda hizi hutoka kwa wasomaji ambao wamejiadhimu kwa dhati kusoma kwa kurudia mafundisho husika.

Tafadhali simulia uzoefu wako mpya

Ombi la kirafiki: Unapopata uzoefu maishani mwako kwa mguso wa Roho Mtakatifu – katika uzoefu wa imani binafsi au katika kuwashuhudia wengine – basi tutashukuru iwapo utatuma ujumbe mfupi kwenda kwa Helmut Haubeil kwa ajili ya uchapishaji. Kwa kawaida huwa tunachapisha herufi za kwanza tu za jina la mtu.

Tafadhali zingatia kwamba uzoefu wako unaweza kuwahamasisha wengine ili waanze maisha pamoja na Roho Mtakatifu, wakue na kumtumikia Yesu kwa kuwatumikia wengine.

**Mawasiliano:**

Helmut Haubeil

Rosenheimerstr. 49, D-83043 Bad Aibling/Oberbayern, Ujerumani, Barupepe: helmut@haubeil.net

# Wasifu

**Helmut Haubeil** ni mfanyabiashara na Mchungaji. Baada ya kufanya kazi kwa ufanisi kama mwakilishi mfawidhi wa kampuni ya ubaharia, aliukubali wito wa Mungu akiwa na umri wa miaka 37 ili kuwa mchungaji na kufanya kazi kwa miaka 16 kwa ajili ya kanisa. Baada ya hapo, akawa kiongozi wa makazi ya ustajiri ya Kiadventista huko Bad Aibling.

Tangu alipostaafu, yeye ni kiongozi wa kikundi awani kwa ajili ya Uamsho na Utume Ulimwenguni katika kanisa hili.

Hajihesabu binafsi kama mwandishi wa kitabu kiitwacho *Hatua za Uamsho Binafsi,* ambacho ni msingi wa mfululizo huu. Kamwe hakuwa na nia ya kuandika kitabu. Lakini Mungu alimwongoza katika mapito haya. Mamlaka, tunayoweza kujipatia kwa ajili ya maisha yetu ya imani na huduma yetu, hayako kwenye vitabu hivi vidogo, bali katika Mpaji wa Karama – Bwana wetu wa pekee ajabu.

Nimegawa vijizuu au nakala za mahubiri mara nyingi kadiri iwezekanavyo. Bwana wetu adinati alimwonesha mjumbe Wake kwamba nyaraka kama hizo zinaweza kuvunja kuta za nishaha na ushirikina. Na – shauku mpya kabisa inaweza kuibuka. Nina shukrani kwamba niliweza kudhahimu hili mara nyingi na bado ningalifanya hivyo. Natambua jinsi nukuu hii ilivyo ya thamani sana:

“Nimeoneshwa kwamba tayari machapisho yamekuwa yakifanya kazi mioyoni mwa baadhi katika nchi zingine ili kuvunja kuta za nishaha na ushirikina. Nilioeneshwa wanaume na wanawake wakijifunza kwa shauku ya kina majarida na kurasa chache za vijizuu vya ukweli wa sasa. Wangeweza kusoma ushahidi mbalimbali mpya na wa kustaajabisha sana kwao, na wangefungua Biblia zao kwa shauku mpya na ya kina, kadiri ambavyo mada za kweli zilizokuwa giza kwao zilipofafanuliwa bayana, hususan nuru kuhusu Sabato ya amri ya nne. Kadiri walipoyachunguza Maandiko ili kuona endapo mambo haya ndivyo yalivyo, nuru mpya iliangaza kwenye fahamu zao, maana malaika walikuwa wakiangaa juu yao, na kuhimiza kwenye akili zao kweli zilizomo katika machapisho waliyokuwa wakisoma.” (*Christian Service,* uk. 149.7; *ChS,* 149.7)

# Kiambatisho

## Kiambatisho A: Ahadi kwa ajili ya Maombi ya upatanisho

Tunaweza kupata ahadi za nyongeza kwa ajili maombi ya upatanisho ndani ya utangulizi wa Vitabu vya Siku 40 juzuu ya 1, 2 na 3 vya Dennis Smith.

1. Tafadhali Baba, mvute aje Kwako (Yohana 6:44).
2. Tafadhali Baba, weka shauku mioyoni mwake ili akutafute Wewe (Matendo 17:27).
3. Tafadhali Baba, msaidie aliamini Neno Lako (1 Wathesalonike 2:13).
4. Tafadhali Baba, angamiza nguvu ya Shetani dhidi yake (2 Wakorintho 4:4; 10:4-5).
5. Tafadhali Baba, hebu ruhusu aongozwe kwa Roho Mtakatifu (Yohana 16:8-13)
6. Tafadhali Baba, msaidie aghairi dhambi (Matendo 3:19).
7. Tafadhali Baba, msaidie amkubali Kristo kama Mwokozi wake (Yohana 1:12).
8. Tafadhali Baba, msaidie amtii Kristo kama Bwana wake (Mathayo 7:21).
9. Tafadhali Baba, msaidie akue katika Kristo na kuimarika katika Yeye (Kol. 2:6-7).

## Kiambatisho B: Mapendekezo ya Namna ya Kuwafikia Watu

1. Mwoneshe nini cha kuthamini kuhusu juu yake.
2. Mpatie machapisho yajengayo matumaini (Barua kwa Andrew).
3. Mwite na kuomba naye. (Ikiwa yu radhi kwa hili.)
4. Mwalike kwenye chakula nyumbani kwako.
5. Mwalike kwenda kula mgahawani.
6. Mtumie heri ya kuzaliwa katika siku yake ya kuzaliwa.
7. Mtumie kadi yenye kutia matumaini au kitu fulani

kinginecho ambacho Mungu amekugusia moyoni mwako.

8. Mpatie kitu fulani ambacho binafsi umepika au kuoka.
9. Mwalike aungane nawe katika manunuzi, kutembelea makumbusho, nk.
10. Endapo inahitajika, mtumie kadi ya "Nakutakia Ahueni" au kitu fulani kinginecho ili kuonesha huruma yako.
11. Mpatie mtoto wake kadi ya siku ya kuzaliwa au mwandalie zawadi, kama inafaa.
12. Mpatie vijizuu vya Biblia vinavyovutia (mfano, Barua kwa Andrew)
13. Mwalike aje kanisani pamoja nawe.
14. Katika wakati mwafaka, muulize endapo angependa kupata masomo ya Biblia.
15. Ushauri wa thamani: pendekeza kozi ya Mwanzo Mpya katika mojawapo ya vituo vyetu vya afya vya Kiadventista Ujerumani, Austria, Uswisi, Romania, Ukreini, Bulgaria, Estonia, Ureno, Marekani, Israeli, nk. Programu hizi ni za thamani sana kwa ajili ya mwili na nafsi kupitia muunganiko wa tumaini kwa Mungu na tiba asilia. Kwa mujibu wa utafiti fulani, uhusiano chanya pamoja na Mungu ni kigezo kikuu zaidi kwa ajili ya afya bora. Pamoja na hilo, huimarisha vigezo vingine vya kiafya (lishe, mazoezi, pumziko, nk.) kwa zaidi ya mara tatu. Utafiti ulifanyika chini ya uongozi wa Prof. Grossarth-Maticek kwa 35,000 kwa kipindi cha zaidi ya miaka 30. (Daktari Manfred Heide, Marvin H. Heide & Michaela Heide-Fassbender, Medical Wellness with Newstart-Plus, Engelsdorfer 2014, uk. 334)
16. Tunaweza pia kuwapatia watu wamwaminio Mungu kitabu kiitwacho Hatua za Uamsho Binafsi; kinahusu maisha pamoja na Roho Mtakatifu. Kitabu kinatolewa bure katika nchi maskini; kwenye nchi zingine kuna gharama ndogo, na tayari kimewasaidia watu wengi wapate imani hai.

(Anuani ya uagizaji iko ukurasa wa 2 kwenye vitabu husika na pia katika kiambatisho.)

Kadiri tunavyowafahamu vyema wanadamu wenzetu, ndipo mawazo mengine bora yatatujia akilini.

## Kiambatisho C: Njia ya Uzima wa Milele

Kabrasha iitwayo *Njia ya Uzima wa Milele* inaweza kupakuliwa au kutumwa bila gharama kwenye www.steps-to-personal-revival.info. Inaweza kupatikana kwenye: *Kupata uzoefu wa Mungu kwa Andrea*. Inapatikana pia kwenye Seti-Anzilishi.

## Kiambatisho D: Muhtasari wa Barua kwa Andrea

Siku ya 39

**BA Na. 1 – Imani ya Kikristo Yajaribiwa**

Kila kitu hujikita katika kujibu kwa uaminifu maswali matatu. Nimepitia njia hii mara mamia na nimerudia tena na tena kudhahimu matokeo chanya pamoja na mshangao.

1. Je yupo Mungu hai, ajuaye yote na mwenye uwezo wote, awapendaye wanadamu?
2. Hivi Yesu wa Nazareti ni mkombozi kweli aliyetumwa na Mungu?
3. Je Biblia au Maandiko Matakatifu kweli yaliandikwa na watu walioongozwa na mamlaka ya Mungu au ni zalisho tu la wanadamu?

Kuna majibu ya kuridhisha kabisa kwa maswali haya ya msingi Jihakikishie mwenyewe. Pengine hukuwa unafahamu utangulizi huu hadi sasa.

**BA Na. 2 – Upekee upitao Ulinganishi: Yesu wa Nazareti**

Mhusika mkuu zaidi katika historia ya ulimwengu– wapekee na apitaye ulinganishi. Ni matokeo gani aliyokuwa nayo Yesu? Kwa nini Yesu ni wapekee kiasi hicho? Kwa nini maisha yake yaliacha mguso wa kudumu kiasi hicho, kuliko mhusika mwingine yeyote? Yesu alisema Yeye ni nani? Nini walichosema mashuhuda, historia inasemaje? Nini ambacho wenye mashaka halisi waligundua walipochunguza ukweli wa mambo?

**BA Na. 3 – Nini lengo kuu la Biblia?**

Mpango wa Mungu wa ukombozi unabainishwa kwa namna fupi na ya ari kwenye hii *Barua kwa Andrea*. Nini ambacho mtu

anapaswa kufanya ili kupokea utimilifu wa maisha na uzima wa milele? Utafiti mkubwa ulionesha kwamba 98% ya watu waliohojiwa, walikuwa na mtazamo potofu kuhusu nani alikuwa mlengwa kuu wa Biblia. Barua hii huonesha wazi kwamba ukombozi ni karama ya Mungu na haiwezi na wala haihitaji kulipiwa. Ni vizuri pale ukweli huu unapokuwa bayana kwa mtu fulani!

**BA Na. 4 – Unasibu wa Pascal: Je Mungu Yupo au La?**

Uwezekano ni upi? Kijumla, unasibu huu unaitwa "Unasibu wa Pascal." Blaise Pascal alifikia hitimisho kwamba kila mtu mwenye busara alipaswa kuamua kwa ajili ya Yesu Kristo hata kama uwezekano wa usahihi wa mafundisho ya Ukristo ulikuwa 50:50 tu. Dkt. Viggo Olson, daktari mashuhuri mpasuaji na mpinzani mshupavu wa imani, alikutana na kauli za Blaise Pascal. Yeye pamoja na mkewe walipambana kufa na kupona dhidi ya imani ya Kikristo. Lakini baada ya masomo ya kina alikuwa Mkristo thabiti. Lazima kila mtu afanye uamuzi. Mtu ana budi kuyajenga maisha yake ama katika dhana kwamba mafundisho ya Ukristo ni ya kweli au kwenye dhana kwamba ni ya uongo. Yeyote asiyeingia katika wito huu, moja kwa moja huweka unasibu kwenye uwezekano kwamba mafundisho ya Ukristo ni ya uongo.

**BA Na. 5 – Ushindi dhidi ya Tumbaku na Pombe**

Uzoefu makini wa Adolf inasimuliwa katika barua hii. Alikuwa dereva wa lori mwenye umri wa miaka 39, aliyevuta sigara 60-70 kwa siku. Wakati huohuo, huu ni utangulizi wa thamani wa kuomba kwa ahadi. Kwa vile kuna ahadi zaidi ya 3,000, tunaweza kuombea maeneo mengi ya maisha tukiwa na uhakikisho kwamba maombi yetu yatajibiwa. Ni kama kupata ruhusa ya kuchukua fedha bila ukomo kwenye "akaunti ya Mungu." Karama hii ya Mungu ya kustaajabisha ni muhimu sana kwa kila mmoja anayehitaji kuishi maisha ya Ukristo yenye ushindi. Jinsi gani mtu anaweza kuwa huru papohapo na kikamilifu dhidi ya uraibu, kwa msaada wa Mungu? Yeyote ambaye angependa kujua hili anapaswa kusoma hii *Barua kwa Andrea*.

**BA Na. 6 – Unajuaje yaliyopo kwenye mustakabali ujao?**

Haya ni masomo yalengayo kujifunza kitabu cha kinabii cha Danieli, sura ya 2. Ni msingi wa kuelewa vitabu vya Biblia vya “Danieli” na “Ufunuo,” hivyo vyote vikiwa vimeandikwa kwa ajili ya wakati wetu. Unabii huu hudhihirisha kuibuka kwa himaya fulani za ulimwengu na kuanzishwa kwa ufalme wa Mungu. Miongoni mwa matukio sita ya utabiri, tayari mitano imetimizwa kisahihi. Hivyo basi tunaweza kutarajia kutimizwa pia kwa utabiri wa sita. Nini ambacho kingali kinakuja? Utafurahi kujifunza kuhusu unabii huu.

**BA Na. 7 – Uzuiaji au uponyaji?**

Hii *Barua kwa Andrea* ni muhimu sana ili, kwa namna isiyo ya moja kwa moja, kusuluhisha nishaha katika eneo la imani na afya. Hili huoneshwa kwa uzoefu wa Dkt. Semmelweis. Je sayansi ya utabibu wa kuzuia maradhi unatoka kwa nani? Nani aliyesaidia kuokoa maisha mamilioni katika karne ya 14 kwenye tauni na katika karne ya 18 kwenye ugonjwa wa kuhara damu, kipindupindu na taifodi? Biblia ilikuwa miaka 4,000 mbele ya sayansi katika kupunguza saratani ya mji wa uzazi. Jinsi gani? Uchunguzi wa kiwango kikubwa wa mtindo wa maisha wa Waadventista Wasabato huonesha manufaa ya mwenendo bora wa kiafya. (Jambo ambalo ni muhimu maradufu katika wakati wa mlipuko kwa vile mfumo-kinga huutegemea.)

**BA Na. 8 – Mafunuo ya unabii kuhusu Yesu Kristo Unasibifu wa Utimizwaji 1:1017**

Hii *Barua kwa Andrea* hususan huimarisha tumaini katika Yesu wa Nazareti kuwa Mkombozi wa kiungu, na pia ukweli kwamba Biblia imevuviwa na Mungu. Matukio mbalimbali ya unabii na utimizwaji wake kuhusu maisha ya Yesu vimelinganishwa. Vidokezo nane huonesha kwa nini utimizwaji wa matukio haya ya unabii hauwezekani kwa mtazamo wa kibinadamu.

**BA Na. 9 – Mafunuo ya unabii kuhusu miji minne**

Haya yalitimizwa kihalisia, japo katika hali ya kihesabu ulikuwa 1:200 trilioni.

– Lango la Dhahabu la Yerusalemu
– Mji wa ajabu wa Petra wenye mwamba
– Babeli Mashuhuri
–Kuinuka na kuanguka kwa Tiro

**BA Na. 10 – Yesu na Sabato**

Kuna uhusiano gani kati ya Yesu na Sabato ya Biblia? Hii *Barua kwa Andrea* huonesha jinsi gani Sabato inahusiana na Yesu kama Muumbaji, kama kiongozi wa watu wa Mungu, kama Mtoaji wa kiungu, kama Mkombozi, kama kamishna wa manabii, kama mwanadamu, kama Yule aliyesulubiwa na kufufuka, kama mshauri wa wanafunzi, kama Mwanakondoo wa Mungu, kama Bwana anayekuja tena, kama hakimu wa ulimwengu na Mfalme wa dunia mpya. Hapa utapata kile ambacho Sabato humaanisha kwa Yesu Kristo na kwa watu wote.

**BA Na. 11 – Nini alichosema Yesu kuhusu Yerusalemu, Ujio Wake wa pili na mwisho wa ulimwengu?**

Nini tuwezacho kujifunza kutoka "hukumu ndogo" iliyofanyika mnamo mwaka 70 B.K.? Hii *Barua kwa Andrea* huonesha jinsi gani tumaini kamilifu katika maneno ya Yesu lilivyo la thamani na lenye msaada. Katika wakati huo, Wakristo wote waliokolewa, kwa sababu walijielekeza nafsi zao kwenye maneno ya Yesu tu. Kimtawalia, watu milioni moja walio thabiti kidini, waliokuwa wamesafiri kwenda Yerusalemu kwa ajili ya Pasaka, walikabiliwa na janga la kutisha. Nini tuwezacho kujifunza kutokana na kisa cha Yerusalemu kuhusu mwisho wa ulimwengu na ujio wa Yesu mara ya pili? Je tutafanya uamuzi gani?

**BA Na. 12 – Ishara ya Yesu Kurejea**

Je hatua kuu ya mageuzi inakuja – au. . . ule mwisho? Wanafunzi waliuliza: Tutajuaje kwamba unakuja na kwamba mwisho wa dunia uko hapa? Maelezo ya kina yanawasilishwa kwenye ishara nane zilizotajwa. Hali ilikuwaje kabla ya anguko la Yerusalemu na hali ikoje leo? Swali la mwisho: Je tunakabili hatua kuu ya mageuzi au hivi karibuni utakuwa ule mwisho?

**BA Na. 13 – Jitwalie Uzima Bora kupitia Uhusiano Binafsi pamoja na Mungu**

Tukichukulia kwamba ungeweza kufa leo (shambulio la moyo au ajali). Je una uhakikisho sasa wa uzima wa milele pamoja na Yesu Kristo? Usibaki gizani! Mambo matano ya kweli yatakusaidia kulipata jibu. Yeyote anayechunguza uhusiano wake pamoja na Mungu, atafanya ugunduzi wa maisha yake yote!

**BA Na. 14 – Maisha katika Nguvu ya Mungu – Kivipi?**

"…*Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele*." (Yohana 10:10) Yesu anataka tupate uzoefu wa maisha haya mapya sasa na kuyaendeleza baada ya Ujio Wake wa Pili kama uzima wa milele katika ufalme wa Mungu. Hii *Barua kwa Andrea* inahusu jinsi tunavyoweza kupata hamasa na nguvu kwa ajili ya uhusiano wenye furaha na linganifu wa maisha pamoja na Yesu.

**BA Na. 15 – Manufaa kutokana na kusoma Biblia – Kivipi?**

Pengine wakati fulani ulikuwa umepanga kujifunza mwenyewe kitabu kinachosomwa zaidi ulimwenguni, Biblia. Baadhi wameanza kukisoma, lakini baada ya hapo wanatelekeza mpango wao. Pengine kwa sababu hawakuwa wamepata njia sahihi ya kuanza. Utapata kipimo cha siku 14 kwenye hii *Barua kwa Andrea*.

**BA Na. 16 – Jinsi gani naweza kudhahimu upendo na msamaha wa Mungu?**

Jinsi gani naweza kuupata msamaha? Kwa namna gani tatizo la hatia yangu linaweza kusuluhishwa? Je hatia hujitokeza kwa namna gani? Kwa nini kuna hisia za hatia bila hatia halisi? Kwa nini kuachiliwa huru kutoka kwenye hatia ni lazima kwa ajili ya furaha yetu? Ipi njia bora ya kushughulikia hatia?

**BA Na. 17 – Je una kitu fulani dhidi ya mtu fulani?**

Nawezaje kusamehe na kusahau? Msamaha huweka huru pande zote mbili! Napokeaje nguvu ya kiungu ya kusamehe? Nawezaje kutambua endapo nimemsamehe mtu fulani kweli? Hilo lina matokeo gani juu yangu na wengine pale ninapowasamehe?

**Seti-Anzilishi Barua kwa Andrea**

Seti-anzilishi ina tarakimu zote ambazo ni muhimu ili kuanza. Hizi ni pamoja na Na. 1, 2, 3, 4, 5, 8, 13, 14 na Z1. Tarakimu hizi tayari pia zinapatikana kwenye tovuti.

*Barua zote 17 kwa Andrea* zitapatikana ifikapo mwishoni mwa mwaka 2020. Anuani ya uagizaji, ofa mbalimbali na gharama za umishenari zinapatikana kwenye "Vitabu vya Ofa" katika ukurasa wa 2020. Unaweza pia kupakua na kuwatumia watu bila malipo, kwenye www. steps-to- personal-revival.info *–Letters to Andrew*

## Kiambatisho E: Orodha ya Maombi ya Kila Siku

**Mapendekezo:**

Kama inawezekana, tafadhali zingatia kuandika kwa kila mtu:

*Jina la Kwanza na la Mwisho:* ____________________

________________________________________

*Namba ya Simu:* ____________________________

*Baruapepe:* ________________________________

*Mahitaji ya Maombi:* __________________________

________________________________________

*Anuani:* __________________________________

________________________________________

*Maelezo ya Awali:* ___________________________

________________________________________

*Mpango wa Kukutana:* _________________________

________________________________________

## Kiambatisho F: Mfululizo wa Video za Kufundishia Imani



**Tovuti kwa ajili ya Vijana na Watu Wamtafutao Mungu**

Leo hii watu wana nyenzo bora kabisa ili kufundishia na kukuzia imani katika Mungu na Neno Lake, kama hakuna mwalimu yeyote aliyepo. Ili kufundisha injili, tafadhali tafuta mfululizo wa mafundisho ya injili yenye kweli za Biblia zote muhimu. Mfululizo husika, wenye mawasilisho 20 au zaidi, kwa kawaida unafaa. Hebu nipendekeza kwamba kiongozi asikilize mada fulani yeye mwenyewe mapema, ili aweze kuhamisha juu ya mfululizo huo kwa kutaja vipengele fulani na ili aweze kutathmini endapo washiriki wako tayari kwa ujumbe huo.

**Ujumbe wa Siku za Mwisho kutoka kwa Yesu**

Umeandaliwa na Shirikisho la Kichungaji la Kanisa la Waadventista Wasabato; juzuu 6, mahubiri 86: Unabii, Itakidi, Mahubiri kuhusu Afya, Mahubiri kwa ajili ya Familia, katika hili, tunaamini. https://www.gcevangelism.net/sermons/

**Ujumuishwaji Timilifu wa Washiriki**

Tovuti kutoka Konferensi Kuu ina ushauri wenye manufaa na anuani za tovuti: Ujumuishwaji Timilifu wa Washiriki https://tmi.adventist .org/ – Nyenzo vidokezo vya TMI: Kuna vidokezo kwa ajili ya Uinjilisti, Ugawanyaji wa Machapisho, Afya na Siha, Kisukari, Utengamano kutoka katika Mfadhaiko, Shule ya Mapishi.

**Miongozo 27 ya Kujifunza Biblia**

Miongozo ya Kujifunza Biblia ya *Amazing Facts* huweza kusomwa mtandaoni bure na hata kuchapishwa kwa ajili ya kugawa ama kujifunza. Lugha kadhaa zinapatikana! www. amazingfacts/bible/study guides

**Mianzo Mipya – Sanifi ya Vijana**

Unaweza kuwasilisha Masomo 26 ya Biblia yenye vielelezo pamoja na picha tarihisi zenye uangavu mkubwa zilizosheheni maelezo ya mwasilishaji. (Kiingereza, Kihispania, Kireno, Kifaransa)
https://asiministries.org/newbeginnings/

**Kumwinua Yesu**

Upakuaji bila malipo wa masomo 30 katika lugha 10, na masomo 16 ya watoto http://www.liftingupjesus.net

**Kufunua Mafumbo ya Danieli**

Pakua mada 12 bila gharama, zilizoandaliwa na Mark Finley https://www.itiswritten.com/bible-studies-unsealing-daniels-mysteries

**Tumaini Huamsha – Mfululizo wa Mkutano wa Injili**

Mawasilisho 20 kutoka kwa John Bradshaw: Je unajaribu kupambanua nyakati za sasa ambazo hazijawahi kamwe kutokea? Je umejiandaa kwa ajili ya kile kinachokuja hapo mbeleni? Hivi tunaishi kweli katika nyakati za mwisho? Masomo ya Tumaini Huamsha yanaleta urajufu kuhusu mada za sasa zenye mguso mkubwa. CD zinauzwa dola 59.99

https://itiswritten.tv/programs/hope-awakens

**Muda Unayoyoma – Mawasilisho 20**

Pastor Doug anasema kuhusu mfululizo huu wa pekee wa masomo ya Biblia yaliyosheheni nguvu: "Nakutana na watu wengi sana wenye shauku ya kuyafahamu matukio ya wakati ujao, lakini hawataki kuhanikizwa kwa dini. Katika mfululizo huu, tunayachunguza Maandiko bila kuhusisha ufahamu wa kidini uliozoeleka, ili tuweze kubaini historia na ujeo halisi wa sayari yetu. … Natazamia kuwashirikisheni utafiti wangu.

https://www.amazingfacts.org/media-library/watch/archives/o/144/t/ time-is-ticking-away

**Ugunduzi wa Kale katika Ufunuo**

Mawasilisho 26 (3ABN); Mark Finley anachunguza matukio makuu ya unabii wa Biblia yakidhihirisha mpango wa Mungu kwa ajili ya hatima ama ujeo wetu. https://www.youtube/revelation's ancient discoveries

**Video juu ya Roho Mtakatifu na Maombi**

Mawasilisho 26 ya Dennis Smith, 3 ya Roy Rugless, 5 ya Colin Hone – unayapata kwenye rasifi iitwayo "Video" na

"Media". Unaweza kuviagiza Vitabu vya Siku 40 na zaidi kwenye anuani ileile.

https://www.spiritbaptism.org/

**Jinsi ya kubatizwa na Roho Mtakatifu?**

Dwight Nelson – mahubiri 3 https://steps-to-personal-revival.info/

**Hatua za Uamsho Binafsi**

Kitabu-lahani(Audio), vipengele 7, Mhutubu: Mike Fenton

Mahubiri-video, vipengele 7 kutoka kwa Helmut Haubeil http://steps-to-personal-revival.info

**Itakadi, Uchawi na Mlipuko wa Ushetani** Huburi Na. 11 https://www.gcevangelism.net/sermons/

**Mfululizo wa Injili wa Truth 4 Youth**

Kwa watoto wenye umri wa miaka 5-13

Mfululizo wa DVD wa Mwanafunzi Kijana uitwao *Truth 4 Youth* DVD hukupatia vifaa na nyenzo unazohitaji ili kuwasilisha programu nzima ya uinjilisti kwa kundi-jamii moja, na muhimu zaidi tunaloweza kulifikishia ujumbe. Mfululizo kamili wa uinjilisti kwa ajili ya watoto! "Dirisha" la wakati lenye ufanisi mkubwa zaidi kwa ajili ya kuwafikishia watoto injili ni umri kati ya miaka 5 na 13. Kwa kweli, **utafiti uliofanywa na Taasisi ya Barna huonesha kwamba watoto wenye umri kati ya miaka 5 na 13 wana uwezekano zaidi ya mara 5 kuliko watu wazima kufanya taadhima kwa Kristo."** $ 129,99

www.itiswritten.shop/product/truth4youth

**Programu ya vijana iitwayo "Maswali Muhimu Zaidi" – Mawasilisho 10**

https://www.amazingfacts.org/media-library/watch/archives/o/116/t/ most-important-questions--miq-

**Kusudi Hatimati – Mawasilisho 4** – Mfululizo mfupi wa Kusudi Hatimati ni mzuri kwa maswali haya ya msingi vilevile:

https://www.amazingfacts.org/medialib-ray/watch/archives/o/125/t/ulti- mate-purpose

**Fomula ya Imani – Mawasilisho  6**

Huwasilisha kikamilifu kuhusu misingi ya wokovuv– Pastor Doug Batchelor hukupitisha katika safari ya Biblia ibadilishayo maisha ili kubainisha hatua muhimu za wokovu, akikuongoza kwa kukushirikisha katika imani tasihali ya kiroho ... https://www.amazingfacts.org/medialibray/watch/archives/o/156/t/formula-4-faith

## Uzoefu Ugusao Moyo Mwishowe

**Louisa M. R. Stead** alizaliwa Dover/Uingereza kisha akahamia Marekani pamoja na mumewe katika miaka ya 1880. Miezi ya kwanza ilikuwa migumu sana hadi mumewe akapata kazi. Likizo yao ya kwanza ilikuwa siku tatu baharini. Mumewe alijaribu kumwokoa mvulana aliyekuwa akipigania maisha yake kwenye bahari yenye dhoruba. Hawa wawili walipigwa na wimbi kali wakazama.

Sasa Luisa hakuwa na mumewe na akiwa peke yake pamoja na binti yake mwenye umri wa miaka mitatu. Baada ya majuma machache, alilazimika kuondoka kwenye chumba chake cha kupangisha kwa sababu hakuweza kumudu kulipa kodi. Aliandika kwenye shajara yake:

**“Siwezi kuthubutu kuendelea kudumisha macho yangu kwenye tatizo ilhali ninaye Mungu wa pekee ajabu aliyekufa kwa ajili yangu. Nataka kuangalia mbali na matatizo yangu na kumwangalia Yesu kwa sababu yu radhi na anaweza kutusaidia. Endapo yuko pamoja nami, wala siogopi.”**

Alilala kwenye benchi nje akiwa na mwanawe mikononi mwake ili kumpa joto. Katika kipindi chote hicho, hakuomba msaada, bali alimsifu Mungu. Alisema:

**“Bwana, sina chochote sasa hivi, lakini watu kwenye Biblia ambao wamepoteza kila kitu na bado wanakusifu. Wala huhitaji kunibariki ili niweze kukusifu. Nakutumaini na kukusifu kwa ajili ya chochote ninachopata uzoefu nacho.”**

Akiwa katikati ya bustani hiyo – ilikuwa mwaka 1882 – Louisa alianza kuandika wimbo:

**“Kumtegemea Mwokozi Kwangu Tamu kabisa”**

Alipouimba wimbo huu, bwana mmoja akasimama na kuhoji: “Lazima utakuwa umefanikiwa sana, kwa sababu unaimba kwa mvuto mkubwa.” Akajibu: **“Wala siimbi kwa vile mambo yangu ni maridhawa. Naimba kwa sababu namtumaini Yesu.”**

Katika harakati ya mazungumzo haya, bwana huyo akagundua kwamba hakuwa na kazi, mumewe alikuwa amefariki, chakula chao kilikuwa kinaisha na alilazimika kulala usiku huo kwenye benchi hii pamoja na binti yake. Alitikisa kichwa chake kwa mashaka. “Na bado unaimba ...?”

Akajibu: **“Ni suala la muda tu kabla Yesu hajaingilia kati. Nina furaha kulifikiria hasa jambo hilo.”**

Matokeo yalikuwa kwamba kijana huyu muungwana alikuwa mmojawapo wa watu matajiri zaidi wakati huo. Alimiliki miundombinu yote ya reli nchini Marekani. Alimpatia kazi ofisini, jambo alilofurahia sana kuliafiki. Aliifanya kazi hii vizuri sana kiasi kwamba baada ya muda mfupi alimwambia mama huyu: “Unafanya kazi kana kwamba una mcha Mungu. Unaifanya vizuri sana, bila kujali kama mtu fulani anatazama au la.” Alijibu: “Hufahamu vizuri, wala sikufanyii wewe kazi, namfanyia Yesu.”

Kazi yake makini na talanta yake bayana ya uratibishaji ilisababisha apandishwe cheo daima na kwamba hatimaye alikuwa msimamizi wa shirika zima la reli katika njia zote za reli. Mmiliki wake aliliweka hivi: “Namwamini kuliko ninavyojiamini mimi mwenyewe.” Hali yake ya maisha ikabadilika. Alipata mshahara mzuri sana, na aliweza kununua nyumba kubwa na pia kumhudumia vyema binti yake.

**Baada ya miaka miwili, alisumbuliwa na swali, nini ambacho Yesu angefanya kama angekuwa mahali pake?**

Aliiacha kazi yake adhimu, akauza nyumba yake na kwenda Afrika Kusini pamoja na binti yake ili kufanya kazi kwenye misheni miongoni mwa watu weusi hasa kwa ajili ya watoto. Baada ya miezi sita alikuwa amemaliza fedha zake zote. Alisafiri kwenda kutafuta pesa tena. Kisha akarudi Zimbabwe pamoja na binti yake. Aliendelea na mfumo huu wa maisha kwa kipindi

kilichofuata cha miaka 32, hadi mauti yake huko Zimbabwe mnamo mwaka 1917. Binti yake aliendeleza kazi ya mama yake. Louisa aliishi maisha ya tumaini na kujitoa kwa Bwana wake, aliyempenda sana.

(Ilisimuliwa kwenye hubiri huko Austria na P.G. Ilifasiriwa tena kutoka Kijerumaini kwa msaada wa Google.)

## Kumtegemea Mwikozi

1. Kumtegemea Mwokozi, Kwangu tamu kabisa;
   Kukubali neno lake Nina raha moyoni.

   *Marudio*

   Yesu, Yesu namwamini, Nimemwona thabiti;
   Yesu, Yesu yu thamani, Ahadi zake kweli.

2. Kumtegemea Mwokozi, Kwangu tamu kabisa
   Kuamini damu yake Nimeoshwa kamili.

3. Kumtegemea Mwokozi, Kwangu tamu kabisa;
   Kwake daima napata, Uzima na amani.

4. Nafurahi kwa sababu Nimekutegemea;
   Yesu, M-pendwa, Rafiki, Uwe nami dawam.

Oh, kumtumaini Yeye ili kuipata neema! (Lahani: www. Louisa M.R.Stead)

## Seti-Anzilishi – Barua Kwa Andrew Ili Kuwaongoza Watu Kwa Yesu

Jinsi gani tunaweza kufanya kazi kwa kutumia Barua kwa Andrew ikiwa imejumuishwa kwenye Seti-Anzilishi imeelezewa katika ukurasa wa 160. Bahasha ina nakala ya kila moja ya barua zilizotajwa hapa kwa ajili yako. Pamoja na hilo, unahitaji bahasha kwa ajili ya kila roho ya thamani unayohitaji kuiongoza kuja kwa Kristo kwa msaada wa Mungu. Utaratibu wa kawaida kwa ajili ya usambazaji ni:

4 Unasibu wa Maisha: Je Mungu Yupo au La?
1 Imani ya Ukristo Yajaribiwa
8 Mafunuo ya Unabii kuhusu Yesu Kristo
2 Faharidi na Apitaye Ulinganishi: Yesu wa Nazareti
3 Nini taanani kuu ya Biblia?
Jitwalie Uzima kupitia Uhusiano Binafsi pamoja na Mungu
(evtl. Z1 Njia ya Uzima wa Milele (na Eiden K. Walter))
Maisha katika Nguuv ya Mungu – Jinsi gani?
5 Ushindi dhidi ya Tumbaku na Pombe

Mabainisho mafupi kuhusu maudhui ya Barua zote kwa Andrew yanaweza kupatikana katika Kiambatisho D, ukurasa wa 192. Maelezo ya kina zaidi ya mpangilio ambapo hupitishwa yamewasilishwa katika sura ya 9.

**www.steps-to-personal-revival.info:**

Barua kwa Andrew

Barua kwa Andrew zinaweza kupakuliwa pia bila malipo au kutumwa kwa mtu fulani kutoka kwenye tovuti hii.

"Lakini Mungu ashukuriwe, atupatiaye ushindi kupitia Bwana wetu Yesu Kristo." (1 Wakorintho 15:57 NKJV)

KITABU CHA 1: www.steps-to-personal-revival.info

**HATUA ZA UAMSHO BINAFSI**

*Kujazwa Roho Mtakatifu.*

**Bwana wetu Mwenye ametupatia amri:[1] Ruhusuni nafsi zenu kwa ulinganifu na mara kwa mara zijazwe upya kwa Roho![2]**

1. E.G. White, Mount of Blessing, MB 20.3 (egwwritings.org)
2. Johannes Mager, Auf den Spuren des Heiligen Geistes (Lüneburg, 1999), uk. 101

Taarifa za Uagizaji ukurasa wa 2 www.steps-to-personal-revival.info

KITABU CHA 2: www.steps-to-personal-revival.info
HATUA ZA UAMSHO BINAFSI

**KAENI NDANI YA YESU**

UNAFANYAJE HILO?

"Kaeni ndani Yangu, Nami ndani yetu." Kukaa ndani ya Kristo humaanisha upokeaji wa Roho Wake daima, maisha ya kujisalimisha kikamilifu kwa huduma Yake.

E.G. White *(Desire of Ages, DA uk.676.2)*

Taarifa za Uagizaji ukurasa wa 2
www.steps-to-personal-revival.info

"Kukaa ndani Yake siyo kazi tunayolazimika kuifanya kama sharti fulani ili kufurahia wokovu Wake. Badala yake, ni kuridhia kwetu kumruhusu afanye kila kitu kwa ajili yetu, ndani yetu, na kupitia kwetu. Ni kazi anayoifanya kwa ajili yetu—matokeo na nguvu ya upendo Wake ukomboao. Wajibu wetu ni kujisalimisha tu, kutumaini tu, na kumngoja Yeye atekeleze kile ambacho ameahidi." (Andrew Murray)

SIKU 40 – KITABU CHA 1:

**MAOMBI NA IBADA**

**Ili Kujiandaa kwa ajili ya Ujio wa Pili**

Dennis Smith

Agiza: www.spiritbaptism.org

Je unatamani usomaji na maisha ya maombi ya maana zaidi? Je unahisi hitaji la kuwasiliana na wengine kwa ajili ya Kristo?

Ikiwa ndivyo, umekuja mahali sahihi. Kitabu hiki kina siku 40 za masomo ya maombi yaliyokusudiwa kuimarisha uhusiano wake pamoja na Kristo na kukuwezesha kuwaongoza wengine waje Kwake.

Kwa nini siku 40?

Biblia hutuambia matukio kadhaa muhimu yaliyodumu kwa kipindi hiki mahususi:

- Mvua ilinyesha kwa siku 40 wakati wa Gharika.
- Musa alikuwa juu ya Mlima Sinai pamoja na Mungu kwa siku 40.
- Wapelelezi wa Israeli walitumia siku 40 kuichunguza Nchi ya Ahadi.
- Yona aliionya Ninawi kwa siku 40.
- Yesu alitumia siku 40 jangwani baada ya ubatizo Wake.
- Yesu alitumia siku 40 pamoja na wanafunzi Wake baada ya ufufuo Wake.

Mungu anataka kufanya kitu fulani muhimu maishani mwako, vilevile. Siyo tu kwamba anatamani kukuvuta uje katika ushirika wa karibu zaidi pamoja na Yeye – pia anataka kuwahudumia wengine kupitia wewe. Na kadiri unavyotumia siku 40 za kustaajabisha pamoja na Mungu, atakuandaa kwa ajili ya zahama ya mwisho duniani na ujio wa pili wa Kristo ambao umetarajiwa kwa muda mrefu.

SIKU 40 – KITABU CHA 2:

**MAOMBI NA IBADA**
**Ili Kuhuisha Uzoefu Yako pamoja na Mungu**

Dennis Smith

Agiza: www.spiritbaptism.org

Ni tofauti gani ambayo siku 40 zinaweza kufanya?

Tofauti maridhawa, kama unaomba Ungana na Dennis Smith kwenye safari ya kiroho ya Siku 40 itakayobadili maisha yako.

Kadiri jutolea kikamilifu kwenye siku 40 za usomaji wa kiibada na maombi binafsi, maisha yako ya maombi yatakuwa linganifu na fanisi, imani yako itakua kadiri unavyoshuhudia maombi yaliyojibiwa, na muunganiko wako na waumini wenzako utakuwa wa kina.

Mwenendo wa kila siku wa usomaji wa kiibada uinuao hufuatiwa na huduma ya maombi husika pamoja na tafakari binafsi na mjadala wa maswali. Umetamani sana ushindi wa kiroho lakini hukujua wapi pa kuanzia, anzia hapa. Smith atakuongoza kupitia siku 40 za mafundisho kivitendo ya Biblia yaliyo muhimu kwa ajili ya kila Mkristo kujifunza.

Katika mtindo wa Siku 40 mashuhuri za Smith: Maombi na Ibada ili Kujiandaa kwa ajili ya Ujio wa Pili, kitabu hiki kinaweza kusaidia kuhuisha uzoefu wa kiroho wa watu binafsi, vikundi vidogo, na makanisa yote. Gundua mwenyewe ni tofauti ilioje ambayo siku 40 zinaweza kufanya.

WWW. STEPS-TO-PERSONAL-REVIVAL.INFO
**Kujazwa Roho Mtakatifu**
Tovuti hii hutembelewa na nchi 143.

Unaweza kusoma, kutoa nakala, kuwatumia marafiki vitu na nyenzo zote bila gharama katika lugha zote zilizotumika na kutafsiriwa.

**Jinsi gani "Hatua za Uamsho Binafsi" zimebadilisha maisha yangu**
Ushuhuda wa Dwight Nelson, Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Chuo Kikuu cha Andrews

**Waadventista Wasabato na Roho Mtakatifu**
Inatokeaje kwamba tunakoswa Roho Mtakatifu? Sababu, Matokeo na Ufumbuzi

**Kitabulahani, "Hatua za Uamsho Binafsi" Mhutubu: Mike Fenton**

**Jinsi Gani ya Kubatizwa Roho Mtakatifu? – vipengele 3**
Mahubiri ya Video kutoka kwa Dwight Nelson

**"Hatua za Uamsho Binafsi"**– vipengele 7 na

**“Kaeni Ndani ya Yesu”** – vipengele 5
Mahubiri ya Video kutoka kwa Helmut Haubeil

**Barua 17 kwa Andrew**–Nyenzo za kimishenari zilizo-jaribiwa na kupimwa kwa ajili ya kujenga imani (zaidi katika Washirika wa Yesu Waliojazwa Roho, Sura ya 7 na 9)

# Washirika wa Yesu Waliojazwa Roho

Jinsi gani tunakuwa watu hao?

*Nini maana ya kuwa na mafanikio maishani? Ni ahadi gani ambazo Mungu ametupatia kwa ajili ya kuishi maisha yenye mafanikio? Hakuna nguvu kwenye mipango midogo. Mungu wetu wa pekee ajabu anataka tufikirie mambo makuu. Je unataka kuwa mshirika Wake kazini?*

*Yesu anatamani kuwa na watendakazi-wenza, waliojazwa upendo Wake. Washirika ambao kupitia kwao anaweza kuwapenda wengine. Hivyo, ni muhimu kwamba nidhahimu kiwango kamilifu cha upendo wa Mungu mimi binafsi. (angalia Waefeso 3:17).*

*Ni wazo mahiri ilioje aliyo nayo Mungu kwa ajili yetu kuhusu kutumika, kutoa, na kusaidia! Kimsingi ni suala lisiloaminika kuhusu kile ambacho Mungu ametuandalia. Na, jinsi gani tunamtumikia Mungu? Je tunamtendea Mungu kazi kwa uwezo wetu wa kibinadamu, au Mungu anafanya kazi kwa uwezo Wake wa kiungu kupitia sisi? Tofauti ni nini?*

*Yesu alisema: "Nifuateni, Nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu." (Mathayo 4:19) Ni kwa namna ipi ya kushangaza ambapo Yesu huwafanya wavuvi wa watu kutokana na sisi?*

*Helmut Haubeil anasimulia jinsi alivyojifunza kuwaongoza watu hatua kwa hatua kuja kwa Yesu. Uhusiano binafsi pamoja na Yesu ni uhusiano wa thamani zaidi uliopo. Nawezaje kuwaonesha wengine jambo hili? Ni swali gani la ufunguzi linaweza kutumika ili kufika kwenye wazo kuu kwa ustadi na moja kwa moja? Ni nyenzo gani zilizopimwa na kujaribiwa zilizopo ambazo hufanya iwe rahisi zaidi kwa wasaidizi na washiriki wakati wa kuzungumzia imani? Nyenzo hizi za thamani zimejumuishwa kwenye masomo mbali mbali yajulikanayo kama "Starter-set".*

*Kisha wazo la kiroho la umishenari linabainishwa, ambalo huonesha jinsi gani sisi kama watu binafsi au vikundi, kama kanisa au konferensi, tunaweza kusonga mbele kwa ushindi chini ya uongozi wa Mungu.*

*Hebu Mungu atupatie kila mmoja wetu furaha ya kuwa mshirika wa Yesu aliyejazwa Roho!*

**ISBN 978-9987-726-23-3**

Kibidula